

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 1 Julai, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kuwasilisha Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

### **MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo bahati nzuri Kiongozi wa Kambi ya Upinzani yupo. Kwa hiyo, nitamwita awe mwulizaji wa kwanza kufuatana na Kanuni zetu. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, mahasimu wawili! (*Kicheko*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo wa Rukwa hawapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi hivi karibuni imeendelea na zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Visiwani Zanzibar. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeupa uwakala Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Daftari la Wapiga Kura la Zanzibar, lina idadi ya wapiga kura wapatao 408,000, Daftari la Wapiga kura la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina wapiga kura kama 465,000. Wakati ZEC ni Wakala wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wa Zanzibar, Daftari hilohilo linatumika kwa kuwapigia kura Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, lakini lile la Jamhuri ya Muungano linatumika katika Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, huoni hapa kuna utata wa Kikatiba na wa Kisheria kwamba, Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hatumii Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika kuwapata Wabunge kutoka Zanzibar tofauti na Wabunge wenzao wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali inasema nini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Hamad, swali lake gumu sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu Bunge limepewa Mamlaka ya kutunga Sheria na moja ya Sheria zilizotungwa ni ile inayohusiana na Uchaguzi Mkuu. Sheria hiyo inatawala taratibu zote za Uchaguzi kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Visiwani, iko Sheria nyingine ambayo nayo imetungwa kuongoza na kusisimamia taratibu hizo za Uchaguzi. Ile inahusika zaidi na masuala yote ya Uchaguzi yanayohusiana na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Hamad kwamba, Sheria hii ambayo sisi tunaitumia hapa kwa ajili ya kupata Wabunge, kwa kuwa ndiyo Sheria hiyo hiyo ambayo inatumika Zanzibar kwa ajili ya Wabunge ambao wanakuja kuingia katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kimantiki ilitakiwa Sheria moja ndiyo isimamie maeneo yote mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu kwa upande wa Sheria ya Zanzibar kwa mfano, masharti kama yale ya ukazi wa miezi 36 sisi huku hatuna. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba iko tofauti kidogo kati ya Sheria hii pamoja na ile ya upande wa Visiwani.

Kwa hiyo, mimi ninadhani rai ya msingi ipo kwamba, pengine Serikali ingetazama namna tunavyoweza kuwianisha Sheria hizi mbili kwa upande wa hawa Wabunge wanaotoka upande wa Zanzibar kwa ajili ya kuja kujumuika na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vingenevyo itaendelea kuonekana kwamba, kuna migongano ya kisheria ambayo ingetakiwa kwa kweli kuwa katika Sheria moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninafikiri ni jambo zuri, tutamwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliangalie, awasiliane na Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenzake waone hii hitilafu ni namna gani inaweza ikarekebishwa. Pengine kitakachohitajika ni marekebisho ya kisheria tu ili Sheria moja tu iweze kutawala kwa maana ya yale ambayo yanahusiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulielewa hili na kukubali kwamba, kuna tatizo la kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa Bunge hili sasa lina muda mfupi na hayo ni marekebisho ya kikatiba na kisheria na hatuna muda wa kuyafanya, na kwa kuwa tunaingia kwenye uchaguzi ambao tayari una utata wa kisheria na kikatiba, huoni kwamba inawezekana kabisa Mbunge akachaguliwa na hatimaye watu wakaenda Mahakamani na kudai kwamba, huyu Mbunge hakuchaguliwa kihalali kwa sababu

utaratibu wa kupiga kura kumchagua siyo sawa na vile ambavyo Sheria ya Jamhuri ya Muungano inasema.

Je, huoni kunaweza kutokea hitilafu ya Wabunge kuondolewa na Mahakama kwa sababu Sheria haikufuatwa?

**WAZIRI MKUU:** Ukiniuliza hilo ni gumu kwa sababu itabidi ningoje sasa nione mkienda Mahakamani, busara za Mahakama zitasema kitu gani, kwa sababu, kikubwa hapa ni kuona masharti ambayo yako kwenye Katiba yetu na yale ambayo yako upande wa Zanzibar. Kama nilivyosema kumbukumbu yangu ya haraka haraka eneo moja ambalo ninaliona kweli linaleta kasoro au tofauti kidogo ni lile la ukazi.

Lakini, kama ni la ukazi tu, mimi ukiniuliza nitasema pengine kinachohitajika hapa ni kutafuta tu namna ya kuondoa hiyo hali kwa ajili ya Mbunge huyu. Lakini, kimsingi sidhani kama Wabunge wa upande wa Zanzibar wana tatiizo, na hilo la ukazi sidhani kama ni suala kubwa hilo. Hapa ni ile kasoro ya kisheria ambayo nadhani ndiyo ninaiona kama Sheria ni lazima ikae vizuri isiwe na hitilafu ambazo zinaleta kasoro. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni tumepata taarifa kutoka maeneo mbalimbali na tuna nyaraka zinazohusika na hilo kwamba, Wakuu wa Wilaya wamekuwa wakitumia ofisi za Serikali, muda wa Serikali, vyombo vya Serikali kuwaalika na kuwaita wafanyabiashara katika Ofisi zao au katika Ofisi mbalimbali za Serikali bila hata kuwaambia wanaitiwa nini, jambo linaloashiria kwamba, mtu anaitwa bila hiari yake na wakifika huko wanatakiwa kuchangia Chama cha Mapinduzi. Kwenye maeneo mengine tumepokea pia hata Watendaji wa Vijiji. Mfano halisi ni Nzega, *WEA* anatakiwa achangie shilingi 20,000/= na *VEO* achangie shilingi 10,000/= na hata kuna vitisho kwamba wasipofanya hivyo watafutwa kazi.

Je, Serikali inatoa tamkoaa gani kuhusu hali hii ambayo inatengeneza uwanja usio sawa kwa kutumia Ofisi ya Serikali ambayo ni mlezi wa sisi wote? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningetaka kumjibu Ndugu yangu Dr. Slaa. Kiungwana ningesema, si na wewe ukawaombe wa kwako. Lakini, ninajua nikisema hivyo atasimama haraka haraka kwamba siyo jibu nililokuwa nataka lipatikane.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ninasema tu kwamba, nichukue hii sehemu ya kwanza ya Mkuu wa Wilaya ambaye anawaita wafanyabiashara, pengine bila kujua

unaitiwa nini, anakwenda wanakutana pale na anamwambia bwana ninaomba mchango wako kwa ajili ya Chama cha Mapinduzi, hiari yake kukubali au kukataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitafurahi sana kama nitapata mfanyakishara ambaye anasema alishurutishwa au akafungwa kamba ili aweze kukichangia Chama cha Mapinduzi. Mimi ninadhani hilo ndiyo litakuwa hasa la msingi katika hilo na ninafikiri wafanyakishara ni watu wazima, na sidhani kama wanaweza wakashurutishwa kama wao mwenyewe hawapendi, sidhani lakini kama wapo *fine* tunaweza tukalipokea tukamwuliza huyo *DC* tukapata maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Wilaya huyu, kwa mfumo ulivyo hapa tusije tukasahau kwamba, vile vile ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya na ni Kamisaa wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kwa maana hiyo anao vilevile wajibu wa kusaidia kutafuta michango kama kiongozi ambaye yuko ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Tatizo hapa litakuwa ni moja tu endapo atatumia dola au uwezo wake kumshurutisha mtu kuweza kuchangia. Hilo ndiyo ninaliona litakuwa tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mtendaji wa Serikali ya Kijiji au *WEO* kwamba na yeche analazimishwa kuchangia. Labda nirudi nyuma kidogo kwamba, kwa taratibu tulizonazo hapa nchini Mtumishi wa Serikali anaruhusiwa kuwa mwanachama wa chama chochote, ndiyo maana huko ndani tunao wanachama wa *CUF*, *CHADEMA* na kadhalika na wanaruhusiwa vile vile kuchangia vyama vyao pale watakapokuwa wameombwa na kwa masharti watakayokuwa wamekubaliana kwenye chama kinachohusika.

Hapa unaloliona kama tatizo ni pale ambapo umekwenda umemshurutisha huyu mtumishi hata kama ni mwanachama wako wa Chama cha Mapinduzi au hata kama angekuwa mwanachama wa chama kingine. Kama ni hiari halina tatizo, hasa sisi huku ndani Serikalini tunachangia chama chetu kwa hiari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna ushahidi wa namna yoyote ambao pengine ni mabavu yametumika, mimi nitakuwa tayari na pengine niharakishe tu kutoa kama tahadhari tu kwa viongozi wenzangu hawa kwa kweli kwa kiasi kitakachowezekana ni vizuri michango hii ikaendelea kuwa ni ya hiari na wala siyo ya lazima, siyo ya shuruti. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu Waziri Mkuu wangu daima anajaribu kuwa muungwana, amejibu kistaarabu lakini amehalalisha kitu kimoja ambacho sijui kama ndiyo nia yake. Mtumishi wa Serikali kwa maadili ambayo sasa hivi yameaandaliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa maadili

yenewe ya kazi yake hategemewi kutumia Ofisi ya Serikali kufanya kazi ya chama chake.

Nje ya saa zake za kazi mimi sina shida, lakini anapotumia nyaraka za Serikali tena za Ofisi ya Waziri Mkuu, na kwa mathalani huyu kutoka Sumbawanga anaambiya kabisa, ameteuliwa sina hakika kama aliteuliwa na Waziri Mkuu kama ndivyo kweli anatumia vifaa vya ofisi ambayo tumepitisha kwenye Bajeti hii ambayo ni ya Watanzania wote, wenye vyama na wasio na vyama, ambao hawana hospitali na wangependa pesa yao Mkuu wa Wilaya afanyiekazi ya kujengea hospitali, asukume shule zao anafanya uchangishaji. Vifaa vya Ofisi ni mabilioni, ratiba iliyoandikwa hapa ni kubwa kweli kweli anazunguka Kata zote, Vijiji vyote ni hela ya Serikali ya watu wasio na chama na wenye chama.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa Waziri Mkuu atuambie matumizi haya ya fedha za umma kwa kazi ya Chama Cha Mapinduzi. Je, haya pia hata angekuwa kada ni halali au siyo halali, na kwa kutokutoa tamko sahihi . Je, hahalalishi aina fulani ya ujisadi kwa kutumia fedha za umma? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kubwa analolisema hapa ni ile kwamba, jamani eeh, mnatuonea sisi wenzenu, hao ma-*DC* wanatumiza huko mawilayani. Mimi nadhani ndiyo ujumbe kubwa ambayo nadhani pengine ndiyo ya kuchukua zaidi.

Sasa labda nikuombe tu kwamba, wewe tukabidhi hayo makaratasi na tutayafanyiakazi, tutatoa maelekezo ambayo yatasaidia zaidi kuweza kuwawezesha Wakuu hawa katika utekelezaji wa mambo yao hayo, basi wajiepushe na matumizi ambayo pengine yanaweza yakatafsiriwa kama Dr. Slaa alivyolielewa. Nadhani tutakuwa tumesaidia. (*Makofit*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kumwuliza swali moja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa hivi majuzi Serikali ilitutangazia maeneo mapya ya utawala kwa maana ya Kata mpya, Tarafa mpya na Wilaya mpya, na maeneo haya yanahitaji kujitegemea na kwa kuwa tunaingia katika Uchaguzi Mkuu.

Je, ni utaratibu upi utatumika kuunda Halmashauri katika Wilaya na Tarafa katika Kata mpya zilizoanzishwa katika maeneo haya ya utawala?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Vita Kawawa, swali lake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ambayo Rais amekubali yaanzishwe kwa sehemu kubwa kabisa yamezingatia mipaka ya majimbo na vilevile mipaka ya Kata. Kama kuna eneo ambalo unakuta pengine Kata tumelazimika kuigawa kwa namna moja au nyingine kwa kumega kipande kutoka kwenye ile Kata, hiyo itahitaji ufumbuzi wa

haraka kwa sababu uchaguzi wa Serikali za Mitaa umeishakamilika sasa tunakwenda kwenye uchaguzi ambao utahusisha Kata.

Kama Kata imebaki nzima, imehama ikiwa Kata kamili hakuna mgogoro utakaojitokeza hata kidogo, maana ni Kata yote imehama kuingia katika eneo jipya. Tunachofanya sisi sasa ni kuhakikisha tu kwamba hizo Kata zinatangazwa mapema, tume taarifiwa mapema ili na wao waweze kuingiza katika taratibu zao za mipaka. Kwa hiyo, kwa upande huo sidhani kama litakuwa ni tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Halmashauri zitakazoundwa hizi kwa sehemu kubwa hazina tatizo kwa sababu mipaka ya jimbo kama haikuharibu kitu chochote, Halmashauri itatengenezwa kama ilivyo kwa kuzingatia mipaka kama ni ya jimbo, au ni ya Kata na usisahau kwamba, hivi ni vyombo viwili ni tofauti ingawa vinafanyakazi katika eneo moja.

Kwa hiyo, kwa upande wa Halmashauri zikiishatengenezewa utaratibu wa kisheria, basi itatangazwa tu kwamba, sasa *formaly* Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imekamilika, Mkurugenzi atateuliwa na taratibu nyingine zitafuata. Kwa hiyo, sidhani kwa sasa kwamba tutakuwa na tatizo kubwa isipokuwa katika maeneo mawili ambayo tunanadhani kwamba, yatakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni Wilaya ya Kahama ambapo tumeanzisha Wilaya ya Ushetu. Lakini hilo tutalitazama kwa undani tuone namna tutakavyoliondoa. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Sina swali napenda tu kuishukuru Serikali kwa kutupa Kata mpya 6. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Jamani !!!!!. Haya tunaendelea sasa tunakwenda *CUF* nimwite Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. Maana yake inabidi Waziri Mkuu apumue kidogo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu leo tarehe 1 Julai, 2010 kwa mujibu wa mtangamano wa ushirikiano mpya huu wa Afrika Mashariki ni siku ambayo tunategemewa kuingia

hatua ya pili ya Soko la Pamoja. Hatua hii kimsingi inatoa fursa kwa watu kuingia katika nchi hizi kwa urahisi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma.

Je, unatoa kauli gani ya Serikali kwa wale Watanzania watakaotumia fursa hii wakauza ardhi ya nchi yetu kinyemela?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimjibu Mheshimiwa Khalifa swali lake kama ifuatavyo. Kwanza nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli makubaliano yale yanataka leo ndiyo iwe tarehe rasmi ya utaratibu wa Soko la Pamoja kuanza kutumika. Ni kweli kwamba linafungua milango katika maeneo mengi.

Lakini nataka vile vile niendelee kusema kwamba chini ya makubaliano hata chini ya utaratibu huu yako maeneo mengi sana ambayo bado yatafuata sheria za kila nchi isipokuwa pale ambapo nchi mbili zimekubaliana kufanya watakavyoona inawapendeza. Lakini kwa sehemu kubwa bado sheria zitatawala.

Kwa hiyo, kwa upande wa Tanzania masuala ya ardhi kwa makubaliano yalivyo ni kwamba yattatawaliwa na sheria za hapa Tanzania, kama ilivyo katika masuala mengine ya pasipoti na vitu vingine kama hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nadhani rai kwa Watanzania maana hii naitoa kwa ujumla kabisa. Kwa kutambua kwamba sheria hii ya ardhi au sheria za ardhi bado zipo kwa lengo la kulinda ardhi ya Tanzania. Si busara na wala haitakubalika kwa mujibu wa sheria mtu yoyote kujaribu kuuza ardhi kwa kutumia maneno yako kinyemela. Kwa sababu ikigundulika ni dhahiri mauzo haya yatafutwa, kwa sababu ni kinyume cha utaratibu.

Lakini nisaidie vile vile kwamba ni muhimu sana kwa Watanzania kujua kwamba mtu ambaye bado hajatimiza masharti yanayomwezesha kumiliki ardhi hapa hawezi kumiliki ardhi kama ni mtu kutoka nje, isipokuwa kwa madhumuni ya uwekezaji peke yake ambayo ina masharti yake ya miaka na masuala mazima ya uendelezaji.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ufanuzi huo mzuri sana kwa faida ya nchi yetu. Swali moja la nyongeza.

Ujio huu unaweza vile vile ukatumiwa na waajiri binafsi katika kuwadhalilisha Watanzania ama kwa kuwafukuza kazi au kwa kuwapunguza uwezo wao wa kazi kwa sababu tu wanakuja wageni kutoka nchi zingine eti wana uwezo zaidi. Unawaambiaje waajiri hawa kama wakigundulika wamechukua vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na taratibu zetu? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama ndio niseme nini ndiyo hisia ya Wabunge wote. Kwa sababu naanza kupata picha kwamba pengine eneo hili linahitaji labda huko tunakokwenda kupata siku moja hivi ya semina ili Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki aweze kutupitisha katika eneo hili tena kwa sababu tusiende na hofu au bila kuelewa hasa nini kiko mbele yetu. Kwa sababu hata upande wa ajira si kwamba dirisha lile la ajira limefunguliwa tu kiholela, hapana. Ukipitia ule mkataba utaona tumetengeneza programu kabisa kwamba katika eneo fulani tutaruhusu ajira ya watu wa aina fulani kuanzia kipindi fulani.

Kwa hiyo, kila kitu kimewekwa ili tuweze kuhakikisha kwamba tunatetea na kulinda maslahi ya Tanzania.

Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba halitakuwa jambo la holela tu kwamba kila mtu anakuja hapa basi shamba la bibi, hapana. Lakini bado rai yako ni ya msingi kwamba ni vizuri tukaendelea kuwakumbusha na kuwaasa Watanzania hasa wale wafanyabiashara kwamba jamani tuenzi kwanza nyumbani. Tunao wataalamu wa kutosha, tunao watu ambao wanaweza kutusaidia kufanya kazi hapa vizuri wapeni fursa ya kwanza Watanzania na ni pale tu inapoonekana fursa hiyo hatuna wataalamu wa aina hiyo ndipo tunaweza tukaruhusu watu wa kutoka sehemu nyingine kuja kutusaidia.

**MHE. LUCAL L. SELELII:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na mwelekeo wa Serikali katika hatua ya kuzibana Halmashauri wanapokuwa wanashughulikia Wakurugenzi ambao wamefanya vibaya katika mahesabu yao au kwa hesabu chafu au kutofanya vizuri kuandika mahesabu yao ya Halmashauri wanawanyima ruzuku za maendeleo katika Halmashauri zao. Sasa jambo hili naliona ni kuwaumiza wananchi ambao hawana hata kosa moja katika hayo mahesabu ambayo Wakurugenzi wanayafanya.

Je, hili nalo Waziri Mkuu huoni kwamba ni tatizo, ni kero kwa wananchi ambao Halmashauri zao zimenyimwa ruzuku?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Selelii kama imetokea hiyo ni dhahiri kabisa nje ya taratibu zetu. Lakini inawezekana kwa Mheshimiwa Selelii ana Halmashauri mahsusni ambayo hasa ameilenga. Yaani nataka nikuombe sana Mheshimiwa nikabidhi hilo jukumu la kushughulikia huyo Mkurugenzi ambaye amefanya haya ambaye unayoyaeleza ili tuweze kumchukulia hatua tu za kinidhamu. Kwa sababu nadhani ndiyo dawa kwa watu kama hawa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa na Halmashauri moja mahsusni, lakini juzi kwenye vyombo vy ya habari kama sijakosea ni gazeti la juzi tena la Serikali lilisema ni Halmashauri 14 zimenyimwa ruzuku ya Maendeleo.

Sina Halmashauri moja mahsusni nasema kiujumla? Mara nyingi inapotokea hivyo wananchi hawana kosa, mimi ningedhani *Kamati ya Fedha* na *Ukaguzi* ya Halmashauri husika zingeimarishwa zaidi kuliko kuwanyima wananchi hao fursa ya kimaendeleo, sina Halmashauri moja ambayo ni mahsusni lakini ni nyingi. (*Makofit*)

**WAZIRI MKUU:** Basi vizuri Mheshimiwa Naibu Spika, tutalipitia na watu wa TAMISEMI. Lakini labda niseme tu kwa sababu kwenye eneo hili viko vigezo vingi ambavyo vinatumika inawezekana kabisa si vyote ambavyo tunaweza tukamlundikia Mkurugenzi kwamba amesababisha kasoro hiyo ambayo imemnyima mwananchi kupata ruzuku ile ya Maendeleo. Kwa hiyo, itabidi tuangalie kila Halmashauri na masharti yaliyokiukwa yale yanayomhusu Mkurugenzi moja kwa moja sawa. Lakini inawezekana mengine ni ya mfumo amba pengine huwezi ukasema moja kwa moja kwamba ni ya Mkurugenzi.

Lakini tutalichukua tutalifanyia kazi Mungu bariki kabla hatujaondoka kama tunaweza kuwa tumefikia mahali pazuri tutakujulisha. Lakini nataka nitoe wito kwa Halmashauri chonde chonde, fedha hii inapelekwa kule kwa lengo la kusaidia wananchi ndiyo maana inaitwa ni fedha ya kusaidia maendeleo katika Halmashauri zetu. Ni fedha ambayo masharti yake si magumu ni masharti ya kawaida ambayo lengo lake ni kutaka Halmashauri zisimamie vizuri masuala ya fedha kwa mujibu wa sheria na taratibu. Mkurugenzi mwenye akili na timu yake hawezi kushindwa kwa sehemu kubwa kutojua sheria gani itumike na taratibu gani zitumike ili kumhakikishia kwamba fedha hizi hazikosi. Kwa hiyo, tutaliangalia tutaona ni hatua gani tuchukue kwa ajili ya Halmashauri hizo 14.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Sio swali la nyongeza ni swali lako.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Safi. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa unyenyekevu napenda kuuliza kwamba Jaji Mkuu wa Tanzania amewahi pia kuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar na amefanya kazi na Majaji wengi akina Jaji Mfalila na Jaji Mapigano.

Lakini pia Jaji Mkuu huyu amefanya kazi na Jaji Makani akiwemo baba yake Mheshimiwa Hamad Rashid na hakukutokezea tatizo lolote tokea wakati huo. Sasa hapa Bungeni wewe mwenyewe uliwahi kutueleza kwamba katika kipindi kama hiki mchakato wa Mahakama ya Kadhi unaendelea na karibuni utakamilika tuvute subira. Ni sababu gani za msingi zilizopelekea mpaka leo kushindwa Serikali kutekeleza suala hilo wakati ilikuwepo wakati wa ukoloni na halikuleta matatizo yoyote? (*Makofî*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili kundi la ndugu zangu hapa mara nyinyi huwa sio zuri sana. (*Makofî*)

Lakini hili analoliuliza Mheshimiwa Eng. Mohamed Mnyaa ni kweli unawenza ukalifanya dogo pengine ukaona kama katika mazingira yetu ni jepesi na mimi nachelea kusema hapana. Unajua kila jambo lazima izingatie mazingira halisi ya nchi inayohusika na ni vizuri ukawa mwangalifu sana katika kufanya maamuzi unapokuwa na jamii ambayo ina hisia za namna tofauti tofauti. Ndiyo maana katika jambo hili tumetaka kuwa waangalifu sana. Ndiyo maana Rais alielekeza kwamba vizuri hebu kutaneni na

wazee hao na wanazuoni pamoja na masheikh kaeni chini jaribuni kulizungumza hili muone tutafikia muafaka gani. (*Makofi*)

Sisi viongozi tunafikiria kwamba jambo hili kwa sababu ni jambo la imani ni vizuri kama zilivyo madhehebu mengine ya dini likajengewa misingi yake ndani ya dhehebu linalohusika. Ukifanya hivyo utakuwa umeondoa kabisa sababu za kulumbana na misuguano ambayo sio za lazima kati ya makundi ya madhehebu ya dini mbalimbali. Ndicho kilichotufanya tukaenda tukakaa chini na kujaribu kuona kwamba je wenzetu hili mnaona lina ugumu gani, kwa nini jambo hili lisiwe lenu. Serikali tuwasaidieni namna tu ya kuona ni namna gani muanzishe na tuwashauri juu ya maeneo ambayo tunaogopa msije mkayaingiza ili ibakie ni sehemu ya ibada yenu. (*Makofi*)

Tulikutana limeundwa jopo kubwa mchanganyiko wa masheikh na wasomi wazuri akiwemo Bwana El Maamry, tumekaa chini tumejaribu kulizungumza wametoa maoni yao na Serikali nasi tumelitafakari tukatengeneza maoni yetu. Yako maeneo tunakubaliana, yako maeneo ambayo bado tunatofautiana. Hatujakata tamaa, mambo makubwa bwana hayataki haraka. Ni vizuri ukaenda nayo taratibu mpaka mfike mahali muelewane.

Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba mazungumzo yanayoendelea baina ya wenzetu mchanganyiko kutoka dhehebu hili la Kiislamu na Serikali kwa sababu yana dhamira nzuri yatafika mahali pazuri na yataisha kwa namna ambayo kama Watanzania tutaendelea bado kujumuika pamoja, tutaendelea bado kujenga umoja na hatutafarakana kwa sababu zozote zile. Kubwa ni kuheshimu imani za kila upande wa dhehebu la dini. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu yako mazuri kwa kiasi fulani. Naamini kwamba katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM yako mambo ambayo hayakutekelezeka kikamilifu katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita kama vile mambo ya kuzalisha umeme vile vituo vya umeme Mchuchuma.

**NAIBU SPIKA:** Rudi kwenye swali lako.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Lakini pengine yanaweza yakaendelea kuwemo katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka huu. Je, hili la Mahakama ya Kadhi litaendelea kuwemo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Unataka uliingize kwenye Ilani ya *CUF*? (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Sasa Ilani ya Chama cha Mapinduzi wewe mtu wa CUF inakuhusu nini? (*Makofi/Kicheko*)

Sisi ndio tutakaoamua kulingana na mambo tunavyoyaona yanakwenda kama liendelee kuwekwa au kwa namna mambo yalivyo tuliondoe kwa sababu sasa limepata mwelekeo wa namna ya kupata suluhu. Hilo ni jukumu la Chama cha Mapinduzi (CCM) tuwaachie wenyewe wenyewe chama chao. Ndugu yangu usituingilie.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, bahati mbaya sana tumbaki.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote tunapenda tukushukuru sana kwa kujibu maswali magumu sana ya Katiba kwa ufasaha mkubwa sana nadhani wote tumeridhika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaomba tukupongeze sana kwa sababu siku zenyewe zinakaribia pengine muda unabakia mfupi sana kwa ajili ya kumwuliza Waziri Mkuu huyu kwa kipindi hiki. Sasa tunaendelea na shughuli za Bunge. (*Makofi*)

#### **MASWALI YA KAWAIDA**

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya Kawaida leo tunakwenda kwenye Ofisi ya Rais (Utawala Bora). Mheshimiwa Richard Ndassa atauliza swali hilo.

Na. 150

#### **Ukamilishaji wa Miradi ya TASAF I & II**

**MHE. RICHARD M. NDASA** aliuliza:-

Katika Awamu ya kwanza *TASAF ONE* imefanya vizuri kukamilisha miradi yake yote kwenye Wilaya arobaini (40) zilizopendekezwa na kuwafanya wafadhili kuja na Awamu nyingine ya *TASAF TWO* iliyokusudia kuwa na miradi nchi nzima lakini kutokana na miradi mingi iliyobuniwa na wananchi haikuwezekana kukamilika yote na kama imekamilika haitoi huduma katika ukamilifu wote:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo ili kuikamilisha miradi hiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo. Katika kutekeleza miradi inayoibuliwa na wananchi, kila Halmashauri ilitengewa mgao wa fedha zake za utekelezaji wa miradi hiyo ya jamii

na kushauriwa kutenga 10% ya mgao wake kwa ajili ya kugharamia ongezeko lolote la bei za vifaa vya ujenzi kama lingetokea ili miradi hiyo ya wananchi iweze kukamilisha.

Aidha, katika mapitio ya *TASAF* pamoja na Benki ya Dunia yaliyofanyika mwezi Machi mwaka huu, ilionekana wazi kuwa kutokamilika kwa miradi ya wananchi ni tatizo kwa miradi mdingi ya jamii. Miiongoni mwa sababu zilizosababisha hali hiyo ni:-

- (i) Upandaji wa bei za vifaa vya ujenzi kutokana na mfumuko wa bei.
- (ii) Wananchi kutochangia miradi hiyo kutokana na uhamasishaji mdogo.
- (iii) Wataalam wa Halmashauri kutokutoa ushauri wa kina wakati wa kubuni na utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Serikali yetu imefanya mazungumzo na Benki ya Dunia na Benki ya Dunia imetoe Dola milioni 35 kama fedha za nyongeza ambapo kati ya hizo Dola Milioni 20 zitumike kukamilisha miradi ambayo haijakamilika. Benki ya Dunia iltiliana sahihi na Tanzania hapa Dodoma mwezi Juni, 2010.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri mbalimbali zimekwishaleta maombi ya fedha *TASAF* kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo na tayari *TASAF* kwa kushirikiana na wataalam wa Halmashauri, wamefanya ukaguzi wa miradi yote.

Hivi sasa *TASAF* inapitia maombi hayo ili waweze kuzipatia Halmashauri fedha za kukamilisha miradi hiyo ili iweze kutoa huduma zilizokusudiwa kwa wananchi. Fedha zitaanza kutolewa mwezi Julai, 2010 na tumekubaliana na Benki ya Dunia kuwa fedha hizo zitatumika kumalizia miradi kati ya mwezi Julai mpaka Desemba 2010. (*Makofii*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja. Kwa sababu miradi katika Wilaya ya Kwimba ni mdingi zaidi ya kumi na fedha iliyotajwa kwamba ni shilingi Dola za Kimarekani milioni 20 ndizo zimetengwa.

Je, kwa sababu Wilaya ya Kwimba katika zahanati ya Mwampulu, Bujingwa, Nyambiti, Ilula, Shilembo na Nyamilama.

Vile vile shule ya Lyoma, Mwandum, Mwang' alaga na Mande jumla zinahitaji shilingi zaidi ya milioni 600, Serikali iko tayari kupeleka shilingi milioni 600 ili miradi hiyo ikamilike?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Serikali imejitahidi kuzungumza imezungumza na *World Bank* ili kutoa fedha za kuweza kuongeza na kumalizia miradi hiyo na fedha zilizotolewa ni dola milioni 35. Wilaya ya Kwimba ilipata katika kipindi hiki fedha bilioni 128.5. Walijiwekea pesa za ziada na ile *10 percent* milioni 108. Kati ya hizo kuna salio la milioni 97.1 ambalo bado halijatumika. Namwomba Mheshimiwa Diwani tukae ili tuangalie jinsi gani kwa sababu inaonekana bado zipo pesa za nyongeza ambazo hazijatumika. Inaelekea katika Halmashauri kuna matatizo ya *ku-account* hizi pesa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu Mbunge pia ni Diwani kwa hiyo na Madiwani ndiyo wanasubiri. Mheshimiwa Ndugai.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa Majibu mazuri, amezungumzia habari ya miradi ya *TASAF II* ambayo haijakamilika na mpango wa kuikamilisha jambo ambalo tunaishukuru sana Serikali kwa sababu miradi mingi kwa kweli ya *TASAF II* bado haijakimilika na amesema kwamba dola milioni 35 tayari Serikali imeshaingia mkataba na Benki ya Dunia kwa ajili ya kumalizia majengo hayo.

Mheshimiwa Waziri hajaongelea chochote kuhusu *TASAF III* baada ya *TASAF II* kwisha. Sasa *way forward* je, kuna *TASAF III* au nini?

**NAIBU SPIKA:** Maneno yote hayo kumbe hilo tu. Mheshimiwa Waziri majibu. Je, *TASAF III* ipo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utekelezaji mzuri wa *TASAF I* na *TASAF II* Serikali pia inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia ili kuwepo na *TASAF III*. Lakini uelekeo uliopo ni kwamba *World Bank* wamefurahishwa sana na tuna matumaini makubwa kwamba tutapata pesa kwa ajili ya *TASAF III*.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na kazi nzuri sana ambayo imetekelvezwa na miradi ya *TASAF* nchi nzima.

Je, Serikali sasa itaweka mkakati gani wa kusimamia, kwa sababu Kamati ya LAAC kila mahali ilipopita ilikuta miradi mizuri sana lakini tatizo lingine la kutokamilika miradi au ramani hazikufuatwa au kuna kutokusimamiwa miradi hiyo au hata

udanganyifu kama ilivyotokea kwenye Zahanati ya Ndagodi kule Mafia ambapo Taarifa zinapelekwa mbili tofauuti?

Moja kwa Madiwani na nyingine kwa TASAF. Kwa hiyo, hata *TASAF* hawajui ni kitu gani ambacho hatimaye kimefanyika nchini. Serikali imefanya mkakati gani wa kusimamia ili fedha hizi kweli zifanye kazi na zikamilishe miradi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi *TASAF* inajitahidi. Ina waratibu wa *TASAF* ambao wanashirikiana na viongozi ambao wamewaelimisha katika Halmashauri. *TASAF* ni mradi kwa hiyo hauwezi kuwa na watu wengi sana, mpaka sasa hivi tunajaribu kuifanya *TASAF* iwe taasisi.

Lakini katika hali yake ya ki-*TASAF* tunatumia zaidi Halmashauri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Slaa mnapokwenda kuzikagua Halmashauri mhimize hili kwamba miradi ya *TASAF* washirikiane vizuri na waratibu ili tupate matokeo ambayo yametegemewa katika jamii.

Na. 151

### **Ukiukwaji wa Sheria ya Maadili**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Viongozi wakubwa wa nchi wanakiuka Sheria ya Maadili:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, iko haja sasa ya kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge juu ya Sheria ya Maadili?

(b) Kabla ya kutoa mafunzo hayo. Je, Serikali haioni kuwa, ni wakati muafaka sasa wa kumpatia kila Mbunge nakala ya Sheria hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS , UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbni, Mbunge wa Chake Chake, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya Mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 5 ya Mwaka 2001, inamtaka kila Kiongozi wa Umma aliyetajwa katika Sheria hiyo kuwa mwadilifu.

Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungno wa Tanzania ni mionganoni mwa Viongozi wa Umma wanaohusika na Sheria hiyo. Kwa maana hiyo,

Waheshimiwa Wabunge ni sehemu tu ya Viongozi wapatao 7600 wanaowajibika na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Viongozi wote wa Umma wamekuwa wakipewa msisitizo wa umuhimu wa kuwa waadilifu kwa mujibu wa matakwa ya Sheria hiyo ambayo ilitungwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chake Chake, swalii lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Waheshimiwa Wabunge kupewa mafunzo kuhusu Sheria ya Maadili ni jambo jema ila pia Viongozi wote nao wanatakiwa kulelewa vyema na kuitekeleza Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, kutokana na ukosefu wa fedha, imekuwa vigumu kutoa mafunzo kwa viongozi wote. Hata hivyo jitihada za kutoa mafunzo kwa baadhi ya viongozi wa umma walijotajwa na Sheria hiyo zimefanyika. Kwa mfano, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambacho ndicho chombo kinachosimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imetoe mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wengine wa ngazi ya Halmashauri wapatao 400 katika Halmashauri zipatazo 13 nchini kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 na 2008/2009.

Aidha, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitoa mada kuhusu Sheria ya Maadili wakati wa Semina ya mafunzo kwa Wabunge wapya mwezi Januari, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kuwafikia viongozi wengi iwezekanavyo na kutoa mafunzo ili waielewe vyema Sheria hiyo na waitekeleze. Ni mategemeo ya kila mwananchi kwamb Waheshimiwa Wabunge, kwa vile ndiyo wanaotunga Sheria mbalimbali nchini ikiwemo Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, wawe na uelewa mpana zaidi kuhusu sheria hizo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina utaratibu wa kutoa nakala za Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Viongozi wanapotumiwa fomu za Tamko la Mali na Madeni kwa mara ya kwanza. Aidha, endapo kiongozi atahaitaji nakala zaidi, huwa anafanya mawasiliano na Ofisi husika. Nakala hizi zinapatikana katika Ofisi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu, Dar es Salaam na katika ofisi zote sita za kanda ambazo zipo katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Tabora, Mbeya na Mtwara.

Kwa vile sheria hii inatarajiwa kufanyiwa marekebisho na Bunge hili Tukufu, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itahakikisha kuwa Waheshimiwa Wabunge wanapatiwa tena nakala za Sheria hiyo baada ya kurekebishwa. (*Makofî*)

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swalii langu la kwanza ni kwamba viongozi wanapoingia madarakani huwa tunajaza fomu zile lakini

wakati wa kutoka kama hivi saa sisi tunatoka, Waziri haoni haja ya kutulazimisha kujaza fomu za mali gani tunazo na madeni kiasi gani tunayo?

Swali langu la pili ni kwamba katika Kamati, tunapouliza ni viongozi gani hawajazi fomu za maadili au hawarudishi huwa tunaambiwa ni madiwani. Je, Waziri haoni haja sasa ya kuharakisha kuwa madiwani wote nchini wakapate mafunzo haya kabla hata ya Wabunge. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Maghimbi umefanya vizuri sana kutuulizia swali hili. Naamin kila Mbunge ameshapata fomu kujaza kabla ya tarehe 16 Julai, 2010. Basi mtaenda kwa Katibu wa Bunge mkachukue fomu na mnatakiwa kujaza, kama hunazo jitahidi uwe nazo inawezekana jina lako lisiende mbele ya safari.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunisaidia kujibu swali la kwanza. Naomba niongezee hapo kwa kumwambia, unapozungumzia fomu za mwisho fomu ya mwisho ambayo unajaza ni hii fomu unayojaza mwaka huu baada ya hapo unapokuwa si kiongozi tena na kama unaendelea uongozi utapata fomu nyingine. Kwa hiyo, si kweli kwamba mwisho hatujazi tunakuwa tumejaza ambapo mwezi wa kumi inatakiwa tuwe tumeipeleka.

Kwa madiwani kutokujaza. Ni kweli tumepata ugumu kidogo wa madiwani kutokujaza hizi fomu kwa wakati na kama nilivyojibu kwenye jibu la nyongeza tumefanya jitihada kubwa kuwaelimisha madiwani na viongozi wa Halmashauri mbalimbali kuhusu umuhimu wa kujaza fomu hizi na mara nyingi madiwani wamekuwa wakitoa sababu mbalimbali za kutokujaza lakini bado jitihada zinafanyika kuhakikisha madiwani wanajaza pamoja na kwamba wanakuwa na sababu mbalimbali ambazo sisi Sekretarieti ya Maadili imeweza kuwaelimisha.

**MHE. JOHN S. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa inaonekana wote humu ndani hatuna hizo fomu. Je, anaweza kutuhakikisha kwamba fomu hizo kabla ya kesho wote tumezipata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malecela najibu mimi, ofisi yetu ya Bunge inazo hizo fomu. Kwa hiyo, naomba kila Mbunge akazichukue na barua nimewaandikiensi kwamba mrudishe kabla ya tarehe 16 Julai, 2010 Bunge litakapovunjwa. (*Makofi*)

Na. 152

#### **Ukingaji Maji ya Mvua kwa Matumizi ya Binadamu**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Sasa hivi Watanzania wengi hasa wa vijijini hawapati maji kwa matumizi yao ya kawaida na wakati wa masika hasa kwenye Mikoa yapo makorongo na mito ambayo huja maji ambayo huishia kwenye maeneo ambayo hayana watu:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba ni busara kukinga maji hayo yasipotee ili yatumike kwa manufaa ya watu wetu?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa ni vema baada ya kuyakinga, maji hayo yakawa mengi ndipo sasa ifanye utaratibu wa kuyasambaza kwenye maeneo yote yanayohitaji maji hayo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikwisha kuchukua hatua ya kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua na ujenzi wa Mabwawa. Kuanzia mwaka 2006/2007 mpaka 2009/2010, Serikali imekuwa na mpango wa kukinga maji kwa kutumia teknolojia ya Mabwawa. Katika kipindi hicho Serikali imeratibu ujenzi wa mabwawa katika Wilaya 13.

Aidha kuanzia mwaka 2002/2003 mpaka 2004/2005 Serikali imekuwa ikitoa mafunzo ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba. Wilaya zilizofaidika na mafunzoo haya ni Wilaya ya Iramba, Manyoni, Wilaya ya Sikonge, Wilaya ya Chunya na Wilaya ya Magu.

Kwa sasa utaratibu wa ujenzi wa mabwawa na uvunaji maji ya mvua umehamishiwa katika Halmashauri za Wilaya ambazo zitashirikiana na wataalam

washauri waliwaajiri chini ya programu ndogo ya usambazaji wa maji na usafi wa mazingira mijini katika programu ya Maendeleo ya sekta ya maji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesambaza maji yaliyokusanywa kwenye mabwawa katika miji ya Muhonozi, Wilayani Meatu na Maswa katika Wilaya ya Maswa.

Katika Wilaya ya Iramba mabwawa yaliyopendekezwa ni Gumangu na Ujungu ambayo yanaweza kutumiwa kusambaza maji katika eneo husika. Kwa upande wa uvunaji wa mvua kuitia mapaa ya nyumba maji huhifadhiwa kwenye matanki kabla ya kutumika kulingana na mahitaji. (*Makofî*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Jimbo la Iramba Mashariki sasa ni Wilaya kamili na kwa kuwa tuna mabonde mengi ya Kitumbili, Iguguno, Iyende Msio na kadhalika. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kupanga mipango kamili kwa ajili ya Wilaya mpya Mkalama juu ya umwagiliaji?

Swali la pili, kwa kuwa huko nyuma tulikuwa na skimu mbili za kijiji cha Mwangeza na Kijiji cha Msingi lakini skimu hizi zikaharibiwa na mafuriko miaka mitatu iliyopita na kwa kuwa Serikali iliahidi kutoa fedha na mpaka sasa hizo fedha hazijapatikana. Je, Serikali inasemaje juu ya kufufua skimu hizi ambazo zilishaanza kuwanufaisha wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana wananchi wa Mkalama ambao wanatoka katika Jimbo la Mheshimiwa Mgana Msindai, kwa kupata Wilaya mpya. Nataka niseme tu kwamba mimi sitapata taabu sana kujibu swali hili kwa sababu tukimsikiliza Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji na Waziri wa Kilimo kila wakati wamesisitiza hapa kuhusu kilimo ambacho kinahitaji matumizi ya kilimo cha umwagiliaji.

Sasa kama tutawaambia watu wa Mkalama waendelee kutumia mvua hicho kilimo tulishasema ni duni na cha kikoloni mamboleo. Mimi sitapata taabu kwenda kumwambia Waziri kwamba Mkalama ambayo sasa ni Wilaya mpya inaomba ipelekewe miradi hii ya umwagilianii.

Kuhusu upya wa Wilaya hii, kwa kawaida katika kipindi cha mpito Wilaya ile mama ambayo iko pale ndiyo inayofanya kazi ya kusimamia ile miradi mpaka Bajeti itakapokuja kwa sura hiyo ambayo tunaizungumzia hapa.

Naibu Spika, namba mbili miradi ambayo imeshatengenezwa lakini imeharibiwa. Kwa kawaida maeneo ya mabonde na hii Wilaya anayoizungumzia Iramba nilifanya ziara kwa hiyo nafahamu Mheshimiwa Mbunge anachokizungumzia.

Ninataka kusema kwamba ziko fedha zinazotokana na *PADEP* na zile ambazo zinaingia katika eneo hili la *ASPD* hizi hela zinaweza zikatumika kwa kazi hiyo ya kuhakikisha kwamba wanakarabati hayo maeneo.

Lakini nimalizie kwa kusema kwamba tunampongeza sana Mheshimiwa Msindai kwa msukumo mkubwa ambao amekuwa anatoa katika eneo hili la maji ya umwagiliaji. Amefanya kazi nzuri na nafikiri wananchi wanajua kwamba kazi hii ni nzuri na sisi tutakuwa tayari kushirikiana nae. (*Makofit*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa maji haya yanayoporomoka katika maporomoko mbalimbali yanaingia katika maeneo ya asilia ambayo yanatunza maji lakini yanatunza maji kwa muda mfupi sana.

Je, Wizara haioni umuhimu wa kuyaendeleza yale maeneo ambayo ni asilia badala ya kutafuta eneo jipya kwa ghamra kubwa ili maeneo yale yakaendela kutumika kama ilivyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, zile sifa ambazo nilimmiminia hapa Mheshimiwa Mgana Msindai zinamhusu pia na Mheshimiwa Killimbah kwa sababu wote wanatoka katika Wilaya hiyo hiyo. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi kabisa.

Kwa hiyo, ushauri huu ni mzuri na jana nilikuwa nalizungumzia jambo hili na wataalam. Kwa hiyo, tunalipokea na tutampelekea Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Na. 153

#### **Madai ya Wakulima Katika Vyama vya Ushirika**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuwalipa Wakulima waliokopwa na Vyama vya Ushirika vya Wilaya au Mikoa na imeanza kutekeleza azma hiyo:-

Je, kwa nini Serikali hajjawalipa Wakulima waliokopwa na Chama cha Ushirika Wilayani Mbinga (MBICU) ambacho kilifilisiwa tangu miaka ya 90?

## **NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne, chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ipo makini katika kutekeleza ahadi zake na za awamu zilizotangulia na hivyo ndivyo ilivyofanya kwa Wakulima waliokuwa wanakidai Chama Kikuu Wilayani Mbinga cha *Mbinga Farmers Cooperative Union Limited (MBIFACU)*. Madai ya Wakulima hao ya jumla ya shilingi milioni 106.6, yalilipwa Novemba 2008. Ulipaji wa madai hayo, ulifuatia kukamilishwa kwa Taarifa ya Mchakato na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2006. Mchakato huo haukuhusisha madai/madeni yaliyokuwa chini ya utaratibu wa ufilisi wa Vyama vya Ushirika kama *Mbinga Cooperative Union (MBICU)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kufuatia Wakulima wenzao waliokuwa chini ya *MBIFACU* kulipwa madai yao, Wakulima waliokuwa wanaidai *MBICU* chini ya ufilisi, nao wamefikisha madai yao Serikalini ya jumla ya shilingi milioni 419 mwezi Februari, 2010. Madai hayo ya Wakulima yatalipwa kwa kufuata utaratibu wa ufilisi.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwanza, ninataka niishukuru Serikali kwa malipo hayo ambayo walilipwa *MBIFACU* ya shilingi milioni 106.6 na pondezi zangu za kipekee, napenda kumpelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipoitembelea Wilaya Mbinga Kijiji cha Utiri, alipokea malalamiko ya Wanaushirika ambayo ni sehemu ya *MBICU*, waliokuwa wanadai shilingi milioni nne na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Waziri Mkuu, wamelipa hilo deni. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa nini Serikali katika mchakato wake wa Mchakato na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukagua hayo madeni muhimu na kuweza kuyahakiki; madeni ya *MBICU* hayaku hakikiwa na ambayo yalikuwa ni ya muda mrefu?

(b) Kwa kuwa uamuzi wa kuweka ufilisi au kutofilisi ulikuwa ni wa Serikali; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu iliamua kulipa haya madeni ya Wakulima na Serikali ya Awamu ya Nne imeamua kutekeleza; na kwa kuwa Wakulima wa Chama cha Ushirika cha Musoma wako chini ya mafupi; na kwa kuwa *MBICU* wamekwishalipwa na Wakulima wa Chama cha Utiri kule Mbinga amba pia ni sehemu hii ya *MBICU* wamekwishalipwa; na kwa kuwa barua ya Waziri Mkuu ...

**NAIBU SPIKA:** Jamani maswali yakiwa mafupi yanakuwa mazuri.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa ipo barua ya Waziri Mkuu inayolekeza Wizara ya Kilimo ilipe deni hilo: Je, Serikali

haiwezi kuamua sasa kumpeleka Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwenda kuhakiki hayo madeni ili iweze kuyalipa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kayombo, kwa jitihada zake za kusaidia sana Wakulima wake hasa wa Zao la Kahawa. Mambo mengi kule Mbinga yamefanyika kuhusiana na Zao la Kahawa kutokana na juhudi za Mheshimiwa Mbunge pamoa na Serikali. Swali lake la kwanza kuhusu Chama cha *MBICU* kuhakikiwa ni kwamba, taratibu za ufilisi zilishaanza mwishoni mwa miaka ya 1990, lakini akawepo mfanyakishara mmoja ambaye anakidai Chama hiki takriban shilingi milioni 100, ambaye anaitwa *GOLDEN IMPEX*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *GOLDEN IMPEX* akakipeleka Chama hiki Mahakamani; kwa hiyo, taratibu zote za ufilisi na taratibu za uhaki zilisimama mpaka hivi ninavyozungumza mwezi wa nane ndipo huyu mfanyakishara ameshakubaliana kwamba wakutane na mfilisi ili waweze kuliondoa hili suala Mahakamani ili Chama hiki kiweze kutafuta fedha na kuwalipa. Suala kuhusu Chama hiki cha Mara kilikuwa na mali zenyet thamani ya shilingi milioni 229 ambazo wakulima wale walishalipwa kutokana na fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali ilichukua mali ambazo zina thamani ya shilingi bilioni 1.5, ambazo zote hizo zilikiwezesha Chama hiki kuwalipa Wakulima wao. Sasa kuhusiana na vyama vingine, niseme kuwa vyama ambavyo viko kwenye utaratibu wa mufilisi ni lazima madeni yao yaorodheshwe, wanaodai wafahamike na wanaodaiwa wafahamike kusudi ufilisi unapokamilika, madeni yalipwe kutokana na vyama vilivyoko kwenye mufilisi.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ningeomba nimuuilize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa msimu wa ununuzi wa kahawa ambayo imeiva umeshaanza kule Mkoani Kilimanjaro; na kwa kuwa Wabunge wa Kilimanjaro tunaotoka katika maeneo yanayolima kahawa tumeshaiomba Serikali ikisaidie Chama Kikuu cha Ushirika Mkoani Kilimanjaro (*KNCU*) ili waweze kulipwa fidia kutokana na mdodoro wa uchumi na bado malipo hayo hayajafanyika. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kulisukuma hili suala kwa haraka zaidi ili Chama chetu cha *KNCU* kiweze kufanya shughuli zake zinazotakiwa za kununua mazao hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Vyama hivi vya Ushirika kutoka kwenye maeneo ya kahawa walipeleka madai yao. Wengine walipeleka wakati *deadline* ilikuwa imeshapita, kwa maana hiyo wale waliofuata taratibu watapewa fedha za kusaidia kutokana na mdororo wa uchumi lakini ambao walichelewa na wakafikisha baada ya *deadline* kupita, kwa kweli hao hawatapata.

### **Vijiji vya Mninga na Kihanga Kucheleweshewa Umeme**

#### **MHE. BENITO W. MALANGALILA aliuliza:-**

Kwa kuwa ni miaka zaidi ya kumi na nne sasa umeme umepita juu ya nyumba za Wananchi wa Kijiji cha Mninga na ni miaka zaidi ya sita umeme juu ya Kijiji cha Kihanga; na kwa kuwa tathmini za gharama za kuingiza umeme katika vijiji hivyo viwili haifiki hata shilingi 150:-

(a) Je, ni sababu gani za ukweli zinazosababisha Wananchi hao wasipatiwe umeme kwa muda wote huo?

(b) Je, Serikali inaelewa kuwa Wananchi hao ndiyo waliota ardhii yao kwa mwekezaji anayezalisha nguzo za kusambazia umeme sehemu nyingi za ndani na nje ya nchi?

#### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, katika usafirishaji wa umeme kutoka kwenye vyanzo vya uzalishaji kwenda kwenye maeneo ya usambazaji, hutokea kwamba nyaya za umeme zikapita karibu na maeneo ya makazi ya watu vijijini na umeme huo usishushwe. Hatua ya kushusha umeme kutoka kwenye usafirishaji wa KV 33 au zaidi na kuupoza ili uweze kutumika na Wananchi, una gharama kwa kuwa hatua hizi zinaambatana na uwekezaji wa ujenzi wa ziada wa *substation, transfroma*, nguzo na nyaya stahili. Hivyo, kabla ya kuingia kwenye gharama hizi, hufanywa tathmini ya awali ya uhalali wa kiuchumi, kibashara na kijamii (*Economic, Commercial and Social Viability*). Tathmini hii huzingatia vigezo mbalimbali ili kuongoza ufanyakaji wa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme (TANESCO), katika mwaka huu wa fedha imepanga kutekeleza Mradi wa Kufikisha Umeme katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya Mninga na Kihanga. Kazi ya kusambaza nguzo imekamilika, ambapo nguzo 80 za njia ndogo ya umeme katika vijiji vyote viwili zimepatikana na uvutaji wa nyaya za njia ndogo utafanyika baada ya kufunga transfroma hizo. Aidha, sababu zilizochelewesha utekelezaji wa miradi hii ilikuwa ni ukosefu wa fedha. Kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi milioni 110,

ambapo shilingi milioni 60 ni kwa ajili ya Kijiji cha Mninga na shilingi milioni 50 ni kwa ajili ya Kijiji cha Kihanga.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Wananchi wa Vijiji hivi katika kusaidia harakati za kuleta maendeleo nchini. Hivyo basi, hatua ya kutoa eneo la ardhi hiyo ambayo inasaidia na inaongeza upatikanaji wa nguzo za kusambaza umeme sehemu nyingi hapa nchini ni hatua ya kutambua umuhimu wa ushiriki wa Wananchi katika shughuli za maendeleo katika ngazi zote na inabidi wapongezwe. Aidha, naomba kwa makusudi kabisa, nitambue juhudzi za Mheshimiwa Benito William Malangalila, kwa kufuutilia kwa karibu sana masuala ya huduma ya umeme Wilaya ya Mufindi na kwa mud a mrefu amekuwa analifuutilia suala hili la Vijiji vya Mninga na Kihanga. Ninaamini kabisa, hatua hizi zinazochukuliwa, zinatupeleka katika kumaliza tatizo hili na ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mlangalila kwa ushirikiano wake katika suala hili.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nililetewa barua ilioandikwa na Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini kwamba, hivi vijiji viwili vitakuwa vimekamilishiwa umeme wake tarehe 31 Desemba, 2009 na barua hiyo haijatekelezwa hadi sasa; je, ni lini umeme huo utakamilika?

Pili, kwa kuwa hivi juzi tu umeme umepita pale Kijiji cha Kasanga lakini haukuteremka kijijini pale; ni lini utateremshwa pale Kasanga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi nimesema kwamba, tayari ile kazi imeshaanza kufanywa, tayari nguzo zimekwishakwenda pale, nyaya zinakwenda na transfoma zinakwenda na zimeshafika. Kwa hiyo, ninaamini kwamba, pamoja na ucheleweshaji ambao sababu zake kimsingi zinaeleweka, tunakuwa na ucheleweshaji kwa vifaa lakini pia na upatikanaji wa fedha. Suala hili linakwenda vizuri na ninaamini kwamba, kama unataka tarehe hasa ya *implementation* lini wanatarajiwa wamalize, basi baadae tuwasiliane na Meneja wa Mkoa wa Iringa anipatie tarehe maalumu ili nikupatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili la pili la Kijiji cha Kasanga, tayari kuna umeme pale kwenye Shamba la Chai la Kisigo nadhani na tumeshaongea na Mheshimiwa Mbunge, tunaamini tutaliwasilisha pia kwa Meneja wa Mkoa ili atufanyie tathmini ajue. Kutoka pale *Kisigo Tea Factory* kwenda Kasanga ambapo siyo mbali na pana hospitali na shule, ninaamini kabisa kuwa hilo nalo linawezekana tukalifanyia kazi na nitampatia majibu Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tumekopa dakika tano na maswali yamekwisha kwa hiyo tunaendelea. Naomba niwatambue wageni tulionao katika Ukumbi huu, nitawatambua baadhi waliopo wengine hawapo.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Viwanda na Biashara, ambao wapo katika makundi mbalimbali

kama ifuatavyo: Kwanza ni Watendaji mbalimbali wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bi Joyce Mapunjo; alah! Mimi nilidhani kwaya kumbe! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Dr. Shabani Mwinjaka, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, halafu wapo Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Wizara kama vile SIDO, IPZ, BRELA na kadhalika; wasimame hapo walipo wote walioko katika makundi hayo. Wizara ya Viwanda na Biashara mmeleta mpya safari hii; asanteni sana.

Wapo wawakilishi kutoka Chama cha Wenye Viwanda, Wafanyabiashara na Kilimo (TCCIA), ambao wanaongozwa na Ndugu Mutalemwa Lushaju. Ndugu Mutalemwa Lushaju uko wapi na Wanachama wako; wakisimama tutafurahi.

Mheshimiwa Waziri pia ana wageni wake binafsi ambao ni watoto wake; naomba watoto wake wasimame. Yupo Esther Mathias na Innocent Matutaye; asanteni sana, ninyi hamkuva sare haya.

Wapo Waheshimiwa Madiwani kutoka Hanang, ambao wanaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Michael Bayo. Mheshimiwa Michael Bayo na Waheshimiwa Madiwani wako wapi? Ahsanteni sana Waheshimiwa Madiwani, tunawatachia heri muweze kupita vizuri kwenye kinyag'anyiro huku mkimsaidia Mheshimiwa Waziri katika mambo ya huko.

Tunao Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Hanang pamoja na wapiga kura wake 52; sijui wako wapi nao wasimame huko waliko; yaani Hanang yote leo imehamia hapa, nashukuru sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni Wahadhiri, Viongozi wa Serikali ya Wanafunzi na Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*), wakiongozwa na Ndugu Hongoa. Ndugu Hongoa yuko wapi na wale wanafunzi wasimame walipo; asante sana.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambaye ni Afisa Uhamiaji Mstaafu, Ndugu Patrick Mwarabu. Wapo Wanafunzi wawili wa Shule ya Msingi Bahi; Habel Patrick na Steven Patrick; wasimame aah wadogo kabisa. Pia, kuna Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jitegeree; Deoglas Mushi na Winfrida Mushi; ahsante sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa William Shellukindo, ambao ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Mamba na Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Bumbuli; Mheshimiwa Ndege; Mheshimiwa Diwani uko wapi? Vilevile yupo ndugu yake anaitwa Samwel Shemgaa. Ahsanteni, karibuni sana.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, ambao ni Mhamasishaji Mkuu wa CHADEMA, Ndugu Farida Ahmed. Yuko wapi huyu Mhamasishaji Mkuu? Kumbe mdada, haya ahsante sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, ambao ni Caroline Fidels Owenya na Yohane Fidelis Owenya. Hawa ninadhani ni watoto wake; karibuni sana kuja kumwona mama anafanya vitu vtake huku Bungeni.

Yupo Ndugu Chacha Daniel Okong'o, Mwenyekiti CHADEMA Wilaya ya Nyamagana Mwanza. Pia ni Mgombea Ubunge Jimbo la Nyamagana Mwanza. Ametangaza nia. Yuko wapi huyu? Kumbe Nyamagana yuko huyu jamaa; ahsante sana Bwana Chacha.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Alhaji Dr. Juma Ngasongwa, ambao ni Wakulima na Wanafunzi sita wakiongozwa na Ndugu Michael Pawa; na wengine wote wasimame tunashukuru sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, ambao ni Katibu wa CUF Wilaya ya Geita, Bwana Severine Malugu Magese; yuko wapi huyu aha! Ahsante sana. Pia yupo Mjumbe wa Mkutano Mkuu CUF Taifa na Mgombesa Mtarajiwu wa Ubunge, hajasema Bunge gani; Bwana Peter Michael Marebo. Bila shaka ni Geita hukohuko; karibuni sana, tunawataki heri huko.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Devota Likokola, ambao naomba wote wasimame wakiongozwa na Mwenyekiti UWT Mkoa wa Ruvuma, Ndugu Kuruthumu Mhagama; Mwenyekiti wa UWT Songea Manispaa, Agnes Hinju; Mwenyekiti wa UWT Songea Vijijini, Maria Ngonyani; Mwenyekiti wa Namtumbo, Asumta Ndauka; Mwenyekiti wa UWT Tunduru, Fatuma Kaisi; Mwenyekiti wa UWT Mbanga, Luciana Ndunguru; na Katibu wa Msafara, Ana Ndumbaro. UWT tunawashukuru sana kwa umoja wenu wakati Mbunge wa Peramiho Jenista Mhagama alipofiya na mume wake, tuliwaona wote mkiwa mmeshiriki sana na tunafurahia sana umoja wenu huo.

Wapo akina mama 50 kutoka Kanisa la *Assemblies of God Tanzania*, wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Wako wapi hao akina mama 50? Ninaamini watakuwa wamekosa nafasi watakuwa *Basement*, lakini jana walikuwepo.

Wapo wanafunzi 17 na walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Mugabe iliyoko Sinza Dar es Salaam; wako wapi? Ahsante sana, tunafurahi kuwaoneni. Mimi ni jirani yenu kule Dar es Salaam.

Tuna Wanafunzi kutoka Bunge la Wanafunzi la Chuo cha Biashara Mwanza (*CBE*), ambao ni Spika wa Bunge, Mariana Robert. Mnaona Spika huyo mambo hayo! Yupo na Naibu Spika wake, Robert Chakudika. Aah wewe ndiyo *counterpart* wangu. Halafu yupo Katibu wa Bunge, Anna Messiah Mrema. Ahsante sana na *gender* imezingatiwa kwa uhakika.

Waheshimiwa Wabunge, ninao Wageni wa Mheshimiwa Dokta Charles Mlingwa, ambao ni Mama Makune na wanae, anatoka Shinyanga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba niwatangazie

Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na Kamati ya Maendeleo ya Miundombinu kwamba, kutakuwa na kikao cha Kamati zote mbili leo Alhamisi tarehe 1, kuanzia saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kuwa, kesho tarehe 2, saa moja asubuhi, kutakuwa na usafiri hapa Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuondoka kuelekea Dar es Salaam kushiriki kwenye ufunguzi wa Maonesho ya 34 ya Biashara ya Kimataifa. Kwa hiyo, mnakutana hapa Bungeni kesho saa moja, kwa ajili ya kusafiri kwenda Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, jana niliwatangazia wale Wabunge wa Mtwara na Lindi kwamba, kesho tarehe 2, kungekuwa na ndege saa moja asubuhi; Mwenyekiti wenu Mheshimiwa Mrope anasema, mnatakiwa muwepo sasa saa mbili na nusu badala ya saa moja kwa ajili ya uzinduzi wa umeme wa gesi pamoja na ile meli inayochimba mafuta.

Waheshimiwa Wabunge, tuna tangazo lingine ambalo nadhani siku mbili zilizopita tulikuwa tumeelezwa na Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba, tulipata ajali ya Ndege ya Kijeshi ya Mafunzo na tukapoteza marubani wetu wawili. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane Dodoma leo katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma, saa sita na nusu ili kupokea miili ya Marehemu Maafisa hawa. Miili ya marehemu itaingia katika uwanja wa ndenge wa Dodoma saa sita na nusu. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, mnaombwa mkutane ili kutoa heshima zenu na wengine ambao wataweza kuwepo kule itakuwa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa matangazo, tunaendelea na hatua nydingine ya kazi.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyonayo kwangu, kwa kuendelea kunikabidhi madaraka ya kuongoza na kusimamia majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Kiuchumi wa Dunia kuhusu

Afrika (*World Economic Forum for Africa*), uliofanyika tarehe 5 hadi 7 Mei, 2010 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo umewezesha kujitokeza kwa fursa nyingi za uwekezaji wa kiuchumi na kitalii na ajenda ya Kilimo Kwanza kutangazwa kwa wawekezaji Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa jitihada zake kubwa alizofanya katika kutafuta wawekezaji na kushawishi taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kuongeza rasilimali zao na hivyo kuongeza uzalishaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi wake wa kuteua Sekta ya Viwanda kuwa moja ya ajenda yake ya kwanza katika muhula wa pili wa uongozi wake, ambao ninahakika ataupata. Hii inatokana na kutambua kuwa, historia ya maendeleo inaonesha hakuna nchi iliyoendelea bila ya Sekta ya Viwanda kupewa umuhimu unaostahili. Namtakia Mheshimiwa Rais, ushindi wa kishindo na hasa leo anaporudisha fomu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushiriki wake mkubwa katika kuhamasisha maendeleo endelevu katika Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa kuzingatia usafi na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo aliyotoa kwa ajili ya kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, nawashukuru Mawaziri wenzangu, kwa ushirikiano wao mzuri ambao umerahisisha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu ni muhimu sana kwa nchi yetu, kwani Utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, unahitimisha muhula wake wa kwanza. Imani yangu ni kuwa, Chama cha Mapinduzi, kitapewa fursa ya kuongoza nchi kwa muhula mwingine kutokana na sera nzuri ambazo zimevezesha ukuaji wa uchumi na kuwaletaa wananchi maendeleo na maisha bora. Aidha, tunaiombea nchi yetu kufanya Uchaguzi Mkuu kwa amani, utulivu na haki na ambao utatoa fursa zaidi kwa CCM kuwezesha ukuaji wa kasi wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko kama mhimili muhimu wa ukuaji endelevu wa uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii pia, kuwashukuru wadau wote, hususan asasi za sekta binafsi zikiwemo TNBC, TPSF, TCCIA, CTI, ACT, VIBINDO, TWCC na LAT, kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko, ambayo Wizara yangu inazisimamia. Aidha, ninawashukuru Wananchi kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote nilichoongoza Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko. Naomba waendelee na ushirikiano huo ili tuweze kuendeleza Sekta hizo ambazo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, ningependa kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Hanang, kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote nilichokuwa mwakilishi wao hapa Bungeni na endapo watanipa ridhaa nyingine kupitia chama changu, ninaahidi kuwakilisha ipasavyo ili wafikie matarajio yao. Vile vile

nawashukuru sana kwa kuja na kwa kujitolea kuja kushuhudia hotuba yangu inapotolewa leo. Aidha, namshukuru mume wangu, Prof. Joseph Nagu, pamoja na watoto wetu; Tumaini, Neema, Deo na ndugu wengine, licha ya mimi kuwa na muda mdogo kwao, kwa ushirikiano na upendo ambao wamenipa na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu inavyopaswa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Wabunge wapya walioteuliwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Wabunge hao ni Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene. Uteuzi wao ni ishara ya imani aliyonayo Mheshimiwa Rais kwao. Aidha, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kifo cha Mheshimiwa Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mbunge wa miaka mingi na mmoja wa Waasisi wa Taifa letu. Mheshimiwa Kawawa, hata baada ya kustaafu, aliendelea kuwa mhimili mkubwa wa Taifa letu na tegemeo kubwa la uongozi wa Taifa letu. Vilevile, nawapa pole familia yake, jamaa na marafiki kwa ujumla. Pia, tulipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa. Tunawapa pole Wananchi wa jimbo hilo, ndugu, jamaa na marafiki. Tunaomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahala pema peponi - Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, naishukuru Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi (CCM), akisaidiwa na Makamu wake, Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Jimbo la Mkinga (CCM), kwa mchango na ushauri wao wenye uwazi na ubunifu katika kujadili Makadirio ya Wizara yangu. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hoja na michango ya Kamati imezingatiwa katika hotuba ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wabunge wote, kwa michango yao mizuri na ushirikiano walionipa mimi binafsi na Wizara yangu na kufanya kazi yangu ya kuiongoza Wizara kuwa nyepesi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki (CCM) na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake fasaha na inayoonesha mafanikio ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne ikijumuisha sekta hii. Pia, napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa (CCM), kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa uchumi wetu, ikiwa ni pamoja na malengo ya Bajeti ya Serikali. Hotuba hizo zimejielekeza katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuzingatia utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza kwa Mwaka 2010/2011.

Ninaomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Kamati mbalimbali, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Bunge, pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa ushirikiano tunaopata katika

kuwasilisha Miswada mbalimbali ya Sheria na mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu. Napenda kukuhakikisha wewe na Waheshimiwa Wabunge kuwa, mchango na ushauri wenu utazingatiwa ili kuhakikisha kuwa, malengo tuliojiwekea yanafikiwa kwa manufaa na ustawi wa nchi yetu na jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Viongozi wenzangu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ambao ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami; Katibu Mkuu, Bibi Joyce Mapunjo; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Shabani R. Mwinjaka; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, nawashukuru Wataalamu na Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa kujituma katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ninajua nimewakimbiza mchakamchaka ili twende kwa kasi ya sekta binafsi, ambao ndiyo wadau wetu wakuu na mmeitikia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kumshukuru Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara yangu. Aidha, Watendaji wote wa Kiwanda cha Uchapishaji cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, kwa kuchapisha Hotuba hii kwa makini na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu ni mwaka wa mwisho wa Kipindi cha Kwanza cha Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzingatia hili, ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu maendeleo ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko katika kipindi hicho cha miaka mitano (2005 - 2010). Maendeleo ya Sekta kama ilivyo Sekta zingine, yametokana na misingi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, MKUKUTA, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda ni Sekta Kiongozi yenyeye jukumu la kubadilisha uchumi kuwa uchumi wa kisasa katika shughuli za sekta nyingine zote zikiwemo za kilimo, mifugo, madini, uvuvi na maliasili. Ili kufikia azma hii, katika kipindi cha miaka mitano, Sekta ya Viwanda ilijiwekea mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda; kuandaa Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini; kuendeleza zoezi la uwekezaji katika viwanda vinavyotumia malighafi inayopatikana nchini hususan viwanda mama kama vile Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma, Chuma cha Liganga na Mradi wa Magadi (*soda ash*) wa Ziwa Natron; kurekebisha Sheria ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*EPZ*); na kuanzisha utaratibu wa kutenga Maeneo Maalumu ya Uwekezaji (*Special Economic Zones – SEZs*) kwa ajili ya uzalishaji utakaolenga masoko ya ndani na nje. Mikakati mingine ilikuwa kuendelea kutafuta wawekezaji kwenye Viwanda ambavyo Serikali kwa makusudi haikuvibinafsisha; kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo; kutoa elimu ya ujasiriamali; na kuimarisha Usindikaji wa Mazao ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mikakati hii, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwa ni pamoja na ukuaji wa Sekta ya Viwanda na Mchango wake katika Pato la Taifa; kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa viwandani; kuongezeka

kwa mauzo ya bidhaa za viwandani; kuendeleza viwanda vya kusindika na kutengeneza bidhaa za ngozi nchini na kuongezeka kwa ajira. Mchanganuo wa mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2005 – 2009, kumekuwa na ongezeka la uzalishaji wa bidhaa viwandani, ambalo limechangia ukuaji wa Sekta ya Viwanda kufikia asilimia 9.9 mwaka 2008. Kwa wastani, ukuaji wa Sekta ya Viwanda katika kipindi hicho ulikuwa asilimia 9.0. Aidha, mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa nao uliongezeka kutoka asilimia 8.9 mwaka 2005 na kufikia asilimia 9.4 mwaka 2005 - 2008. Kwa wastani, mchango wa Sekta katika kipindi cha 2009 ni asilimia 8.0. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa Sekta na mchango wake kwa Pato la Taifa haukuwa kama ilivyotarajiwu, kutokana na athari za mtikisiko wa uchumi duniani, ambao ulisababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji, kushuka kwa bei ya bidhaa zinazouzwa nje na baadhi ya wawekezaji kujitao.

Kwa ujumla, uzalishaji wa bidhaa za viwanda nchini uliongezeka mwaka hadi mwaka katika kipindi cha 2005 hadi 2009. Ongezeko hilo ni kwa viwanda vingi ikiwa ni pamoja na konyagi, mabati, dawa za pareto, unga wa ngano, pombe ya kibuku, saruji, bia, soda, ngozi zilizosindikwa, rangi, sigara, biskuti, tambi na nguo. Uzalishaji wa konyagi uliongezeka kutoka lita 4,489,000 mwaka 2005 hadi kufikia lita 10,201,000 mwaka 2009. Uzalishaji wa dawa za pareto nao uliongezeka kutoka tani 24 mwaka 2005 hadi tani 266 mwaka 2009. Aidha, uzalishaji wa pombe ya kibuku nao uliongezeka kutoka lita 11,106,000 mwaka 2005 hadi kufikia lita 16,141,000 mwaka 2009. Uzalishaji wa mabati pia uliongezeka na kufikia tani 50,664 mwaka 2009 kutoka tani 29,737 mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji halisi (*actual production*) wa saruji uliongezeka kutoka tani 1,366,000 mwaka 2005 hadi kufikia tani 1,941,000 mwaka 2009. Uzalishaji huo uliongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na upanuzi wa viwanda vyote vya saruji nchini. Kiwanda cha *Tanzania Portland Cement* kimeongeza uwezo wa uzalishaji kutoka tani 700,000 hadi 1,400,000; *Tanga Cement* kutoka tani 500,000 hadi 1,200,000; na *Mbeya Cement* kutoka tani 250,000 hadi 350,000. Kwa ujumla, uwezo wa uzalishaji wa saruji kwa viwanda vyote vitatu, umeongezeka kutoka tani 1,454,992 mwaka 2005 hadi kufikia tani 2,950,000 mwaka 2009. Vile vile, uzalishaji wa biskuti na tambi uliongezeka kutoka tani 10,912 mwaka 2005 hadi tani 15,200 mwaka 2009. Uzalishaji wa bia uliongezeka kutoka lita 216,604,000 kwa mwaka 2005 hadi 284,906,000 mwaka 2009. Uzalishaji wa sigara ulipanda kutoka sigara bilioni 4,445 mwaka 2005 hadi bilioni 5,831 mwaka 2009.

Katika kipindi cha mwaka 2005 - 2009, Sekta ya Nguo na Mavazi imeimarika kutokana na matumizi ya teknolojia za kisasa pamoja na uongezaji wa mitaji kwa Viwanda kama vile Polytex, Sunguratex, Mwatex, NIDA na Tabotex. Vile vile kumekuwepo na uanzishwaji wa Viwanda vipywa ikiwa ni pamoja na A-Z (Arusha) cha kuzalisha vyandarua, Jambo Spinning Mills (Arusha) na Mazava (Morogoro) cha kuzalisha mavazi. Kwa ujumla, Sekta ya Nguo na Mavazi imekuwa na ongezeko la uzalishaji kwa wastani wa mita za mraba 129,408 (2006 - 2009), ikilinganishwa na mita za mraba 99,134 zilizozalishwa mwaka 2005. Ongezeko hilo ni sawa na asilima 30.5

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkakati Uganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini umekuwa na mafanikio ambapo usindikaji wa ngozi uliongezeka kutoka futi za mraba 6,038,000 mwaka 2005 hadi futi za mraba 37,305,215 mwaka 2009 kwa kiwango cha *wet-blue*. Mauzo ya ngozi zilizosindikwa yaliongezeka ambapo thamani yake iliongezeka kutoka shilingi bilioni 1.6 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 16 mwaka 2009. Aidha, baadhi ya viwanda vimeanza kusindika ngozi hadi kiwango cha kati (*crust leather*) na cha mwisho (*finished leather*), kwa ajili ya kutengenezea bidhaa za ngozi hapa nchini. Vile vile, ajira katika Sekta ya Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi imeongezeka kutoka 280 mwaka 2005 hadi 520 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa ajira katika viwanda na thamani ya bidhaa za viwanda zilizouzwa nje; ufufuaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa; uanzishwaji wa viwanda vipyta; uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda katika maeneo ya EPZ; na Sekta ya Viwanda Vidogo; kwa kiasi kikubwa vimechangia ongezeko la ajira katika Sekta ya Viwanda. Kwa mfano, katika maeneo ya EPZ, ajira imeongezeka kutoka 3,100 mwaka 2005 hadi 9,300 mwaka 2009.

Kwa ujumla, idadi ya wafanyakazi walioajiriwa katika viwanda vikubwa na vya kati walikuwa 89,316 kwa mwaka 2005 na kuongezeka hadi wafanyakazi 92,927 mwaka 2009. Katika ajira hizo, viwanda vinavyoongoza ni viwanda vya kusindika vyakula - ajira 45,287, ufumaji na ushonaji – ajira 10,480; na Tumbaku na Sigara – ajira 7,131. Vile vile, katika kipindi cha 2005 hadi 2009, ajira mpya 92,547 zilipatikana kutokana na miradi iliyowezeshwa na SIDO. Hata hivyo, ipo miradi mingine mingi ilioanzishwa kutokana na mikopo na jitihada za taasisi nyingine zinazohudumia wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ukusanyaji wa takwimu za msingi (*Baseline Survey*) ya Sekta linaloendelea na ambalo linatarajiwa kukamilika Desemba 2010, litatupatia takwimu sahihi za ajira katika Sekta hii. Aidha, katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa za viwandani zilizouzwa nje ziliongezeka kutoka Dola za Marekani 156.1 milioni mwaka 2005 hadi Dola za Marekani 497.6 milioni mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 218.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira na mapato kwa Wananchi wa kawaida. Katika kuendeleza Sekta hii, Wizara imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ambayo ni pamoja na kuongeza uwezo wa SIDO katika uwezeshaji wa kitaalamu na mitaji; kuboresha huduma kwa wanaviwanda na wafanyakabiashara wadogo na wa kati; kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Sekta Binafsi katika kutenga maeneo na kujenga mabanda mikoani kwa ajili ya viwanda vidogo na biashara ndogo; na kuanzisha Programu ya Muunganisho wa Wajasiriamali Vijijini, ambayo inalenga kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2009, kumekuwa na jitihada mbalimbali za kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyakabiashara wadogo na wa

kati, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa miradi ya viwanda vidogo vijijini na utoaji wa huduma maalumu kwa makundi mbalimbali. Jumla ya miradi ya uzalishaji ilioanzishwa vijijini, iliongezeka kutoka miradi 440 mwaka 2005 hadi kufikia miradi 2,506 mwaka 2009. Aidha, idadi ya wajasiriamali waliopata huduma za ugani wa biashara iliongezeka kutoka 5,723 mwaka 2005 hadi kufikia 47,356 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wajasiriamali waliopata huduma ya mafunzo iliongezeka kutoka 3,074 mwaka 2005 hadi kufikia wajasiriamali 28,619 mwaka 2009 na mafunzo kwa wahanzi yaliongezeka kutoka 831 mwaka 2005 hadi kufikia 6,519 mwaka 2009. Aidha, ushiriki wa wajasiriamali wadogo kwenye maonesho uliongezeka kutoka washiriki 3,074 mwaka 2005 hadi kufikia 8,254 mwaka 2009. Ushiriki wao uliwawezesha kuuza bidhaa za thamani ya shilingi bilioni 4.532. Upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo uliongezeka kutoka mikopo 3,990 ya thamani ya shilingi bilioni 2.506 mwaka 2005 hadi kufikia mikopo 23,523 ya thamani ya shilingi bilioni 16.485 mwaka 2009, kwa Serikali kuchangia mtaji kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujasiriamali (*National Entrepreneurship Development Fund – NEDF*).

Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi mwaka 2009, Wizara imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara, ambayo ina lengo la kuinua ufanisi na kuweka uhusiano mpana katika uzalishaji na kujenga uchumi unaohimili ushindani katika masoko ya nje. Katika kuendeleza Sekta ya Biashara, Wizara imetekeliza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanua soko la bidhaa zetu na uimarishaji wa masoko ya ndani ya nchi na mipakani; kuvutia wawekezaji kwa kuimarisha ushirikiano kati ya nchi na nchi, Jumuia za Kikanda (EAC na SADC) na Kimataifa chini ya mfumo wa Shirika la Biashara Duniani (*WTO*); kuanzisha Mkakati Maalumu wa Kukuza Mauzo Nje (*Export Development Strategy - EDS*); kuongeza thamani mazao, bidhaa na huduma nje ya nchi ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini; kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje ambao umelenga mazao, bidhaa za huduma za kipaumbele zenye fursa na uwezekano wa kuendelezwa kwa haraka na kutoa matokeo ya haraka (*Quick Wins*) na Mpango Uunganishi wa Biashara ya Tanzania. Utekelezaji wa mikakati hiyo kwa kiasi kikubwa umefanikisha kuongezeza kwa thamani ya mauzo ya bidhaa nje kutoka Dola za Marekani 1,679.1 milioni mwaka 2005 na kufikia Dola za Marekani 3,096 milioni mwaka 2009. Aidha, kwa mwaka 2009, mauzo ya bidhaa asilia yalichangia asilimia 18 na bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 82 ya thamani ya mauzo ya bidhaa nje. Kiasi hicho cha mauzo ya bidhaa zisizo asilia, kimetokana na mauzo ya madini (54%), bidhaa za viwandani (23%), samaki na bidhaa za samaki (6%), mbogamboga na maua (2%) na mauzo mengine kwa pamoja (28%).

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya uagizaji wa bidhaa iliongezeka kutoka bidhaa za thamani ya Dola za Marekani milioni 2,997.6 mwaka 2005 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 6,483.40 mwaka 2008. Aina ya bidhaa zilizoagizwa ni bidhaa za ukuzaji wa mitaji - asilimia 44, bidhaa za kati - asilimia 32 na bidhaa za matumizi ya kawaida - asilimia 24. Kutokana na juhudhi mbalimbali za serikali, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ununuza wa bidhaa za ndani kwa kupitia kaulimbiu ya “Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania” thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje (*f.o.b*), ilipungua kwa asilimia 10.9 na kufikia Dola 5,775.7 mwaka 2009. Upungufu huo ulichangwa na

kupungua kwa uingizaji wa bidhaa za kati ambazo ni mafuta, mbolea na malighafi za viwandani. Kuongezeka kwa thamani ya Dola pia kulichangia kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,078.1 mwaka 2005, ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 2,648.6 mwaka 2008. Aidha, uagizaji wa vifaa nya usafiri ulipungua kutoka Dola za Marekani milioni 787.8 mwaka 2008 hadi Dola za Marekani milioni 741 mwaka 2009. Vile vile, uagizaji wa vifaa nya ujenzi ulishuka kwa asilimia 9.3 kutoka Dola za Marekani milioni 619.5 mwaka 2008 hadi Dola za Marekani milioni 562.1 mwaka 2009, sawa na asilimia 9.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati uliongezeka kutoka bidhaa zenyet thamani ya Dola za Marekani milioni 1,166.3 mwaka 2005, ukilinganisha na Dola za Marekani milioni 2,551.30 kufikia mwaka 2008. Aidha, zilipungua hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,870.6 kwa mwaka 2009, ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 26.7. Upungufu huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa uagizaji wa mbolea kwa asilimia 36.7 kutoka Dola za Marekani milioni 150.4 mwaka 2008 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 95.2 mwaka 2009. Thamani ya uagizaji wa mafuta ulipungua kwa asilimia 28.9 na uagizaji wa malighafi za viwandani ulipungua kwa asilimia 16.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida umeongezeka. Mwaka 2005 bidhaa zilizoagizwa nje ya nchi ziliongezeka kutoka thamani ya Dola za Marekani milioni 751 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,392.1 mwaka 2009. Kuongezeka huko kumechangiwa na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za vyakula na bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa biashara kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo iko katika hatua ya kuanzisha Umoja wa Forodha, mauzo ya Tanzania kwenda Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 96.4 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 263.7 mwaka 2009. Mauzo ya bidhaa kwenda Kenya yaliongezeka kutoka Dola za Marekani 76.3 milioni mwaka 2005 na kufikia Dola za Marekani Milioni 177.3 mwaka 2009. Mwaka 2005 mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Uganda yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 20.1 na yaliongezeka na kufikia Dola za Marekani milioni 47.7 mwaka 2009. Vile vile, thamani ya bidhaa zilizouzwa nchini Burundi ziliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 19.5 kwa mwaka 2008 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 23.6 kwa mwaka 2009. Aidha, bidhaa zenyet thamani ya Dola za Marekani milioni 310.4 ziliagizwa mwaka 2009 kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikilinganishwa na bidhaa zenyet thamani ya Dola milioni 174.4 mwaka 2006, ambayo inaashiria ukuaji wa biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Biashara ya Tanzania katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), imekuwa ikiongezeka. Mauzo ya Tanzania katika Soko hilo yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 322.3 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 374.1 mwaka 2009. Aidha, manunuzi ya bidhaa kutoka SADC yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 625.9 kwa mwaka 2006 hadi Dola za Marekani milioni

953.6 mwaka 2008. Tanzania imeendelea kunufaika na fursa za masoko nafuu ya Jumuiya ya Ulaya na Uswisi, chini ya mpango wa Uza Kila Kitu Isipokuwa Silaha (*Everything But Arms – EBA*). Kwa mwaka 2005, mauzo ya bidhaa na mazao ya Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 619.6 hadi Dola za Marekani milioni 928 kwa mwaka 2009. Aidha, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi tunazofanya nazo biashara kwa wingi kama vile China, Japan, India, Hong Kong na Umoja wa Falme za Kiarabu, yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 175.2 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Marekani 864.4 mwaka 2009.

Sekta ya Masoko; mafanikio ya mifumo bora ya masoko yanategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa miundombinu bora ya masoko, kupatikana kwa mitaji na mikopo, kuwepo kwa stadi za biashara zinazoongozwa na taarifa sahihi za masoko. Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara imeandaa na kuendelea kuboresha Kitabu cha Orodha ya Wanunuzi na Wasindikaji wa Mazao (*Agri-business Directory*) na kukisambaza kwa wadau; imeendelea kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao na mifugo kwa walengwa; kuandaa Mkakati wa Kuendeleza Soko la Ndani inayojumuisha kukamilisha Sera ya Masoko ya Mazao na bidhaa za kilimo; kurahisisha taratibu za kupata usajili wa shughuli za biashara chini ya Sheria Mpya Namba 14 ya Mwaka 2007; kuanzisha Mamlaka ya Maendleo ya Biashara Tanzania (*Tanzania Trade Development Authority - TANTRADE*); na kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Aidha, Wizara imeweka Mikakati itakayoliwezesha Taifa kuhimili ushindani wa biashara kimataifa na kuwa na uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya kimataifa katika mazingira ya utandawazi kama vile mikakati ya kusimamia utekelezaji wa viwango vya ubora wa bidhaa; kudhibiti bidhaa bandia kabla hazijamfikia mlaji; kuhakiki vipimo na kudhibiti matumizi ya vipimo batili; kukusanya mirabaha na kuadhibiti wanaotumia kazi za wasanii bila idhini; na kuhakiki makampuni hai na kusajili makampuni, majina na alama za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2005 hadi 2009, kwa ujumla, kumekuwa na ongezeko la bei kwa mazao makuu ya chakula ambayo ni mahindi, mchele, ngano, uwele, ulezi, mtama na viazi mviringo. Wastani wa bei ya jumla ya mahindi iliendelea kupanda kutoka shilingi 26,767 mwaka 2005 na kufikia shilingi 42,133 mwaka 2009, kwa gunia la kilo mia moja. Mwaka 2005 hadi 2006, bei ya maharagwe kwa gunia lenye uzito wa kilo mia moja ilishuka kutoka shilingi 72,750 hadi shilingi 57,365 na kuongezeka kufikia shilingi 105,092 mwaka 2009. Hali kadhalika, kwa mwaka 2005 hadi 2006, wastani wa bei ya mchele kwa gunia lenye uzito wa kilo mia moja, ilishuka kutoka shilingi 76,830 hadi shilingi 57,779 na kuongezeka hadi kufikia shilingi 99,790 mwaka 2009. Kupanda huko kwa bei ya mazao ya chakula kulisababishwa na ongezeko la mahitaji ikilinganishwa na ugavi. Aidha, ongezeko la bei ya nishati ya mafuta kumesababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji na hivyo ongezeko la bei za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2005 na 2009, wastani wa bei ya mazao asilia katika Soko la Dunia imekuwa ikiongezeka kwa baadhi ya mazao hususan kahawa, chai, tumbaku na pamba. Kupanda kwa bei hizo, kulichangwa zaidi na kuongezeka kwa

mahitaji ya mazao hayo katika Soko la Dunia. Hata hivyo, kutokana na athari za m dororo wa uchumi, bei za mazao hususan kahawa na pamba nyuzi, zilishuka mwaka 2008 kutokana na makampuni ya nje yaliyokuwa yakinunua mazao hayo kusitisha uagizaji kutokana na kukosa mitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya washiriki kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar Es Salaam – *DITF*, imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Jumla ya washiriki binafsi iliongezeka kutoka 1,508 mwaka 2005 hadi kufikia 2,103 kwa mwaka 2009. Kati ya washiriki hao; 1,760 ni wa hapa nchini na 343 ni kutoka nje ya nchi. Kuongezeka kwa washiriki wa ndani kumetokana na kuongezeka kwa ushindani ndani ya soko na hivyo haja ya kutangaza bidhaa husika na kuongezeka kwa mabanda makubwa yaliyotoa fursa kwa washiriki wengi zikiwemo Wizara na Taasisi za Serikali.

Kwa upande wa idadi ya nchi washiriki, kumekuwa na ongezeko kutoka nchi 18 mwaka 2005 hadi nchi 27 mwaka 2008. Hata hivyo, mwaka 2009 idadi ya nchi washiriki ilishuka kwa asilimia 14.8 ambapo jumla ya nchi 23 tu zilishiriki. Sababu za kushuka kwa nchi shiriki ni pamoja na mtikisiko wa uchumi ulioathiri nchi nyingi duniani. Aidha, Maonesho hayo yameendelea kuwa ni fursa za kutangaza bidhaa zetu na kuweza kupata masoko ambayo mauzo ya bidhaa za thamani ya Dola za Marekani milioni 137.8 yalipatikana mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 kuhusu Viwanda, Biashara na Masoko. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ukurasa wa 36–46 hususan Ibara ya 36, 37, 40 na 41 yamewekwa malengo ya maendeleo endelevu ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko ya kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2005 – 2010. Napenda nichukue nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu mafanikio yaliyopatikana kwa kutekeleza malengo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa Sekta ya Viwanda kufikia asilimia 15 ifikapo 2010. Nia ya Serikali imekuwa ni kutekeleza mikakati na programu zitakazotumia fursa mbalimbali zilizopo katika kilimo, uchakataji na usindikaji wa mazao ya kilimo na madini ili kuongeza thamani badala ya kuuza nje malighafi. Mkakati na proram hizo ni pamoja na: Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*EPZ*) na kutekeleza Mkakati Uganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda Nchini. Kutokana na hatua hizo, yamekuwepo mafanikio ya Ukuaji wa Sekta ya Viwanda. Mafanikio hayo ni pamoja na utumiaji wa uwezo wa uzalishaji - *capacity utilization*, ambapo kumekuwepo na ongezeko kutoka wastani wa asilimia 30-40 mwaka 2005 hadi wastani wa asilimia 40-50 mwaka 2009. Viwanda vingine vimeweza kufikia zaidi ya asilimia 80 kama vile viwanda vya sigara, saruji na bia. Kutokana na utekelezaji wa mikakati na programu hizo, ukuaji wa sekta ulifikia asilimia 9.9 mwaka 2008 kama ilivyoainishwa katika aya ya 17 ya hotuba hii:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini umeendelea kutekelezwa na Wizara kwa kufanya yafuatayo: Kukamilishwa kwa programu inayolenga kusaidia na kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa Vijiji vya Viwanda - *Industrial Villages Development Support Programme* vitakavyokuwa maeneo maalumu ya uzalishaji na uboreshaji wa bidhaa za ngozi kama vile viatu, mabegi na mikanda kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi; Utekelezaji wa programu ya kujenga uwezo ili kuimarisha vituo vya mafunzo na uzalishaji katika Mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro; kujenga uwezo wa ujuzi na stadi kwa wajasiriamali katika utekelezaji na uboreshaji wa bidhaa za ngozi; kuendeleza mafunzo ya usindikaji wa ngozi kwa njia ya asili - *rural tanning technology*. Vile vile, Wizara kuitia chama cha wadau wa ngozi (LAT) iliendelea kusimamia na kudhibiti ulipaji wa ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuwezesha Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) na Nanenane pamoja na maonesho ya nje ya nchi kwa bidhaa za Nguo, Ngozi na Sanaa. Wajasiriamali wengi walijitokeza katika maonesho haya kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya 25 ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na juhudzi za kufufua na kuendeleza Chuo cha Taaluma ya Ngozi *Tanzania Institute of Leather Technology (TILT)* ambacho kwa sasa kipo chini ya *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)*. Vile vile, Wizara imeandaa vielelezo vya picha - *Video Documentary* inayoonesha shughuli mbalimbali za sekta ya ngozi ili kuonesha fursa za uwekezaji kwenye sekta ya ngozi pamoja na kuchochea na kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta hiyo. Aidha, *TIRDO* imetoa mafunzo kwa washiriki 50 huko Morogoro ya jinsi ya kutumia teknolojia za kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kupima sampuli za uchafuzi wa mazingira katika viwanda vya kusindika ngozi. Lengo la hayo mafunzo ni kujifunza taratibu za kurekebisha matatizo yatokanayo na uchafuzi wa mazingira yanayofanywa na viwanda vinavyosindika ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudzi za kupata wawekezaji katika miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga zimefanywa na Wizara kuitia *NDC* ambapo tayari makampuni tisa yamechaguliwa kuandaa mapendekezo ya uwekezaji katika mradi wa Mchuchuma na makampuni matano kwa ajili ya Mradi wa Chuma wa Liganga. Lengo ni kuhakikisha kuwa mchakato wa kuwapata wawekezaji kwa miradi hii unakamilika ifikapo Desemba 2010. Pia, Wizara kuitia *NDC* inatekeleza mradi wa makaa ya mawe ya Ngaka katika Mkoa wa Ruvuma kwa ubia na mwekezaji binafsi wa Kampuni ya *Pacific Corporation East Africa (PCEA)*. *NDC* na *PCEA* wameunda kampuni ya *Tancoal Energy Limited* ambayo inaendeleza mradi huu. Uwekezaji unalenga kuanzisha mgodi wa makaa ya mawe ambaa unatarajia kuzalisha tani milioni mbili za makaa ya mawe kwa mwaka na kituo cha kuzalisha umeme wa megawati 400 ifikapo 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi wa ‘Mpango wa Kasi Mpya’, wa kuzalisha chuma ghafi tayari eneo la Maganga Matitu lenye ukubwa wa kilomita za mraba 14.33 kwa ajili ya chuma na eneo la Katewaka lenye ukubwa wa kilomita za mraba 28.4 kwa ajili ya makaa ya mawe yametengwa. Maeneo haya 25 *MWVBM Budget new.qxp: Layout 1 6/28/10 6:09 PM Page 25* yapo sehemu ya Liganga

katika Wilaya ya Ludewa. Mradi huu unasimamiwa na kampuni ya *Maganga Matitu Resource Development Limited* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya kampuni ya *MM Steel Resources Public Limited (MMSRPL)* ya Dar es Salaam na NDC. Kampuni hiyo imeanza maandalizi ya kufanya uchorongaji ili kubainisha wingi wa chuma na madini ya Vanadium na Titanium na kukamilisha upembuzi yakinifu -*Bankable Feasibility Study*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya uuzaaji nje (*Export Processing Zones – EPZ*) na uwekezaji wa Viwanda ndani ya maeneo hayo. Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imeendelea kubainisha maeneo ya uwekezaji ya *EPZ* na kuhamasisha uwekezaji ndani ya maeneo hayo. Kwa ujumla mpaka sasa leseni 67 za *EPZ* zimetolewa ambapo leseni 31 zimetolewa kwa wawekezaji waliojenga miundombinu ya *EPZ* na leseni 36 kwa wale walioanzisha viwanda vinavyozalisha bidhaa chini ya *EPZ*. Viwanda hivi vimewekeza jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 350 na vimetoa ajira 9,300 za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha uandaaji wa dhana ya *Economic Development Zones (EDZ concept)* inayounganisha mifumo ya *EPZ* na *Special Economic Zones (SEZ)*. Dhana hii imepitia hatua mbalimbali za Kiserikali na kwa sasa inasubiri kupata kibali cha Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uendelezaji wa maeneo ya uwekezaji, tayari maeneo ya *EPZ* yenyeye ukubwa wa kati ya hekta 500 hadi 9,000 yamekwishabainishwa katika mikoa kumi na minne. Maeneo haya kwa sasa yapo katika hatua mbalimbali za uendelezaji ambapo katika Mikoa ya Mara, Ruvuma na Manyara, zoezi la upimaji na uthaminishaji wa mali limekamilika wakati zoezi hilo lipo katika hatua za mwisho kwa mikoa ya Tanga, Arusha, Morogoro na Kagera. Aidha, Mamlaka imekamilisha zoezi la upembuzi yakinifu – *Feasibility Study* katika eneo la Mbegani Bagamoyo na tayari mshauri mwelekezi atakayeandaa mpango mpana (*Master Plan*) wa kuendeleza eneo hilo amepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha uendelezaji wa maeneo maalumu ya *EPZ*, Wizara inafanya juhudhi maalum za kuhusisha sekta binafsi. Kutokana na uhamasishaji huo, tayari maeneo matatu makubwa ya *EPZ (Industrial Parks)* yameanzishwa na Sekta Binafsi. Maeneo hayo ni eneo la *Millenium Business Park* na lile la Hifadhi *EPZ* yaliyopo Ubungo Dar es Salaam; pamoja na eneo la Kisongo *EPZ* lililopo Arusha. Aidha, Kampuni ya *Kamal Alloy Steel Ltd* kutoka India inaendelea na ujenzi wa *EPZ* ya kisasa katika eneo la ekari 300 katika kijiji cha Zinga wilayani Bagamoyo. Eneo hili liliwekwa jiwe la msingi na Mheshiwa Dr Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha utaratibu wa kutenga Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (*Special Economic Zones - SEZs*), kwa ajili ya uzalishaji utakaolenga masoko yote ya ndani na nje. Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imekamilisha ujenzi wa Eneo Maalumu la Uwekezaji la Benjamin William Mkapa *Special Economic Zones (BWM-SEZ)* ambapo eneo hilo lilizinduliwa rasmi na Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Mei, 2010. Eneo hilo lina miundombinu

yote ya msingi kama vile maji, umeme, gesi ya asili na mawasiliano na kadhalika na ujenzi wake umegharimiwa na Serikali kupitia bajeti yake. Jumla ya Wawekezaji kumi na wawili wamepewa leseni za kujenga viwanda ndani ya eneo hilo.

Kati ya wawekezaji hao, sita wameanza kujenga viwanda na sita wapo katika hatua mbalimbali za kukamilisha taratibu za fedha za ujenzi na usanifu wa majengo ya viwanda. Jumla ya mitaji inayotarajiwa kuwekezwa ni Dola za Marekani milioni 90 na ajira za moja kwa moja zitakazozalishwa ni 4,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea na utekelezaji wa Programu inayolenga katika kuimarisha usindikaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Chakula. Wizara iliendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya kilimo. Mazao hayo ni pamoja na matunda, mbogamboga, ngozi, pamba, katani, mbegu za mafuta ya kupikia, viungo na nafaka. Serikali ilitoa ruzuku ya Shilingi 80 kwa kila kilo ya pamba iliyonunuliwa kutoka kwa wakulima na wenyewe viwanda vya kuchambua pamba (*ginneries*) ambayo imewezesha bei ya Pamba kwa mkulima kuongezeka kutoka shilingi 360 kwa kilo hadi shilingi 440 kwa kilo. Hatua hii imesaidia kuwapunguzia athari zilizowakumba kutokana na mdororo wa uchumi duniani. Aidha, Serikali imefungua maabara ya kupima ubora wa pamba ya wakulima ili ikidhi ubora na ushindani katika soko la kimataifa. Maabara hii itasaidia pia kupima sampuli za pamba kutoka nchi zilizo Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubuni mpango wa kuandaa mabingwa katika fani mbalimbali za Sayansi na Teknolojia ya Viwanda, Taasisi zetu zimeendelea kujengewa uwezo na Wizara ili kuandaa wataalamu mabingwa katika fani za sayansi na teknolojia kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Chuo cha Elimu ya Biashara licha ya kujikita kwenye stadi ya biashara pia hutoa wataalamu wa fani ya vipimo na mizani. Aidha, katika kujenga uwezo wa mabingwa watakaotumika kuendeleza sekta na viwanda vya ngozi, Wizara kwa kushirikiana na *DIT* zimeanza hatua za kukifufua na kukiimarisha Chuo cha Taaluma ya ngozi kilichopo Mwanza (*TILT*) ambacho kitajikita katika kuzalisha wataalamu wa ngozi hususan *Leather technologists, footwear and leather goods technologists and designers, machinery operators* na teknolojia nyingine zinazohitajika katika sekta. Pia, Taasisi za *CAMARTEC, TEMDO, TIRDO* na *SIDO* zinaendeleza teknolojia kwa kutumia mikakati ya viatamizi - *incubators* ambapo miradi michanga hulelewa hadi hatua ya kuingia kwenye soko. Vile vile, taasisi hizi zimetoa mafunzo yanayolenga kuongeza ubora wa bidhaa. Aidha, Vyuo vya Elimu ya Juu navyo vimeendelea kutoa wataalam wa fani mbalimbali wakiwemo wahandisi, wahasibu, wachumi na kadhalika wanaohitajika viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuvutia uwekezaji katika Viwanda vya kuongeza Thamani Mazao mbalimbali ya Kilimo, Mifugo, Madini, Uvuvi na Maliasili. Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) na *EPZA* imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje katika jitihada zake za kuvutia wawekezaji nchini. Katika kipindi cha 2005/2010, *EPZA* imesajili wawekezaji 67 wa kuongeza thamani katika mazao ya Kilimo, Mifugo, Madini, Uvuvi na Maliasili. Aidha, Serikali itaendelea kuweka

vivutio maalumu kwenye sekta zinazolenga uongezaji thamani ili kuhamasisha uwekezaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea na ubinafsishaji na ukodishaji wa Viwanda na Mashirika ya Umma yaliyobaki, Viwanda ambavyo bado havijabinafsishwa chini ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko ni kiwanda cha *Morogoro Leather Goods (MLG), Songwe Water Company na General Tyre East Africa Limited (GTEA)*. Zoezi la kubinafsisha kiwanda cha *MLG* linaendelea. Hata hivyo, kazi ya uthamanishaji mali za *MLG*, ili kupata bei elekezi limekwamishwa na uvamizi wa eneo la Kiwanda hadi ufumbuzi utakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudzi za kumpata mwekezaji wa kufufua kiwanda cha *GTEA* zinaendelea. Uthamanishaji wa mali za *GTEA* umefanyika ili kubainisha thamani halisi na hivyo kuwezesha kufanyika maamuzi sahihi ya hatua za kuchukua. Mawasiliano kati ya Serikali na kampuni ya *Continental AG* ya kuwaita katika majadiliano yanaendelea kwa lengo la kusitisha makubaliano ili taratibu za kuingia ubia na mwekezaji mwingine ziweze kuanza. Majadiliano yalitarajiwa kufanyika mwezi Aprili 2010 lakini ilishindikana kutokana na mbia huyo kutokuwa tayari katika tarehe na mahali palipopendekezwa na Wizara kufanya majadiliano. Lengo la majadiliano hayo ni kukubaliana utaratibu wa kuachana na mbia huyo kwa vile hayuko tayari kuwekeza katika Kiwanda cha *GTEA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imehamishia *NDC* umiliki wa mali zilizokuwa za kampuni za *Tanzania Sheet Glass, Nyanza Glassworks, Kilimanjaro Machine Tools (KMT)* na *TAMCO*. Kwa sasa *NDC* imekamilisha michoro kwa ajili ya *layout plan* ya *TAMCO*. Aidha, *NDC* imeshapata wabia wa kuendeleza *KMT* na kiwanda cha *Tanzania Sheet Glass Limited* cha Mbagala. Juhudi za kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kufunga mitambo mipyka katika majengo ya kilichokuwa kiwanda cha *Nyanza Glass Works* cha Mwanza kwa ajili ya uzalishaji hazijafanikiwa.

Katika jitihada za kuboresha mashamba ya Mpira ya Muheza, Tanga, Kilombero na Morogoro, *NDC* imeingia mkataba wa miaka miwili na mwekezaji wa kusafisha mashamba yenye ukubwa wa hekari 807 na kufufua mitambo iliyochakaa, na kuongeza ubora wa mpira. Aidha, mwendelezaji anawajibika kuandaa miche ya mpira kwa ajili ya kupanda sehemu ya mashamba ambayo haijaendelezwa kwa kushirikiana na *NDC*. Upandaji wa miche katika eneo hilo utasaidia kuondoa wavamizi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha uperembaji wa viwanda vyote vilivyobinafsishwa chini ya sekta ya Viwanda Biashara na Masoko. Waraka wa Baraza la Mawaziri wa kuwasilisha mapendekezo ya hatua za kuchukua kwa wawekezaji ambao hawajatekeleza majukumu yao ya kimkataba ya kufufua na kuendeleza viwanda walivyonunua umeandaliiwa na kuwasilishwa Serikalini kwa maamuzi ili kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo *SIDO* na Sera yenyewe ya Viwanda Vidogo itatazamwa upya ili kuhakikisha inakidhi lengo kuu

la kujenga msingi wa uchumi wa kisasa Majukumu na sheria ya *SIDO* yamepitwa na mtaalamu mwelekezi na kutoa mapendekezo. Hatua inayofuata ni kujadiliwa kwa rasimu na wadau wa sheria hiyo ili kupata maoni na mapendekezo yatakayoboresha marekebisho husika. Vile vile, Wizara inaendelea na Uperembaji na Tathmini (*M&E*) ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kuona kama inakidhi lengo kuu la kujenga uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza ushiriki wa Sekta isiyo Rasmi na Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati (*SMEs*) katika uzalishaji wa bidhaa. Katika kuongeza ushiriki wa sekta isiyo rasmi, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) imeendelea kutambua umuhimu wa kupeleka huduma kwa wananchi mahali walipo. Huduma hizo ni pamoja na kuwezesha makundi mbalimbali kuanzisha miradi ya uzalishaji na kutoa huduma za kuendeleza wajasiriamali vijiji. Kama ilivyoelezwa katika aya ya 26 miradi ya uzalishaji ilianzishwa katika maeneo ya useketaji wa nguo, uzalishaji wa chumvi, ubanguaji wa korosho, usindikaji wa muhogo, usindikaji wa vyakula, uhunzi, useremala, ukamuaji wa mafuta ya kula, utengenezaji wa chaki, usindikaji wa ngozi, utengenezaji wa sabuni, utengenezaji wa mishumaa, utengenezaji wa mizinga bora na uzalishaji wa asali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na Uperembaji na Tathmini (*M&E*) ya utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwenye eneo la uboreshaji wa sheria na taratibu za biashara kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Pia, uboreshaji wa maeneo ya kufanya kazi umefanyika - *working premises* kwa wajasiriamali wa Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Singida. Vile vile, katika uongezaji wa mitaji, Serikali imeendelea kuchangia mtaji wa *NEDF* kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 25. Aidha, Wizara kupitia *SIDO* imesambaza teknolojia mbalimbali kwa vikundi na wajasiriamali wapatao 2,691 kwenye mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Lindi, Tabora, Mwanza, Arusha, Mara, Kilimanjaro na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza uwezo wa *SIDO* katika uwezeshaji wa Kitaalam na Mitaji katika Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati, Programu ya Muunganisho Ujasiriamali Vijiji (MUVI) inayofadhiliwa na *IFAD* kwa Dola za Marekani milioni 25.3 imeendelea kujengea *SIDO* uwezo wa kuendeleza viwanda vidogo vijiji. Aidha, programu ya usindikaji wa vyakula imeongezewa nguvu na Serikali ya Korea ya Kusini kwa kufadhili ujenzi wa vituo vya mafunzo na uzalishaji wa vyakula wenyewe thamani ya Dola za Marekani milioni tatu. Vile vile, Serikali imeendelea na azma yake ya kuboresha mfuko wa *NEDF* kama ilivyoiezwa kwenye aya ya 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuendelea kushirikiana na Asasi mbalimbali kuboresha mazingira ya uzalishaji Viwandani ikiwa ni pamoja na Miundombinu, Sera za Fedha na Kodi na kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Kama ilivyoiezwa kwenye aya ya 61, Wizara imeendelea kuhamasisha Manispaa na Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Aidha, Wizara ilishiriki katika majadiliano ya maboresho na

marekebisheso ya sera za kodi ambapo iliwasilisha mapendekezo kuhusu kurekebisha kodi kwa baadhi ya bidhaa za viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Biashara, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ilibainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji. Kuendelea Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda (*EAC, SADC*) na wa Kimataifa (*WTO*) kwa Lengo la Kupanua Soko la Bidhaa Zetu na Kuvutia Wawekezaji, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wake na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha na kushiriki katika majadiliano ya kuanzishwa kwa soko la pamoja la *EAC*. Majadiliano ambayo yalikamilika na Itifaki ya kuanzishwa kwa Soko la Pamoja ilisainiwa mwezi Novemba 2009. Aidha, Itifaki hiyo iliwasilishwa katika Mkutano wa 19 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuridhiwa. Utekelezaji wake unategemewa kuanza rasmi mwezi Julai, 2010 baada ya Itifaki hiyo kuridhiwa pia na nchi zote wanachama. Nchi wanachama ikiwemo Tanzania zinaendelea kuboresha maeneo ya viambatisho ambayo ni sehemu ya Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya kuimarisha umoja wa kikanda wa *SADC*, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa *SADC*. Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu maeneo muhimu katika kuunda Umoja wa Forodha wa Jumuiya hiyo. Tanzania Vile vile, inashiriki kikamilifu katika kuanzishwa kwa Itifaki ya Biashara ya Huduma ya *SADC* ambayo imeshafikia ngazi ya rasimu ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi za pamoja zimeanzishwa na *EAC, SADC* na *COMESA* kurazinisha Sera zao za biashara kwa lengo la kuanzisha Eneo Huru la Biashara kwa Kanda hizo tatu na kuondoa tatizo la mwingiliano wa Jumuiya za kikanda - *Multiple Membership*. Sambamba na juhudhi hizo Jumuiya hizo tatu zinatekeleza programu ya pamoja yenye lengo la kurahisisha biashara kwa kupunguza na hatimaye kuondoa vikwazo visivyokuwa vya kiushuru (*NTBs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara vile vile, imeendelea kuongoza majadiliano ya Ubia wa Uchumi *EPA* kati ya *EAC* na *EC*. Makubaliano yamefikiwa katika maeneo mengi muhimu na hasa katika suala la ushirikiano wa kiuchumi na maendleo. Majadiliano bado yanaendelea ili kukamilisha na hatimaye kusainiwa kwa mkatuba kamili wa *EPA* ambayo yanazingatia maslahi ya nchi na makubaliano ya Shirika la Biashara la Dunia *WTO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano ya biashara ya Duru la Doha yanayofanyika chini ya Shirika la Biashara la Dunia (*WTO*) hayajakamilika kutokana na nchi wanachama kutokubaliana katika masuala ya kilimo na hasa ruzuku inayotolewa na nchi zilizoendelea kwa wakulima wao zikiwepo nchi za Marekani, Ulaya na Japan. Katika kuendelea kutetea maslahi ya nchi masikini duniani, Tanzania ilichaguliwa kuratibu na kuwa mwenyeji wa mkutano wa Mawaziri wa nchi 49 masikini zaidi duniani (*LDCs*) Oktoba 14-16, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huo ulilenga kupata msimamo wa pamoja wenye maslahi kwa nchi za *LDC* katika kila agenda ya majadiliano ya Doha. Msimamo

huo uliwasilishwa *WTO* katika Mkutano wa 7 wa Mawaziri wa Biashara wa nchi zote wanachama uliofanyika Novemba 30 hadi Desemba 2, 2009 mjini Geneva, Uswisi. Msimamo wa *LDC* ni kwamba tuenze kunufaika na fursa za masoko ya upendeleo katika maeneo ambayo makubaliano yamefikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa elimu ya Kanuni na Taratibu za Masoko na Biashara na nchi za nje hususan Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na Nchi Nyingine ambazo zinatoa upendeleo kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi zinazoendelea. Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi na Asasi Zisizo za Serikali (*AZISE*) imeendelea kuelimisha umma kuhusu Kanuni, Taratibu za Masoko na Biashara katika nchi za nje zikiwemo Jumuiya za *SADC* na *EAC*.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na kampuni ya *Export Path* ya Marekani imetoe mafunzo kwa wajasiriamali 215 juu ya kuzalisha bidhaa kulingana na matakwa ya soko la Marekani kwa kupitia *AGOA*. Vile vile, jitihada za kuelimisha Maafisa Biashara na wakusanya taarifa za masoko walioko katika ngazi ya Wilaya na Mikoa yote ya Tanzania bara zilifanyika Mei 2010, kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu fursa mbalimbali za masoko zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhimiza Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) katika Biashara, Kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya TEKNOHAMA katika biashara (*e-commerce*), Wizara imeendelea kuboresha kitengo cha kuratibu shughuli za TEKNOHAMA na kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano cha Wizara. Vile vile, Wizara imeendelea kuimarisha tovuti yake ([www.mitm.go.tz](http://www.mitm.go.tz)) ambapo taarifa kuhusu masuala ya viwanda, biashara na masoko zikiwemo bei na fursa za masoko zilizopo ndani na nje ya nchi zinapatikana. Aidha, Wizara inaandaa tovuti ya biashara *National Business Portal* ambayo inategemewa kuharakisha utekelezaji wa biashara mtandao katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia TIRDO, kwa kushirikiana na wafadhili wa mfuko wa *Small and Meduim Enterprises Competitiveness Facility (SCF)*, imewezesha makampuni yapatayo 28 kutengeneza tovuti za kuweza kutangaza biashara zao. Aidha, Mfumo wa Taarifa za Masoko umekuwa ukitimia teknolojia za kisasa za mawasiliano kama vile simu za kiganjani, tovuti, barua pepe, magazeti pamoja na usambazaji wa Taarifa za Masoko ya Mifugo kwa kutumia mfumo wa *Livestock Information Network and Knowledge System - LINKS* na mfumo wa Mazao unaojulikana kama *FAO AgriMarket*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Masoko. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 pia ilibainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji. Kuendeleza Programu Maalum ya Uuzaji Bidhaa Nje (*Export Development Strategy- EDS*), na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mauzo Nje (*Export Development Fund – EDF*), Wizara iliandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje kupitia Mkakati Uganishi wa Biashara Tanzania - *Tanzania*

*Trade Integrated Strategy - (TTIS)* ambao umeanza kutekeleza shughuli zifuatazo; Kupanga hoteli katika madaraja ambapo zoezi hili limekamilika katika mikoa ya Dar es salaam na Pwani na shahada za Nyota 66 zilitolewa kwa mahotelii tarehe 19 Juni 2010.

Vile vile, mafunzo yametolewa kwa vikundi nya wakulima wadogo na wauzaji wa mbogamboga, maua na matunda kuhusu ulimaji kwa ufanisi na utoaji wa mazao bora. Mafunzo haya yanaendelea katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Mafunzo kama haya yataendelea kutolewa katika Mikoa ya Morogoro na Tanga. Aidha, mradi wa kuongeza uzalishaji na ufanisi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi unaendelea kutekelezwa katika mikoa ya Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango umewezesha maandalizi ya kufufua Baraza la Wasafirishaji kwa Njia ya Bahari -*Tanzania Shippers Council*, kwa lengo la kuboresha huduma ya usafirishaji kwenye maji. Kamati mbalimbali za usimamizi na utekelezaji wa TTIS ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Uratibu ya TTIS katika Wizara yangu zimeimarishwa. Aidha, programu kabambe ya utekelezaji wa TTIS yaani *Trade Sector Development Programme (TSDP)* inaanndaliwa. Mpango huu utawezesha kuundwa kwa Mfuko Maalumu - *Basket Fund* wa kuchangia fedha. Pia, mchakato wa kufanyika kwa *Diagnostic Trade Integration Study (DTIS)* visiwani Zanzibar umeanza na utabainisha vikwazo katika maendeleo ya biashara na kutoa mapendekezo ya kukabiliana na vikwazo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa ukusanyaji, utunzaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao ya kilimo, pembejeo, mifugo na mazao ya mifugo umeendelea kuimarishwa na kupanuliwa. Hadi sasa taarifa za mazao 62 zinapatikana katika Wilaya 114. Aidha, taarifa za masoko ya mazao ya mifugo zinazokusanya zimefikia minada 30 katika mikoa 18. Taarifa hizo hiso husambazwa kwa kutumia ujumbe mfupi wa simu za kiganjani, magazeti, radio na mtandao wa kompyuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuandaa Kitabu cha Orodha ya Wanunuzi na Wasindikaji wa Mazao (*Agri-business Directory*) na kuisambaza kwa wadau, Wizara inahuisha na kuboresha taarifa na orodha ya wanunuzi na wasindikaji wa mazao ya kilimo ili kuwapatia wadau taarifa zinazoendana na mahitaji ya wakati. Mkataba wa mzabuni umesainiwa na *inception report* imepokelewa. Ni matarajio ya Wizara kuwa kitabu hicho kitakuwa tayari kabla ya mwisho wa mwaka 2010 na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa mafunzo ya jinsi ya kutumia taarifa mbalimbali za masoko kwa vikundi nya wazalishaji, wasindikaji na wafanyakishara wa kati ili waweze kuzalisha na kuuza kwa kufuata mahitaji ya soko, Wizara imetoa mafunzo ya namna ya kutumia taarifa za masoko kwa Chama cha Wafanyakishara wa Mifugo Tanzania -*Tanzania Livestock and Meat Traders Association- (TALMETA)*. Kwa upande wa mazao ya kilimo, mafunzo yametolewa kwa wafanya biashara wa mazao katika Mkoa wa Dar es Salaam Manispaa ya Temeke (Soko la Tandika na Mbagala).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufuutiliaji wa mahitaji ya taarifa za masoko umefanyika kuitia programu ya kuendeleza mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo;

mkutano wa wakusanya taarifa za masoko ya mazao ya kilimo na mifugo na Warsha ya Maafisa Biashara. Wizara imeendelea kutoa elimu na mafunzo kuhusu utumiaji wa taarifa za masoko kwa wadau kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wamefanya utafiti juu ya namna bora ya kuboresha masoko na biashara ya mifugo kwa kupitia upatikanaji wa taarifa sahihi. Vile vile, Wizara ikishirikiana na Wakala wa Vipimo, imeendelea kutoa elimu maalum ya matumizi ya vipimo sahihi katika biashara. Kutokana na jitihada hizi, sekta binafsi sasa imeanza kuhamasika na kushiriki katika kukusanya taarifa na kuzisambaza kwa njia za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwezesha Halmashauri za Miji na Wilaya kuwa na vitendea kazi vya kukusanya, kuchambua na kutunza taarifa za masoko katika maeneo yao, Wizara imeendelea kuwapatia vitendea kazi wakusanyaji wa taarifa za masoko ya mazao na mifugo walioko katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji 114 kwa upande wa mazao na 18 wa mifugo. Vifaa vinavyotolewa kila mwaka ni pamoa na mavazi maalumu (vatu vya mvua na koti), simu za viganjani na vocha za muda wa maongezi kwa wakusanya taarifa za mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuandaa Mikakati ya kuendeleza soko la ndani. Wizara yangu inakamilisha taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Nchini *TanTrade* itakayoshughulikia Biashara ya ndani na nje. Kanuni za kutekeleza Sheria ya *TanTrade* zimekamilishwa na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutangazwa kwenye gazeti la Serikali kwa utekelezaji. Aidha, katika kuimarishe soko la ndani, uhamasishaji wa jamii kuhusu Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (*BARA*) umefanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan TAMISEMI na sekta binafsi. Kazi hii imefanyika katika Halmashauri 24 zilizoteuliwa kuanza utekelezaji wa Sheria hiyo.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau muhimu ikiwemo TAMISEMI, Sekta Binafsi na VIBINDO imechambua na kukubaliana utaratibu wa utekelezaji wa sheria hii mpya inayotegemewa kuanza Septemba 2010. Wizara inaendelea na utoaji wa mafunzo kwa watendaji wilayani hususan Maafisa Biashara na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupanua na kuimarishe soko la ndani, mwezi Novemba, 2009 *BET* ilifanya utafiti wa biashara katika mipaka ya Zambia na Malawi kwa nia ya kubaini wafanyabiashara na bidhaa zinazohusika katika biashara. Aidha, utafiti huu uliainisha mikakati ya kurasimisha biashara kwa kushirikiana na mamlaka za mitaa katika maeneo hayo. Aidha, utafiti juu ya upatikanaji wa zao la dengu ulifanywa katika mkoa wa Shinyanga kwa lengo la kubaini wazalishaji na kiasi kinachozalishwa kwa ajili ya kuwaunganisha na soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuratibu na kufanya tathmini ya ubora wa Miundombinu ya Masoko, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake hususan *SIDO, TBS*, Wakala wa Vipimo na Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania imefanya tathmini ya miundombinu ya masoko ya ndani na ya mipakani ili kuandaa mikakati ya kuyaendeleza

kwa lengo la kukuza biashara kati yetu na nchi jirani. Aidha, hatua hii ni mojawapo ya mkakati wa makusudi wa kuwaandaa wakulima na wafanyabiashara kutumia fursa ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia mwezi Julai 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeingia mkataba na Chuo Kikuu cha Ardhi kukamilisha mpango kabambe -*Master Plan* ya masoko ya kimataifa maeneo ya Segera na Makambako. Mipango ya kuwezesha ujenzi wa masoko hayo kuititia Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani na Mitaji Vijijini - *Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing* unaotarajiwा kuanza mwaka 2011/2012 inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuweka Mfumo utakaowezesha matumizi ya maghala kama dhamana ya kukopea. Mfumo wa Stakabadhi za Maghala unawezesha mazao kutumika kama dhamana na hivyo kuwawezesha wakulima kupata mikopo toka taasisi za fedha. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha, kukuza na kupanua matumizi ya mfumo huo kwa mazao ya korosho, kahawa, mahindi na mpunga. Pia, mfumo umeanza kutumika katika mazao ya alizeti na ufuta mikoa ya Singida na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhimiza matumizi ya maghala kwa kuhifadhia mazao ya wakulima kama mkakati wa kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno. Wizara kuititia Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania (*TWLB*) na kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuendesha mafunzo ya kuhamasisha jamii kuhusu mfumo huo ambao unasadnia kutunza mazao katika maghala na hivyo kupunguza upotevu. Aidha, *TWLB* imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhimiza ujenzi wa maghala yenye viwango vinavyotakiwa na kutoa leseni za uendeshaji wa maghala na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka mikakati itakayoliwezesha taifa kuhimili ushindani wa biashara kimataifa na kuwa na uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara ya kimataifa katika mazingira ya utandawazi. Wizara imeendelea kushinikiza katika majadiliano mbalimbali kama vile Doha, *EPA*, *EAC* na *SADC* ili tupatiwe masharti nafuu ya masoko ya bidhaa zetu na misaada ya fedha na ufundi. Aidha, Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani zimeendelea kudhibiti ushindani usiokuwa wa haki kibiashara pamoja na kumlinda mlaji. Mpango Mkakati wa Baraza wa miaka minne (2009-2013) ambao umeandalishi na unatarajiwা kuliwezesha Baraza kuongeza ufanisi katika utendaji wake. Aidha, Shirika la Viwango Tanzania – *TBS* limeendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi pamoja na bidhaa za viwanda vyta ndani ikiwa ni pamoja na kufungua kituo kipyaa cha ukaguzi wa ubora wa bidhaa katika eneo la mpakani la Namanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kupambana na uharamia dhidi ya Hakimiliki, Wizara kuititia *COSOTA* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mikoani imekuwa ikiendesha kampeni ya kuzuia utengenezaji na usambazaji wa kanda, *CD* na vitabu bandia. Wakala wa Vipimo imeendelea kushauri wazalishaji wadogo na wa kati kuhusu usahihi katika ufungashaji wa bidhaa kwa kuzingatia vipimo sahihi kwa mujibu wa sheria na hivyo

kuweza kupata soko kwa kuhimili ushindani, hususan katika masoko ya Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti, mafunzo na maendeleo ya teknolojia. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, ilibainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji: Serikali Kutafuta Wabia wa Kuendeleza Miundombinu ya Kiufundi iliyopo nchini yenyewe uwezo wa kutengeneza mashine na mitambo (*Machine Tools*) na Kukuza Uwezo wa Kutengeneza Vipuri Mbalimbali, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) limeingia ubia na Kampuni ya Serengeti *Telecom Group (T)* ili kuendeleza uzalishaji katika Kiwanda cha *KMTC*. Vile vile, *NDC* kwa kushirikiana na *TIRDO*, *CAMARTEC* na *TEMDO* wanaendelea na upembusi yakinifu na utafiti wa soko ili kubainisha mahitaji ya vipuri na mashine ambazo zilikuwa zinazalishwa katika kiwanda cha *KMTC* hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembusi huo utasaidia kuainisha uwezo wa mashine zilizopo sasa, matengenezo - *modifications* yanayohitajika na mapendekezo ya kutengeneza machine mpya za kisasa ili kukidhi mahitaji ya soko. Aidha, utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga utawezesha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya kutengeneza mashine, mitambo na vipuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango wa 2009/2010 na malengo ya mwaka 2010/2011, utekelezaji wa mpango wa Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010 na malengo ya mwaka 2010/2011 kwa kila Sekta na Taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Viwanda. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Rasimu ya kwanza ya Mkakati Uunganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Viwanda Nchini - *Intergrated Industrial Development Strategy and Master Plan - (IIDS & MP)* imekamilika na kupata maoni ya wadau. Maoni hayo yanafanyiwa kazi ili kuboresha mkakati huo ili uweze kukamilishwa na kuanza kutekelezwa. Mkakati huu utawezesha uendelezaji wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda, *Sustainable Industrial Development Policy – (SIDP) 1996 – 2020* sanjari na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Nia ya Mkakati huo ni kuunganisha nguvu za wadau wengine na Serikali katika kutekeleza Sera hiyo kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, uainishaji wa fursa za uwekezaji na miradi ulipewa kipaumbele katika Kanda za Maendeleo za Mtwara, Kati na Kaskazini. Aidha, Wizara katika kutekeleza Mpango Kabambe wa Kuendeleza Viwanda Nchini imeandaa mkakati wa sekta ndogo za viwanda kwa kuainisha sekta za kipaumbele zikiwemo usindikaji wa mazao ya kilimo yatakayozalishwa katika kanda hizo kwa ajili ya malighafi za viwanda kwa Mikoa ya Tanga na Morogoro.

Vile vile tafiti za uanzishwaji wa viwanda vya nyama katika maeneo ya Arusha, Dodoma na Ruvu zimefanyika na tayari ujenzi umeanza. Sekta zilizoainishwa ni zile

zinazotokana na malighafi inayopatikana nchini. Katika ukanda wa kaskazini, sekta za kipaumbele ni za kuzalisha nguo nyama, ngozi na bidhaa za ngozi, maziwa na bidhaa zake na matunda na mbogamboga.

Katika ukanda wa kati, kipaumbele ni kwa sekta ya mafuta ya kula ngozi na bidhaa zake, nguo, saruji na vifaa vingine vya ujenzi vikiwemo nondo na mabati. Katika ukanda wa Mtwara, kipaumbele ni katika sekta za korosho, chuma na bidhaa za chuma, pembejeo na zana za kilimo (mbolea), saruji na kemikali ambazo vinatokana na gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, kama ilivyoanishwa katika aya ya 43 na 54 hapo juu, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, TAMISEMI na Chama cha Wadau wa Sekta ya Ngozi - *Leather Association of Tanzania*- (LAT) imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta ya Viwanda vya Ngozi kwa kuhimiza usindikaji katika viwanda vikubwa vya ngozi. Vile vile, Wizara imeweza utafiti wa masoko ya bidhaa za ngozi na ngozi ghafi katika soko la ndani na nje ya nchi na kuandaa programu ya kuendeleza Vijiji vya Viwanda *Industrial Villages Development Support Programme* katika kanda nne. Kanda hizo ni Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha na Tanga), kanda ya Ziwa (Mwanza, Shinyanga, Kigoma na Mara), Nyanda za Juu na Kati (Mbeya, Dodoma na Singida) na Mashariki (Dar es Salaam, Pwani na Morogoro).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa maonesho mbalimbali kama vile maonesho ya kisekta yanayo julikana kama *Maonesho ya bidhaa za Nguo, Ngozi na Sanaa* ambayo yamefanyika mwezi Mei 2010, pamoja na Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam na Nane Nane ya kila mwaka. Vile vile, jitihada mbalimbali ziliendelea katika kuhamasisha uwekezaji zaidi kwa kusambaza fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi nchini kwa wawekezaji na kuandaa makala *video documentary* kama njia mojawapo ya kuhamasisha uwekezaji na kuonesha maendeleo ya sekta kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, kama ilivyobainishwa kwenye aya ya 47 ya hotuba hii, Wizara imeweza Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) kutekeleza mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na Ngaka, Chuma cha Liganga, mradi wa kasi mpya na mradi wa kujenga kiwanda cha kutengeneza madawa ya kuua mazalia ya mbu kitakachojengwa Wilayani Kibaha Mkoa wa Pwani. Aidha, Wizara imetoe shilingi bilioni 23.4 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, NDC imeendelea kufanya utafiti kuhusu Mradi wa Magadi wa Ziwa Natron ili kuhakikisha athari za mradi huo katika mazingira na kijamii zinaepukwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu. Aidha, NDC kwa kushirikiana na *Geological Survey of Tanzania* (GST) imekamilisha utafiti *Geophysical Surveys* katika eneo linalozunguka Ziwa Natron ili kubaini uwezekano wa kuwepo kwa hazina ya magadi chini ya ardhi - *subsurface soda resource*. Vile vile, NDC imefanikiwa kupata Hati za umiliki wa eneo mbadala la Engaruka lenye ukubwa wa kilomita za mraba 293 kwa ajili ya kufanya utafiti wa magadi kwa njia ya uchorongaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na utata uliojitokeza kuhusu suala la kuharibu mazingira katika mradi wa *Soda Ash* wa Ziwa Natron. Wizara kupitia *NDC* imefanya ziara ya mafunzo (*study tour*) nchini Botswana ili kujifunza jinsi nchi hiyo ilivyofanikiwa kuchimba magadi bila ya kuharibu mazingira. Katika ziara hiyo, ilibainika kuwa Kiwanda cha Botswana *Ash (Pty) (Botash)* kinaendelea na uzalishaji katika eneo ambapo wanyama kama vile pundamilia, swala, ndege aina ya flamingo, pelicans, bata na ndege wengine wengi wanaishi kuzunguka eneo hilo bila tatizo lolote. Hivyo, mradi wa soda ash katika ziwa Natron unawenza kuendelezwa bila kuharibu baionuai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *NDC* imeendelea na jitihada za kufufua kiwanda cha *KMTC* na mradi wa *Nyanza Glass Works*. Aidha, Kiwanda cha *TAMCO* tayari kimekodishwa kwa mwekezaji. Vili vile, jitihada za kuboresha mashamba ya Mpira ya Muheza, Tanga, Kilombero na Morogoro, kama ilivyolelezwa kwenye aya ya 58 katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, kama ilvyobainishwa kwenye aya ya 52, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imekamilisha ujenzi wa eneo maalum la uwekezaji la Benjamin William *Mkapa Special Economic Zone (BWM-SEZ)*. Aidha, wawekezaji waliopewa leseni za kujenga viwanda ndani ya eneo hilo wameshaanza ujenzi. Wawekezaji hao ni *Paper Kraft International Limited, Tembo Agro Limited, Quality Pulse Limited, Steel One Limited pamoja na Rehnat Beverages and Food Limited*.

Aidha, Mamlaka ilitoa leseni 11 kwa *High Grade Cashew Limited, Mount Meru Millers (Singida) Limited, Dardam Limited, APM Gold Limited, Mazava Fabrics EA Limited, Sir Bolt Export Company Limited, Alibaba Tanzania Limited, Poleypipe Limited, De Auto Group Tanzania Limited, Hibao Tanzania Limited* pamoja *Synergy Tanzania Limited* ambao wana viwanda vya uzalishaji katika maeneo mengine ya nje ya eneo la *BWM SEZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama nilivyokwisha eleza awali, Wizara kupitia *EPZA* imeendelea na shughuli za utathimini wa upimaji wa maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji wa *EPZ* na *SEZ* katika mikoa 8 kati ya mikoa 14 iliyotengwa ambapo mazoezi haya yamekamilika katika mikoa ya Mara, Ruvuma, Manyara na sehemu ya eneo la Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya *EPZ* pia imeanza kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano - *Five Years Strategic Plan* uliotengenezwa kwa ushirikiano na Benki ya Dunia. Mpango Mkakati huu ambao pamoja na mambo mengine uliweka bayana utaratibu wa kuendeleza maeneo mapya ya *EPZ* kwa awamu - *Infrastructure Development Strategy*; utaratibu wa kuhudumia wawekezaji - *Facilitation Strategy* na utaratibu wa kuhamasisha uwekezaji wa *EPZ - Promotion Strategy*. Katika kutekeleza mpango huo, vipaumbele vya kuendeleza maeneo ya *EPZ* vimebainishwa. Pia, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau imeanza mchakato wa kuanzisha kituo cha kutoa huduma kwa wawekezaji - *One Stop Service Centre*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea na uhamasishaji wa uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Uwekezaji ya EPZ na SEZ kwa kutumia njia mbalimbali kama vipeperushi, mabango, majarida, tovuti ya Mamlaka ya EPZ, matangazo kwenye vyombo mbalimbali vya habari (magazeti, runinga, radio) na kwa njia ya ushiriki katika maonesho na makongamano ya kibashara yanayofanyika ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia wawekezaji wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Taasisi zake zinazotoa huduma za utafiti na teknolojia kwa sekta ya viwanda kwa kuziongezea uwezo wa kifedha kadri bajeti ya Wizara inavyoongezeka. Taasisi hizo ni *TIRDO*, *CAMARTEC* na *TEMDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (*NBS*), *UNIDO* na Muungano wa Wenye Viwanda (*CTI*) ilifanya tathmini ya Viwanda ili kupata takwimu sahihi za utendaji wa viwanda nchini. Aidha, Wizara imekamilisha uperembaji na tathmini ya makampuni na viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo viko chini ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Rasimu ya Waraka kuhusu taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wawekezaji na mapendekezo ya hatua za kuchukua kwa mashirika ambayo hayajaendelezwa umeandaliwa ili uweze kujadiliwa katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilikutana na wawekezaji kutoka nchi mbalimbali wenye nia ya kuwekeza katika sekta ya viwanda. Wawekezaji hao ni kutoka Madagaska, India, China, Uturuki, Urusi, Japoni, Afrika ya Kusini, Uingereza na Armenia. Aidha, kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 54 wawekezaji 67 wameonesha nia ya kuanzisha viwanda kupitia EPZA. Kwa mfano, kiwanda cha Mazava cha wawekezaji kutoka Madagascar kimeanzishwa mkoani Morogoro na tayari kimeuza nguo katika soko la AGOA za thamani ya Dola za Kimarekani 302 498.49 katika kipindi cha Mwezi Februari hadi 8 Juni 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara iliandaa mkakati wa kuvikuza, kuviendoza na kuvilinda viwanda vyetu vya ndani. Mkakati huu uliwasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi mwezi April, 2010. Wizara iliandaa taarifa kuhusu matumizi ya lazima ya magunia ya katani na ilijadiliwa na IMTC ambayo ilielekeza uandaliwe Waraka kuhusu viwanda vyote ambavyo vilibinafsishwa na havijaendelezwa vikiwemo vya magunia ili maamuzi ya kulinda viwanda yatolewe kwa viwanda vyote vinavyostahili. Waraka wa Viwanda kuhusu mapendekezo ya viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havijaendelezwa umeandaliwa na kuwasilishwa Serikalini kama ilivyoainishwa katika aya ya 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuwasilisha mapendekezo katika vikao vya kurekebisha mfumo wa kodi ya kutaka Serikali kuondoa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye mafuta yanayozalishwa kutohata na mbegu za mafuta zinazolimwa hapa nchini. Tayari Serikali imeondoa kodi hiyo kuanzia July 1, 2010 hivyo napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi kwa

kutekeleza mapendekezo haya. Hatua hii ina lengo la kuvilinda na kuviwezesha viwanda hivyo kuzalisha zaidi na kukidhi soko la ndani na hata kuuza nje ya nchi hususan mafuta ya alizeti ambayo inazalishwa kwa wingi katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara imeandaa waraka wa *BLM* ili kupendekeza kuwekwa kwa mfumo wa usimamizi na udhibiti wa biashara ya chuma chakavu katika hatua mbalimbali za uzalishaji, ukusanyaji, usambazaji, uuzaji (ndani na nje) na uyeyushaji wake kwa kuzingatia upungufu wake, afya na usalama wa wadau, hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa manufaa ya Taifa. Waraka huo uko katika ngazi ya serikali kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Kwa upande wa programu ya MUVI, katika mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha uchambuzi wa kina wa mazao ambayo yataongezewa thamani. Mazao na mikoa husika ni: alizeti na muhogo (Mwanza na Ruvuma), alizeti na bidhaa za mifugo (Manyara), matunda na muhogo (Pwani), alizeti na matunda (Tanga) na alizeti na nyanya (Iringa). Aidha, mikataba kati ya *SIDO* naWataalamu Elekezi imeandalishi na utekelezaji wa mradi unatarajia kuanza rasmi mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *SIDO* imeendelea kutoa huduma ya ushauri na ugani ambapo jumla ya wajasiriamali 15,467 walifikiwa kama ilioainishwa kwenye aya ya 62. Aidha, katika kuendeleza huduma za ugani vijijini kupitia Mkakati wa Bidhaa Moja kila Wilaya *One Product One District*, huduma za ugani katika maeneo mbalimbali ya kiufundi zilitolewa kwa jumla ya viwanda vidogo 456 vilivyopo katika wilaya ambapo kati ya hivyo 152 ni vipy. Uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda hivyo umewezesha kuwepo kwa ajira mpya 1,403 katika viwanda vipy. Asilimia 95 ya viwanda vidogo vilivyoanzishwa au kuendelezwa ni vya sekta ya usindikaji wa vyakula vya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wajasiriamali 9,280 walipata mafunzo ya stadi mbalimbali za biashara na teknolojia katika kipindi cha mwaka 2009/2010. Kati ya hao akina mama 3,898 (42%) walishiriki. Aidha, washiriki 1,578 (17%) walitoka maeneo ya vijijini. Katika jitihada za kuendeleza ujasiriamali kwa wanawake, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine iliandaa maadhisho ya Siku ya Mwanamke Mjasiriamali katika harakati za kukuza maendeleo ya ujasiriamali nchini.

Vile vile, jumla ya miradi mpya ya uzalishaji 306 ilianzishwa vijijini na mashine 694 zimeweza kusambazwa vijijini. Sekta ya viwanda vidogo imefanikiwa kutengeneza ajira 21,196 inayotokana na miradi mpya. Huduma hizi zilitolewa katika mikoa 21 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, *SIDO* iliweza kutoa huduma za masoko kwa wajasiriamali 1,575 kushiriki kwenye maonesho 8 ya bidhaa za wajasiriamali ndani ya nchi. Washiriki 1,313 (62%) walikuwa ni wanawake na jumla ya fedha zilizopatikana kutokana na mauzo zilikuwa ni shilingi bilioni 1.41. Aidha, *SIDO* kupitia Programu ya Maonesho ya bidhaa ya Kikanda iliawezesha wajasiriamali

wadogo 634 kushiriki katika maonesho ya Kanda za Mashariki (Morogoro), Kati (Kigoma), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na kanda Kaskazini (Arusha). Jumla ya bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi milioni 796,109 ziliuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea na zoezi la kukusanya takwimu za sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo - *baseline survey* ambalo linatarajiwu kukamilika mwezi Septemba 2010. Zoezi hilo litawezesha kupata takwimu sahihi kuhusu ukubwa wa sekta na kiwango cha mchango wake katika Pato la Taifa. Aidha, changamoto zinazoikabili sekta hiyo zitabainishwa na takwimu zitakazopatikana zitawezesha Wizara kuanda mkakati wa kuendeleza sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Biashara, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea na jitihada za kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 65. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali kwa nia ya kuhakikisha kuwa Watanzania wanalitumia soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa *SADC*. Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu maeneo muhimu katika kuunda Umoja wa Forodha hasa maeneo yanayohusu Wigo wa Pamoja wa Forodha - *Common External Tariff*; Taratibu za Ukusanyaji na Ugawanaji wa Mapato na utaratibu wa fidia - *Revenue Collection, distribution and Compensatory Mechanism*; Muundo na Sheria - *Legal and Regulatory Framework* na Taratibu za Sera na Urazinshaji - *Policy and Harmonisation*. Baada ya kazi hiyo kukamilika majadiliano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha yanategemewa kuanza rasmi. Aidha, Tanzania inashiriki kikamilifu katika kuanzishwa kwa Itifaki ya Biashara ya Huduma ambayo imeshafikia ngazi ya rasimu ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kupunguza tatizo la mwingiliano wa kikanda ambalo linasababisha migongano ya kisera kwa kanda za *EAC*, *SADC* na *COMESA*, nchi wanachama wa kanda hizo zimekubaliana kuchukua hatua mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye aya ya 67 hapo juu. Kwa kuanzia, Jumuiya hizi tatu zinatekeleza programu ya pamoja yenye lengo la kurahisisha biashara kwa kupunguza na hatimaye kuondoa vikwazo visivyokuwa vya kiushuru (*NTBs*), uanzishaji wa vituo vya mipakani, miradi ya barabara, bandari, na nishati kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeandaa na kuratibu uanzishwaji wa vituo vya pamoja vya mipakani - *One Stop Border Post* - (*OSBP*) kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria - *transit trade* kwa lengo la kupunguza gharama za kufanya biashara. Kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Zambia mazungumzo kuhusu uanzishwaji wa kituo cha pamoja cha Tunduma/Nakonde yalianza mwezi Januari 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya mikutano mitatu iliyohusisha Maofisa wa nchi hizi ilifanyika na kufanikiwa kuandaa Hati ya Makubaliano - *Bilateral Agreement* ambayo imesainiwa na Mawaziri wa Biashara wa nchi mbili tarehe 7 Juni 2010. Kituo hicho kitarahisisha biashara kati ya nchi yetu na nchi za jirani za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Aidha, jitihada za kuanzisha vituo vya pamoja mipakani katika maeneo ya Namanga kwenye mpaka wa Tanzania/Kenya; Rusumo - Tanzania/Rwanda na Sirari- Tanzania/Kenya na Daraja la Umoja Mtambaswala – Tanzania/Msumbiji zimeanza kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu imekamilisha tathmini ya awali ya athari zinazoweza kujitokeza kwa kusaini Mkataba wa *EPA*. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa mkataba wa *EPA* utakuwa na faida na changamoto zake kwa Taifa. Mapendeleko ya tathmini hiyo yalizingatiwa katika kuandaa Waraka uliowasilishwa Serikalini. Hatua hii inakusudia kuhakikisha kuwa Mkataba huo unakuwa chombo kitakachosaidia kuharakisha maendeleo katika Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko hususan Kilimo Kwanza kwa kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kuongeza thamani na ubora wa bidhaa, biashara na masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Mkataba wa Mpito wa *EPA* - *Framework for Economic Partnership Agreement (FEPA)* kati ya nchi za *EAC* na *EU* haukuwezekana kusainiwa kutokana na majadiliano yaliyofanyika mwezi Juni 2010 kutokufikia muafaka. Maeneo yenye changamoto ni pamoja na aya ya 15 ya Mkataba wa Mpito inayokataza nchi za *EAC* kutoza kodi kwa bidhaa ziendazo Jumuiya ya Ulaya baada ya kusainiwa kwa mkataba wa *EPA* na aya ya 16 kuhusu kutoa upendeleo sawa kwa Jumuiya ya Ulaya pale nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zitakapotoa upendeleo zaidi wa kibiashara kwa nchi nyingine na maeneo ambayo majadiliano hayajaanza. Aidha, changamoto nyingine katika majadiliano ya *EPA* ni pamoja na kushughulikia masuala ya uzalishaji duni na vikwazo vingine vikiwemo vya kiufundi na ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilitakiwa kuainisha miradi yote ya maendeleo ambayo itahitaji msaada wa fedha na kiufundi kupitia *EPA*. Jumuiya ya Afrika Mashariki imeandaa jedwali la miradi ambayo imeainisha gharama na kuwasilishwa kwenye Jumuiya ya Ulaya kwa ajili ya kuingizwa kwenye mkataba. Changamoto kubwa ya mahitaji ya *EAC* katika jedwali la miradi yako kwenye miundombinu na ufadhili wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na changamoto zilizoainishwa kwenye aya ya 118, majadiliano ya *EPA* yamepangwa kukamilishwa ifikapo mwezi Novemba 2010 na hatimaye kupangwa kwa tarehe ya kusainiwa mkataba kamili wa *EPA* iwapo makubaliano yatafikiwa kuhusu changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Majadiliano ya Duru la Doha chini ya Shirika la Biashara la Kimataifa yalianza tena mwezi Februari, 2009 kama ilivyoainishwa katika aya ya 69. Aidha, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika

majadiliano ya kibiashara ya Duru la Doha na kwa kushirikiana na kundi la nchi changa (*LDCs*), imeendelea kusisitiza ukamilishwaji haraka wa Duru la Doha bila kuathiri malengo ya nchi changa (*LDC's*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa madhumuni ya kuendelea kupanua masoko na nchi mbalimbali imesaini Mkataba wa Biashara na Uturuki pamoja na Mkataba wa fursa ya soko la upendeleo *Special Preferential Tariff – SPT* unaotolewa na Jamhuri ya watu wa China uliosainiwa Januari 2010. Mkataba huo umeongeza idadi ya bidhaa kutoka 442 mwaka 2009 hadi kufikia idadi ya bidhaa 4,723 kwa mwaka 2010.

Aidha, katika kipindi hicho, Tanzania imeweza kuuza bidhaa za thamani ya Dola za Marekani Milioni 10.449. Vile vile, katika mwaka 2009/2010, Tanzania imeweza kuuza bidhaa za thamani ya Dola za Marekani milioni 1.255 kupitia fursa za upendeleo maalumu wa ushuru na forodha (*SPT*) unaotolewa na serikali ya India kwa nchi zinazoendelea za Afrika ikiwemo Tanzania. Kuhusu fursa ya soko la *AGOA*, Tanzania imeweza kuuza bidhaa za thamani ya Dola za Marekani Milioni 1.542. mwaka 2009 ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa za thamani ya Dola za Marekani milioni 1.925 mwaka 2008. Kushuka kwa mauzo kumechangiwa na athari za m dororo wa uchumi duniani ambao uliathiri manunuzi ya bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Masoko. Kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 80, Wizara imetoa kipaumbele kwa maendeleo ya biashara ya ndani kwa kutambua kuwa uimarishaji wa biashara ya ndani ni msingi wa kukuza biashara ya nje. Aidha, ustawi wa biashara ya ndani umechochea ukuaji wa wafanyabiashara pamoja na wajasiriamali wadogo na wa kati, kuboresha bidhaa na biashara zao na kuendeleza teknolojia mbalimbali. Hivyo, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha kanuni za kutekeleza sheria ya TanTrade ambayo moja ya majukumu yake ni kuendeleza biashara ya ndani.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha Jukwaa la Kitaifa la Maendeleo ya Masoko – *National Marketing Development Forum*. Jukwaa hilo litakuwa ni chombo cha kuwaunganisha wakulima, wafugaji, wafanya biashara na Wizara kwa lengo la kujadili maendeleo na changamoto za sekta ndogo ya masoko

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilifanya ukaguzi wa utekelezaji wa Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972 na Marekebisho yake ya mwaka 1980 katika Mkoa wa Dar es Salaam. Zoezi hilo lililenga kubaini na kutafutia ufumbuzi changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na; kukosekana kwa mfumo madhubuti wa ushirikiano kati ya Taasisi mbalimbali za udhibiti ambazo ni Kituo cha Uwekezaji, Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Halmashauri za Manispaa/Miji/Wilaya, Wizara ya Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana, Shirika la Viwango Tanzania, Mamlaka ya Chakula na Dawa pamoja na Wizara za Serikali na athari zinazotakana na kufutwa kwa

ada za leseni katika ngazi ya Halmashauri. Aidha, changamoto zimeanza kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara - *BARA* ambayo inalenga uunganishaji wa Taasisi mbalimbali kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na BRELA katika utekelezaji wa BARA imefanya tathmini ya kutambua uwezo wa Halmashauri za Wilaya zilizoteuliwa ili kuzijengea uwezo kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo. Zoezi hilo limehusisha Halmashauri za Wilaya 24 ambazo ni Tanga, Babati, Arusha, Moshi, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Temeke, Kinondoni, Ilala, Lindi, Mtwara, Singida, Kibaha, Mbeya, Sumbwanga, Iringa, Njombe na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhamasishaji wa jamii juu ya utekelezaji wa sheria ya *BARA* na uainishaji wa mahitaji ya vitendea kazi pamoja na rasilimali watu katika Halmashauri hizo pia umefanyika. Changamoto zilizojitekeza ni pamoja na kukosekana kwa mfumo imara wa ufuatiliaji wa wawekezaji na wafanyabiashara wanaopewa leseni za uwekezaji pamoja na leseni za biashara, ufinyu wa bajeti kwa Ofisi za Biashara za Halmashauri za Manispaa hizo na elimu duni kwa wajasiriamali kuhusu sheria zinazosimamia uendeshaji biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imekutana na Maafisa Biashara kutoka katika mikoa na Wilaya zote mwezi Aprili 2010 ili kuweka mikakati ya kuendeleza biashara ya ndani na kuondoa vikwazo vinavyokwamisha uwekezaji na biashara nchini kama nilivyoeleza katika aya ya 70. Changamoto zilizoainishwa ambazo tayari zimeanza kufanyiwa kazi ni pamoja na uratibu utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za sekta ya Viwanda Biashara na Masoko katika Mamlaka za Halmashauri za Manispaa/Miji/Wilaya. Wizara imekubaliana na TAMISEMI kuanzisha dawati la uratibu wa shughuli hizi ili kufanikisha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za sekta ya viwanda, biashara na masoko katika ngazi ya Halmashauri. Aidha, changamoto za maendeleo ya kitaaluma na kimuundo ya kada ya Maafisa Biashara ziliainishwa na mikakati ya uboreshaji inaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, ilishiriki kikamilifu kuandaa mwelekeo - *road map* wa kuondoa vikwazo vinavyosababisha Tanzania kuendelea kuperomoka katika tathmini ya kila mwaka ya urahisi wa kuanzisha na kufanya biashara katika mataifa mbalimbali duniani - *Doing Business Report*, 2010. Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na masuala ya usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni, na upatikanaji wa leseni za biashara kutoka katika Halmashauri zote nchini pamoja na uanzishwaji wa masoko ya mipakani na Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi Mpakani - *One Stop Border Post*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Masoko na Bidhaa za Kilimo. Mkakati huu unazingatia Azimio la Kilimo Kwanza na kutoa mwongozo wa maeneo ya kimkakati yatakayopewa kipaumbele na kutengenezewa programu maalumu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kuitia Bodi ya Leseni za Maghala na kwa kushirikiana na wadau wengine wamekuwa wakiendesha mafunzo kwa lengo la kuhamasisha jamii juu ya mfumo huo ambaao unasadia kutunza mazao katika maghala na hivyo kupunguza upotevu, kuongeza thamani ya mazao, kupata bei nzuri na kuwezesha upatikanaji wa mikopo. Aidha, elimu ya matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani imeendelea kutolewa katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tanga, Pwani, Morogoro, Lindi, Mbeya, Kilimanjaro, Mtwara, Ruvuma, Singida, Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama iliyobainishwa katika aya ya 84 na 85, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya mfumo ili kubainisha changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi. Kikosi kazi kimeanzishwa kushughulikia matatizo yatakayojitekeza katika mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Aidha, Wizara imeendelea na juhudhi za kukuza matumizi ya mfumo huu kwa kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu na kupanua wigo wa mazao kama ufuta, alizeti na karanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya maghala mapya 28 yalijengwa na kusajiliwa kwa ajili ya kuendesha mfumo huo kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika (Jedwali Na 10). Aidha, baadhi ya benki za Biashara kama *CRDB* na *NMB* zimekubali kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa maghala. Hatua hii imefanya mikopo inayotolewa na benki kwa wakulima pia kuongezeka na kuwezesha wakulima wengi kufaidika na ongezeko la bei za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imefanya tathmini ya masoko katika mikoa yote ya mipakani. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na uduni wa miundombinu ya masoko katika maeneo ya mipakani, gharama kubwa za ushuru wa mazao kuitia kodi za Halmashauri, ada za usafirishaji wa mazao kuitia kitengo cha ukaguzi wa mazao, vizuizi vya barabarani, msongamano wa magari mipakani na baadhi ya mazao kuzuiliwa kuuzwa nchi jirani.

Aidha, hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuibuliwa kwa miradi ya ujenzi wa masoko katika maeneo ya mipakani kwa Wilaya za Ngara, Karagwe, Misenyi, Tarime na Rorya ambayo itatekelezwa kuitia Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo - *District Agricultural Sector Investment Project –DASIP* unaotekelizwa katika mikoa ya kanda ya Ziwa. Majadiliano yamefanyika kati ya Wizara na wahisani wa maendeleo kuhusu ujenzi wa masoko. Vile vile, Wizara itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu katika ujenzi wa masoko ya mipakani - *Strategic Border Markets* kuitia Programu ya Kuendeleza miundombinu ya Masoko na Usindikaji wa Mazao pamoja na Mitaji - *Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support Programme*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea na jitihada za kuvutia wawekezaji ili kuanzisha miji/vitovu vya kibiashara - *trade hubs* na kukamilisha mazungumzo na wawekezaji ya kuanzisha kituo cha kwanza cha kibiashara cha kimataifa - *Satellite Town and Trade Hub*. Hivyo, Wizara inafanya vikao vya pamoja na sekta binafsi kwa lengo la kujadili, kupata ufumbuzi wa matatizo yanayokwamisha

maendeleo ya viwanda, biashara na masoko na kutoa mapendekezo Serikalini. Aidha, Wizara imeendelea na utaratibu huu ikiwa ni pamoja na kutoa nafasi za kuungana nao kwenye misafara ya nje, kushawishi taasisi za fedha kutoa mikopo yenyenye masharti nafuu ili waweze kuongeza raslimali zao na hivyo kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*) iliongoza msafara wa wafanyabiashara wa Tanzania kwenye maonesho ya kibashara ya Kimataifa ya Afrika Kusini yaliyofanyika mwezi Julai mwaka 2009. Aidha, *BET* iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye maonesho yaliyofanyika sambamba na mkutano wa *AGOA* uliofanyika mjini Nairobi, Julai 2009. Jumla ya makampuni 36 kutoka Tanzania yalishiriki kwenye maonesho hayo na 10 kati ya hayo yalifadhiliwa na *BET*. Katika maonesho hayo mauzo ya papo kwa papo yalifikia Dola za Marekani 16,995.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *BET* ilishiriki kwenye maonesho ya kibashara na uwekezaji ya *Xiamen China* mwezi Septemba 2009 na makampuni manne ya kitanzania yalishiriki. Katika maonesho hayo Tanzania ilitoa mada juu ya Vivutio vya Uwekezaji Vilivypo Nchini. Aidha, *BET* iliongoza ushiriki wa nchi kwenye Maonesho ya 12 ya Kibashara ya Rwanda yaliyofanyika Julai hadi Agosti 2009. Jumla ya wafanyabiashara 16 wa Tanzania walishiriki kwenye maonesho hayo. Maulizo ya bidhaa yalikuwa Dola za Marekani 42,650 na mauzo ya papo kwa papo yalifikia Dola za Marekani 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika aya ya 80 ya hotuba hii, katika mwaka 2009/2010, *BET* imeshiriki kikamilifu katika tafiti za masoko mpakani mwa Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma. Katika kuimarisha Udhibiti wa Ushindani, Ubora wa Bidhaa na Huduma, kwa mwaka 2009/2010, Taasisi za *TBS*, *FCC*, *FCT*, *COSOTA*, *VIPIMO* na *BRELA* zimefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) kwa mwaka 2009/2010 liliendelea kutayarisha viwango vya kitaifa; kutoa leseni za ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazoagizwa kutoka nje. *TBS* iliendelea na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa viwanda vidogo kwa nia ya kuvisaidia viweze kuzalisha bidhaa zenye ubora. Hadi kufikia mwezi Machi 2010, Shirika limeweza kutembelea jumla ya viwanda 161 katika mikoa ya Ruvuma (17), Lindi (4), Mtwara (5), Kilimanjaro (17), Manyara (19), Tabora (33), Dodoma (18), Rukwa (32), Morogoro (4) na Mbeya (12).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa Fedha 2009/2010, Shirika limetoea jumla ya leseni 10,481 za ubora wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Aidha, Shirika limekamilisha maandalizi ya uanzishwaji wa mfumo wa upimaji wa ubora wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja Tanzania - *Preshipment verification of conformity to standards* na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia TBS imeendelea kushirikiana na mashirika ya viwango ya nchi za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda katika uandaaji na uwekaji wa viwango. Aidha, TBS imesaidia kuinua ubora wa bidhaa mbalimbali zinazotengenezwa na wajasiriamali wadogo na wa kati (*SMEs*). Kwa mwaka 2009/2010, jumla ya leseni za ubora wa bidhaa 32 zilitolewa kwa viwanda vya wajasiriamali wadogo na wa kati katika bidhaa za mafuta ya alizeti, chaki, maji ya kunywa, asali, jemu, juisi, mvinyo, maziwa, unga, sabuni, viungo na achari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Shirika linaendelea na juhudi za kuziwezesha maabara zake kufikia viwango vya upimaji vya kimataifa - *Laboratory Accreditation* Lengo ni kuziwezesha maabara za Shirika, kupima sampuli na kutoa taarifa za upimaji -*Test reports* zinazotambuliwa duniani kote. Aidha, Maabara za Kemia na Upimaji Kondomu za Shirika la Viwango Tanzania zilifanyiwa ukaguzi wa kuthibitishwa Umahiri wa Upimaji na wakaguzi kutoka Afrika ya Kusini na kufanikiwa kupata vyeti vya Umahiri wa Utendaji wa kazi zake - *Laboratory Accreditation to ISO 17025* katika upimaji wa maji na kondomu za kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 maabara za *TBS* za Uhandisi Umeme, Uhandisi Mitambo na Uhandisi Ujenzi zimekamilisha miongozo yao ya ubora kulingana na kiwango cha kimataifa *ISO 17025* kabla ya kufanyiwa ukaguzi wa kuthibitishwa Umahiri wa Upimaji wa nyaya za umeme, nondo na saruji. Hatua hizi zitawezesha ripoti za upimaji na ugezi zitakazotolewa na Shirika hili kutambulika Kimataifa na hivyo kuongeza kukubalika kwa bidhaa za Tanzania duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *TBS* imekamilisha Ujenzi wa maabara ya kupima ubora wa pamba na ununuzi wa vifaa vya upimaji kupitia Mradi wa Upimaji wa Ubora wa Pamba - *Commercial Standardization of Instrument Testing of Cotton – CSITC*. Mradi huu unalenga kuinua ubora wa pamba na kuongeza ushindani wa pamba ya Tanzania katika soko la nje. Aidha, mradi huu utahudumia nchi za Uganda, Zambia, Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imefanikiwa kukagua vipimo 730,482 sawa na ongezeko la asilimia 19.24 ikilinganishwa na kiwango cha mwaka wa 2008/2009. Wahalifu 6,210 wa makosa ya vipimo walitozwa faini, kati yao wakiwemo 1,009 wa makosa ya kufungasha kwa mtindo wa lumbesa. Aidha, katika kuhakikisha wafanyabiashara wanatumia vipimo sahihi ili kumlinda mlaji, Wizara kupitia tangazo la Serikali - *Government Notice* namba 233 la tarehe 3 Julai 2009, ilipiga marufuku matumizi ya mizani aina ya *steel yard* baada ya kubainika kuwa mizani hiyo ni rahisi kuchezewa na hivyo kuwaibia wakulima hasa wakati wa ununuzi wa pamba. Utekelezaji wa sheria ya kupiga marufuku mizani aina ya *steel yard* utaanza kutekelezwa msimu wa ununuzi 2011/2012 ili kuruhusu maandalizi ya ununuzi wa mizani ambazo si rahisi kuchezewa na wanunuzi. Hii itaenda sambamba na uimarishaaji wa ukaguzi wa mizani hii wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha 2009/2010, Wizara kupitia Tume ya Ushindani ilipokea na kushughulikia maombi ya muungano wa makampuni katika sekta

za mawasiliano, fedha, bia na madawa baridi na kuyaruhusu kwa kuzingatia kuwa muungano wao hautaathiri ushindani bali kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa biashara katika sekta hizo. Aidha, Tume ilipokea malalamiko yanayohusu ushindani usio sawa katika biashara kutoka katika makampuni mbalimbali. Baada ya uchunguzi, malalamiko mengi yameamuliwa na mengine yanaendelea kusikilizwa na kutolewa uamuvi. Tume imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Ushindani imeendelea na udhibiti wa bidhaa bandia ambapo katika kipindi cha 2009/2010, Tume ilikamata na kuharibu bidhaa bandia zenyenye thamani zaidi ya Shilingi bilioni moja. Kiasi kikubwa cha bidhaa bandia zilizokamatwa zinatoka Bara la Asia. Tume imefanya ukaguzi na kuharibu bidhaa bandia katika maeneo makuu ya kuingilia nchini - *entry points*. Aidha, Tume imeanza kufanya ukaguzi katika mkoa wa Ruvuma (Songea) na imefanikiwa kukamata bidhaa bandia zenyenye jumla ya thamani ya shilingi milioni 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (*FCC*) imeendelea kuelimisha umma na watumishi wake kuhusu masuala ya ushindani, haki na wajibu wa mlaji na vita dhidi ya bidhaa bandia. *FCC* iliendesha semina kwa Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa mwezi Septemba, 2009. Mwezi Machi, 2010, *FCC* kupitia Baraza la Taifa la kumtetea mlaji (*NCAC*) iliendesha semina yenye kauli mbiu “Fedha ziwiiane na Thamani ya Huduma” kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya mlaji duniani Kitaifa. Aidha, Wizara kupitia *FCC* ilifanya tafiti katika masoko ya tumbaku na saruji ili kubaini masuala ya ushindani na kumlinda mlaji kwa lengo la kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuongeza ufanisi wa masoko husika pale tafiti hizo zitakapo kamilika. *FCC* imeendelea kusikiliza na kuhukumu mashauri ya ushindani yaliyofikishwa mbele yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Baraza la Ushindani, Wizara kupitia Baraza hili, kwa mwaka 2009/2010, limeanza kutoa elimu kwa umma juu ya shughuli za Baraza na hatua za kufunga, kusikiliza na kuamua kesi zinazoletwa mbele ya Baraza. Elimu hii ilitolewa kwa Waheshimiwa Madiwani, Wanasheria, Waandishi wa Habari na Jumuia ya Wafanyabiashara. Aidha, kwa lengo la kusogea huduma karibu na wananchi Baraza linatarajia kufunga ofisi za kanda huko Mwanza, Arusha, Dodoma, Mbeya na Mtwara. Baraza pia limesikiliza na kuamua kesi 15 kati ya 36 zilizofunguliwa ambazo hazijaamuliwa bado ziko katika hatua mbalimbali za usikilizwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *COSOTA* iliendelea na jitihada za kujenga uwezo wa Taasisi kwa kuajiri mchambuzi wa Mifumo ya Kompyuta ambapo pamoja na kutunza programu za kompyuta zilizopo, anaendelea na zoezi la kuboresha tovuti ya *COSOTA*. Vile vile, maafisa sita wa *COSOTA* wamepata mafunzo juu ya masuala ya Hakimiliki hapa nchini na katika nchi za Malawi, Kenya, Namibia na Marekani

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *COSOTA* imekusanya mirabaha yenye thamani ya Sh. 109,345,000 na kuzigawa zote kwa wasanii 1,275 wa fani ya muziki, maigizo na maandishi. Aidha, *COSOTA* imetua leseni 523

katika fani muziki, maigizo na maandishi. Vile vile *COSOTA* ilisajili wanachama 1,566 katika fani hizo. Jumla ya kazi 8,994 zimesajiliwa katika fani ya muziki, maigizo na maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, kama ilivyoelezewa kama katika aya ya 85, Wizara kupitia *COSOTA* imeendesha kampeni dhidi ya uzalishaji na usambazaji wa bidhaa bandia na jumla ya kesi kumi (10) zimefunguliwa. Aidha, kanda na *CD* zenye thamani ya Sh milioni 35 ziliharibiwa na vitabu bandia vyatya somo la kemia 297 vilikamatwa katika mji wa Himo vikitokea nchini Kenya. Vile vile, katika usuluhishi wa migogoro ya hakimiliki *COSOTA* imepokea migogoro 45 kati ya hiyo migogoro 26 imesuluhishwa na kwisha na usuluhishi wa migogoro iliyobaki bado unaendelea. Aidha, *COSOTA* imeshafungua ofisi Mikoa ya Mwanza (Kanda ya Ziwa), Mbeya ( Kanda ya Nyanda za Juu Kusini) na Dodoma (Kanda ya Kati na Magharibi).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *BRELA* imeendelea na shughuli zake za kusimamia sheria za Makampuni, usajili wa Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma na Hataza Viwanda. Hadi kufikia Aprili 2010, jumla ya Makampuni 4,325, Majina ya Biashara 8,927, Alama za Biashara na Huduma 605, Hataza 25 na Leseni za Viwanda 83 yalikuwa yamesajiliwa na ushuru wa stempu wa shilingi milioni 137.6 umekusanywa.

Aidha, Wizara kupitia *BRELA* imeendelea na zoezi la kuhakiki makampuni na matokeo ya awali yamebaini kuwa makampuni 13,850 yamejitokeza kuwasilisha taarifa zao za kila mwaka (*Annual returns*). Vile vile, *BRELA* imekwisha weka mfumo wa kuweza kuhakiki majina ya Makampuni na majina ya Biashara - *Online Name Search* kwenye tovuti yake [www.brela-tz.org](http://www.brela-tz.org), ikiwa ni pamoja na kumwezesha mteja kupata fomu za usajili na kufanya malipo kwa njia ya mtandao. Vile vile, *BRELA* imeshirikiana na Wizara katika kutoa elimu ya *BARA* kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 85.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uimarishaji wa Mafunzo, Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia, kwa mwaka 2009/2010, Taasisi za *TIRDO*, *TEMDO*, *CAMARTEC*, na *CBE* zimefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *TIRDO* imebuni na kutengeneza kaushio la mihogo aina ya *tunnel drier* lenye ukubwa wa mita za mraba 14.64 kwa matumizi ya kibashara na linatumia mwanga wa juu. Kaushio hilo limekwisha fanyiwa majoribio ya ufanisi katika kukausha na lina uwezo wa kukausha kilo 750 za unga wa muhogo kwa siku. Makaushio mawili ya mbogamboga na matunda yalitengenezwa kwa wajasiriamali wa Wilaya ya Chunya na kupewa mafunzo. Wajasiriamali 53 walifundishwa juu ya matumizi ya vifaa vya uzalishaji wa bidhaa za vyakula kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Iringa. Katika Wilaya ya Mbinga, wajasiriamali 32 walifundishwa juu ya uzalishaji wa unga wa muhogo kwa kiwango cha hali ya juu na walipewa mashine nne za kisasa kwa ajili ya uzalishaji wa unga huo. Wazalishaji 132 kutoka katika Mashirika na viwanda katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Lindi wamepata mafunzo juu ya – *good manufacturing practices (GMP)* na mfumo wa ufuutiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *TIRDO* ilichukua jumla ya sampuli 162 za vyakula na maji katika makampuni na viwanda ili kuongeza ubora na usalama wa bidhaa za maji na vyakula. Aidha, shirika lilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 322 katika mikoa ya Kilimanjaro, Iringa, Arusha na Dar es Salaam hususan akina mama yanayohusu ukulima na usindikaji wa uyoga kama njia ya kujipatia kipato na pia chakula chenye virutubisho vya mwili. Vile vile shirika limeendelea kutoa huduma ya uzalishaji mbegu za uyoga (*spawn*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *TIRDO* ilitoa mafunzo kwa mafundi - *technicians* 13 kwenye fani ya uyeyushaji vyuma -*foundry technology* kutoka viwanda vidogo vifuatavyo: Kitutu Pattern Making, *Eagle Foundry Works, Ngosha Blacksmith Co., Goma Investment, Durable Casting Materials* na *M.M. Foundry Works* katika mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, shirika liliendesha mafunzo kwenye teknolojia ya uchomeleaji wa vifaa vya kutengeneza bidhaa za vyakula - *stainless steel welding technology* kwa wajasiriamali 40 katika manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/2010, Maabara ya chakula -*Food and Microbiology* ya *TIRDO* imethibitishwa kimataifa katika kutoa huduma bora za ukaguzi wa vyakula na mazao ya viwandani katika njia tano za ukaguzi na *SANAS - South African National Accreditation Systems*. Uthibitisho huu umepatikana mwezi Novemba, 2009. Wataalam 34 wamepata mafunzo katika *standard* ya *ISO-17025:2005* na ya - *Good Laboratory Management Practices*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, *TIRDO* imetoea mafunzo kwa wadau wa sekta ya kahawa na sekta ya samaki wabichi katika matumizi ya mfumo wa ufuutiliaji wa bidhaa -*traceability* kwa kutumia TEKNOHAMA. Aidha, Mkoani Mwanza, viwanda vine na mialo miwili inayosimamia ubora wa samaki kwa ajili ya kuuza nje ya nchi ilihakikiwa na kupata mafunzo. Viwanda 87 vimehamasishwa na kupatiwa mafunzo ya matumizi ya huduma za *global standard one* (GS 1) kwenye mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Ruvuma, Mbeya, Mtwara, Lindi, Iringa, Mwanza, Kagera na Mara. Jumla ya wafanyakazi 120 pamoja na uongozi wa viwanda walihuksika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TIRDO* imeshiriki katika mkutano wa kitaifa uliofanyika Dar es Salaam kwa wadau wa GS 1 uliohusisha washiriki 67 wakiwepo watengenezaji, wasambazi na wauzaji pamoja na vyama vyao *TCCIA, CTI, TPSF, TWCC*. Mkutano uliunda kamati itakayosimamia mchakato mzima wa kuanzisha chombo hicho hapa nchini pamoja na maandalizi kwa ajili ya kuijandikisha Brussels, Ubeligiji unaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *TIRDO* imefanya ukaguzi wa uchafuzi wa hewa, maji na udongo katika makampuni makubwa manne (4) yanayohusisha uathirikaji wa wafanyakazi kwa kelele za *mashine* na vumbi. Kampuni tano zimefanyiwa ukaguzi usio wa uharibifu -*non-destructive testing* ili kuangalia ubora wa matenki ya petroli, machemshio (*boilers*) na bomba za mafuta. Aidha, Shirika limetoea huduma ya ukaguzi wa vifaa vya kihadisi bila kuharibu – *non*

*destructive testing* kwenye makampuni matatu (3) ya mafuta, moja la uzalishaji bia na jengo la kale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Kituo cha Kueneza Teknolojia Rahisi Vijiji, *CAMARTEC* imeendelea kuhamasisha wajasiriamali kuchukua na kueneza teknolojia zilizokwisha kuthibitika ikiwemo majiko, mashine ndogo za kukamua mafuta, mikokoteni ya ng'ombe na punda. Pia, Kituo kimeendelea kujenga miundombinu na kuagiza mashine za karakana katika kujipanga upya baada ya kuhamia eneo la Themi Arusha. Programu nyingine zinazoendelea ni kujenga karakana ya uzalishaji wa mlolongo - *flexible assembly line* kuimarisha TEKNOHAMA na shughuli za majaribio. Kwa kuanzia, karakana ya uzalishaji wa mlolongo imekamilisha uundaji wa trekta ndogo sita za matumizi zaidi ya moja (*multi purpose*) lililobuniwa na *CAMARTEC*. Aidha, matrekta haya madogo kwa mara ya kwanza yataoneshwa kwenye maonesho ya 34 ya *DITF* na Nane Nane katika kanda ya Ziwa, Kati, Kaskazini na Mashariki. *CAMARTEC* pia inaendeleza programu ya viatamizi ili kueneza kwa kasi teknolojia zilizokwishathibitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Taasisi yake ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo *TEMDO* imeendelea kutoa huduma katika Kiatamizi cha Teknolojia na Biashara kilichopo *TEMDO*. Jumla ya wajasiriamali wa kiatamizi wapatao ishirini (20) wamesajiliwa kati yao saba wakiwa ni wanawake. Aidha, *TEMDO* inatoa kipaumbele kwa wateja wanaozalisha siagi ya karanga, kusindika matunda na nishati mbadala. Nia ni kuwezesha wajasiriamali katika maeneo hayo matatu kukuza miradi yao ifikie viwanda vyatani vyanje uwezo wa kuuza bidhaa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia *TEMDO* imeendelea kubuni mitambo ya kukamua na kusindika mafuta yatokanayo na mbegu za mafuta; kusindika matunda na nishati mbadala. Vile vile *TEMDO* imeendelea kuboresha na kuendeleza mtambo salama wa kuchoma taka za hospitali – *hospital incenerator*. kusambazwa kibiashara na wajasiriamali ikiwa ni pamoja na *SIDO*. Mtambo huu unalinda mazingira kwa kuharibu kabisa taka mbaya za hospitali bila kutoa moshi mchafu. Mtambo huu umefungwa katika Hifadhi ya Ngorongoro na lengo ni kufunga mitambo ya aina hii katika hospitali nyingi nchini.

Aidha, *TEMDO* imeendelea kufanya majaribio ya teknolojia ya kutengeneza mkaa unaotokana na vumbi la mkaa, vumbi la mbao pamoja na mkaa unaotokana na mabaki ya mimea kama vile *jatropha* na kutoa huduma ya ushauri na mafunzo kwa viwanda vyatani, sukari, bia, chai, kahawa, pamba, katani na vifaa vyatani umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) imenunua eneo lenye ukubwa wa ekari 38.2 huko Nzuguni, Dodoma ili kujenga madarasa, ofisi, kumbi za mihadhara na maktaba. Juhudi zinaendelea kuboresha Kampasi ya Dar es Salaam na Kampasi ya Mwanza. Aidha, kampasi ya

Mwanza inatarajiwa kujengwa katika Wilaya ya Ilemela na kiasi cha shilingi milioni 50 kimelipwa na Wizara kama sehemu ya fidia ya eneo la hekta 8.2. Vile vile, Chuo cha *CBE* kimekuwa na ongezeko la udahili wa wanachuo 7,539 ikiwa ni ongezeko la wanachuo 532 ambayo ni sawa na asilimia 7.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali, mwaka 2009/2010 *CBE* kwa kutumia mitaala yake mipy, imeingiza somo la ujasiriamali katika ngazi zote za mafunzo ili kuwajengea wahitimu wake uwezo wa ujasiriamali na kuwapa mbinu mbalimbali za biashara. Aidha, Chuo kimetayarisha mitaala ya kozi ya ujasiriamali katika ngazi ya cheti na diploma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2009/2010, *CBE* imeimarisha mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEKNOHAMA katika programu zake zote. Aidha, Chuo kwa kutumia mitaala mipy imeingiza somo la kompyuta (*ICT*) katika ngazi ya Cheti na Stashahada ili kuwawezesha wahitimu wake kukabiliana na changamoto nyingi zilizopo katika soko huru la biashara. Vile vile, Chuo kilikamilisha mradi wa kuweka mtandao wa mawasiliano - *Fibre Optic Network* na kuunganisha kompyuta zote katika maabara na ofisi katika Kampasi zake mbili ambazo ni Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, *CBE* inatarajia kujenga jengo la mizani na vipimo lenye kumbi za miadhara pamoja na ofisi za wahadhiri na kuimarisha maabara ya mizani na vipimo. Tayari Mtaalamu Elekezi wa kushauri amepatikana na michoro na - *Bill of Quantity* imeandalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala mtambuka. Kudhibiti Rushwa Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea na harakati za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kutoa mafunzo ya elimu ya huduma kwa mteja, Maadili ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa watumishi wake. Aidha, Wizara imetoea mafunzo kwa waajiriwa wapya 19 kuhusu umuhimu wa kutekeleza majukumu yao kiadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Janga la UKIMWI, kuhusu janga la UKIMIW. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, wafanyakazi wameendelea kukumbushwa umuhimu wa kujikinga na UKIMWI na kupima afya zao kwa hiari kila mara. Aidha, huduma ya lishe, virutubisho - *food supplements* na nauli ya kwenda hospitali imeendelea kutolewa kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Vile vile, kwa kushirikiana na *TACAIDS* na wadau wengine, Wizara imetoea elimu ya mbinu za kujikinga pamoja na kutoa kinga mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Sera na Sheria za Utunzaji na Usimamizi wa Mazingira kwa kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa wadau wa sekta mbalimbali, zikiwemo za ngozi, nguo na chuma ambazo zinalalamikiwa kwa kiasi kikubwa na wananchi kwa kuchafua mazingira. Kama ilivyoainishwa katika aya ya 160, *TIRDO* imechangia kulinda mazingira kwa

kubuni na kuendeleza mtambo salama wa kuchoma taka za hospitalini – *hospital waste incinerator*. Aidha, *TEMDO* imebuni na kuendeleza mtambo wa kutengeneza mkaa kutohana na taka za mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jinsia, Katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuwajengea uwezo maafisa wa Wizara na Taasisi zake wa kubuni miradi na kufanya uchambuzi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia jinsia - *Gender Mainstreaming*. Aidha, Wizara na Taasisi zake imewajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Jinsia wa kuratibu programu zinazolenga kukabiliana na changamoto za kijinsia zinazozua maendeleo ya kiuchumi - *Gender and Economic Growth*. Pia, Wizara kwa kutumia Mtaalamu Elekezi ilifanya “*Gender Audit*” ya sera na programu za Wizara ili kubaini maeneo yanayohitaji maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Mwaka 2010/2011, Mpango na malengo ya utekelezaji kwa Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko katika mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda, Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 Wizara imelenga kutekeleza yafuatayo katika Sekta ya Viwanda:-

(a) Serikali kupitia *NDC* itawekeza kwenye viwanda nyeti na vya msingi (*Strategic and basic Industries*) ambavyo wawekezaji hawana motisha wa kuwekeza kwa kuwa viwanda hivyo huchukua muda mrefu kupata faida na vile ambavyo Serikali imeamua kutokuvibinafsisha ikiwa ni pamoja na *GTEA*.

(b) Kuendelea kutoa kipaumbele kwa Viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo;

(c) Kuendeleza zoezi la uwekezaji katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na mradi wa magadi (*soda ash*) wa ziwa Natron na tafiti za miradi mingine ikiwemo uanzishaji wa viwanda vya mbolea katika Kanda za Maendeleo;

(d) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati Uganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini hususan kuandaa mikakati ya sekta ndogo za viwanda;

(e) Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vipyta vya kusindika ngozi na bidhaa za ngozi;

(f) Kuandaa na kutekeleza programu mahsusini inayolenga kujenga miundombinu (*Industrial Villages/Clusters*) itakayowezesha viwanda vidogo na vya kati *SME* kuongeza uzalishaji wa bidhaa;

(g) Kuhamasisha Watanzania kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu ikiwa ni juhudhi mojawapo za kukuza soko la ndani na ajira; na

(h) Kutoa mafunzo ya uzalishaji unaozingatia hifadhi na kulinda mazingira katika shughuli za usindikaji na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, malengo ya Shirika la Maendeleo *NDC* ni pamoja na kuweka kipaumbele katika utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ifuatayo:-

(a) Kukamilisha Mchakato wa kutafuta wawekezaji katika miradi ya Mchuchuma na Liganga;

(b) Kuendeleza mradi wa magadi wa Ziwa Natron katika kukamilisha tafiti zinazohitajika;

(c) Ujenzi wa Maeneo ya Viwanda (Tanga, Pwani na Kilimanjaro);

(d) Uendelezaji wa kilimo kwa ajili ya malighafi za viwandani;

(e) Utekelezaji wa Kanda za Maendeleo za Mtwara (*Mtwara Development Corridor*) na Kati (*Central Development Corridor*) kwa kuendelea kuibua fursa za uwekezaji;

(f) Kuboresha njia bora za kuzalisha dhahabu katika mpango wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo;

(g) Kusimamia ukamilishaji wa tafiti za mwisho za mradi wa makaa ya mawe wa Ngaka kwa kushirikiana na kampuni ya *Tancoal Energy Limited* ili kuanza uzalishaji wa makaa ya mawe na umeme;

(h) Kukamilisha tafiti na uanzishaji wa viwanda vya nyama katika Mikoa ya Pwani, Arusha na Dodoma; na

(i) Kuanzisha kiwanda cha kutengeneza madawa ya kuua mazalia ya mbu wilayani Kibaha kwa kushirikiana na kampuni ya LABIOFAM kutoka CUBA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, malengo ya *EPZA* ni pamoja na kuweka kipaumbele katika utekelezaji na ukamilishaji wa yafuatayo:-

(a) Kukamilisha zoezi la ubainishaji wa maeneo ya *EPZ* na *SEZ* katika Mikoa sita iliyobaki. Mikoa hiyo ni Dodoma, Tabora, Rukwa, Singida, Iringa na Shinyanga;

(b) Kujenga mfumo wa kituo kimoja cha utoaji huduma kwa wawekezaji - *One Stop Service Centre* katika eneo la *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone* kitakachotoa huduma za papo kwa hapo kwa wawekezaji hivyo kupunguza urasimu;

(c) Kukamilisha taratibu za kutungwa sheria itakayounganisha mifumo ya *EPZ* na *SEZ* na kuanzisha mfumo mpya wa Maeneo Maalumu ya Uwekezaji utakaojulikana kama *Economic Development Zone*;

(d) Kukamilisha taratibu za umiliki na kuanza ujenzi wa miundombinu katika eneo la kipaumbele la Bagamoyo *Economic Development Zone*; na

(e) Kuendelea kuhamasisha wawekezaji wa kujenga miundombinu na wale wa kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, malengo ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ni pamoja na:-

(a) Kuendelea kujengea uwezo *SIDO* ikiwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya Sheria husika;

(b) Kukamilisha ukusanyaji wa takwimu sahihi za Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo -*baseline survey*;

(c) Kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani katika maeneo yote waliko wajasiriamali hasa vijijini;

(d) Kuhakikisha teknolojia zinazofaa zinatafutiwa utaratibu wa kuzalisha kwa wingi na kuzisambaza kwa watumiaji;

(e) Kutoa ujuzi maalumu wa kubadilisha malighafi hasa mazao ya kilimo na mifugo kuwa bidhaa;

(f) Kujenga miundombinu itakayowafanya wajasiriamali hasa wa vijijini kupata sehemu za kufanya kazi;

(g) Kuwawezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma zao kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambaza habari za kibiashara na sehemu za kuonyeshea bidhaa za wazalishaji wadogo; na

(h) Kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapojidhihirisha kuhitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, malengo ya *SIDO* ni pamoja na kuweka kipaumbele katika utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ifuatayo:-

(a) Kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani katika maeneo yote waliko wajasiriamali hasa vijijini;

- (b) Kuhakikisha teknolojia zinazofaa zinatafutwa, utaratibu wa kuzibalisha kwa wingi, na kuzisambaza kwa watumiaji;
- (c) Kutoa ujuzi maalumu wa kuzibadilisha malighafi hasa mazao ya kilimo na mifugo kuwa bidhaa;
- (d) Kujenga miundombinu itakayowafanya wajasiriamali hasa wa vijijini kupata sehemu za kufanya kazi;
- (e) Kujenga msingi na kusaidia utengenezaji wa bidhaa mpya kutokana na mawazo ya wajasiriamali binafsi;
- (f) Kutoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara;
- (g) Kuwawezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma zao kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara na kutengeneza sehemu za kuonyeshea bidhaa za wazalishaji wadogo;
- (h) Kutoa ushauri kuhusu huduma za kifedha; na
- (i) Kujenga uwezo wa uzalishaji wa zana za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Biashara. Katika mwaka 2010/2011, malengo ya Sekta ya Biashara ni pamoja na:-

- (a) Kuhamasisha utumiaji wa fursa za masoko ya ndani ya nchi mbalimbali, Kikanda na Kimataifa;
- (b) Kuendeleza juhudzi za kukuza uhusiano wa kibiashara baina ya nchi na nchi;
- (c) Kuendelea kushiriki kwa lengo la kukamilisha majadiliano ya biashara ya Kimataifa ya Doha na kuhakikisha kwamba maslahi ya Tanzania yanatiliwa maanani katika makubaliano yatakayofikiwa;
- (d) Kuendelea kushiriki katika majadiliano ya kukamilisha Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (e) Kuendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ;
- (f) Kuendelea kushiriki mchakato wa kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Nchi za *SADC* na majadiliano ya kuanzishwa kwa Itifaki ya Biashara za Huduma ya *SADC*;

- (g) Kukamilisha majadiliano ya Ubia wa Uchumi (*EPA*) kati ya *EAC* na *EU*;
  - (h) Kuendelea kuimarisha vituo vya biashara kwenye nchi mbalimbali hususan vituo vya Dubai na London;
  - (i) Kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kwa ujumla kuhusu fursa mbalimbali za masoko baina ya nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa;
  - (j) Kuendelea kushiriki katika majadiliano ya kuanzishwa kwa eneo huru la biashara kwa kanda za *COMESA*, *SADC* na *EAC (Tripartite)*;
  - (k) Kupeleka Waambata wa Biashara nchini Marekani na China; na
    - (l) Kuandaa na kukamilisha *Trade Sector Development Programme (TSDP)*; kufanyika kwa *Diagnostic Trade Intergration Study (DTIS)* visiwani Zanzibar; na kufanyika tathmini ya uwezo wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi za Serikali (*MDAs*) katika kutekeleza majukumu yanayohusu biashara.
- Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*) itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-
- (a) Itaendesha Maonesho ya Kimataifa ya 34 ya Dar es Salaam (*DITF*);
  - (b) Itaongoza ushiriki wa nchi kwenye maonesho ya kimataifa ya biashara ya Nampula-Msumbiji, Nairobi-Kenya, Bulawayo- Zimbabwe, Kigali-Rwanda, Lubumbashi-Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, Mzuzu-Malawi na Bujumbura-Burundi;
  - (c) Itafanya utafiti wa biashara za mpakani mwa Tanzania na Uganda na Tanzania na Burundi ili kubaini wafanyabiashara na bidhaa zinazouzwa na kununuliwa, mfumo wa biashara na kubaini mikakati ya kurasimisha biashara katika maeneo haya.
  - (d) Itaendelea na mradi wake wa Mafunzo ya Biashara na mbinu za kuuza bidhaa na huduma nchi za nje (*Export Readiness Training*) kwa wafanyabiashara wadogo katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha;
  - (e) *BET* itaendesha mradi wa Mafunzo ya Biashara (*Training for Trade*) kwa wafanyabiashara wa kati katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha; na
  - (f) *BET* itaendelea kuongoza ushiriki wa nchi kwenye maonesho ya muda mrefu ya ulimwengu (*Expo Shang'hai 2010*) yanayofanyika jijini Shang'hai-China.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Sekta ya Masoko itaendelea kushughulikia upatikanaji na utumikaji wa fursa za masoko ya Kikanda na Kimataifa na kuimarisha mikakati ya kuimarisha soko la ndani. Ili kutimiza azma hii Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukamilisha Kanuni za *TANTRADE* kwa lengo la kuimarisha soko la ndani na nje ya nchi;
  - (b) Kukamilisha Mkakati wa kutekeleza Sera ya Kuendeleza Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo;
  - (c) Kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni na kutekeleza mikakati ya masoko ya ndani, Kikanda na Kimataifa;
  - (d) Kuendeleza na kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko;
  - (e) Kuratibu uaandaaji wa Mpango Kabambe wa masoko ya Kimataifa ya mazao na bidhaa za kilimo;
  - (f) Kufanya tathmini ya matumizi ya taarifa, maonesho na uboreshaji wa miundombinu ya masoko.
- (g) Kuendeleza miundombinu ya masoko ya ndani na mipakani pamoja na Vituo vya Pamoja vya Ulagazi Mipakani - *One Stop Border Post*.
- (h) Kuwaelimisha wadau kuhusu maendeleo na fursa za masoko zilizopo ndani ya nchi na nje;
  - (i) Kufanya utafiti - *Market Intelligence* wa masoko;
  - (j) Kuimarisha uwezo wa Halmashauri na Manispaa wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko;
  - (k) Kuendeleza utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kama njia mojawapo ya kujikinga na mporomoko wa bei ya mazao na upotevu wa mazao;
  - (l) Kuendeleza jitihada za kukuza soko la ndani kwa kukuza matumizi ya mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini;
  - (m) Kuboresha ubora wa bidhaa, kupanua wigo wa masoko, upatikanaji wa mitaji, usambazaji wa teknolojia zinazofaa kwa lengo la kuongeza tija;
- (n) Kushirikiana na sekta binafsi kwa lengo la kutekeleza azimio la Kilimo Kwanza;
- (o) Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara;
- (p) Kuwezesha uanzishwaji na uimarishaji wa Kilimo cha Mkataba;

- (q) Kuhamasisha biashara na kutumia fursa za masoko; na
- (r) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje (*EDS*) na Mpango Uunganishi wa Biashara Tanzania (*TTIS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, malengo ya Bodi ya Leseni za Maghala ni pamoja na:-

- (a) Kuendelea kutoa elimu ambayo itasaidia kuongeza wigo kuhusu Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani;
- (b) Kushirikiana na vyuo na taasisi mbalimbali za elimu kuanzisha mitaala ya kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani;
- (c) Kuimarisha na kuhuisha mfumo wa ukusanyaji, utunzaji, utumiaji wa taarifa za Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ili ipate nafasi ya kuendeleza Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani;
- (d) Kuongezea mazao thamani ili kuongeza wigo wa soko na hasa Soko la Afrika Mashariki;
- (e) Kushirikisha Sekta Binafsi na mamlaka husika kuwekeza katika miundombinu ya maghala na barabara;
- (f) Kubuni mbinu bora za kisasa za soko la uuzaji wa mazao yaliyo hifadhiwa kwenye maghala mfano *Commodity Exchange Market*;
- (g) Kutoa leseni kwa maghala yenye uwezo wa kuhifadhi kati ya tani 3000 na kuendelea ili kupunguza gharama ya uendeshaji na usimamizi;
- (h) Kuhakiki Waendesha Maghala na kusaini *Performance Guarantee* kabla ya kupewa leseni ya kuendesha maghala; na
- (i) Kupitia upya baadhi ya taratibu zilizowekwa na kuziongeza uwezo wa kisheria ili zitekelezeke kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma. Malengo ya Shirika la Viwango Tanzania kwa mwaka 2010/2011 ni pamoja na:-

- (a) Kutoa mchango katika sekta ya ufungashaji wa bidhaa kupitia kituo cha Ufungashaji (*Packaging Technology Centre*);

- (b) Kutoa mafunzo ya huduma za kupima sampuli za viwanda vya ufungashaji na kuhakiki vifungashio (*packaging materials*) kwa bidhaa zile zinazotoka nje ya nchi;
- (c) Kupanua wigo wa nyanja za uthibitishwaji wa umahiri wa maabara za Ugezi, Chakula, Kemia na Nguo;
- (d) Kuongeza idadi ya leseni za ubora wa bidhaa kwa viwanda vidogo;
- (e) Kuboresha miundombinu yake na nyenzo zingine zinazotumika kupima na kudhibiti ubora wa bidhaa mbalimbali;
- (f) Kutayarisha viwango vya taifa vikiwemo viwango vya sekta ya huduma pamoja na utoaji wa leseni za ubora wa bidhaa;
- (g) Kutoa vyeti vya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje; na
- (h) Kupima sampuli za bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Baraza la Ushindani kwa mwaka 2010/2011 ni pamoja na:-

- (a) Kutekeleza Mpango Mkakati wake wa miaka minne (2009- 2012) ya kujiimarisha;
- (b) Kusikiliza kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa Udhibiti wa Ushindani na Ubora wa Bidhaa na Huduma;
- (c) Kujenga uwezo zaidi wa Baraza kushughulikia kesi hizo;
- (d) Kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza na umuhimu wake;
- (e) Kuimarisha Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003; na
- (f) Kujenga uwezo wa kuhimili ushindani wa biashara ya kimataifa na kufaidika na mfumo wa biashara ya kimataifa katika mazingira ya utandawazi kwa kuhakikisha ushindani sawa na udhibiti wa haki unakuwepo katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2010/2011, Wakala wa Vipimo itaendelea na:-

- (a) Kuhakikisha matumizi ya vipimo sahihi katika biashara, sekta ya afya na mazingira;
- (b) Kuendelea kuinua uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya Vipimo katika uzalishaji, biashara na huduma za jamii;

- (c) Kuwashauri wazalishaji wadogo na wa kati kuhusu usahihi katika ufungashaji wa bidhaa ili kuhakikisha bidhaa zao zinafungashwa kwa mujibu wa sheria na hivyo kuweza kupata soko kwa kuhimili ushindani hususani katika masoko ya Kikanda na Kimataifa;
- (d) Kuweka stika maalum kwenye pampu za kuuzia mafuta ili kudhibiti wateja kuuziwa kiwango cha mafuta kisicho sahihi; na
- (e) Kuhakiki mita za mafuta bandarini (*KOJ flow meters*) ili kuhakikisha kuwa kodi sahihi kwa kiasi halisi cha mafuta kilichoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2010/2011, Tume ya Ushindani itaendelea na:-

- (a) Kuendelea na udhibiti wa bidhaa bandia;
- (b) Kukabiliana na makampuni yanayokula njama kwa pamoja kwa kupanga bei na mambo mengine yanayoathiri ushindani; na
- (c) Kufanya tafiti zenye kuongeza tija na ufanisi katika masoko, kutoa elimu kwa mlaji juu ya haki na wajibu wake na kumlinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, *COSOTA* itaendelea kufanya yafuatayo:-

- (a) Kuhamasisha jamii kuhusu Hakimiliki na Hakishiriki;
- (b) Kufanya ukaguzi na ukamataji wa *CD* bandia kila mkoa Tanzania bara; na
- (c) Kutoa elimu na kufanya mikutano na vyama vya wafanyabiashara Mikoani juu ya utekelezaji wa sheria ya Hakimiliki kwa kukagua na kukamata bidhaa bandia katika fani ya sanaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, *BRELA* itaendelea na:-

- (a) Kurahisisha na kuboresha taratibu za utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo ya *TEKNOHAMA*;
- (b) Kupanua wigo wa watumiaji wa huduma na kupeleka huduma hizo karibu na wateja, *BRELA* kwa kushirikiana na *TCCIA* itatekeleza mpango wa kutoa baadhi ya huduma zake Wilayani;
- (c) Kuhamasisha na kuelimisha watumishi na watumiaji wa huduma za Wakala, ili kuharakisha urasimishaji wa Biashara;

(d) Kuendeleza elimu juu ya umuhimu wa matumizi bora ya Miliki Ubunifu ili kuwawezesha wananchi kutumia fursa zilizopo katika raslimali hizo;

(e) Kukamilisha upitiaji wa sheria za Miliki Ubunifu, Majina ya Biashara, Leseni za Viwanda na kuendelea kutathmini utekelezaji wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 ili iweze kwenda na mabadiliko yanayoendelea sasa hivi duniani;

(f) Kuandaa mfumo mkakati wa Miliki Ubunifu Tanzania - *Intellectual Property Strategy Framework*;

(g) Kuimarisha ushirikiano uliopo katika eneo la miliki ubunifu na mashirika ya nje kama vile Shirika la Miliki Ubunifu la Kanda ya Afrika *African Regional Intellectual Property Organization (ARIPO)*, Shirika la Miliki Ubunifu la Dunia *The World Intellectual Property Organization, (WIPO)* na Shirika la Biashara Duniani *World Trade Organization, (WTO)*;

(h) Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi - *bilateral arrangements* katika maeneo ya Miliki Ubunifu na maeneo mengine ambayo *BRELA* inayasimamia; kutekeleza sheria ya usajili wa shughuli za Biashara (*BARA*) kwa kushirikiana na Halmashauri za Serikali za Mitaa *Local Government Authority (LGA)*; na

(i) Kupata kiwanja au jengo kwa ajili ya ofisi za Wakala kwa ajili ya utoaji huduma na kuiwezesha wakala kutumia tekinolojia ya kisasa katika kutoa huduma zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti na maendeleo ya teknolojia na mafunzo. Katika mwaka 2010/2011, malengo ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*) ni pamoja na:-

(a) Kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi ili kupunguza uharibifu wa mazingira;

(b) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo ikiwa na pamoja na kusindika mafuta ya kula kutokana na mbegu kufikia viwango stahili;

(c) Kuhakiki maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi kwenye kiwango cha Kimataifa;

(d) Kujenga viatamizi (*incubators*) vya usindikaji wa mazao ya kilimo na kusambaza teknolojia za kutumia nishati endelevu hususan kukaushia vyakula kwa nishati ya juu.

(e) Kuimarisha matumizi ya teknolojia bora katika viwanda vya uyeyushaji vyuma pamoja na kutoa huduma zitakazowezesha uzalishaji bora viwandani bila kuchafua mazingira;

(f) Kuendeleza mfumo wa mlolongo wa ufuatiliaji (*traceability*) wa mazao hususan ya kilimo;

(g) Kuwezesha sekta binafsi kutumia mfumo wa huduma za *Global Standard One (GS 1 Tanzania)*; na

(h) Kuwezesha viwanda kutumia TEKNOHAMA hususani tovuti ili kuongeza mauzo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, malengo ya Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (*TEMDO*) ni pamoja na:-

(a) Kubuni, kuendeleza na kuwezesha utengenezaji kibiashara wa mitambo ya kusindika kahawa, mashine za kutengeneza bidhaa za ngozi na mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji;

(b) Kuboresha mitambo ya kusindika mazao ya kilimo, kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya upopo na kutengeneza mkaa unaotokana na taka za mijini na mabaki ya mimea, pamoja na kuwezesha wajasiriamali watengenezaji (*Manufacturing SMEs*) kuvitengeneza kibiashara;

(c) Kuhudumia viwanda vidogo na vya kati (*SMEs*) ili viongeze mchango wake katika kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa kusindika mazao ya kilimo karibu na sehemu za uzalishaji; na

(d) Kufanya tathmini ya mahitaji ya kiteknolojia katika viwanda ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa havifanyi kazi. Lengo ni kutoa ushauri kwa wenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, malengo ya Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundsi Vijijini (*CAMARTEC*) ni pamoja na:-

(a) Kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani katika maeneo yote waliko wajasiriamali hasa vijijini;

(b) Kuhakikisha teknolojia zinazofaa zinatafutwa, utaratibu wa kuzizalisha kwa wingi, na kuzisambaza kwa watumiaji;

(c) Kutoa ujuzi maalumu wa kuzibadilisha raslimali hasa mazao ya kilimo na mifugo kuwa bidhaa;

(d) Kujenga miundombinu itakayowafanya wajasiriamali hasa wa vijijini kupata sehemu za kufanya kazi;

e) Kujenga msingi na kusaidia utengenezaji wa bidhaa mpya kutokana na mawazo ya wajasiriamali binafsi;

(f) Kutoa elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara;

(g) Kuwawezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma zao, kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara, kutengeneza sehemu za kuonyeshea bidhaa za wazalishaji wadogo;

(h) Kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapoijidhihirisha kuhitajika; na

(i) Kujenga uwezo wa uzalishaji wa zana za kilimo ikiwemo matrekta madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Chuo cha Elimu ya Biashara kinalenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la mizani na vipimo; ununuzi wa vitendea kazi kama vile kompyuta, mizani na vipimo;

(b) Kuimarisha mafunzo ya kompyuta na mafunzo kwa vitendo katika idara ya mizani na vipimo;

(c) Uandaaji wa *Master Plan* ya eneo la Chuo katika kiwanja cha Kiseke;

(d) Kuimarisha ushauri wa kitaalamu (*consultancy*) ili kuongeza ushiriki wake katika shughuli za jamii; na

(e) Kujenga uwezo wa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuimarisha utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mtambuka; kuhusu kudhibiti rushwa. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu majukumu ya Wizara pamoja na kutekeleza mkakati wa kubaini na kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu janga la UKIMWI. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuwawezesha wafanyakazi kupata huduma ya kupima, lishe, virutubisho (*food supplements*) na kuwapatia nauli watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Vile vile, Wizara itaendelea na juhudzi zake za kuwaelimisha watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake mbinu za kujikinga na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira. Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine itaendelea kutoa mafunzo ya matumizi bora ya raslimali, uzalishaji endelevu, unaozingatia hifadhi na kulinda mazingira *Sustainable Consumption and Cleaner Production* katika shughuli za viwanda hususan vinavyoharibu mazingira ya jamii, kama vile viwanda vya ngozi na nguo. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa maafisa wake katika kozi mbalimbali yanayohusu uhifadhi wa mazingira katika viwanda ili kusimamia vyema Sera na Sheria ya mazingira na utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jinsia. Katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kuendelea kuwajengea uwezo Viongozi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuwawezesha kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia jinsia - *Gender Mainstreaming*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maendeleo ya Rasilimali Watu. Wizara imefanya jitihada mbalimbali katika uboreshaji wa rasilimali watu kulingana na mahitaji ya ikama katika kipindi cha mwaka 2005 – 2009. Jumla ya watumishi 77 wa kada mbalimbali walijiriwa, kati yao wanawake walikuwa ni 34 ikiwa ni sawa na asilimia 44. Aidha, jumla ya watumishi 40 walithibitishwa kazini, kati yao wanawake 27, sawa na asilimia 67. Katika kipindi hicho, Wizara iliwaendeleza kitaaluma wafanyakazi 95 kati yao wanawake walikuwa 62 ikiwa sawa na asilimia 65.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara iliajiri watumishi wapya 19 na kuwaendeleza kitaaluma watumishi 35 kulingana na mpango wa mafunzo wa Wizara. Kati ya hao watumishi 10 walikwenda mafunzo ya muda mrefu na 25 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Wizara iliendesha mafunzo ya ndani kuhusu Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wazi (*Open Performance Review and Apraisal System-OPRAS*) na Kanuni za Maadili katika Utumishi wa Umma (*Public Service Code of Ethics and Good Conduct*) kwa wafanyakazi wake wote ili kuongeza ufanisi wao wa kazi. Aidha, ili kuwapa motisha walioko kazini wanaotekeliza majukumu yao vizuri kwa kuzingatia utaratibu wa *OPRAS* iliwapandisha vyeo watumishi kumi na sita (16) waliofikia malengo yao.

Vile vile, ili kutekeleza dhana ya utawala bora kwa vitendo, mwezi Desemba 2009, Wizara iliendesha mafunzo ya uongozi kwa Watendaji Wakuu wa Wizara yaani: Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo. Mada zilihusu namna ya kufanya kazi kwa ushirikiano *teamwork*, usalama kazini *safety at work*, kukabiliana na msongo wa mawazo *stress management* na umuhimu wa kujali muda *time management*. Mafunzo haya yaliwawezesha washiriki kutambua nafasi walizonazo katika kutoa huduma bora kwa wakati huu wa utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea na jitihada za kuongeza watumishi wenye elimu, ujuzi na utsalamu katika fani mbalimbali kwa kuzingatia suala zima la jinsia. Ili kufikia azma hiyo, Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 25 wenye sifa zilizolezwu kwenye Sera ya Ajira na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na nyaraka za Miundo ya Utumishi wa Umma za

mwaka 2002. Aidha, itawaendeleza kitaaluma jumla ya watumishi thelathini (30) kwa kozu fupi na za muda mrefu na kuwapandisha vyeo wafanyakazi 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto katika utekelezaji. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mipango ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko, zipo changamoto za jumla zilizojitokeza wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa Sekta hii ambazo zinahitaji ushirikishwaji wa Sekta nyingi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Changamoto zinazoikabili Wizara hii ni:-

(a) Wizara kutotengewa bajeti ya kutosha ili kuweza kutekeleza jukumu lake la kuweza kuchangia ipasavyo katika uchumi wa nchi;

(b) Uwezo wa Wizara kuendeleza na kuiwezesha Sekta Binafsi ili itekeleze majukumu yake kama muhimili mkuu wa uchumi;

(c) Utekelezaji wa hatua za makusudi za kuwalinda wajasiriamali wadogo dhidi ya ushindani usio wa haki;

(d) Upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji na biashara ikiwa ni pamoja na kuendeleza miundombinu ya kuwezesha na kuimarisha uzalishaji katika biashara na masoko;

(e) Kuhakikisha uzalishaji unakidhi mahitaji ya soko ili kuhimili ushindani; kuhakikisha bidhaa zinazosalishwa katika viwanda vyetu zinakidhi ubora unaotoa ushindani katika soko la ndani na nje;

(f) Kuendeleza na kujenga uwezo wa wajasiriamali wa kuibua na kutumia fursa za uzalishaji, biashara na masoko;

(g) Kuendeleza na kuibua viwanda vipyta vitakavyotumia malighafi za hapa nchini ili kuongeza ajira;

(h) Kujenga mazingira yatakayowezesha matumizi ya teknolojia bora na za kisasa;

(i) Kukabiliana na msukosuko wa soko la mitaji, soko la fedha na uchumi wa dunia ambayo kwa kiasi kikubwa imesababisha upungufu wa mauzo nje; na

(j) Kuweka mazingira wezeshaji na kuhimiza kusindika mazao ili kuyaongezea thamani, kuongeza ubora wa bidhaa ili kuweza kutoa ushindani, kunadi na kuongeza juhudzi za kukuza mauzo nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambao wametoa misaada mbalimbali kusaidia Wizara yangu pamoja na wote ambao wameahidi kusaidia sekta hii muhimu hapo baadaye tutakapokamilisha taratibu za kuanzisha *Basket Fund*. Misaada na michango yao imesaidia kwa kiasi kikubwa Wizara

yangu katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija. Nchi hizo ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uhlanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika ya Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), CFC, DFID, FAO, IFAD, ILO, IRISH AID, ITC, JICA, Jumuiya ya Ulaya KOICA, OPEC Fund, UNCTAD, UNDP, UNIDO, WIPO WTO.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 31,542,839,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili iweze kutekeleza majukumu niliyoelezea ya kuendeleza sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Kati ya fedha hizo, Shilingi 21,885,826,000 ni kwa matumizi ya mishahara na Shilingi 9,657,013,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara inaomba jumla ya Shilingi 28,917,667,000 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo katika Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha hizi Shilingi 16,387,859,000 ni fedha za ndani ambazo zitatumika katika shughuli za maendeleo katika taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 12,529,808,000 ni fedha za nje kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge waone kwamba katika hotuba yangu tumefanya marekebisho ili fedha hizi zifanane na vitabu vya Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Wabunge na wewe kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB – MWENYEKITI WA KAMATI BUNGE YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 99(7) na Kanuni ya 114 (11), Toleo la 2007, naomba kuwasillisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilikutana tarehe 4 na 5 Juni, 2010 katika Ofisi ndogo ya Bunge, Jijini Dar es Salaam ili kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda,

Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na kupitia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao hicho Mheshimiwa Daktari Mary Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko aliwasilisha Taarifa yake kuhusu Dira, Dhamira na majukumu ya Wizara yake. Aidha, alieleza mambo ambayo yametekelezwa na Wizara yake kwa kipindi cha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010. Katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali ambao umeainishwa katika kitabu changu cha hotuba ambayo ni maoni 14 ufuatao:-

- (i) Kutowana na hali ya uchumi Duniani kuyumba, Kikundi kazi kinachoongozwa na Gavana wa Benki Kuu kitoe mapendekezo yake kwa wakati kuhusiana na sekta ya Viwanda na Biashara na Serikali iyafanyie maamuzi mapendekezo ya umuhimu wa kuweka mikakati ya kujihami na kujinasua na janga hili kubwa na la kihistoria;
- (ii) Serikali ikamilishe Kanuni za *TANTRADE*.
- (iii) Serikali ikamilishe utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara.
- (iv) Sekta ya Kilimo ihusishwe na sekta ya Viwanda na Biashara; kwa sababu ya kutegemeana kwa sekta hizo;
- (v) Serikali ifanye tathmini ya Muundo na Majukumu ya Wizara na Taasisi zake kwa ajili ya kuboresha utendaji.
- (vi) Serikali kuwianisha na kuunganisha shughuli za Taasisi za *SIDO*, *TEMDO*, *CARMATEC*, na *TIRDO* kwa lengo la kupunguza gharama na kuongeza ufanisi; (
- (vii) Serikali iharakishe kutunga Sheria mpya ya *NDC* itakayokidhi mazingira ya uwekezaji kwa wakati huu;
- (viii) Kutowana na majukumu mazito yanayoikabili *NDC* na mtaji kidogo ambao hautoshelezi mahitaji, Serikali ione uwezekano wa kutunisha mtaji huo;
- (ix) Serikali iisaidie Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa ajili ya Mauzo ya Nje (*EPZA*) kupata Ofisi yenye hadhi ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje;
- (x) Serikali iandae utaratibu wa kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuwekeza na hasa kwa wazawa;

(xi) Serikali ichukue hatua za kukabiliana na changamoto zinazokabili maeneo yafuatayo:- Viwanda; Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Wakala wa Vipimo,

(xii) Kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi nzuri ya Wakala wa Usajili na Leseni (*BRELA*), ili waweze kujenga Ofisi nzuri na yenze hadhi;

(xiii) Serikali iharakishe ufufuaji wa Kiwanda cha Matair;

(xiv) Kuhusu Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Serikali ione umuhimu wa kufanya yafuatayo:— Kuhamasisha Viwanda vya ndani kushiriki katika Maonyesho:-

- Kutenga eneo maalum kwa ajili ya wauzaji wa bidhaa zinazotengenezwa nchini.
- Litengwe eneo litakalojengwa hoteli kubwa nzuri itakayokidhi mahitaji ya wafanyabiashara wanaoshiriki kwenye Maonyesho na hasa wageni kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Kwa mfano, Mamlaka ya Uwekezaji kwa ajili ya Mauzo ya Nje (*EPZA*) imeshatengewa Ofisi nzuri yenze hadhi ndani ya eneo la Benjamin William Mkapa Dar es Salaam. Aidha, elimu ya uwekezaji imeendelea kutolewa na hivyo kuongezeka kwa wawekezaji wa ndani kutoka 30 hadi 55.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria mpya ya *NDC*, Waziri alieleza kuwa Rasimu ya Waraka wa Sheria mpya imeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Usajili na Leseni, Wajumbe walielezwa kuwa Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kufanikisha ujenzi huo. Kutokana na ujenzi kutokuanza kwa sababu ya kukosa eneo, Kamati inasisitiza upatikanaji wa eneo uharakishwe ili Ofisi hizo zianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutenga eneo kwa ajili ya wauzaji wa bidhaa zinazotengenezwa nchini, *BET* imeshatenga eneo maalum na imanzisha utaratibu wa kutenga siku maalum wakati wa Maonyesho ili kutangaza bidhaa zinazozalishwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza juhud katika kutekeleza maoni mbalimbali ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kabla ya kuomba fedha kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Mheshimiwa Waziri alieeleza Kamati kuhusu

malengo ya Wizara yake ambayo amerudia kuyaeleza mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo kabla ya maoni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Waziri aliiambia Kamati kuwa Wizara yake inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha Shilingi Milioni Moja Laki Mbili (1,200,000/=) kutokana na faini kwa kukiuka sheria ya leseni, uuzaji wa nyaraka za tenda pamoja na makusanyo mengine. Kuhusu Makadirio ya Matumizi, Mheshimiwa Waziri aliomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi, 31,542,839,100/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 32,717,666,500/= kwa ajili ya kugharamia miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Hakuna hata nchi moja iliyoendelea bila kupitia uchumi unaoongozwa na viwanda kwa sababu viwanda ndio kichocheo kikubwa cha maendeleo. Viwanda ndivyo vinavyovuta sekta nyingine za uchumi na huduma. Aidha, Wizara hii ina majukumu mengi, yakiwemo ya kuhakikisha upatikanaji wa fursa za masoko na uwekezaji kupitia majadiliano ya kibiashara baina ya nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa katika kutafuta na kujenga miundombinu ya masoko. Pamoja na umuhimu huu, *ceiling* ya Wizara hii ni ndogo sana wakati wote kutokana na ukweli kuwa *ceiling* za Wizara hutegemea sekta za vipaumbele na Wizara hii sio mojawapo ya sekta hizo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Wizara hii na Taasisi zake katika kukuza uchumi wa nchi yetu na hasa kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza, Kamati inasisitiza na kushauri kwamba Wizara hii iwe moja kati ya sekta za kipaumbele. Hii ni pamoja na Wizara kuongezewa *Ceiling*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Utafiti na Maendeleo na za Huduma chini ya Wizara hii zikiwemo *CARMATEC, TEMDO, TIRDO, SIDO, NDC, BET, CBE, TBS* na Vipimo zilianzishwa kwa madhumuni ya kuchochea ukuaji wa viwanda na biashara nchini kwa kutekeleza majukumu ya kuoanisha teknolojia ya nje na ya ndani ili kukidhi mazingira yetu, kujenga uwezo wa matumizi ya malighafi zinazopatikana nchini kwa ajili ya viwanda vyetu kwa kutumia teknolojia rahisi kwa mazingira yetu na kutafiti na kujenga teknolojia rahisi kwa matumizi ya kilimo hususan vijijini. Kutokana na Taasisi hizi kutengewa fedha kidogo sana zimeshindwa kujenga na kuongeza uwezo wa kufanya shughuli za utafiti na maendeleo ya teknolojia. Kamati inashauri Serikali kuzijengea uwezo wa kifedha Taasisi hizi ili ziweze kutimiza azma ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*) inakabiliwa na deni kubwa kwa Serikali kiasi cha Shilingi 903,589,768.05 (Shs. Milioni Mia Tisa na Tatu, Laki Tano Themanini na Tisa Elfu Mia Saba Sitini na Nane na Senti Tano) kwa muda mrefu ambao kwa kiasi kikubwa yanaleta sura mbaya katika ripoti ya Hesabu za Shirika (*current ratio*) na *ratio* nyingine ambazo ni vigezo muhimu katika kutathimini uhai wa shirika.

Mchanganuo wa madeni ni kama ifuatavyo:-

- Deni la kodi ya Ardhi- Sh. 161,103,279.85. Wakati *BET* inamilikishwa Uwanja wa Mwl. J. K. Nyerere, kodi iliyokuwa ikitozwa ilikuwa Sh. 590,000/= kwa mwaka. Ilipofika mwaka 1995, kodi hiyo ilipanda na kufikia Sh.3,386,322/= kwa mwaka na mwaka 2000 ikafikia Sh. 10,617,300/=.

- Deni la kodi ya Mapato (*PAYE*) Sh. 218,191,426.20. Deni hili ni malimbikizo ya kodi ya mapato ya wafanyakazi ambayo hayakuwasilishwa kwa mujibu wa sheria ingawa fedha hizo ni sehemu ya mishahara ya wafanyakazi toka Hazina. Hili ni deni la kipindi cha 2000- 2005 ambalo *BET* iliwasilisha maombi ya kusaidiwa kulipa kutokana na deni hili kusababishwa na mapungufu ya ndani ya *BET* chini ya Kurugenzi ya Fedha na Utawala. Bodi ya Wakurugenzi ilichukua hatua ya kumwajibisha na hatimaye kumfukuza kazi Mkurugenzi aliyesababisha deni.

- Limbikizo la kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) –Sh. 524,295,062/=.

Mnamo mwaka 2007, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), baada ya kupitia mapato ya *BET*, iligundua kuwa nyaraka zilizokuwa zinatakiwa kuwasilishwa kwao (*VAT Returns*) ziliwuwa haziwasilishwi kwa utaratibu unaotakiwa. Pia hata zilizokuwa zikiwasilishwa nyingine ziliwuwa si sahihi hasa kwa kipindi cha 2001-2006. Baada ya zoezi zima la ukaguzi kukamilika, iligundulika kuwa *BET* ilitakiwa kulipa kiasi cha Sh. 524,295,062/=, ikiwa ni malimbikizo ya kipindi cha 2001-2006 ikijumuisha adhabu na riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwa kipindi cha sasa makato yote huwasilishwa kwenye taasisi husika kwa wakati, isipokuwa lile deni la ardhi ambalo mjadala wa kiwango kinachotozwa bado unaendelea. Kamati inashauri Serikali kuona uwezekano wa kuifutia *BET* deni hili ili kuipa sura katika hesabu zake na hivyo kuwa na mwonekano mzuri zaidi hasa kwa nchi nyingine zinazoshiriki Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya majukumu makubwa ya *EPZA* ni kutenga maeneo maalum ya uwekezaji, kuyawekea miundombinu na kuyakodisha kwa wawekezaji kwa ajili ya kujenga viwanda. Kwa kuzingatia jukumu hilo, *EPZA* kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa, imebainisha maeneo ya uwekezaji katika Mikoa 14. Kati ya maeneo hayo, tathmini imefanyika katika maeneo manne na kuthibitishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali ambapo jumla ya fedha za fidia zinazohitajika ni Sh. 26.3 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Fedha za Maendeleo ya Wizara, kiasi kilichotengwa kwa *EPZA* ni Sh. 271 milioni tu. Kulipa fidia hii ni muhimu kwani kutaiwezesha *EPZA* kumiliki maeneo hayo, hivyo kuwavutia wawekezaji kutoka sekta binafsi kujenga miundombinu ya msingi katika maeneo hayo vikiwemo viwanda vya

uzalishaji. Aidha, viwanda vitaongeza ajira na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi wetu. Kuchelewa kulipwa kwa fidia hiyo, licha ya kuleta malalamiko kwa wananchi wanaomiliki maeneo hayo, kutasababisha kuongezeka kwa gharama ya fidia kutokana na ongezeko la riba na vilevile kukosa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuzingatia kauli ya Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 17/5/2010 wakati akifungua Kituo cha Uwekezaji cha Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (*BWM - SEZ*) alipozungumzia umuhimu wa *EPZA* kuongezea fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Inasikitisha kwamba pamoja na msisitizo huo wa Rais bado kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ya *EPZA* ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NDC* imepewa jukumu la kuendeleza miradi mikubwa ya viwanda kwa kushirikiana na wabia wa ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, bajeti inayotengwa kwa *NDC* chini ya *ceiling* ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni ndogo sana na hivyo inakuwa vigumu kutekeleza jukumu hilo muhimu. Kwa mfano *NDC* ina jukumu la kuendeleza miradi ya Liganga na Mchuchuma, Mradi wa *Soda Ash*, Kiwanda cha uzalishaji wa Dawa za Kuua Mazalia ya Mbu ambalo ni la msingi kwa Taifa letu.

Kutokana na majukumu mazito iliyonayo *NDC*, Kamati inashauri Serikali kwamba ni vema bajeti ya *NDC* ikawa nje ya *ceiling* ya Wizara ili iweze kutimiza majukumu yake ipasavyo. Aidha, Serikali itoe dhamana (*Guarantee*) ili *NDC* iweze kukopa au kuingia ubia na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PPF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vimekuwa vinatozwa kodi mbalimbali na Halmashauri zikiwepo *Industrial cess*, kodi ya VETA, VAT, *Corporation tax*, *Land rent*, *Property tax*, ambazo ni mzigo mkubwa kwa wenye viwanda. Hii inasababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na hivyo kuongezeka kwa bei ya bidhaa. Kwa kawaida wazalishaji huhamishia gharama hizi za kodi kwa walaji na hivyo kununua bidhaa kwa bei ya juu sana. Ili kupunguza ongezeko la bei za bidhaa na kuweza kuhimili ushindani, Kamati inashauri kodi hizo zipunguzwe zikiwepo za Halmashauri (*Industrial cess*).

Kodi hizi ni nyingi ikizingatiwa pia kuwa gharama za uzalishaji ni kubwa kutokana na miundombinu duni, ikiwemo barabara, reli, bandari, umeme na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia utekelezaji wa mageuzi ya uchumi na utekelezaji wa mfumo wa soko huru, kumekuwa na uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora na za bandia na baadhi ya bidhaa hizo hupewa ruzuku huko zinakozalishwa na hivyo kuuzwa kwa bei ndogo na kusabababisha ushindani usio wa haki katika biashara kwa viwanda vya ndani. Ukwepaji wa kodi unaotokana na *under invoicing*, *under declaration*, kukwepa kodi (*tax evasion*) na kadhalika, vinaongeza tatizo la ushindani usio wa haki kwa viwanda vya ndani hasa kutokana na mazingira ya uzalishaji ambayo yanakabiliwa

na matatizo ya miundombinu duni kama vile barabara, reli, bandari, na upatikanaji wa maji na umeme usioridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matatizo haya, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kulinda viwanda vyetu vya ndani ili kuviepusha na matatizo niliyoyataja hapo juu.

Hii ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa uzalishaji, kutatua matatizo ya miundombinu, kuweka kodi kubwa kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ambazo viwanda vyetu vina uwezo wa kuzizalisha, kuhakikisha kuwa viwanda vilivyobinafsishwa, ambavyo havijatekeleza ipasavyo mikataba ya uuzwaji, vinatekeleza wajibu wake wa kimkataba ili viweze kuchangia katika kujenga uwezo wa uzalishaji wa viwanda vyetu na hivyo kuchangia katika uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na uhaba wa vipimo halali nchini unaosababisha matumizi ya vipimo batili kama madebe, visado, mafungu na lumbesa hasa kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo. Kamati inashauri Serikali kuondoa kodi kwa mizani za kupimia mazao kama ilivyo kwa pembejeo za Kilimo. Hii itasaidia kupunguza bei ya mizani. Aidha, Kamati inashauri Wawekezaji kuhamasishwa na kupewa vivutio ili watengeneze mizani hapa nchini, ikiwa ni pamoja na Serikali kuanzisha na kuipa ruzuku taasisi itakayohusika na uagizaji wa mizani na vipuri vyake hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vidogo na Biashara ndogo ni muhimu katika uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kutoa ajira na kipato na pia kuyaongezea mazao thamani. Ili kuchochea uwezeshaji wa Wajasiriamali wadogo nchini, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

- Kuendelea kujengea uwezo Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*);
- Kubuni mikakati itakayowezesha wajasiriamali wadogo kuifikia mikopo inayotolewa na taasisi za fedha zenyenye masharti nafuu;
- Serikali na taasisi zake kuchukua hatua za makusudi za kununua bidhaa kutoka kwa wajasiriamali wadogo ndani ya nchi;
- Kubuni vivutio kwa ajili ya wajasiriamali wadogo;
- Ujasiriamali kuingizwa katika mitaala ya *CBE* na vyuo vingine vya mafunzo; na
- Programu ya *SIDO* ya Wilaya moja zao moja iimarishe ili kuchochea maendeleo ya viwanda vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikizuia wakulima kuuza mazao ya chakula nje ya nchi na hivyo kusababisha wakulima kukabiliwa na umasikini mkubwa na kusababisha chakula hicho kuuzwa ndani ya nchi kwa bei ndogo ambayo haiendani na gharama za uzalishaji. Kutokana na hali hii, wakulima wengi walio mipakani huuza mazao yao nje ya nchi kwa kutumia njia za panya. Kwa kuwa nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa pato la wakulima linaongezeka na kupunguza umasikini, kuongeza thamani ya mazao yao na kuondokana na kufanya biashara kuitia njia za panya. Kamati inaishauri Serikali kujenga uwezo wa Akiba ya Taifa ya Chakula (*Strategic Grain Reserve*) na kununua mazao kwa wakulima kwa bei inayokubalika ili kuhakikisha nchi inakuwa na chakula cha kutosha wakati wote na kusimamia mfumko wa bei.

Aidha, Serikali iimarishe Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani ili kuhakikisha kuwa mkulima anapata thamani ya mazao yake, ikiwa ni pamoja na kuandaa utaratibu wa kuuza mazao ya chakula nje ya nchi ambao hautaathiri akiba ya chakula ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina pamoja na maoni yaliyotolewa na Kamati, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko jumla ya Shilingi 63,660,505,600/= (Bilioni Sitini na Tatu, Milioni Miasita Sitini, Laki Tano na Elfu Tano na Mia Sita). Kati ya fedha hizo Shilingi 31,542,839,100/= zinazombwa kugharamia Matumizi ya Kawaida na Shilingi 32,717,666,500/= kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Aidha, niwashukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kuendesha Vikao vya Bunge kipindi chote cha uhai wa Bunge kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Michael Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko; Mheshimiwa Daktari Cyril A. Chami, Naibu Waziri; Katibu Mkuu Ndugu Joyce Mapunjo, pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Kamati wakati wote na hususan wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao walionipa kipindi chote wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati na hasa kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Bajeti hii. Naomba kwa heshima kubwa niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatibu, Mwenyekiti; Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, Mjumbe; Mheshimiwa Ame P. Ame, Mjumbe; Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mjumbe; Mheshimiwa Muhammad A. Chomboh, Mjumbe; Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mjumbe; Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mjumbe; Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mjumbe; Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mjumbe; Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mjumbe; Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mjumbe; Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mjumbe; Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mjumbe; Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mjumbe; Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Mjumbe; Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mjumbe; Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mjumbe na Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mjumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini uongozi mahiri wa Dr. Thomas D. Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza Majukumu yake. Kipekee nawashukuru ndugu Charles Mloka, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Angelina L. Sanga na Ndugu Chipanda Chilemeji, Makatibu wetu wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kukamilisha Taarifa hii kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa imani yao kwangu na kunichagua kuwa Mbunge wao kwa vipindi vitatu mfululizo. Niwashukuru wote kwa ushirikiano walionipa katika juhudi za kuleta maendeleo katika Jimbo la Makunduchi. Ni matumaini yangu kwamba watampa ushirikiano wa kutosha mrithi wangu atakayechaguliwa baada ya kustaafu kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za dhati na za pekee kwa wake zangu Fatma na Fadhila kwa upendo, faraja na uvumilivu wao kwa muda wote wa miaka 15 nilipokuwa natekeleza majukumu yangu ya Kitaifa kama Naibu Waziri wa Fedha na Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele yenu leo na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa Chama changu CHADEMA, chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mwenyekiti. CHADEMA kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni, pia nalishukuru Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) kwa kuendelea kuonyesha imani kwangu. Naahidi nitaendelea kuifanya kazi niliyotumwa na chama changu kwa moyo mmoja na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawajibika kwa moyo wa dhati kuwashukuru viongozi wangu wakuu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa imani kubwa walijonayo juu yangu kunitua kuwa msemaji wa Wizara hii. Aidha, napenda kumshukuru Naibu wangu Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy kwa ushirikiano alionipa katika kuoandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu wa pekee, napenda kuishukuru familia yangu hasa wanangu Caroline, Yahone na mume wangu mpenzi Dr. Fidelis Owenya kwa kuendelea kunivumilia wakati nikiwa mbali nao nikilitumikia Taifa katika shughuli za siasa. Aidha, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Dr. Mary Nagu na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na kuleta hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa uchumi ulio endelevu unatokana na mfumo mzima unaobadilisha shughuli za kiuchumi, hasa katika mtazamo wa kuoanisha nyanja za msingi za uzalishaji kama kilimo, madini na maliasili na sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkazo wa kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo, madini na mazao ya maliasili bila ya kuwa na uoanisho na viwanda ili kuongeza thamani kwa bidhaa hizo ni sawa na kuchota maji kwa pakacha. Kwani juhudhi hizo kamwe haziwezi kuleta uchumi ulioendelevu kwa nchi yetu kama ilivyo kwa wenzetu wa nchi za mashariki ya mbali (*Mini-Tiger Countries*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuwa bei za mazao mengi ya kilimo (*traditional crops*) katika soko la dunia hufuata *law of demand and supply*, hivyo basi hata kama bei itakuwa ni nzuri kiasi gani, bei hiyo haiwezi kushindana na bei ya bidhaa zilizopitia viwandani na kuongezewa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kuimarisha sekta ya viwanda ilianza pale sera ya ubinafsishaji ilipopewa Baraka na Serikali. Lakini hadi sasa sekta nzima ya viwanda bado haijabadilisha mwelekeo wetu kiuchumi wa kutegemea zaidi kuuza mazao ghafi na kuagiza bidhaa nyingi toka nje kuliko tunazouza sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya nguo, mbao na ngozi bado havijaweza kuzalisha bidhaa za viwango vya kuweza kuwa shindani katika soko la nje na hata katika soko la ndani zinaonekana zina bei kubwa kuliko zile zinazotoka nje. Hii inatokana na gharama za uzalishaji kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaiona hii kuwa ni changamoto kubwa katika kuwa na uchumi ulioendelevu kwa ujumla wake. Tatizo lingine ni uwezo mdogo wa Watanzania kufanya manunuzi kwa ujumla na kupelekea bidhaa zetu kukosa soko ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa viwanda vyetu bado vinashindana kuwa *import substitution* badala ya kuwa *export-led* kwa dhana hiyo ni vigumu kwa uchumi wetu kuwa endelevu. Kwani viwanda vinajitahidi kuzuia bidhaa za nje kweneye soko la ndani badala ya kujitahidi kufungua milango kweneye masoko ya nje. Hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa ili kuwa na sekta endelevu ya viwanda inatakiwa kurekebisha mfumo mzima wa sekta ya fedha na Sekta ya nishati kama vichocheo muhimu ili kufanya sekta ya viwanda kuwa shindani na nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kubadlisha mfumo wa sekta ya fedha kwa dhana kuwa mikopo inayotolewa kwa wawekezaji wa viwanda uwe tofauti na ule unaotumiwa kwa wafanyabiashara wa kawaida (*Manufacturing and trade to be served from different windows of commercial lending*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema hili kwa kuwa sasa hivi Serikali imeanzisha dirisha maalum kwa ajili ya mikopo kweneye uwekezaji wa kilimo tu, vivyo hivyo, ifanyike kweneye uwekezaji katika sekta ya viwanda. Kwa njia hii tuna imani Tanzania itainuliwa na kuendelezwu na Watanzania wenywewe tofauti na ilivyo sasa kuwa tunategemea watu wa nje waje kujenga viwanda na waende kukopa kweneye mabenki ya nje, madhara yake mtindo huo yamekwishaonekana kweneye sekta ya madini, kwani faida yote imekuwa ikirudi kwao na sisi kubaki mikono mitupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilani ya uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2005 iliahidi ukuaji wa sekta ya viwanda utafikia 15% ifikapo mwaka 2010, lakini takwimu za hali ya uchumi zinaonyesha ukuaji wa asilimia 8.0% kwa mwaka 2009/2010, kwa kulinganisha na asilimia 9.9% mwaka 2008 na hivyo kufanya lengo la Ilani ya CCM kushindwa kufikiwa kwa asilimia 7%. Uzalishaji wa nguo ulipungua kutoka mita za mraba 7,913,000 mwaka 2008 hadi mita za mraba 7,783,000, uzalishaji katika tabaka la mbaao ulipungua kwa 16.6%. Aidha, gharama za uzalishaji bidhaa ziliongezeka hadi sh. 1,764,341 milioni kutoka sh.1,747,351 milioni mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa takwimu hizi zinathibitisha hoja zetu tulizotoa hapo juu. Tunasisitiza kuwa Serikali ni lazima ibadili mfumo mzima kweneye sekta ya fedha na nishati ili kuleta tija katika uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 ya uchaguzi ilisisitiza ufufuaji wa viwanda na kuanzisha vipyta. Lakini kati ya Mashirika ya Umma 336

yaliyokwishabinafsishwa tayari ni aslimia 19 tu ndiyo utendaji kazi wake ni mzuri, asilimia 44 yanaendeshwa kihasara na asilimia 37 yamefungwa kabisa au yamebadilisha kazi zake za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo mashirika kama, Kumburu *Sisal estate* - Tanga, Mtwara *Cashewnut Processing Plant* - Lindi, Newala *Processing Plant* - Lindi, Ilemela *Fish Processing Plant* - Mwanza, *Concrete Roof Tiles Plant* - Dodoma, *CDA Zuzu plant* - Dodoma na vingine vingi ni mfano tu wa viwanda ambavyo hadi sasa hatima yake haijulikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imetoa takwimu hizo kuonyesha ni kwa jinsi gani wananchi katika maeneo husika walivyopoteza ajira na ile dhana ambayo kila siku inaongelewa kuwa ubinafsishwaji umeongeza ajira ni siasa tu. Kinachoonekana hapa ni kuwa wale tuliuwapa dhamana ya kutufanyia kazi hiyo hawakuifanya kwa umakini na hivyo kuwaletaa Watanzania matatizo na umaskini mkubwa kwani wengi wao hadi sasa hawajawahi pata haki zao. Hadi sasa bado wanadai na viwanda vyao havijulikani ni lini vitafunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani inamtaka Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko alieleze Bunge lako Tukufu hatua ambazo Serikali imeshachukua mpaka sasa katika kufufua viwanda vilivyokufa mkoani Dodoma, Mtwara, Shinyanga, Lindi, Tanga, Mbeya na Kilimanjaro?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipitisha sheria hapa Bunge kuwa inatakiwa kutumia magunia yaliyotengenezwa kwa mkonge wa Tanzania (*Mandatory use of sisal bags*). Hili lilipendekezwa na kukubalika kwa lengo la kuwalinda wakulima wetu wa zao la Mkonge ikiwa ni pamoja na kuivilinda viwanda vinavyozalisha bidhaa itokanayo na mkonge. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa utekelezaji wa sheria hiyo umefikia wapi? Je, kwa mtindo huu kweli Serikali ina nia ya dhati ya kuivilinda viwanda vyta ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika hotuba zetu za nyuma tumekuwa tukiuliza Serikali kuhusiana na hatua gani zinachukuliwa ili kuvifufua viwanda vya *General Tyre, Kilimanjaro Machine Tools* na viwanda vya ngozi (Mwanza, Morogoro na Moshi). Kwa kipindi chote tumekuwa tukiambiwa utaratibu unafanya. Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na majibu hayo kwani hadi sasa Tanzania tumpoteza fursa nyingi sana ambazo zingepatikana katika soko la ndani na nje, kwa kutokuwa na mipango inayoeleweka ya kuinua viwanda vyetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kiwanda pekee cha matairi katika nchi yetu na Afrika ya Mashariki kwa ujumla, kilikuwa na uwezo wa kuzalisha takribani matairi 300,000 kwa mwaka yenye ubora unaokidhi viwango vya Kimataifa. Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa ni kwa vipi kiwanda hiki ambacho kina *comparative advantage*

katika uzalishaji na soko kinakuwa chini ya mufilisi? Tunadhani unatakiwa umakini mkubwa katika kufanya maamuzi, na inatubidi tuepuke maamuzi ambayo yanakuwa na *motive* za kisiasa badala ya kuweka mbele maslahi ya Taifa. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze nini kinaendelea hadi kiwanda hicho kikawekwa chini ya mufilisi. Tuna uhakika wa masoko kwa ajili ya matairi ambayo yangezalishwa na *General Tyre E.A Limited*, Magari ya Serikali yenye na mashirika ya umma yanatosha kwa sehemu kubwa kutoa soko kwa magurudumu hayo.

Aidha, Kambi ya upinzani inataka kujua katika kikao cha majadiliano kati ya Serikali na mbia mwenza kilichokuwa kifanyike mwezi april 2010 je, kilifanyika na kama kilifanyika ni nini hatima ya kiwanda hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya biashara na masoko nchini, sekta ya biashara na masoko katika Taifa letu imekuwa haina uhakika na mwenendo wa masoko hauwezi kutabirika. Aidha, Serikali iliahidi katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005 kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko kwa wasindikaji na wafanyabiashara wa kat. Kama haitoshi Serikali iliwaahidi tena wananchi kuwa kila Wilaya na Halmashauri ya Mji kupewa vitendea kazi ili kukusanya taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya leo imekuwa na bidhaa nyingi bandia toka nchi za nje, hali hii imepelekea kutokea madhara makubwa katika uchumi wa wananchi na kwa Taifa pia. Bidhaa mbalimbali ambazo hazina ubora unaokidhi viwango zimekuwa ziliingizwa kwa wingi na wafanyabiashara na kuonekana kila kona ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani imekuwa ikihoji mara kwa mara hatua zinazochukuliwa na mamlaka husika katika kukabiliana na tatizo hili, lakini taratibu zinazochukuliwa tunaona haziwezi kukomesha uingizaji huo. Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni vyema Serikali kupitia Mamlaka zinazo hakiki ubora wa bidhaa kwa nchi ambazo bidhaa hizo zinatoka kwa wingi, ili kuwepo ushirikiano wa karibu. Ikitokea bidhaa hizo zisizo na ubora kukamatwa basi Mamlaka hizo na washirika wa Serikali ziwajibike moja kwa moja badala ya kuhangai na wafanyabiashara. Aidha, tunashauri kuanzishwa kwa mawakala wa *TBS* na wa Tume ya Ushindani katika mipaka ambayo inaingiza bidhaa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ilani ya CCM iliahidi katika Ilani ya Uchaguzi 2005 kutoa mafunzo ya jinsi ya kutumia taarifa za masoko kwa vikundi mbalimbali vya wafanyabiashara. Hali halisi ilivyo kwa sasa ni kwamba wafanyabiashara wengi nchini hawana taarifa za masoko na hata zile chache zinazopatikana haziko katika lugha rahisi kuweza kueleweka kwa wafanyabiashara wa kawaida. Kambi ya upinzani inataka kujua mpaka mwaka huu ni wafanyabiashara wangapi na wa maeneo gani waliopatiwa mafunzo hayo na ipi tahthimini ya utekelezaji wa mafunzo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na kutohwepo kwa mfumo mzuri na unaoeleweka wa masoko ya bidhaa za kilimo, Kambi ya Upinzani inasema mpango wa Kilimo Kwanza hauwezi kuleta tija ukizingatia tatizo kubwa la wakulima kutohuelewa

bei katika masoko ya ndani na nje na hivyo mazao yao kuishia kuharibika. Mfano mzuri ni msimu wa viazi vitamu Gairo, je, kuna haja ya kuwahamasisha wakulima wa maeneo hayo kulima viazi kwa wingi wakati kile wanachozalisha hakina soko la uhakika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado juhudini za kina zinahitajika kuendeleza sekta ya Biashara za Matunda. Tanzania tunazalisha matunda mengi kwa misimu mingi mfano, katika Mkoa ya Kigoma, mananasi yanaptikana kwa bei ndogo kati ya ya Tsh.50- 200/= na matikiti maji linapatikana kwa Tsh.150/= hadi 500/= matunda haya yanaweza kisindikwa kama viwanda vikianzishwa maeneo haya ili kuongeza thamani ya bei na kutoa ajira kwa wananchi na kuongeza kipato cha wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi zinatuonesha wazi kuwa katika sekta hii ya Matunda bado kuna fursa kubwa ya kuendeleza viwanda na kilimo lakini pia kuna uzembe mkubwa sana unaofanywa kutoimarisha miundombinu, kwani mazao haya yanaozea shambani kwa sababu ya barabara mbovu, jambo linalosababisha Taifa kupata hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano huo ni mmoja tu bado kuna:- mihogo, matunda mengine kama machungwa, maembe, nyanya na mboga mboga. Wakati wa msimu wakulima wanakosa soko la uhakika kwa mazao yao, wakati Serikali inasema zalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzalisha kwa wingi maana yake ni kuongeza gharama katika kuzalisha na gharama hizo zinatakiwa zifidiwe wakati wa kuuza, kama hakuna soko maana yake ni kumzidishia umasikini Mkulima. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inasema kuwa Kilimo kwanza bila kuwa na mfumo mzuri wa masoko kwa bidhaa za kilimo inaweza kuwa ni kauli mbiu ya kuwafukarisha wakulima, ili CCM iendelee kuwatawala vizuri. Kuna usemi unaosema kuwa “ukitaka kumtawala mtu vizuri, mfanye awe tegemezi kwa fedha na elimu”. Tunaona huu unaweza kuwa ndio mkakati wa Serikali kwa wakulima wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa mifuko katika sekta ya biashara, Serikali ya CCM iliahidi katika ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005 kuwa ingeanzisha mfuko wa *Export Development Fund (EDF)* ili kuendeleza sekta hii, Kambi ya Upinzani inatakiwa kujua, je Mfuko huu ulishaundwa na umepangiwa fedha kiasi gani? Serikali inaweza kueleza ni yapi mafanikio katika mifuko hii inayoanzishwa ili isije kuwa mwanya wa Ufisadi?

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji na ulindaji wa viwanda vidogo, kama ambavyo nimeeleza hapo awali kuwa ili sekta ya viwanda iweze kuendeleza Serikali inatakiwa kuweka mfumo mzuri kwa taasisi za fedha kuwa na dirisha maalum kama ilivyofanyika kwa mikopo ya kilimo, kwa ajili ya mikopo ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati. Kwani mikopo ya *SIDO* haiwezi kusaidia kuleta mapinduzi ya viwanda vidogo na vya kati, bali *SIDO* kama taasisi yenye taaluma inaweza tu kutoa ushauri wa kitaalam (*Technical Advice*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia bajeti ya Wizara imetenga kiasi cha sh.1.9 billioni kwa *SIDO* kwa ajili ya kutimiza majukumu yake. Je, fedha hizi kweli zinaweza kuendeleza viwanda vidogo nchi nzima? Tukumbuke kuwa viwanda vidogo ndio chanzo cha viwanda vikubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za utafiti (*RIRDO, CARMATEX na TEMDO*) maendeleo ya nchi yoyote duniani yanatokana na kazi nzuri inayotokana na taasisi za utafiti, taasisi za utafiti zinajukumu la kubuni njia bora na rahisi katika uzalishaji wa msingi (*primary production*). Nchi yetu kwa kiasi kikubwa inategemea kilimo, hivyo basi ni jukumu la taasisi hizi kubuni njia bora na rahisi kumwezesha mkulima katika hatua zote za kilimo (utayarishaji wa ardhi, upandaji, utiaji mbolea, palizi na uvunaji na uhifadhi).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutamka bayana kuwa, Serikali itatenga asilimia moja ya bajeti kwenda kwenye utafiti. Kambi ya Upinzani inauliza, je, ni kiasi gani kimetengwa kwa taasisi hizi ili ziweze kufanya kazi ya kutoa teknolojia itakayoiwezesha nchi kuhimili ushindani katika Soko la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kambi ya upinzani inazidi kusisitiza serikali iongeze uwezo kwa taasisi za utafiti ziweze kuwasaidia Watanzania wazalishaji. Taasisi hizo ni *TIRDO, CARMATEC, TEMDO, SIDO NA TBS*, bado bajeti za taasisi hizi ni ndogo kuweza kuzisaidia kufanya kazi nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa shirika la maendeleo la Taifa (*NDC*) kwa mujibu wa Taarifa ya *CAG*, Shirika hili lilifanya uwekezaji katika miradi mitano ambayo kwa mujibu wa ripoti hiyo uwekezaji haukuwa na tija na hivyo *NDC* kupoteza jumla ya sh.968,589,000 kwa uwekezaji huo. Kambi ya Upinzani inaiuliza Serikali je huu ni uwekezaji au matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi? Je, miradi hiyo bado ipo na inaendelea na uzalishaji au imekwishafilisika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoptaka na majukumu ya msingi ya *NDC* ni aibu kuwekeza katika miradi ambayo haikufanyiwa upembusi yakinifu na hivyo kuliingizia Taifa hasara ambayo ingeweza kuepukika. Hili linawapa wasiwasi wawekezaji makini kupata ushauri toka kwa wataalam wa shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo maalum ya kuzalisha kwa mauzo ya nje (*export processing zone authority – EPZ*), pamoja na nia nzuri ya Serikali kutenga maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo ya nje (*Export processing Zone*) katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje. Kambi ya Upinzani ingependa kujua ni wawekezaji wangapi mpaka sasa wamewekeza na ipi mikakati madhubuti iliyowekwa ili kuongeza uwekezaji hasa kwa wazalendo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni utaratibu gani maalum ulioandaliwa kama motisha (*incentives*) kwa wawekezaji wa kizalendo ili kuongeza uwekezaji wa ndani katika *EPZ*. Je, hadi leo ni maeneo mangapi yaliyotengwa kwa ajili ya *EPZ* na kwa shughuli gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Wizara 2010-2011, Waziri wa fedha aliwasilisha hotuba yake na kwa kulieleza Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania wote kuwa Serikali inaratajia kukusanya jumla ya Trilioni 6,003,590 (Trilioni, Bilioni, milioni) kutokana na mapato ya ndani wakati fedha hizo hazipo. Sekta ya viwanda ambayo ingeweza kufanikisha kupatikana mapato ya ndani lakini kuonyesha jinsi Serikali isivyothamini sekta ya viwanda imetengewa Shilingi 63,660,505,600 kati ya fedha hizo Shilingi 31,542,839,100/= kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 32, 717,666,500/= kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kambi ya Upinzani inaona fedha hizi hazitoshii ukizingatia kauli mbiu ya Kilimo Kwanza haiwezi kufanikiwa bila kuwa na viwanda vingi vya kusindika mazao katika maeneo ya uzalishaji ili viletete tija katika kuongeza mapato ya ndani. Tunaishangaa Serikali kutojali umuhimu huu wa viwanda wakati nchi nyingi zilizoendelea waliweka mbele mapinduzi ya viwanda na kuhakikisha viwanda vile vinafufua uchumi wake. Kwa mfano, mzuri ni nchi za Malaysia, Singapore, India na China. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi kubwa ya kuliongoza Bunge hili kwa kipindi chote cha uhai wake. Kwa kuwa hakuna marefu yasiyo na ncha na kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi nina uhakika kuwa turudipo humu Bungeni chama changu kitakuwa tawala. Kwa moyo mkarimu tunawakaribisha Wabunge kutoka CCM kuonja utamu wa Upinzani. Nasi tutawapa ushirikiano na ushauri namna ya kutengeneza hotuba mbadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsanteni kwa kunisikiliza Mungu awabaki na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Lucy Owenya pamoja na Naibu Spika ahamie huko. Ahsante sana Waheshimiwa tunaendelea. Tunao wachangiaji naona wa kutosha sasa nitamwita kwa sababu Mheshimiwa Lucy Owenya, Baba yake ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, nitamwita baadaye Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. Nitaanza na Mheshimiwa Devota Likokola atafuatia na Mheshimiwa Maulida Komu, halafu Mheshimiwa Ndesamburo.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuanza kuchangia. Napenda pia kuchukua nafasi hii kwa kweli kuendelea kuwashukuru sana wanawake wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma ambao kwa kipindi chote hiki tumeendelea kushirikiana na kuleta maendeleo ya Mkoa wetu na maeneo mengine katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Mheshimiwa Katibu Mkuu ambaye kwa kweli ni Katibu Mkuu mwanamke, Dada

Joyce Mapunjo na kazi yake anayoifanya. Watendaji wengine wote wanajitahidi sana katika utendaji wa kazi za Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mojawapo ya Wizara ambazo imefanya kazi moja kwa moja na wananchi wetu katika maeneo yetu ya Mikoa tunayotoka, Vijiji na hata Wilaya. Napenda kupongeza sana Idara mbalimbali na Taasisi mbalimbali za Wizara hii. Zikiwemo kwanza kabisa *SIDO* wamefanya kazi nzuri sana. *BLERA* wamefanya kazi nzuri, *COSOTA*, *CARMATEC*, *TBS*, na nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *SIDO* wamejithidi sana kutoa mafunzo na mafunzo hasa tunayoyahitaji kwa wanawake. Wanawake wengi wamepata mafunzo ya ujasiriamali kutoka Taasisi ya *SIDO*. Lakini vile vile wamepata mikopo mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Ruvuma *SIDO* imefanya kazi nzuri sana. Wilaya zote, Wilaya ya Tunduru wamekwenda kutoa mikopo na mafunzo. Wilaya ya Mbinga wametoa mikopo na mafunzo. Wilaya ya Songea Mjini wametoa mikopo na mafunzo. Wilaya ya Songea Vijijini wametoa, Wilaya ya Namtumbo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba *SIDO* ya Mkoa wa Ruvuma ndiyo ilioongoza kutoa mikopo kwa wajasiriamali hususan wanawake. Tunawapongeza sana. Lakini vile vile niipongeze sana kwa Taasisi ya *BLERA*, wametoa elimu na usajili wa vikundi vingi sana. Hongereni kwa kazi hiyo nzuri. *COSOTA* wamefanya mafunzo, lakini vile vile wamefanya ukaguzi ili kuangalia kazi za wasanii zisije zikachezewa. *CARMATEC* wameendelea kufanya mafunzo ya nishati mbalimbali, lakini niwapongeze hapa kwa nafasi ya pekee sana. *CARMATEC* wana mradi mkubwa wa *bio gas* kueneza katika nchi yetu na wamefanya mafunzo haya ikiwemo pia katika Mkoa wa Ruvuma. Tunawashukuru na tunawapongeza pia. *TBS* wamefanya mafunzo na wametoa ushauri mbalimbali ili kuboresha bidhaa zetu ziweze kuwa na viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hizi zote zinakabiliwa na changamoto kubwa ya pesa. Wasemaji wote katika Kamati wamezungumza, lakini vile vile tunaona kwamba pesa wanazotengewa taasisi hizi ni ndogo, tunaomba ziongezwe. Kwa sababu majukumu yao wanayofanya ni mazuri na makubwa. Kwa hivi bila kuwa na pesa tutakuwa tunaendelea kuwalamu lakini uwezo hatuwawezeshi. Kwa hiyo, niombe tu kwa hizi taasisi zinazofanya moja kwa moja na wananchi kwa kweli Mheshimiwa Waziri hebu zitazame na kwa kweli katika bajeti uongeze zaidi kwenye hizi taasisi zinazofanya na wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa kweli nizungumzie suala la *EPZ*. Tumeona mfano wa *EPZ* mzuri sana pale Mabibo na kwa kweli Mheshimiwa Waziri pongezi kubwa sana tunazitoa. Tumeona jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amefungua ile

*EPZ* na kwa hakika mtu yoyote akienda pale Mabibo anaweza akaona kwamba hapa Tanzania tuna kitu cha kujivunia. Nawapongeza sana wameweka pale Mlima Kilimanjaro alama tu. Ule mlima ni mzuri na hata kama mgeni akija akishindwa kwenda Kilimanjaro basi aende pale *EPZ* ataona ule mlima Kilimanjaro. Lakini niseme suala la *EPZ* tumetengewa maeneo 14 katika nchi yetu. Uendelezaji wake unaenda pole pole. *EPZ* inapata pesa ndogo na ni jukumu kubwa sana ambalo linaweza likaleta uchumi mkubwa sana kwa nchi yetu. *EPZ* inaendeleza viwanda, kwa hivi ni lazima pesa ziwe za kutosha ili viwanda viweze kuendea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi ya *EPZ* inakabiliwa na changamoto kubwa. Watu wengi sana hawaelewii masuala *EPZ* na SES. Kwa hiyo, ni lazima mafunzo na uelewa mbalimbali utolewe. Tuna *EPZ* katika Mkoa wa Ruvuma katika Kata ya Ruwiko, eneo la Luwawasi na Mkuzo. Ile *EPZ* wananchi kwa hiari yao walitoa eneo kubwa sana na wametoa lile eneo kwa moyo radhi ili Mkoa wa Ruvuma sasa ufunguke na maendeleo ya viwanda. Wilaya yetu ya Songea Mjini haina viwanda. Watu wanaokaa mjini jamani wanategemea viwanda. Sasa wananchi wa Luhwiko walitoa eneo la Luwawasi na Mkuzo kwa roho njema kabisa. Lakini cha kusikitisha mpaka leo fidia hawajalipwa. Tunaomba hizo hela za fidia kwa sababu wananchi wametoa lile eneo na linaweza kufungua makubwa sana katika Ukanda wa Kusini. Wale wananchi walipwe fidia jamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwombwa Mheshimiwa Waziri pamoja na bajeti yako yote angalia katika vyanzo vingine pia ili wale wananchi wa Songea wapate fidia tuweze kuendeleza viwanda kule. Maeneo haya tuliyotenga nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri uweke vipaumbele. Maeneo ni mengi lakini vipaumbele yawe ni maeneo ya mipakani. Mkoa wa Ruvuma hatuna viwanda, kule Kigoma hakuna viwanda, kwa hiyo peleka viwanda maeneo haya ili masoko na uuzaaji uende zaidi katika nchi za nje. Sisi tusiwe soko la wenzetu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akiweka vipaumbele katika maeneo yale ya mipakani kwanza atafungua maendeleo. Lakini vile vile atafungua uuzaaji wa bidhaa zetu nje. Kwa hiyo, naomba sana lile eneo la Songea kwa maana ya *EPZ* lipewe kipaumbele lakini vile vile Madiwani wa Manispaa ya Songea wapewe mafunzo kama madiwani waliotoka Manispaa nyingine kujifunza masuala ya *EPZ* ili waweze kuupokea mradi huu kwa vizuri na kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la Vyama vya Wafanyabiashara *Chamber of Commerce, Tanzania Private Sector Foundation* na kadhalika. Nawashauri wafanyabiashara wa nchi yetu wajijunge na vyama vingi ili kuleta umoja, ili kuwe na sauti moja kwa sababu kuna changamoto nyingi sana zinazowakabili wafanyabiashara lakini vile vile tunahitaji zaidi *private sector*. Kwa hiyo, ni vizuri wafanyabiashara wetu waweze kuijunga ili kusudi kuweza kuleta sauti moja na Serikali pia itoe motisha ili

kuweka kwamba watu wote wanaofanya biashara wawepo kwenye hivi vyama, bila kuwepo kwenye hivi vyama manufaa mengi sana na fursa nyingi sana, wafanyabiashara zitawakosa kwa sababu watakuwa nje ya mifumo iliyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana kwa taasisi yetu au chuo chetu cha *CBE* kwa kuanza kutoa mafunzo ya ujasiriamali. Mafunzo haya jamani yatatusaidia. Watu wote tunajua kwamba Watanzania hatuko makini sana katika ufanyaji wa biashara. Kwa hiyo, tunachohitaji ni mafunzo. Kwa hivi tunaomba *CBE* wajitahidi katika hayo mafunzo yaenee, yaenee katika nchi nzima kama Taasisi nyingine nilizozisema hapo juu zinavyojitahidi kufanya kazi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia mafunzo yale yajikite katika uzalishaji. Ndugu zangu kinacholeta maendeleo ya nchi ni uzalishaji na si uchuuzi. Sasa kama ujasiriamali wetu utakuwa ni wa kuchukua pesa kwenda kununua bidhaa za Dubai na kuleta hapa nchi itashindwa kuendelea. Ni lazima tujikite katika uzalishaji ili nchi yetu iweze kuuza huko nje. Sisi Tanzania hatuwezi kuendelea kuwa wanunuvi. Ni lazima tuwe wauzaji ili nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia mafunzo yale yatolewe zaidi kwa wanawake kwa sababu tumegundua kwamba wanawake ni makini sana katika kufanya biashara. Kwa hiyo, wanawake wakiwezesha zaidi, biashara itakuwa kwa haraka katika nchi yetu. Kwa hiyo, wanawake wengi wapewe yale mafunzo ili kusudi waweze kuchangia katika mfumo mzima wa faida kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kuniruhusu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waziri mwenyewe mwanamke. Kwa hiyo, hiyo habari imefika. Kwa hiyo tunakwenda kwa Mheshimiwa Maulidah Komu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndesamburo na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro pia ajiandae.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya uchumi wa nchi hii na duniani kote. Hiki kitabu kimepambwa vizuri kweli na kabla sijakisifia kwanza niwasifu wenyewe Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na pia niwaambie waelewe kwamba mahali pakiwa na akina mama huwa panakwenda vizuri hasa kwa mapambo. Watuwezeshe tutaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianza tu na hiki kitabu Wizara inaeleza dira yake na dhima nzima. Kwa hiyo, ukiisoma dira ya Wizara na dhima ya Wizara ambayo ndiyo dhamira zao za kufanya, utaona kwamba nchi hii ikiendana na yaliyomo humu ndani basi

tutatokana na kutoza kodi ya pombe na sigara na vinywaji. Lazima tutakuwa na kitu kingine mbadala kwenye miaka inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuomba uniruhusu ninukuu kitu kidogo tu Dhima ya Wizara, inasema:-

*“...kujenga na kuimarisha ujuzi katika biashara na kuweka msukumo zaidi katika kutumia fursa za masoko; na kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mkulima. Kama tunazungumza kuhusu viwanda na biashara, ina maana tunazungumzia mkulima. Tunarudi palepale kwenye Kilimo Kwanza, mkulima wa Tanzania aliyetoka kibyongo kwa ajili ya jembe, mkulima wa Tanzania anayelima chakula chake kwa ajili ya senti kidogo za kumpeleka mtoto shule, mkulima wa Tanzania ambaye yuko kwenye dunia ya kufikirika kwamba yeye atawezeshwa kwa *power tiller* ili awe mkulima wa kutoa mazao ya kupeleka kwenye hivyo viwanda tunavyovizungumza ili tupate hayo masoko, tupate hiyo pesa ambayo italeta tija katika nchi yetu, ni mkulima yupi? Hivi tumeshakaa tukafikiria jinsi ya kumwezesha huyu mkulima? Tumeshakaa tukafikiria jinsi ya kuweza kuwaweka hawa wakulima kwa pamoja ili waweze kuwa kitu kimoja? Kwa sababu tunasema penye wengi pana mambo mengi, labda wakikusanya kwa pamoja, wakalima kwa pamoja, wakawezeshwa kwa pamoja, wangeweza kutoa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza kwamba tumefungua milango ya biashara, tunafungua milango ya ajira, tunafungua milango ya kila kitu na nchi zetu za *East Africa*, lakini je, tulizungumza kuhusu viwanda? Kila kwenye matunda kiwekwe kiwanda, ni kwenye matunda yapi wakati embe zetu zina madonda? Kwenye matunda yapi wakati nyanya zinazotoka Tanzania, ukikata nyanya unakuta mdudu? Ni kwenye mazao yapi ambayo tunayategemea bila ya kutoa elimu kwa mkulima, bila ya kuwawezesha na madawa ya kuweza kutibu hii miti ambayo tunayo sasa? Hivi vizalia ambavyo tunavyo sasa, ambavyo vinazalisha vitu vyenye magonjwa, ukiangalia embe ambayo inatoka kwa wenzetu unasikia raha, hata kama haina ladha lakini unaiangalia kwa raha. Sisi embe zetu zenye ladha, ukilikata usipokuta huko mapingili ya vitu vya ajabu, utashangaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumbaki na vitabu hivi, hebu basi kama tumewenza kutengeneza haya mambo ya kitaalamu humu ndani ya hiki kitabu basi tuyafuate. Hata kama itachukua miaka mitano mingine, ni afadhali kuliko zile hadithi kwamba, aah, lakini baada ya miaka mitano mambo yatakwenda vizuri. Sasa watakaokuwa hai, wataona wakati huo, miaka hiyo mitano lakini sio sasa hivi, hali ni mbaya, sasa hivi wakulima wetu hawataweza kutoa hiyo tija tunayoizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi kwenye hivyo viwanda, ni vipi? Viwanda vipi, hivi tulivyoviuwa? Tulivyokula mpaka mzizi? Ndio tunavyovizungmza hapa? Viwanda vipi? Msemaji wa Kambi ya Upinzani hapa amezungumza kuhusu *General Tyre*, kila siku akisimama anazungmza *General Tyre*, kila siku akisimama anazungumza viwanda vyta ngozi, kila siku akisimama anazungumzia viwanda, ni viwanda kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali imesema haiingii huko, sasa ni nani tutamuachia huko ili tuhakikishe kwamba viwanda vyetu kweli vinaimarika? Hii itasaidia ili mazao baada ya kutoka huko kwa mkulima tunapeleka kwenye viwanda vyetu na viwanda vyetu vinatengeneza hivyo vitu na tunapata soko la nje ambalo linatambulika kiulimwengu. Ukizungumza kwamba nakwenda kununua vitu Tanzania, unakwenda kununua vitu vyenye ubora wake. Sasa basi turudi, tukakae kitako tuvitengeneze hivyo viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumza masoko ndio kabisa, masoko haya tuliyoyaacha wazi hivi? Mchini leo anaiza fulana Kariakoo! Masoko yapi? Unategemea mtu atakayetoka nje na milango tumeshaiacha wazi aje Tanzania kuweka hayo masoko, hiyo pesa itabaki Tanzania? Haibaki hiyo. Ulimwengu wa wawamba ngoma, kila anayewamba anavutia kwake, akipata atakwenda kupeleka kwake hataacha hapa. Kwa hiyo, kama hatutakuwa na uangalifu wa kutosha, tatarudi palepale, Mtanzania hana atakachokipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi juzi nilikuwa nazungumza na mtu ninamwambia hee, basi wewe kwenye kiwanda unaweka mpaka washonaji wa kutoka nje kwani sisi hatufai? Akasema mnafaa sana, lakini mimi sasa hivi hapa nitaweza kutoa kazi, huyu anatia mkono, huyu anaweka kola, huyu anapinda, huyu anaweka vifungo, niwape *group* hii wafanye na niwape *group* hii wafanye, uone jinsi Watanzania tulipofikia. Nikasema sawa. Watu wamepewa pale, wenzao wameshatengeneza mashati matatu, manne, wao ndio kwanza wako kwenye shati moja. Basi hata hawa Watanzania wenyeewe inabidi tuwarudie tena, tufanye tena kazi ya kuwaambia Watanzania, ni lazima sasa tuamke. Kama tuna uhuru wa masoko, kama tunataka kurudisha tena uchumi kwenye viwanda, basi na sisi tuamke tena tufanye kazi kama wenzetu wanavyofanya kazi. Tuache hii bla-bla, kuongea, ooh, tunaongea sana. Hatumtaki afanye, eeh, lakini wewe unafanya nini, unaifanyia nini nchi yako wewe mwenyewe binafsi yako? Kama nitakupa shati ulishone kwa masaa matatu na nitampa mungine wa kutoka nje shati hilo hilo akalishona kwa nusu sasa, nitaacha kumuajiri yule wa nje ambaye atanishonea kwa nusu saa? Sasa turudishe tena elimu kwa Watanzania, kama kweli tunataka kufufua masoko, kama kweli tunataka huko tunakokwenda kodi isitoke tena kwenye pombe, kodi isitoke tena kwenye sigara, kodi isitoke tena kwenye *ma-guest house*, basi tuwaelimishe tena Watanzania. Hawa vijana wanaopita, nguvu kazi imejaa tele humu, nguvu kazi imejaa tele, lakini jinsi ya kuitumia ndio tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe siku moja nilisimama hapa nikasema, niliona na Kigoma walifanya, hivi tukikusanya hawa vijana, tukawapa elimu, ardhi hii tuliyonayo humu, wakajua jinsi ya kulima mazao bora, kwa miaka miwili tu,

wao wenyewe watanufaika na nchi itanufaika. Wapi! Watu wanaendelea kutoa mpaka mabati kwenye vituo vya mabasi, usiku wanakwenda wanang'oa mabati, nguvu wanazo, tukae kitako tuzitumie hizo nguvu zao, tunashindwa kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana na ninarudia tena kuiomba Wizara hii, Mwenyezi Mungu amjalie Mheshimiwa dada Mary arudi, lakini asiporudi akirudi mwingine, basi atakayoyaacha Mheshimiwa Mary Nagu, yafuatwe. Haya yaliyomo humu katika hiki kitabu, hiki kitabu sikitupi, ninamuomba Mungu nirudi tena hapa, hiki kitabu ninakitungia kama Msahafu, hiki hiki kitabu ndio nitakuja kukigongea Serikali itakayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba haya yaliyopo humu, ukipata muda kaa kitako, kwa taratibu upitie hiki kitabu uone kama hatutakuwa na mbingu nyininge huku Tanzania. Lakini ni hivyo hivyo, mahodari wa kutengeneza vitabu vizuri, mahodari wa kuandika maneno mazuri, mahodari wa kusema hapa, ooh, Mtanzania hodari sana, lakini sasa tukae tutekeleze, ooh, Ilani ya CCM, Ilani ya CCM, Ilani ya CCM, Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika mada hii iliyoko mbele yetu. Mimi inanipa tabu kidogo kujuua au kuelewa Wizara hii inalindaje viwanda vyetu. Wizara hii inaendelezaje wafanyabiashara wa Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani Wizara hii kazi yake ni kulinda viwanda ili nchi hii tuweze kuwa na uchumi ambao ni mzuri. Lakini tatizo ambalo sidhani kama tumewahi kuli-*address* ni tenda, *Tender Board* inahujumu viwanda vya nchi hii. Nalisema hili kwa sababu *Tender Board* imefanya madhambi mengi sana katika nchi hii. Badala ya kuita tenda iangalie ndani ya nchi ni kipi kinapatikana, lakini msisitizo unakuwa ni chochote kile, hata kama kinapatikana China kwa dola moja na Tanzania dola moja na nusu, atapewa China kwa sababu ni dola moja. Lakini ukweli wenyewe, unahujumu Watanzania, kwa sababu unalinda watu wa China na unawasahau watu wa nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tenda za siku hizi, mimi ninazilaumu sana. Tumejifunza mengi, ndege ya Rais, bei ya tenda iliyopatikana ni mara mbili ya bei ya kiwandani. Lile lilikuwa ni fundisho tosha la kuelewa kwamba tenda haiitendei haki nchi hii. Rada iliyonunuliwa kwa bei mara tatu, ni tenda. Ni nani hawa wenyewe kufanya tenda? Kuna watu watatu au wanne pale Dar-es-Salaam, wala hawazidi, ndio wanatumia *almost 70%* ya *11 trillions* tunazopitisha hapa, *70%* zinakwenda kwenye *procurement*. Sasa kama tunaruhusu tenda zifanye kazi hiyo, ni vipi viwanda vyetu vinaweza kuuza kitu? Hata kama vinazalisha, ni uwongo, havitawenza kuuza katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukue mfano wa viti hivi tunavyovikalia humu ndani, viwanda vyetu vingeweza kuvitengeneza hivi lakini tenda, vyote hivi vinatoka nje. Sasa unajengaje uchumi wa nchi? Unajengaje viwanda katika nchi hii? Unalindaje viwanda vyetu katika nchi hii? Kama hili dude linaloitwa tenda ndilo linafanya manunuvi

yote ya nchi hii na halijali viwanda vyetu. Ni jambo ambalo ni lazima tufikirie sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka katika Awamu ya Kwanza ya Mwalimu, *furniture* za *State House*, walitengeneza Kikundi cha Vijana wa Gezaulole, ndio walitengeneza na alikuwa analinda watu wa nchi yake ambao wanafanya biashara na wana viwanda vidogo vidogo lakini kwa sasa ninadhani ni lazima tubadilishe mfumo wetu wa uendeshaji wa uchumi wa nchi hii. Ni rahisi kabisa kujua bei ya chochote duniani kwenye mtandao, unakwenda kwenye mtandao unajua kabisa kitu hiki bei yake ni fulani lakini *Tender Board* inaweza kutoa mara tatu, hivi tuna wazimu gani? Hivi hawa watu watatu pale Dar-es-Salaam, deski moja na karani, kazi yao ni kuchukua magazeti na kuangalia tenda za nchi hii ziko wapi? Hivi Serikali, hiyo *Tender Board* haina wataalamu au sisi wenyewe hatuna wataalamu wanaojua bei za vitu duniani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalisema hili kwa sababu tumeona bei ya rada ni bei gani, tumeona ndege ya Rais bei ilikuwa ni mara mbili, sio hivyo tu ni vitu vingi. Leo hivi hapa ukitaka ku-order *toilet paper* Uchina, utanunua kwa senti mbili, lakini viwanda vyetu hapa nchini vinakufa kwa sababu hatutawapa zile tenda, hivi kweli tunalinda viwanda vyetu au tunaviuwa? Ni lazima tuliangalie hili dude la *Tender Board*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hiyo tu, hizi tenda zimekwenda mpaka Mikoani, mpaka kwenye Wilaya. Leo hii *power tiller* ambazo ndio tunataka kutumia kwenye Kilimo Kwanza, zimekuja nchini hapa kwa bei tofauti tofauti. Nyingine milioni tatu, milioni tano, milioni sita na zote hizi ni tenda. Hivi hatuna akili ya kwenda kiwandani tukajua bei? Yaani Tanzania nzima tumeshindwa kujua bei ya chombo fulani katika kiwanda? Ni lazima tu-change our mentality, ni lazima tu-change our mindset, sio lazima twende tu kama tulivyozoea, ni lazima tubadilike ndugu zangu. Hili ni la msingi na ni lazima tubadilike. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashangaa, mwaka jana tukiwa na Kamati, nilikwenda *Government Printer*. *Government Printer* wakasema wanaweza ku-print karatasi za kupigia kura za mwaka huu tena kwa bei nusu ya zile za tenda wanazotoa, badala ya kutumia kiwanda chetu cha *Government Printer*, tumeita tenda na hii itakwenda nje. Hivi tuna wazimu au tuna akili? Sisi tumeleta uhuru wa nchi hii, hawa vijana ambao wamechukua nchi hii sasa hivi, wana uchungu na hii nchi? Sisi tuna uchungu na hii nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea labda nitoe pole kwa vijana wangu wa pale Moshi Mjini waliopigwa juzi. Nawapa pole sana na msimamo wao uwe ule ule, wasiwe na mashaka, tutafanikiwa, hakuna shida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie viwanda vidogo. Jimbo langu la Moshi, niliwahi kutamka humu ndani nikasema vile viwanda ambavyo vimebinafsishwa na haviendelezwi, ningeomba nipewe ili niviendeleze. Lakini kwa bahati mbaya, vile viwanda vyote vilikwishauzwa, kwa hiyo Serikali haina tena kiwanda pale Moshi. Ningeara ni vyema tukamuomba Mheshimiwa Rais, aka-revoke zile title, tukaomba vile

viwanja, wakaondoa mabanda yao, tukajenga viwanda na mimi niko tayari kufanya hilo, kwa sababu, vile viwanda vimefungwa, vijana hawana ajira. Kwa hiyo, hilo ni ombi langu tena la pili kwa ajili ya watu wangu wa Moshi. Mheshimiwa Waziri, ninaomba wakati wa kujibu, unijibu, ili njue kama mta-revoke ili tuipate ile ardhi tujenge upya viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Pale Moshi tuna matatizo ya machinga...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji*)

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu. Ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dokta Mary Nagu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zao, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ambayo wanafanya kuendeleza viwanda, biashara na masoko katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia katika kuchangia hoja hii, pengine na mimi ningechukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati sana wananchi wangu, ndugu zangu wa Wilaya ya Mkinga, kwa kunipa ushirikiano mzuri sana kwa miaka 10 mfululizo. Kwa pamoa, tumeweza kutekeleza takribani 95% ya Ilani ya Uchaguzi. Ninapenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano huu. Vilevile nawashukuru viongozi wa Chama na Serikali katika Wilaya na katika Mkoa wa Tanga, kwa ushirikiano huo ambao umetuwezesha kufanya haya tuliyofanya. Sasa hivi mabadiliko yaliyofanyika ni makubwa sana na wale wanaosema kwamba Ilani ya CCM haitekelezeki, walie tu, ni maneno ambayo hayana msingi wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ninapenda kuchangia hotuba hii kwa kusema kwamba kama ambavyo Ilani ya Uchaguzi imebainisha, ilisema kwamba viwanda ni sekta kiongozi na kwa msingi huo, tunaelewa kwamba shughuli nyingi za uchumi zinategemea sana shughuli za viwanda ili kupata msisimko, ili kupata maendeleo. Nilipata faraja kubwa sana wakati tunazungumzia mapendekezo ya bajeti katika kikao kilichopita, tukaainisha kwamba sekta ya viwanda, biashara na masoko, nayo ingekuwa ni sekta ya kipaumbele. Lakini kihalisia kama ambavyo tumeona katika hotuba ya Waziri leo na hotuba nyingine zilizotolewa, kipaumbele hicho hakipo, hii sio sekta ambayo inapewa kipaumbele. Kusema kweli hili ni kosa ambalo inabidi tujisahihishe kwa sababu ili tuendeleze Kilimo Kwanza, kiwanda kina umuhimu mkubwa sana, kwanza katika kuwapatia mahitaji muhimu ya kilimo, majembe ya kulimia, mashine ya kuvunia, vifaa vya kuchukulia bidhaa zile, pembejeo mbalimbali, mitambo ya kusindika mazao yanayotoka kwenye kilimo, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili hayo yaweze kufanyika, tumeweka taasisi nyingi za utafiti za maendeleo na kiteknolojia ambazo zitatusaidia shughuli hizo lakini kama ambavyo imeonekana, fedha ambazo zimepewa taasisi hizi ni ndogo sana. Fedha za Wizara yenyewe ni ndogo sana pengine ingesema hata kwamba fedha baadhi ambazo zilikuwa zimewekwa nyingi hapo awali zilipunguzwa baadaye ili kuweza kuweka bajeti sawa. Sasa nasema jamani hebu tujirekebishe kama tunataka kupata maendeleo, naomba muweke fursa hiyo mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu pamoja na nchi nyingine za Afrika Mashariki, tumeingia katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Sasa hali hii inatubidi sisi tujizatiti, tuingie katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, tuweze kuhimili ushindani kikweli kikweli. Ili kufanya hivyo, hatuna budi kuongeza tija, hatuna budi kujitahidi kufanya vizuri zaidi. Ingawaje takwimu zinaonyesha kwamba mpaka sasa hivi tunafanya vizuri katika soko hili na masoko mengine, mauzo yetu yameongezeka lakini ukifanya uchambuzi wa dhati utaona mauzo hayo mengi ni ya malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwenendo tunaokwenda, ni vizuri tukafanya jitihada za kuziongeza thamani bidhaa hizi na ili kuongeza thamani hatuna budi kuongeza idadi ya viwanda, kuboresha viwanda vyetu vikawa na tija zaidi, kukawa na ufanisi zaidi, tukaweza kushindana na bidhaa zinazotengenezwa katika nchi nyingi na bidhaa zinazotoka nje, ili ndani ya soko letu wenyewe katika soko la Afrika Mashariki na katika Soko la Dunia bidhaa zetu ziweze kwenda vizuri. Kwa hiyo, naamini hii ni changamoto nyingine ambayo tumeepata, zaidi ya fursa ambazo tumezipata katika suala hilo na tutaendelea kutia vipaumbele vinavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, masula ya kuendeleza masoko ni masuala muhimu, nashukuru sana kwa jitihada ambazo Wizara imefanya mpaka sasa hivi lakini bado kuna jitihada kubwa sana ambazo zilihitajika. Kama wengi ambavyo tumesema, tuna matunda mengi, tuna bidhaa ambazo zinaharibika mashambani kwa sababu hakuna utaratibu mzuri wa masoko endelevu. Masoko haya, nashukuru kwamba jitihada kubwa zimefanywa, tumeboresha masoko ya awali, tumeboresha masoko ya kimataifa lakini kuna masoko mawili ambayo tumezungumzia muda mrefu sana na mpaka sasa hivi bado hatujaona dalili ya maendeleo yake. Kuna Soko la Kimataifa la Mbogamboga na Matunda la Segera, tumezungumza siku nyingi lakini mpaka sasa hivi hatujaona hatua ya maendeleo iliyotolewa. Vilevile kuna Soko la Kimataifa la Makambako, tumezungumza muda mrefu sana lakini hatujaona hatua ya maendeleo inatoka pengine hii inatokana na hali ya ufinyu wa bajeti ulipo lakini tuelewe ufinyu huu tunaojinyima sisi, unatupunguzia maendeleo yale ambayo tunayoyataka katika shughuli hizi. Kwa hiyo, naomba hilo lipewe kipaumbele maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NDC* ina miradi mikubwa muhimu sana ya Mchuchuma na Liganga. Miradi hii inahitaji fedha nyingi sana za maendeleo lakini kama ambavyo imeelezwa katika bajeti yetu hii na katika hotuba ambavyo amesoma Mwenyekiti wa Kamati yetu, fedha zilizotolewa kwa ajili hiyo ni ndogo sana na haitowezeka kwa *NDC* kuweza kushiriki katika shughuli ilizopangiwa. Kwa hiyo,

tunashauri na tunasisitiza suala hili liendelezwe na nalitilia mkazo kwamba Serikali ifikirie namna ya kuipatia *NDC* fedha zaidi ama kuwa na bajeti ya pekee ili iweze kutekeleza miradi ile mikubwa ya kimaendeleo ambayo imewekwa katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ina kazi kubwa sana ya kuelimisha wananchi, ina kazi kubwa sana ya kukopesha wananchi, kama inavyoonekana imepewa fedha ndogo sana za kuweza kufanya shughuli hizo na maendeleo yale inayotarajia ya kuwafanya wafanyabiashara wadogowadogo wenye viwanda wadogo wadogo waweze kupata maendeleo, kwa mtindo huo hawawezi. Kwa hiyo, naweka mkazo kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kufikiria shughuli hii ipate fedha za kutosha ili kuweza kuendeleza viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingine za utafiti mfano *TIRDO, CAMARTEC* na nyingine, zina kazi kubwa sana ya kuendeleza teknolojia za sasa hivi. Kwa mfano, haya mambo ya *biogas*, sisi hapa kwetu tumefanya utafiti mkubwa, tumeendeleza suala hili lakini tunashindwa kuendelea mbele zaidi kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kuendeleza utafiti huo. Wenzetu Rwanda, wamechukua teknolojia hizo na sasa wanazitumia kwa fedha kubwa sana yao wenyewe. Kwa hiyo, naomba sana kwamba Serikali katika kupanga bajeti yake kama vile ambavyo Ilani iliainisha kwamba hii ni sekta kiongozi maana yake ni kwamba ipewe upendeleo maalum kuweka kipaumbele iweze kufaidisha wananchi katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mradi huu wa *Soda Arsh*, ni mradi mkubwa sana ambaio utasaidia si tu kukombolea na vitu vingine lakini vilevile kutusaidia nchi nzima katika shughuli zetu. Kwa hiyo, mradi huu ufuliwe haraka uwezekano ili kuweza kuleta hizo faida zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa *General Tyres*, nashukuru Mheshimiwa Waziri ameелеza kwamba jitihada zinafanywa kufufua haraka iwezekanavyo mradi huu. Mimi mwenyewe nimefika pale kiwandani, kuna haja ya kufanya hiyo haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mashamba ya mipera iliyopo Muheza na sehemu nyingine, nayo yanahitaji kupatiwa fedha za kutosha ili kuweza kufufuliwa ili ziweze kuleta msisimko wa kiuchumi unaotakiwa katika maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la Soko la Pamoja, kuna vijana watakuja kuingia katika soko kwa sababu itakuwa ni soko huria la biashara. Sasa kuna taasisi zetu za mafunzo, *CBE* na nyingine zinahitaji zinolewe ili kuendeleza elimu ya wananchi wetu katika shughuli hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kengele imelia.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo nikiwa na afya. Vilevile nikushukuru wewe mwenyewe Naibu Spika, kwa kutambua kuwepo kwangu katika Kikao hiki cha 21 cha Bunge lako Tukufu, Bunge la Viwango na Kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia nisisahau kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, vilevile pongezi hizi zimwendee Katibu Mkuu wa Wizara hii na watumishi waliomo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, ninapenda niongelee sana katika sekta mbili, sekta ya kwanza iwe ni viwanda, ikifuaatiwa na masoko. Nikianza na viwanda, katika uchumi wa nchi yoyote ile, tunatambua wazi kwamba viwanda vinayo nafasi kubwa ili sera tunayoizungumzia kila leo ya Kilimo Kwanza iende vizuri ni lazima iende sanjali na Sera ya Viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazao yetu yawe ya chakula, yawe ya biashara ni vyema tukaliangalia kwa undani sana kwamba mazao haya yamfikie mlaji yakiwa yamesindikwa na usindikaji huu unafanyika katika viwanda, iwe viwanda vidogo au vikubwa. Viwanda si kana kwamba vinaongeza thamani ya mazao na viwanda pia kwa kiwango kikubwa sana huongeza ajira za wananchi wanaozunguka katika maeneo yale na sio suala la kuongeza ajira tu, viwanda hivi hivi pia katika mchango wake wa kodi huongeza mapato ya Serikali, huongeza mapato pia hata ya Halmashauri katika maeneo yaliyojengwa viwanda hivyo. Kwa hiyo, viwanda tuvichukulie kama ni kitu muhimu sana katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Korogwe, hususan nikiongelea Korogwe Vijijini tunayo bahati nzuri, tunao wakulima wazuri sana wa mboga na matunda lakini kwa masikitiko makubwa naweza nikasema kwamba Korogwe hatuna hata kiwanda kimoja. Sisi tumekuwa wauzaji au wapelekaji wa malighafi wa wenzetu. Nchi jirani viwanda vyake vya matunda, mboga vinategemea sana, kwa kiwango kikubwa eneo la Korogwe. Hii inasikitisha na sio kusikitisha tu bali naweza nikasema kwamba ni aibu hata kwa Taifa sisi tuuwiwe *juice* na wazalishaji wakubwa wa vyanzo hivyo vya *juice* ni sisi badala ya sisi kutengeneza *juice* na kuiiza wenyewe hapa nchini na pia ikiwezekana kuisafirisha. Umefika wakati sasa tuliangalie hili. Korogwe tunahitaji viwanda, nahofia kwamba hata tukiingia kwenye huu muungano wa Afrika Mashariki, si ajabu wenzetu hawa majirani, hawatahitaji ardhi yetu bali kuna uwezekano wakatutumia sisi kwa kutumia ardhi yetu wenyewe, kwa kutumia mashamba yetu wenyewe, tuwalimie matunda halafu wao waje wachukue kirahisi, watuuzie vitu ambavyo ni *processed*, hii ni hatari kwa nchi na kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema Korogwe tunalima sana mboga na matunda, lakini si hivyo tu Korogwe kuna wakulima wazuri sana wa chai, Korogwe tuna ushirika

wetu unaitwa Sakari *Joint Cooperative*. Ushirika huu una takriban hekari zisizopungua 400 za chai, chai ambayo inavunwa, hivi sasa tunavyoongea chai hii nyingi inaishia mikononi mwa wenyi viwanda vikubwa. Ushirika huu una watu karibuni 1800 na kama nilivyosema una zaidi wa hekari 400 zinazovunwa hivi sasa. Mimi kwa maoni yangu, ushirika huu ungesaidiwa kupatiwa kiwanda cha kusindika na kukausha chai yake badala ya kutegemea kuiza kwa hawa wenzetu wenyi mashamba makubwa. Najua juhudzi zimefanyika, kwa muda mrefu sasa za kupata kiwanda lakini naiomba Wizara hii ijithadi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chai, kwa maana Bodi ya Chai itupatia kiwanda hiki tusindike wenye hii chai, tuikaushe wenye hii, mtakuwa mmetusaidia wenzetu wa Wizara hii. Wakulima wa zao hili wanapunjwa sana na ndio tegemeo lao kubwa la kipato. Sehemu kubwa ya Korogwe kwa maana ya Kata ya Bungu, Kata ya Dindira, Kata ya Vugiri pato lao litokana na zao hili la chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo kuhusu masoko, tunatambua wazi kwamba masoko ndiyo vituo vyatia kukusanya na kuuza mazao yetu. Napenda niipongeze Serikali au Wizara hii kwamba imetuwezeshea kujenga soko moja katika eneo letu la Korogwe Vijijini eneo la Makuyuni kwa ajili ya kukusanya mazao yanayotoka sehemu kubwa ya Magharibi mwa Jimbo letu la Korogwe, hongera sana, tunawapongeza sana wenzetu wa Wizara kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kutohuna na ukubwa wa Jimbo hili la Korogwe Vijijini, wananchi wa Korogwe Vijijini, upande wa Mashariki, wanaomba kilichofanyika upande wa Magharibi, basi pia kifanyike upande wa Mashariki. Kwa sababu kutoa mzigo kutohuna na gharama za usafirishaji kuwa kubwa. Kwa hiyo, hili ni ombi lao rasmi ambalo wamenituma nililetie kwenye Wizara hii ikiwezekana wenzetu wa Mashariki nao kwa maana ya ukanda huu wa Tarafa ya Magoma, wapatiwe soko kama lile ambalo lipo Ukanda wa Magharibi. Ukanda huu wa Mashariki unafahamika sana kwa mazao hususani ya chakula na si chakula tu hata matunda pia ni wakulima wazuri wa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante. (*Makofii*)

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja na kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika maeneo machache, nianze kwanza kuishukuru Wizara kwa uamuza wao wa kuhakikisha kwamba *CAMARTEC* inahama toka kule ilipokuwa na kuja Mjini Arusha. Nasema ahsante sana *CAMARTEC* imeingia Mjini Arusha. Tumeona walivyoingia, wameingia vizuri, tunawapongeza kwa jinsi walivyoingia Arusha na kazi ambazo wanazozifanya zinazoonekana wazi pale Mjini

Arusha. Mimi nisisitize kwamba kwa kazi hizo nzuri na kubwa wanazofanya wenzetu wa *CAMARTEC*, Serikali isiwe na kigugumizi, iwawezesha kwa nguvu zote ambazo Serikali inazo na sisi kule Arusha tunawahakikisha kwamba watapata ushirikiano wetu wa kuhakikisha kwamba wanafikia kwenye malengo waliyojiwekea, kwa sababu malengo ni mazuri yanaleta matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze *SIDO* kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wilaya yetu ya Arusha, vijana wetu wanafundishwa, wanawezeshwa, wanasaidiwa kuwa wajasiriamali. Tuwapongeze *SIDO* kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika Jimbo langu la Arusha. Kubwa zaidi ni hilo hilo nasema *SIDO* wawezesha ili waweze kufanya *corporation* yao kama walivyojipangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nijikite kwenye hili suala la *General Tyre*, *General Tyre* lazima nikiri sijaridhishwa na hayo ambayo Mheshimiwa Waziri ametueleza na jinsi wanavyosimamia suala zima la *General Tyre*. Ukrejea hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka jana, alitoa ahadi nyingi sana zilizonipa mimi matumaini. Sasa namuomba arudie tena zile ahadi zake mwenyewe tu, ahoji nafsi yake ipi amatekeleza na ipi bado hajatekeleza na aanze kazi ya kutekeleza yale ambayo alisema atayafanya. Pengine hakuwa na sababu ya kutushirikisha sisi, mimi sisemi kwamba lazima tushirikishwe lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba *General Tyre* inafufuliwa kwa sababu hii *strategic industry* ambayo ni muhimu kwa uchumi wetu wa Tanzania, ni muhimu sio tu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunazalisha tairi zinazotosheleza soko letu, lakini pia tairi za kuweza kutosheleza soko la Afrika Mashariki lakini kubwa zaidi ni *rubber industry* hapa Tanzania, *General Tyre* inaweza kuwa ni kichocheo kikubwa cha kufufua *rubber industry* katika nchi yetu ya Tanzania, Mikoa ya Tanga, Morogoro na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya umuhimu wa *General Tyre* kusema kweli siwezi kuelezea zaidi. Kwa hiyo, lazima tuonekana tunaisukuma na tunahakikisha kwamba hii *General Tyre* inafufuliwa upesi iwezekanavyo. Kukaa mwaka mzima tunashindwa hata kuzungumza na wale wabia wetu, hairidhishi. Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, nakuombea Mungu wewe na Naibu wako, mrudi hapa Bungeni mwakani ili mtakaporudi mkamilishe kazi hii mliyosema mtaifanya ya kufufua *General Tyre* na naomba Mwenyezi Mungu mrudi kwenye nafasi hizo hizo mlizonazo ili muweze kukamilisha kazi hii, maana wananchi wa Arusha wanawategemea, sisi wote tunawategemea, tunategemea *General Tyre* ifufuliwe itoe mchango katika safari yetu na mimi naamini naweza kutoa mchango mzuri sana katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la *General Tyre*, yako yale mafao ya wafanyakazi, mpaka leo naona wanazungushana mara *Consolidated Holdings* wana misimamo yao, *PPF* kadhalika wana misimamo yao, wanabishana mambo ya *termination* na *retrenchment*, aah! Mimi naomba bwana tuwaangalie wale wafanyakazi, Mheshimiwa Waziri kabla hujamaliza kazi yako hiyo, tatua tatizo hili la mafao ya wafanyakazi ili

ninaporudi Jimboni nisiwe na hilo tatizo tena. Mheshimiwa Waziri tafadhali sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuzungumza mengi, lakini kubwa zaidi ni kwenye mambo ya *industries*. Serikali isione haya ikionekana inachangia, kusaidia na kuzibeba *strategic industries*, tusione haya kwani kila nchi duniani inaanua *industries* gani ni *strategic* halafu inawekeza nguvu zake katika hizo *strategic industries*, tusione haya! Haya mambo ya kusema tunajitoa, yamepitwa na wakati, nchi zote duniani zinarejea hasa kusaidia vile vitu ambavyo wanaviita ni muhimu katika uchumi wao na ninaomba Serikali izingatie hilo na isione haya. Mimi nasema kama tumeweza kupata *123 million dollars* kwa ajili ya *rescue package* ya kusaidia zile shughuli zilizoathirika na mtikisiko wa kiuchumi, tunashindwaje kupata *10 million dollars* ya kusaidia *General Tyre*? Tufanye kazi hii kwa ari ya ziada na nguvu ya ziada ili tuondoe hii aibu ambayo kusema kweli viwanda vyetu hivi vinaonekana kama havina mwenyewe na wakati ni vya kwetu na ni muhimu kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nimalizie tu kwa kusema nawashukuru sana wananchi wa Arusha, kwa heshima ya kipekee walijonipa ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha zaidi ya miaka 12. Haijapata kutokea katika historia ya Jimbo langu, Mbunge kuwa Mbunge wa zaidi ya kipindi cha miaka 10 lakini mimi nimevunja rekodi. Nawashukuru sana wananchi wa Arusha kwa heshima ya kipekee walijonipa. Katika kipindi chote, tumefanya mambo mengi makubwa kwa pamoja na sina hofu hata kidogo, tumetekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa hiyo, mimi nina imani kubwa kwamba Jimbo la Arusha litaendelea kuwa Jimbo na ngome ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya katika kipindi cha miaka 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kabisa wako watu wengi wameshakuja na wametangaza nia, nawakaribisha, karibuni. Ni haki yao na wengine wameamua kuzinduka dakika hizi za lala salama, wanapitapita pamoja na nafasi zao kubwa na nzuri walizokuwa nazo, nawaambia karibuni.

**MBUNGE FULANI:** Wanakumbuka shuka asubuhi.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Wanakumbuka shuka asubuhi lakini nawaambia karibuni na ninawaambia wananchi wa Arusha nipo, narejea na tutakuwa pamoja katika kuliendeleza gurudumu la maendeleo la Jimbo letu la Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sisi tunakutakia kheri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ruth B.Msafiri na Mheshimiwa Juma S. Kaboyonga ajiandae.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninachukua nafasi hii kumpongeza mtoa hoja Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Wizara hii, nampongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote walioshiriki kwa ufanisi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inahusika katika maeneo makuu matatu kama ambavyo yametajwa na yakaipa Wizara jina. Sehemu ya Viwanda, Biashara na Masoko, ni maeneo ambayo ni mapana sana. Kwa kuwa, muda wetu ni mchache, sitawezza kuyaongelea yote matatu lakini nitaongelea machache kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa jinsi ilivyochangia katika pato la Taifa, katika kipindi hiki tulichomo matatizo makubwa ambayo yalijitokeza kimaitaifa ya mtikisiko wa uchumi wa dunia ambao ulichangia kupanda kwa gharama za uzalishaji ambao ulisababisha hata masoko mengine ya nje yakafungwa. Mtikisiko huo pia ulisababisha hata baadhi ya wachangiaji wetu wakaondoka lakini bado uzalishaji katika viwanda vyetu umeweza kuchangia pato la Taifa kwa kiasi cha 8%, mimi nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba kama kungekuwa hakuna matatizo basi Wizara wangeweza wakafanya kazi nzuri zaidi. Lakini napenda kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuweka bidii na nguvu kabisa katika kazi kwa sababu kazi ni kipimo cha utu. Lakini unapofanya kazi kwa bidii, licha ya kuwa kazi ni kipimo cha utu, unaongeza pato la Taifa na hakuna mtu anayeweza akaishi maisha yaliyo bora bila kuwa anafanya kazi yake kwa bidii inayokuja kuwa ni jibu la maisha bora na ambayo ndiyo mtazamo na mwelekeo wa Chama cha Mapinduzi kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana lakini ni kwa kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukuzaji wa viwanda, Tanzania tumefaidika sana na uzalishaji wa ndani kwa mfano tumefaidika katika uzalishaji wa *cement*. Kuna siku nilipata nafasi na kuzungumza na *TBC*, nawashukuru kwa kunipa nafasi lakini kwa mchana huu ninataka yaingie kwenye *Hansard*. Tumeweza kuzalisha tani nyngi kwa na tunaweza kusafirisha mpaka nje ya nchi. Lakini tatizo ambalo ninaliona mpaka sasa hivi ni kwamba bei ya saruji haishuki, bei ya saruji bado iko juu sana, inatofautiana kutoka Mkoa mmoja hadi mwingine. Sasa hali hii pengine inasababishwa na miundombinu kwamba tunategemea sana kusafirishaji kwa kutumia magari ambayo gharama yake ni kubwa. Labda baada ya Serikali kuwa imetengeneza miundombinu ya reli, tutaondokana na tatizo hili ambalo linaweza kuondoka kwa sababu hatua zimeanza kuchukuliwa. Lakini labda pengine wanategemea wauzaji wadogowadogo wafuate saruji kwenye viwanda na kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo viwanda vingi vya saruji basi wenye viwanda wajipange kuuza saruji hii katika Mikoa wao wenyewe, waweke vituo vyao vya kuuza, wasafirishe wao ili saruji iuzwe kwa bei ya kiwandani isije kuwa watu wanaokaa Tanga

au Dar es Salaam au Mbeya wanunu saruji kwa bei nzuri kuliko mimi ninayekaa Dodoma ambapo hakuna kiwanda, sioni ni kwa nini? Lakini hatuwezi kuwa na viwanda kila sehemu, viwanda hivi viko katika maeneo machache na kwa sababu maalum. Ukienda Kagera sasa hivi sisi tunapata mfuko wa *cement* kwa bei iliyopungua sasa ya shilingi 20,000/= lakini tulishafikia kununua mfuko kwa shilingi 23,0000/= wakati wa bajeti iliyopita. Hatuwezi kujenga, sasa hivi Tanzania majengo ndiyo sera, tunajenga sekondari, madarasa, nyumba za Walimu, maabara ya shule za msingi na sekondari maana tunataka kuyaboresha, hatuwezi kuyaacha majengo ya shule za msingi kwa sababu tunakwenda sekondari ama vyuo, hapana, lakini vyote vinajengwa na tunajenga katika nchi nzima. Sasa hii bei ya saruji ambayo tunaitegemea inatisha, tunaomba bei iwe ile ambayo kila mwananchi ataimudu na iwe bei ya kiwanda katika nchi nzima kwani tunayo saruji ya kutosha, tunaomba mipango mizuri ipangwe na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, bati tunazo nyingi na sasa hivi zimeongezeka sana, kwa sababu ujenzi unakwenda pamoja na bati, ninaomba bati vilevile zisambazwe kwa bei ya kiwandani nchi nzima. Watanzania wawe ndiyo wa kwanza kujivunia vitu vyao wenyewe, kama ambavyo bia imeweza kusambazwa, wanywaji wa bia kwa kweli sasa hivi wana raha, bia zinazalishwa kwa wingi na ziko kila mahali na mtu anapata chaguo lake, bei wamesimamia wao wenyewe hata ushuru ukiongezeka wanasmilia bei wenyewe. Sasa kwa nini mabati na saruji kama bidhaa nilizozichagua, ziko nyingi lakini hizi nimezichagua kuzisemea zinauzwa bei ghali? Ninaomba kwa kweli bei ya bidhaa hizo iangaliwe, bei zibebike na Watanzania wote waweze kupata bidhaa hizo kwa gharama wanayoweza kununulia. Miradi yetu ya maendeleo iende pamoja na hapa tunaangalia miradi ya Watanzania wote amba wanabebe jamii, kuweza kuikomboa kwa wakati mmoja ni lazima kwa kweli bei ziwe ni zile ambazo hazitofautiani. Nimeona sisi tunapokuwa tunapewa na Serikali pesa za kujengea mara nyingi huwa hatumalizi ujenzi kwa sababu bei za vifaa huwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo pengine litakuwa ni la mwisho ambalo ninataka kulizungumzia kama muda utaruhusu ni kuhusu viwanda vidogovidogo. Wakati nachangia katika bajeti iliyopita, nilizungumzia kidogo kuhusu wajasiriamali. Napenda niseme kwamba, ni kweli kabisa wajasiriamali wadogo wadogo ndiyo watakaoweza kukomboa uchumi wa nchi hii. Lakini mimi ninaomba wajasiriamali hawa katika makundi yao, kundi dogo likue, wale wa ngazi ya chini wakue waingie katika uzalishaji wa ngazi ya katni na wale wa ngazi ya katni waingie ngazi ya juu na wale wa ngazi ya juu waingie katika kuchangia uchumi wa Taifa kwa kuwa wanalipa vizuri kodi. Wanapoficha ukweli wa kile wanachokipata, wanaficha usaidizi wao kwa Taifa kwa sababu usaidizi wao unatokana na jinsi wanavyochangia kwenye pato la Taifa na pato la Taifa likikua bajeti yetu inakuwa ni nzuri na misaada itashuka zaidi katika vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika vikundi nya akina mama na katika vikundi nya vijana, japokuwa vikundi vingi nya vijana haviko tayari kufaidika na mikopo hii kwa sababu wao wanataka wapewe kwanza kabla ya kuijunga pamoja na kusema wanataka kufanya nini wakaelekezwa. Sasa hili la vijana lirekebishwe ili vijana waelewe kwamba Taifa hili liko kwa ajili yao, wawe tayari kabisa kupokea maelekezo

wanayopewa ili waweze kufaidika na ujasiriamali mdogo mdogo. Akina mama ambao wameanza mapema na hapa ninaipongeza *SIDO* kwani imefanya kazi nzuri sana katika kuwashirikisha akina mama katika ujasiriamali mdogo mdogo, wengi wameinuka, wana hali nzuri. Lakini wako wengine ambao siyo akina mama walianza mapema wameshakuwa katika hatua ya juu lakini hawako tayari kujirodhesha kuingia kwa wale wazalishaji wakubwa. Kwa hiyo, kila wakati kunakuwa na wazalishaji wadogo wadogo lakini wale walioingia hawakui kibiashara *they don't mature*. Mimi nataka wafike *maturity* na wafike mahali ambapo wanaweza kuondoka katika uzalishaji mdogo mdogo au ujasiriamali mdogo mdogo wakawa ni wazalishaji wakubwa na wakaweza kuliongezea Taifa pato na kisha uchumi wa nchi yetu ukakua pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba muda wangu ni mdogo lakini nimalizie kwa hizi dakika moja au robo iliyobaki suala la viwango vya bidhaa. Ninaomba uzalishaji uzingatie suala zima la viwango kwani bidhaa zisizo na viwango zinatuharibia nchi. Kwa mfano, tunaona mafuta yanaharibu magari, vipuri tunavyotumia havifai, nyaya za umeme tunazofunga hazifai kwani zinapopata hitilafu kidogo tu zinaunguza majumba, hata mafundi ujenzi pia wanajenga chini ya viwango. Ninaomba Tanzania izingatie viwango na Wizara hii naomba itusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na nianze kwa kuwashukuru Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwenye Wizara kwa kazi nzuri. Lakini vilevile kabla sijahau naomba nitamke rasmi kwamba naunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile niwashukuru sana Wanatabora kwa kunipa heshima ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha miaka mitano, tumejitahidi kufanya yale tuliyoweza kufanya na kama Mungu atajaalia nikirejea katika kipindi kijacho, tutaendelea kufanya yale ambayo tumeanza sasa tuyaendeleze tu ili yakae vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niipongeze sana Shirika la *Tanzania Trade Authority* ambalo linachukua kazi ambayo zamani ilikuwa ikifanywa na *Board of External Trade*. Shirika hili linaundwa upya na ndilo linasimamia pamoja na mambo mengine maonyesho ya Sabasaba pale Dar es Salaam. Nalipongeza Shirika hili kwa maandalizi mazuri sana ya Sabasaba na kwa maana hiyo napenda vilevile niiombe Serikali ililee vizuri Shirika hili la *Tanzania Trade Authority* kwa kulipatia misaada stahili ya kifedha pamoja na rasilimali watu na vitendea kazi vingine ikiwa ni pamoja na magari na kadhalika ili shirika hili liweze kufanya kazi iliyokusudiwa kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *propaganda* kule Tabora kwamba Mheshimiwa Mbunge hatogombea safari hii. Napenda nitumie fursa hii niwatoe hofu Wanatabora kwamba mimi bado niko nao na muda muafaka ukifika nitachukua fomu. Hizi ni propaganda za wale ambao wanajaribu kujipenyeza kwenye Jimbo na kuwarubuni wananchi wangu kwamba Mheshimiwa Kaboyonga haji, hapana, ninakuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda, Waheshimiwa Wabunge walionitangulia wamezungumzia umuhimu wa dhana nzima ya viwanda katika nchi na mimi sina haja ya kupoteza muda kurudia hilo. Lakini ukweli ni kwamba viwanda ndivyo vinavyoleta lile fungamanisho linalohitajika ndani ya uchumi wa sekta mbalimbali. Tunazungumzia juu ya Kilimo Kwanza, kilimo hakiwezi kwenda peke yake, kilimo na viwanda ni watoto pacha, wanakwenda pamoja na wanategemeana sana, bila viwanda kilimo hakiwezi kwenda vizuri na kilimo bila viwanda nacho vilevile ni matatizo. Kwa hiyo, ni vitu viwili vinavyokwenda pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pale Tabora tuna Kiwanda cha Nyuzi ambacho kinategemea pamba ambazo zinatoka kwenye kilimo, lakini kwa bahati mbaya nchi hii inauza pamba ghafi nje ya nchi halafu inaagiza vitambaa vyeupe vilivyokwishatengenezwa kwa kutumia pamba ya Tanzania, halafu eti ndiyo tunavibadilisha kuvifanya Khanga na Vitenge. Kwa maana hiyo, ile ajira ambayo ingeweza ikapatikana hapa nchini ya kutumia pamba ukatengeneza uzi, kitambaa ukakibadilisha kuwa Kitenge, Shati au Khanga, tunapoteza. Kwa maana hiyo, nasisitiza kwamba lazima tuwe na utaratibu wa kufungamanisha sekta zetu hapa hapa nchini na hapo ndipo tutakapoweza kujenga ajira za wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara mimi nimekuwa nikizungumzia suala zima la maliasili tuliyonayo hapa nchini ambayo hatujaweza kuitumia ipasavyo. Moja ya hizo maliasili ni *Soda Ash* iliyoko *Lake Natron*. *Soda Ash*, ni *chemical* ambayo inatumika katika viwanda, ni moja ya malighafi muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda. Sasa hivi tunaiagiza *chemical* hii kutoka nje ya nchi, lakini tunayo hapa hapa nchini, tunayo pale *Lake Natron*, lakini tatizo letu ni kwamba bado tunashindana juu ya tathmini ya athari za mazingira kwamba tukiichimba ile *Soda Ash* wale Flamingo walioko kule watakuwa au watahama na kadhalika. Lakini yapo maelezo ambayo yameshatolewa kwamba kuna namna ya kuweza kuzipunguza hizo athari, *Soda Ash* kama itachimbwa na Flamingo wakaendelea kuwepo, lakini kwa nini hatufikii uamuzi? Sasa tatizo la nchi yetu ni katika kufanya maamuzi, jambo zito na muhimu kama hili kwa uchumi wa nchi lakini kila siku tunazungumza hapa kwamba tuko mbioni, tunafanya mkakati, tunaendelea kuchakata na kadhalika yaani hizo mbio haziishi? Sasa tutamaliza lini hii tathmini ya athari za mazingira ili tuweze kujua kama hii *Soda Ash* tunaichimba au hatuichimbi? Hebu tufike mwisho tuweze kufaidika na hii rasilimali muhimu ambayo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *cement*, mimi nitalizungumzia katika sura nyingine. Nitalizungumzia kwa maana ya kwamba ili utengeneze *cement* unahitaji

wafanyakazi ambao sehemu kubwa siyo *skilled labour* ni wafanyakazi tu kama vibarua ambao ni *skilled labour force* katika kiwanda cha *cement* ni asilimia ndogo sana ya wafanyakazi ambao unaweza kuwapata. Sasa kwa bahati nzuri hawa wafanyakazi wa namna hii tunao wengi sana hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, unahitaji malighafi, *cement* inatengenezwa kwa kiasi kikubwa na malighafi inayojulikana kama *Limestone*, takribani 80% ya malighafi ya kutengeneza *cement* ni *Limestone*. Ukienda pale *Dar es Salaam Wazo Hill* ipo na kiwanda kipo pale, wananchi wanaofanya kazi pale na *cement* tunaizalisha, lakini leo hii inakuja kushindanishwa na *Cement* kutoka nchi za nje kama Egypt na Pakistan. Pakistan na Egypt wanasaidia viwanda vyao yaani wanatoa ruzuku ndiyo maana inakuwa rahisi. Dada yangu Mheshimiwa Ruth B. Msafiri ametoka kuzungumza sasa hivi anasema moja ya matatizo ya viwanda yetu ni usafirishaji, ni kweli! Kama huna reli unasafirisha *cement* kwa barabara itakuwa ghali tu. Umeme ni ghali na unatumika sana katika uzalishaji, kwa hiyo, haya mambo yote ni lazima yaangaliwe kwa ujumla wake kwani huwezi tu kusema *cement* ya Tanzania ghali kwa hiyo tunataka ya Egypt na Pakistan, angalia kwa nini *cement* ya Tanzania ni ghali, halafu fanya yale yanayotakiwa kufanya ili *cement* ya Tanzania iweze kununulika. Hilo linawezekana ni suala la uamuza tu kwamba tufanye *study cost structure* ya viwanda vyetu ikoje? Wapi tunaweza kupunguza na wapi tunaweza kusaidia ili tuweze kulinda ajira za wananchi wa Tanzania na viwanda vinavyotumia malighafi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la viwanda mama vya chuma. Chuma cha Liganga ni suala ambalo linazungumzwa siku zote, mpaka leo hii viwanda vinavyoanzishwa hapa nchini kwa ajili ya kuyeyusha chuma, vinayeyusha chuma chakavu, matokeo yake, ili wapate malighafi au chuma chakavu cha kuyeyusha, wanachukua miundombinu kama reli, vyuma vya madaraja, sijui nini, wakati Liganga kule kuna chuma kimelala ambacho kingeweza kuwa ndiyo *inputs* muhimu sana kwenye kiwanda mama cha chuma. Ukishakuwa na chuma, maana yake unazalisha mambo mengine yote. Chuma ndiyo mwanzo sasa. Hebu tuharakishe juu ya jambo hili la kuitumia raslimali chuma kama viwanda mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya *EPZ* na *SEZ* (*Export Promotion Zones* na *Special Economic Zones*). Haya ndiyo maeneo tengefu ambayo kama Serikali ikiisha ya-*identify* yanaweza yakarahisisha utaratibu mzima wa watu kupata maeneo ya kufanya taratibu nzima za viwanda. Hebu tulisaide hili shirika tuliloliunda linaloshughulikia masuala ya *SPZ* ili liweze kusaidia namna ya kuwapatia wale wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika eneo la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa katika sekta hii ya viwanda ni pamoja na kuwa na *skilled labour force*. Lazima kuwe na fungamanisho la kupata watalaaam wanaofundishwa na shule zetu za hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyininge tena, naunga mkono hoja hii muhimu kwa uchumi wetu. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Awali ya yote niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kwa kuendelea kuniamini na kwa kweli yale yote waliyonituma asilimia kubwa tumetekeleza na lililobaki wanalifahamu nalo hilo nadhani liko njiani, tunaweza tukalitekeleza kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Waziri wa Viwanda na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri yenye mwelekeo. Lakini, tokea niingie ndani ya Bunge hili nilipiga kelele sana kuhusu suala la kuanzishwa kwa Kiwanda cha Saruji pale Itigi, na sababu za msingi nilizieleza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya pamoja na suala hili kuchangamkiwa mwanzoni, lakini inaonekana linafifia na hatujapewa sababu za kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *gypsum* iliyoko pale Itigi ambayo inachukuliwa usiku na mchana kupelekwa katika Kiwanda cha Wazo, Kiwanda cha Tanga, Kiwanda cha Mbeya, Rwanda, Burundi na Uganda ni nzuri kuliko hata *gypsum* ya Misri na Iraq. Hili nimelisema sana na ushahidi upo, kwamba ni *the best gypsum* tuliyonayo. Hapa katikati walijaribu kuchanganya changanya masuala yao hayo ya ulanguzi baadaye hili suala liliundulika na likarekebishwa na sasa tuna *the best gypsum*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *red soil*, zile *ingredients* ambazo Mheshimiwa Kaboyonga amezizungumza hapa, zote karibu tunazo. Tunaambiwa kwamba kuna upungufu kidogo wa *lime stones* lakini watafiti na watu wengine ambao wamejaribu kuangalia wanasema maeneo ya Ugwandi sehemu za Wembere kuna *lime stone* ya kuweza kutosha *ku-supplement* ile iliyoko Itigi.

Sasa mahali ambako tuna *gypsum* ya kutosha, tuna *red soil* na *lime stone* ipo halafu ndiyo iliyozuri zaidi, tuna umeme maana tuna miundombinu mingi; tuna umeme, tuna reli, tuna barabara halafu ni katikati ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunashindwa kuelewa kusurasua huko kwa Serikali sababu hasa ni nini, maana sisi tunachoambulia pale ni vumbi tu na mashimo, magari yanayofika pale yanaharibu barabara zetu usiku na mchana. Sasa mimi ningeliomba jibu kutoka Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana gharama za saruji zinakuwa kubwa. Hii saruji inaporudi kutoka Tanga, Dar es Salaam kuturudia tena sisi wenye malighafi tunashindwa tena kuinunua, na sababu ni hizo hizo gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sishangai kwa sababu ni miaka mingi, sisi tumekuwa katika *misallocation* ya viwanda hivi na hasa sababu kubwa ni masuala ya

siasa. Kiwanda kinakwenda kuwekwa mahali ambako hata malighafi hakuna, na ukiangalia kwa undani sana utakuta kwamba ni masuala ya siasa tu kum-*please* mtu mmoja mkubwa au vipi, basi. Lakini, mahali ambapo kuna kila kitu kama nilivyotaja pale Itigi, na kuna magodauni pale ya *former East African Cooperation*, kuna *winches* pale, kuna nyenzo zote za kufanya kazi lakini hawaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba sana hili suala waliangalie na watusaidie. Wamekuja kama wawekezaji wawili, watatu na walionesha nia, wengine Wachina lakini mpaka sasa inasemekana sijui kulikuwa kuna kuyumba kwa uchumi, lakini Serikali yenyewe bado haijaonesha *interest* katika kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye hoja ya pili ni kwamba viwanda hivi vinakopa nguvu ya wafanyakazi, maana *gypsum* inapochimbwa na kusafirishwa kiwandani, wanaochimba ni wengine na wanaosafirisha ni wengine ambao ni Mawakala wa usafirishaji. Sasa wale Mawakala wanaelewana kati yao na viwanda vile, lakini sasa haya malipo hayafiki kule chini kwa wachimbaji, na wale wachimbaji wanaachwa bila ya kuwa na uhakika wa malipo na umasikini unanuka katika utajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana, vibarua hawa wanaochimba kama alivyosema Mheshimiwa Mkapa hawa ni *unskilled labours*, wanategemea nguvu zao wenye ambazo ndiyo mtaji wao, wanachimba hiyo *gypsum*, wale Mawakala wanakuja na magari makubwa na kusafirisha kwa ahadi kwamba watakuja kuwalipa wakishapokea malipo kule, lakini wakiishapokea pesa hawaona. Wanakuwepo wale Wanyapala kule, basi kazi zao ni ahadi tu huku wananchi wanahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii si halali hata kidogo na ningelipenda haki itendeke kwa hawa watu na ijulikane kabisa kama inawezekana, basi wawafanyie utaratibu ambao watawezeshwu kulipwa moja kwa moja. Wawalipe hao mawakala wa usafirishaji na wawalipe wachimbaji ili kusiwe na hila hapa katikati ya kuweza kuwakopa nguvu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushahidi wa kutosha hata mimi mwenyewe nilivamiwa ofisini wakati nafunguliwa ofisi ya Jimbo. Watu wa kwanza kufika ni hao wachimbaji wa *gypsum* kwamba tumechimba *gypsum*, imekuja imechukuliwa, imesafirishwa. Kwa hiyo, nitashukuru sana ikiwa suala hili nalo likiangaliwa ili ndugu zetu hawa waweze kutendewa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna habari kwamba maeneo yetu sasa yana *deposits* za *Uranium* sasa kutoka Bahi hili eneo lote mpaka Manyoni, mpaka kwenye Jimbo langu kule Itigi. Sasa sijui itakuwa ndoto nikianza kuzungumzia habari za kiwanda, au sijui ni nini! Lakini ukweli ni huo kwamba kuna *deposits* hizo na kama kawaida nadhani hiki kiwanda nacho kitawekwa mbali sana na maeneo hayo yenye malighafi hiyo maana sisi tunapozungumza *uranium* tunaizungumzia kwa ajili ya nishati ya amani, kutengeneza umeme na mambo mengine ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuzungumzii habari ya mambo mengine, lakini bado hatujawa na uhakika wa *deposits* zilizo sawasawa kwamba Serikali itafanya nini kuhusu suala hilo. Lakini *deposits* hizo zimepatikana kwa wingi na watu wanaohusika wapo katika maeneo hayo na wanatuambia hivyo. Tungependa kusikia kama sio kwa Wizara hii, basi kwa Wizara husika ya Nishati na Madini ni nini kinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.  
(*Makofî*)

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya bajeti. Tunawapongezeni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, ningeomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Mtwara Mjini kutoa salamu zangu za rambirambi kwa wapiganaji wetu waliopata ajali ya ndege majuzi, Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kuchangia hasa katika ubanguaji wa Korosho. Korosho mpaka sasa hivi bado bei yake ni ndogo, na haikidhi haja na kwamba hailipi gharama za kuzalisha. Sasa inabidi Serikali na vyombo vingine kutafuta namna ya kusaidia wakulima wa zao hili ili wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia mbadala ambayo mimi ninaiona, kuna njia nyangi hasa katika kubangua Korosho na kutumia *bi-products* zake ili ziweze kuchangia zaidi ili wakulima wapate bei nzuri. Kwa mfano, Korosho ukiibangua ganda lake unaweza ukakamua mafuta, yale mafuta yakasaidia katika utengenezaji wa rangi, yakasaidia pia kuhifadhi mbao ili zisiliwe na wadudu na kile kinachobaki unaweza kutengeneza *brake linings au clutch plates*.

Mheshimiwa Naibu Spika, matunda ya Korosho ambayo karibu tani laki tatu yanatupwa mwaka hadi mwaka, tunda hili la Korosho ambalo linaitwa bibo kwa wale ambao hawalifahamu linaweza likatengeneza *jam, syrup, wine* na kadhalika.

Sasa kama matunda haya yangeweza yakatengeza kwa utaratibu huo, ninaamini kwamba wazalishaji wa Korosho nao baada ya kuuza Korosho zenyewe wangeweza kuuza pia matunda yake na kwa namna hiyo tungeweza kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpaka sasa hivi bei haitoshi, Korosho zinaponunuliwa hukopwa na wakulima hawalipwi kwa mkupuo mmoja, lakini, sisi hatuwafikirii kuwakopesha pembejeo. Inabidi nao tuwfikirie, mandhali sisi tunawakopa, basi na wao wakitukopa tukubali, hususani katika pembejeo na pengine na maeneo mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango ambao mimi nilichangia kipindi kilichopita katika Wizara hii kwamba tuanzishe *semi processing plants*, viwanda vidogo vidogo ambavyo vinaweza vikabangua Korosho katika hatua ya mwanzo na baadaye Korosho hizo zikapelekwa katika viwanda vikubwa vikamalizia hatua inayofuata. Hatua hii ingesaidia kutoa ajira kule vijiji na kuongeza faida katika zao hili ili mkulima naye aondokane na bei ndogo hii ambayo inamkabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi semi *processing plants* zingeweza kufanyiwa majoribio kwanza katika vijiji kadhaa ambavyo vingechaguliwa, tukaanza ili tuone tutafikia wapi na nina uhakika tutafanikiwa kwa kutumia viwanda hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mtwara unategemea sana zao la Korosho na pia linatoa mchango mkubwa katika pato la Taifa. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali hususan Wizara hii kujitahidi katika kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya Korosho. (*Makofi*)

Viwanda vidogo vidogo vya Korosho sio ghali sana. India vinauzwa dola 3000-4000, wananchi hawa wangewezeshwa kwa utaratibu, kwa mfano, kama huu wa *power tillers* wakaleta viwanda vidogo vidogo na wakasaidiwa katika kununua Korosho kwa sababu Korosho inabidi uweke kama malighafi kwa kipindi cha mwaka mzima, basi wangesaidiwa pia kupewa mikopo ya masharti nafuu waweze kununua Korosho za kubangua kwa mwaka mzima.

Nadhani katika utaratibu huu Korosho itaweza kutusaidia sana kuliko ilivyo hivi sasa ambapo tunatupa mabibo, maganda tunayachoma moto haikidhi haja na Korosho inakuwa haituletei faida ile ambayo ingeweza kutuletea. Tukitumia utaratibu huu, wananchi wanaolima watapata ari ya kulima na kuongeza zaidi uzalishaji wa Korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona kwa upande wa suala la Korosho nilizungumzie kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Mtwara iko tayari kwa maendeleo, kwa lugha ya kimakonde wanasema Mtwara *kuchele* yaani kumekucha, na Mtwara iko tayari kuchangia pato la Taifa. Naishukuru Serikali kwa jitihada zake za kuimarisha miundombinu na kuikamilisha, tayari kupokea viwanda.

Tunashukuru Serikali kwa umeme wa kutosha, tuna ardhi ya kutosha kuna *Special Economic Zone (SPZ)* hekta karibu 2700, tuna Bandari ya kina kirefu, tuna uwanja wa ndege, tuna gesi na ninaweza kusema kwamba kuna kila kitu ambacho kinahitajika kwa kujenga viwanda. Tunaomba Serikali sasa ipige *about turn* iitazame Mtwara, iwashawishi wawekezaji waje wawekeze ili tutumie kikamilifu miundombinu hii ambayo imeigharimu Serikali pesa nyingi sana lakini haitumiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari haitumiki kikamilifu, umeme hautumiki kikamilifu, gesi haitumiki kabisa. Kwa hiyo, hakuna haja ya kusongamana Dar es Salaam

wakati wote tunapotaka kuanzisha viwanda, viwanda vinaweza vikaja Mtwara na vikatoa ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, majirani zetu wa Lindi pia wana malighafi ya kutosha. Asilimia 75 ya Ufuta inapatikana katika Mikoa ya Kusini, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hautoshi kumpa mchangiaji yejote nafasi ili achangie. Kwa hiyo, tutakaporudi saa 11.00 jioni, wachangiaji watakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwai Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mzindakaya. Haya ndiyo majina niliyonayo kwa ajili ya jioni.

Sina tangazo lingine. Kwa hiyo, ninasitisha shughuli za hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati nasitisha shughuli za Bunge asubuhi nilikuwa nimebakiwa na orodha ya wachangiaji watatu. Kwa hiyo, nitawaita, naanza na Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kushukuru sana kupata nafasi hii adimu ya kuchangia. Lakini nianze kwa kushukuru sana kwa niaba ya Mkoa wa Njombe ambako Naibu Spika ndiko anakotokea, kuishukuru sana Serikali yetu kwa kweli kwa kutupa Mkoa wa Njombe uliojaa maziwa na asali, hivyo tuna imani kabisa hata tutakapokuwa tunapiga hatua tutakuwa tunaelekeea kwenye ile nchi ya ahadi.

Baada ya shukrani zangu hizo, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri - Mheshimiwa Nagu na Naibu wake kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa ilani ambayo kwa kweli walikuwa wakiifanya kwa kipindi cha miaka mitano. Sote tumeshuhudia wamefanya kazi kubwa, kazi nzuri sana katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, wametuboroshea maeneo mengi na mambo makubwa yamekuwa yakifanyika. Baada ya kutambua mchango wao huo, nami nitakuwa na ushauri kidogo kama ifuatavyo:- Pamoja na mambo mengi mazuri na kimsingi, ushauri huu utakwenda zaidi kwa wataalamu wetu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu, tumekuwa tukizungumzia sana maisha bora kwa kila Mtanzania na tunapozungumzia maisha bora kwa kila Mtanzania kwa kweli tunazungumzia kipato cha Mtanzania, tunasema kipato chake ni shilingi ngapi, *GDP* kwa mwezi, kwa mwaka, na kipato cha Mtanzania kinategemeana na shughuli anazozifanya Mtanzania. Shughuli hizi zinaweza zikawa ni biashara, masoko ambayo ndiyo yanalenga masuala ya Kilimo Kwanza, vile vile na masuala ya viwanda. Hivyo, bado tunalo jukumu katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko tuhakikishe kwamba baada ya kufanya hizi shughuli za Viwanda, Biashara na Masoko kuratibu na kufanya yote yanayowezekana, kipato cha yule Mtanzania pia kikaongezeka.

Ni kweli kwamba lipo suala la soko huria na masuala ya utandawazi, lakini pamoja na mambo hayo, Wizara lazima ichukue jukumu lake la kuendelea kuratibu kwa kiasi fulani ili kuweza kuboresha kipato cha Mtanzania. Maeneo mengi sana wananchi wanataka kuwekeza, wawekezaji wa ndani hususan, lakini unakuta wanapokwenda maeneo kama ya Benki bado riba ni kubwa. Kwa hiyo, liwe ni jukumu la Wizara *negotiate* na Benki kama ni *Commercial Bank of Africa*, Benki zetu za ndani, *NMB*, *CRDB*, *Barclays* na wengine wote kwamba kwa masuala ya uwekezaji hususan masuala ya viwanda, basi ule mtaji riba yake uangalie maana inakuwa ni kwa maslahi na manufaa ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nchi nyingine, kuna baadhi ya *field* wao hawaruhusu *foreigner* *ku-operate* viwanda au *institution* za aina hiyo. Nilikwenda nchi kama Ethiopia unakuta kuna baadhi ya viwanda hivyo vinalengwa kabisa kwa ajili ya wao wenyewe. Lakini kutokana na utandawazi, sisi tunasema tuendelee kushirikiana. Tunao Maafisa Biashara katika Halmashauri zetu, wale Maafisa Biashara katika Halmashauri zetu ni muhimu sana wakawasaidia Watanzania.

Sasa hivi kuna Kata mpya nyingi sana zimetengwa zimekuwa ni Kata mpya, Vijiji vipyta ni muhimu maeneo hayo yakatengwa tukapata maeneo ya biashara. Wale Maafisa Biashara, tukapata maeneo ya masoko. Zile Kata mpya na Vijiji vipyta vikawa kama miji mikubwa. Utakuta Dar es Salaam tumejitahidi, kuna maeneo unakwenda unakuta *shopping moles*, *super market* sasa tutafikia huko maeneo ya Mikoani hususan katika Kata mbalimbali na Vijiji mbalimbali bado baadhi ya watu hawajaweza kutenga maeneo hayo. Hiyo niiombe sasa kwa kupitia Wizara hii watoe maelekezo rasmi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo Wilaya mpya zimepatikana, basi maeneo hayo ni maeneo ya masoko yatengwe. Kutokana na soko huria, wakati mwingine wananchi wetu kwa sababu hatuna maeneo maalum ya masoko wanauzia majumbani. Naonglea maeneo ya vijijini. Ni kweli Dar es Salaam kuna watu milioni tano na ni mji mkubwa, lakini bado Watanzania wengi wako mikoani. Tunasema Kilimo Kwanza, Watanzania wengi wanapouza mazao yao kama mahindi, viazi, wengine wanauzia maeneo ya nyumbani na hivyo maeneo hayo inakuwa ngumu kuratibu. Hakuna mizani wanaweka mzigoto mkubwa wanaweka na lumbesa hasa ile biashara isipokuwa *controlled* kutokana na hili soko huria, bado huyu Mtanzania wakati mwingine anaendelea kutonufaika. Kwa hiyo, niombe sana

Maafisa Biashara katika Halmashauri zetu wajitahidi sana kuwasaidia Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la viwanda, tunashukuru sana Wizara imefanya mambo mengi makubwa, viwanda vya saruji, bia wanajitahidi na tuendelee kuomba kwamba viwanda vingine ambavyo vina mitaji mikubwa tena waendelee kuuza hisa kwa wananchi kama jinsi ambavyo viwanda vingine vimikuwa vikifanya. Vipo viwanda tunakuta hisa zao zinapelekwa kwenye *Stock Exchange Market*, ile inatia moyo sana.

Kwa mfano, kiwanda cha *Twiga Cement*, *Tanga Cement* na kadhalika. Sasa sio mbaya hiyo ikawa ni mionganoni mwa sera zetu, *Public Private Partnership*. Viwanda vingine ambavyo waliwekeza mitaji wakadhani ina manufaa, itatusaidia sana, lakini tuendelee kujikita sana katika eneo la viwanda vya *processing*. Kwa sababu tumekuwa tukiwa sana malighafi na malighafi hii thamani yake inakuwa kidogo, ni ya chini ukilinganisha na *finished au processed goods*.

Kwa hiyo, naendelea sana kuomba watalamu wetu katika Wizara tujitahidi tuwe na takwimu, tuwe na *profile* ya kila mkoa. Mkoa wetu wa Njombe sisi tutashukuru sana, miaka mitano ijayo tukishirikiana na Wizara tukapata kiwanda cha kutengeneza kwa mfano viazi vikawa *processed*. Tunalima sana viazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lile umeme upo, maji yapo, barabara zinafikika. Pia masuala ya ngano kutoka Wilaya ya Makete wanalima sana ngano. Lakini tukisafirisha ngano tunaumia sana sisi wananchi kuliko ile ngano ikawa *processed* na ikawa *packed* vizuri ukauzwa unga kutoka eneo husika.

Wilaya ya Ludewa ni wakulima wazuri sana wa mahindi, hasa mahindi yanaweza yakatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Unatengeneza unga, wengine wanasema *popcorn*, kuna makorokoro kibao unaweza uka-*process* kutoka kwenye mahindi. Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara sasa tuenze kuangalia Mikoa hii ya Kusini, unaangalia Mbeya wao wana vitu gani, Rukwa, Ruvuma na hivyo itasaidia tukiwa tuna-*process finished goods* na vinasafirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo kama Chalinze pale Ilula, kuna nyanya na hawa wengi wao kwa kweli ni akinamama ambao wamejikita sana katika kilimo, wanafanya kazi usiku na mchana, wanajitahidi sana kuzalisha hasa wakati mwingine hata tukipata zile *packing materials*, kama ni nyanya za pale Ilula, vitunguu vinakuwa *packed* vizuri kabisa hata kama tuki-*export* hata kwenye soko letu la jirani maana tunesema tuwe na *common market* kati ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi watu takriban milioni 150 tukaanza kuuza hapa hapa jirani. Lakini sasa huyu mtu wa Kenya hawezni kuja kununua kwenye tenga inakuwa kazi kweli!

Kwa hiyo, tukapata *packing material* nzuri, machungwa yale ya Chalinze *packing materials* pia zitatusaidia sana zinapakiwa vizuri. Maana yake matunda ya wenzenetu *apple* unakuta *apple* moja Sh. 600/= kwenye *super market*, lakini *apples* za kwetu bei zake ni ndogo, kumbe ni *packing material* tu! *Style of packing!* Unakuta mchele wa Basmat tu

*super market* kutokana na *packing material* bei yake wanakwambia ni Sh. 5,000/= kwa kilo wakati mchele wa Tanzania labda ni Sh. 2,000/=. Ni *packing materials tu!* Kwa hiyo, hivi vitendea kazi vingetusaidia sana. Nakumbushwa na mafuta ya alizeti, kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo suala lingine la bidhaa bandia, bidhaa zetu sisi hazina *chemicals*, hazina *artificial* za Kitanzania, ni imara sana. Ukila unakuwa na afya, safi kabisa! Lakini bidhaa za wenzetu kwanza zinakuwa ni duni. Kwa hiyo, tunapokuwa tuna-*export* masuala ya biashara haya ni muhimu sana tukaangalia bidhaa bandia. Bidhaa bandia katika nchi yetu zimekuwa ni nyingi sana. Tujaribu kutafakari tunafanyaje kudhibiti masuala haya ya bidhaa bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maonyesho watu wetu wanakuwa wanajifunza sana na sasa hivi tunaelekea kwenye sherehe za Saba Saba. Sherehe hizi za Saba Saba nilipata nafasi kidogo ya kupita jana au juzi hapa unakuta bidhaa za nje ndiyo nyingi zaidi kuliko za Kitanzania asilimia 50 *imported goods*. Mazulia, hasa nikasema vikapu vya wale akina mama wa Mufindi, vyungu vya Njombe pale mbona huku sivioni? Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Mama Nagu, Waziri wangu anisaidie ifikapo tarehe 7, wale akina mama wa kule Iringa waweze kuja na vikapu na tunashukuru sana hata yale mabanda wakiwalipia, maana yake mabanda sio gharama sana. Naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Haiwezekani makapu yaende leo kwa ajili ya kesho kutwa. Waziri anasema yapo. Naomba nimwite Mheshimiwa Zitto Kabwe aendelee na mchango wake halafu atamalizia Mheshimiwa Dr. Mzindakaya.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kupata fursa hii ya kuchangia katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kama jinsi ambavyo wachangiaji wengine walivyozungumza, Wizara hii inaendesha sekta mbili muhimu sana katika uchumi wa Taifa letu, sekta ya viwanda na sekta ya biashara. Wote tunafahamu michango ya sekta hii katika maendeleo ya Taifa letu na ni moja ya sekta ambayo imeonyesha kuendelea kukua vizuri kwa sababu kwa wastani miaka 10 iliyopita ni sekta ambayo imekuwa kwa takriban asilimia 8.6 ambayo ni zaidi ya asilimia zinazotakiwa kwa ajili ya kuwa na uchumi unaokuwa kati ya asilimia nane na kumi ili kuweza kupunguza umaskini wa Watanzania. Kwa hiyo, ni sekta ambayo inaelekeea kwamba kama tukiwekeza vizuri inaweza ikatusaidia sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile sekta ya masoko kwa maana ya biashara na masoko nayo pia ni sekta ambayo imekua katika wastani mzuri katika kipindi cha takriban miaka 10 iliyopita. Lakini sekta hii ina changamoto nyingi sana. Mara zote nimekuwa nikizungumzia suala zima la kwamba kama tunataka kupunguza umaskini katika Taifa letu, ni lazima tuwekeze katika uchumi wa vijiji (*Rural Economy*) ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na *growth* ya uchumi wa vijiji. *Growth* ya uchumi wa vijiji utasababishwa na kilimo na kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo na ndiyo kazi ambayo kimsingi kwa nchi

kama yetu ambayo bado iko nyuma kiviwanda ilipaswa ijielekeze zaidi katika viwanda ambavyo vitaongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Takriban miaka miwili iliyopita nilizungumza katika mchango wa Wizara hii kuhusiana na umuhimu wa kufungua masoko katika maeneo ya vijiini na hasa maeneo ya mipaka na Wizara ikawa imekubaliana na mimi kwamba katika mpaka wa Kagunga katika Kata ya Kagunga jimboni kwangu ambayo ni mpaka unaopakana na nchi ya Burundi. Serikali itaangalia jinsi gani ya kuweza kushirikiana na Halmashauri yetu kwa ajili ya kujenga soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko haijafanya juhudu yoyote ile katika eneo hilo. Sisi kama Halmashauri tumefanya kazi yetu, tumetenga bajeti ya zaidi ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa soko katika eneo hili na mamlaka ya Bandari Tanzania imetusaidia, imejenga ghati pale kwa ajili ya kuhakikisha kwamba meli zinashusha mizigo bila matatizo yoyote na Shirika la Umeme Tanzania, *TANESCO* wanavuta umeme kutokea Burundi.

Lakini Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na kwamba huu ni mpaka muhimu sana, lakini bado hawajafanya chochote mpaka sasa na wamekuwa wakiahidi tu tutakwenda Kagunga na sijamwona sio Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, hakuna mtu yoyote, na wanajua kabisa kwamba maeneo yaliyoko pembezoni mwa nchi *marginalised arrears* yako nyuma sana kiviwanda, kimasoko na kadhalika. Maeneo kama ya Kigoma ni maeneo ya biashara zaidi kwa sababu tunapakana na nchi mbili, Congo na Burundi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri aweze kuangalia ni jinsi gani ambavyo atakavyoweza kutusaidi hili eneo.

Lakini pili, nimesoma katika hotuba hapa Serikali ina mpango wa kuwa na zile wanaita *Border Posts* kwa ajili ya kuweza kusaidia maeneo ya mipakani. Lakini *Borders* zote zilizotajwa hapa hakuna *Border* ya Kigoma hata moja. Maana yake Kigoma tuna *border* katika Wilaya ya Kasulu na Kibondo. Mji wenye wa Kigoma ni *border* pamoja na Mashariki ya Congo na eneo lingine la Kigoma lina *border* na Burundi na Kasulu ni *border*, na Burundi na Kibondo ina *border* na Burundi. Lakini *borders* zote ambazo zimetajwa katika maeneo haya ni *borders* ambazo tayari zimeshaendelezwa sana mpaka sasa. Hakuna *border* hata moja ya Kigoma na tumekuwa tukizungumzia sana *border* zetu. Sasa sijui ni kwa nini kwamba tuko mbali sana na nchi au ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa sana kwamba licha ya juhudu zote ambazo tumezifanya pamoja na Mashirika mengine ya umma kupeleka maendeleo katika yale maeneo kama hiyo *border* ya Kagunga, lakini Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko haijafanya kitu chochote na leo tumeingia kwenye *common market*. Maana yake ni kwamba tutafanya biashara na Burundi. Kama sisi tungewenda *faster* tukamaliza soko letu, tukavuta umeme pale tukamaliza ile bandari yetu, maana yake ni kwamba tungakuwa tmesogea haraka na wafanyabiashara wa Tanzania wangeweza kupata biashara zaidi kwa sababu wafanyabiashara wa Burundi wangeweza kuja kununua bidhaa zao pale Kagunga.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara iweze kuliangalia suala hili kwa kina, waweze kuangalia ni jinsi gani ambavyo watatusaidia na sisi tujisikie kama ni sehemu ya

Tanzania, maana haiwezekani mipango yote, wote tunalipa kodi pamoja, lakini inapofikia wakati wa kugawa, kuna maeneo yanapata zaidi na maeneo yanapunjwa kidogo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ambayo naamini kwa miaka mitano iliyopita haijafanya chochote Kigoma, basi angalau katika hili waweze kuangalia jinsi ya kuweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nilikuwa napenda kulichangia ni suala la *NDC*. Tulipoanzisha *NDC* miaka ya 1960 lengo lilikuwa tuwe na *Holding Company* ya nchi ambayo itachochea ujenzi wa viwanda na Makampuni mbalimbali nchi nzima na ndio kazi ambayo *NDC* ilifanya miaka ya 1960 wakati inaanza Mashirika mengi sana Makampuni Tanzu ya *NDC* yalikuwa yamewekeza na Serikali na ilikuwa ni mali ya *NDC* mengi sana ambayo sasa hivi mengi yameuzwa. Miaka ya 1970 ikawa hivyo hivyo na miaka ya 1980 kutokana na hali ya kiuchumi na Menejimenti na kadhalika ikawa imebadilika.

Lakini sasa hivi hatuendi katika kubadilisha *mind set* jinsi gani tutaifanya *NDC* iwe ni *Holding Company* ya nchi kwa sababu nchi nyingi sana duniani zina vitu vya namna hii. Juzi mwezi uliopita nilikuwa Malaysia tulianzisha nao na wenyewe walikuwa kama na *NDC* yao kama yetu na wamewekeza kwenye maeneo mbalimbali, wamekwenda haraka sana na *NDC* yao sasa hivi iko *listed* kwenye soko la hisa la pale Kuala Lumpur. Sisi tulikuwa na Makampuni Tanzu mengi sana, tumeingia kwenye ubinafsishaji tumeua yale makampuni yote. Tume-specify Makampuni mengi, tumeikatakata *NDC*, tumeondoa maeneo yake mbalimbali. Lakini yale maeneo ambayo yamebaki tunaweza kufanya kazi kwa pamoja ili kuweza kusaidia *NDC* iweze kufikisha hapa ambapo tunakwenda.

*NDC* walikuwa na mradi wa kusaidia wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu, Mradi wa Matinje. Wakati huo *NDC* ikaingia ubia na watu binafsi na Benki Kuu kuanzisha mradi wa *Mwananchi Gold*. Miradi hii ilikuwa na mahusiano kwamba wachimbaji wadogo wadogo watapata dhahabu, watapata soko la uhakika, *Mwananchi Gold* itakuwa kama *refinery*, itatengeneza vito na kadhalika. Kwa hiyo, tulikuwa na uhakika kabisa wa kuongeza thamani ya raslimali yetu ya dhahabu hapa hapa nchini. Ule mradi wa *Mwananchi Gold* ukapata matatizo. Haina maana kwamba vitu vikipata matatizo tusiwe na njia ya kuweza kuviokoa na kuweza kuvirejesha viweze kufanya kazi.

Mwaka jana tarehe 29 Aprili, Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma ilitoa taarifa yake hapa, ikaelekeza na Bunge zima likapitisha kwamba miradi ya Mtinje na *Mwananchi Gold* ireshwe kwa faida ya nchi kwa sababu ni miradi *strategic*. Lakini mwaka jana kwenye bajeti muda ulikuwa mfupi hatukuweza kulisemea hili, lakini tunatarajia kwamba mwaka huu kungekuwa na mpango wa kuhakikisha kwamba miradi hii inaweza ikarejeshwa. Serikali imesema tu kwamba tutaendelea kuwasaidia wachimbaji wadogo, lakini kuna miradi ambayo tayari ipo ambayo ingeweza kusaidia ni kiasi cha kuwekeza vizuri na miradi ambayo inalipa na ingesaidia wananchi wetu, ingetengeneza ajira na ingeongeza thamani ya dhahabu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna tatizo kubwa katika *Mwananchi*, lakini tayari Benki Kuu ime-reverse ule uamuzi wa kuafilisi *Mwananchi* kwa sababu

wametafuta mbia kutoka Benki ya Maendeleo ya China kwa ajili ya kuja kuwekeza katika lile eneo kufanya *refinery*. Sasa hii ni *strategic partnership* kati ya Benki Kuu, *NDC* na mwekezaji huyo kutoka nje. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Wizara iliangilie hili kwa makini ili kuweza kuhakikisha kwamba tunanusuru hali kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni majadiliano ya *Economic Partnerships Agreements*. Serikali imetoa ripoti hapa kwa mujibu wa taarifa ambayo Waziri ameitoa, lakini nilikuwa nadhani kwamba Serikali ingetoa *briefing* kutohana na maeleo ambayo wameeleza kwenye hotuba, wangetengeneza *briefing* kidogo kwenda kuonesha ni maeneo yapi ambayo sisi tuna mashaka nayo ndani ya *Economic Partnerships Agreements* kwa sababu tupo ndani ya dunia na lazima tuhakikishe kwamba tunashirikiana na wenzetu. Sisi ni *member* wa *WTO*, ni lazima tufanye *rules*. Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wangeweza kupata hiyo *briefing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, nimefurahi sana kwa kazi ambayo Wizara imeifanya. Katika ubinafsishaji, ile wanaita uperembaji wa utekelezaji wa mikataba ya mashirika yaliyobinafsisha, nadhani Wizara nyingine zifuate huu mtindo. Tuliiza mashirika yetu, hatukuyafuatilia. Kutohana na maeleo mbalimbali ndani ya Bunge Wizara ya Viwanda na Biashara imefanya kazi kwa mashirika ambayo yalikuwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwa hiyo, sasa hivi kuna kitabu ambacho tunaweza kwenda kuangalia kila Kampuni au shirika lililobinafsishwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, tukajua *status* yake ikoje mpaka mwezi Aprili mwaka huu. Kwa hiyo, ikawa ni rahisi zaidi kwa Wabunge kufuatilia wananchi, kufuatilia na watu wa sera kufuatilia. Ninashauri kwamba Wizara nyingine nazo zifanye kama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza kabisa, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watalaam wote wa Wizara kwamba kwa kweli hotuba waliyoiwasilisha hapa sio tu kwamba imeandaliwa vizuri, lakini pia inasomeka vizuri. Maeleo ni mazuri sana, uchambuzi ni mzuri sana, tena wa kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikushangaa sana kuona kazi nzuri hii kwa sababu Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Mary Nagu ni mtoto wa viwanda, ndiyo kazi yake aliyanza. Vilevile tumeshuhudia kwamba katika mikutano mingi ambayo anawakilisha nchi anatetea kweli maslahi ya nchi kibiashara. Kwa hiyo, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kutoa ushauri kuwa Wizara ya Viwanda, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maliasili watazame maeneo yote ambayo yanatakiwa kujengewa uwiano katika Wizara hizi. Kwa sababu viwanda peke yake haviwezi kufanya kazi wala Wizara peke yake bila uhusiano na uwiano kati ya Wizara ya Kilimo hasa tunapozungumza habari ya viwanda vya kusindika mazao. Vivyo hivyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nasema hivi kwa sababu mimi kwa mawazo yangu ninafikiri nchi hii

ina nafasi ya kujitegemea kwa mambo mengi kuliko nchi za jirani. Lakini kinachotakiwa ni kuwa na mpango na malengo yanayotuelekeza lini tufikie kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mzuri. Tanzania miaka ya nyuma ndiyo ilikuwa inaongoza katika *East Africa* kwa kutengeneza nguo kama kanga na vitenge tena vizuri na tulikuwa tunauza nje. Sasa wale tulikuwa tunawauzia sisi ndiyo wanaanza kutuuzia sisi. Sasa hii sio nzuri. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba tuwe na mpango unaoonesha namna ya kujitosheleza kiviwanda, vyta nguo, vyakula na kadha wa kadha.

Vilevile, kwa mfano tunasema tuna ng'ombe wengi, lakini hatujawa na viwanda vyta kutosha vyta kusindika nyama na ngozi. Yote haya inatakiwa uwe na mpango wa uwiano. Wizara peke yake ya Viwanda haiwezi kufanya kitu. La pili ambalo ningependa kulisema katika hilo hilo, wakati huo amba Serikali yenyewe haiendeshi viwanda moja kwa moja ni wakati mzuri kwa Serikali kubana *investors* na wanaojenga viwanda hapa nchini, wajenge viwanda vitakavyotumia malighafi ya hapa nchini.

Kwa mfano, tunajua kuna baadhi ya wenge viwanda vyta nguo hapa amba wanaagiza *gray sheeting* kutoka nje na wanasmehewa kodi. Lakini kumbe tungewapa na waanze kutengeneza nyuzi hapa hapa. Kwanini waendelee kuagiza *gray sheeting* ije wakati angeweza kutengeneza nyuzi hapa hapa? Kwa hiyo, nyuzi kwanza halafu *gray sheeting* na pamba tunayo. Huo ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa nafikiri kwamba kwa mazao haya nafikiri Mheshimiwa Waziri maonesho yake waliyosimamia mwaka jana yalivunja rekodi na nadhani mwaka huu watavunja rekodi pia. Pale kulikuwa na viwanda vyta kusindika na niliona kiwanda kimoja cha matunda cha Morogoro, wale wameteua wakulima jirani kwa kuingia mikataba nao. Kwa hiyo, mimi nashauri kwenye viwanda vyta mafuta, viwanda vyote vyta kusindika mazao wahimizwe waende mikoani waingie mikataba na wakulima ili wapate mbegu za mafuta na matunda ya kusindika hapa hapa nchini kwa sababu ardhi tunayo na inatosha kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kushauri na naomba kweli Mheshimiwa Waziri jambo hili alitazame, halihusu Wizara yake peke yake, ni la nchi. Lazima Serikali sasa iamue kufanya biashara. Serikali ya Tanzania hatufanyi biashara, tunatawala tu. Hatufanyi biashara. Kenya wanafanya biashara na Serikali itakapoamua kufanya biashara tutawashinda wote hawa majirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, Serikali haifanyi biashara, ni kwa maamuzi tu. Sio kwamba ijenge viwanda ikauze nguo, hapana. Maamuzi yanayotakiwa ili wafanyakibashara wafanye biashara, lazima yafanyike. Inavyoonekana kwa sasa nadhani watu wengi mtakuwa mmeshuhudia, sasa hivi urasimu Serikalini ni mkubwa sana. Hata Waziri mwenyewe anaweza akaagiza jambo labda akalipata baada ya miezi kadhaa. Kwa hiyo, urasimu umekuwa mkubwa mno ndani ya Serikali. Mambo hayaendi, kwa sababu ya urasimu na inaonekana mahali pengine watu wanaogopa kuamua mambo. Kwanini ushindwe kuamua mambo na madaraka umepewa? Amueni mkosee. Bora uamue ukosee kuliko kutoamua kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu nchi ya Singapore ni ndogo sana, lakini ni tajiri kweli kwa biashara tu. Hawana ardhi ya kulima, hawana mazao ya kujenga viwanda, lakini wao wameamua kuwa ni nchi ya biashara. Kwa hiyo, mimi napendekeza Tanzania tufanye vyote. Tuwe nchi ya kilimo na viwanda na biashara. Wenzetu Wakenya wanakwenda kwa *speed* kubwa sana. Juzi Waziri Mkuu alipotoa makisio hapa, zinavyoonesha namna tulivyoshuka nyuma katika *exports* ilionesha waziwazi. Kwa hiyo, mimi nashauri tufanye biashara sasa. Maamuzi yafanyike, tuunge mkono wanaosimamia biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nishauri, pia sisi Tanzania tumejenga mazoea ya kuuza mazao ya asili *tradition crops*. Sasa tunaingia katika soko la Afrika Mashariki, wenzetu majirani zetu wako mbali sana katika viwanda vya kusindika mazao na katika biashara hii ya mazao ya chakula, maziwa, nyama na vingine. Wenzetu waliofaulu kama Brazil ni kwa sababu wameweke *incentives*. Wana misamaha ambayo wanawapa watu wao wauze nje. Sisi hatutauza kwa sababu gani? Hatuna sera ya kusamehe kodi za *exports*. Bado tunaweka kodi, hatuwezi kushindana. Lazima tukubali wala sio Wizara hii peke yake nchi iwe na sera, itambue sekta zake ambazo zinafa kupewa *incentives* kwa wale wanaofanya *export*. Ni kosa kubwa kusamehe kodi kwa *imports*. Ni mafanikio makubwa kusamehe kodi kwa *exports*. Narudia tena dunia ya leo ni biashara, maendeleo ya dunia ya leo ni biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka niseme na naomba Serikali ilipe uzito ni hivi, kwanini tunaendelea na hata nitakapokuwa nje nitakuwa nasema tu. Kwanini tunaendelea kuagiza vitu ambavyo tunatumia fedha za kigeni bure? Maua bandia kwanini tunaendelea kuyaagiza? Hivi tukiyazuia nani atatunyonga shingo? Kwa sababu yanatumia fedha zetu za kigeni. Kila mtu duniani anachunga pesa yake itumike kwa kitu chenye maslahi. Hivi maua ya bandia yana maslahi gani kwa nchi yetu? (*Makofit*)

Pili wekeni lengo la kusema *chemicals* za *juice* na soda, vitu hivi viwekewe vilevile lengo kwamba wewe mwenye kiwanda unatengeneza *juice* za *chemicals* baada ya miaka mitano hatutaki uendelee kutengeneza *juice* za *chemicals* na hivi vitu sio vya lazima. Vilevile *furniture*, samani zote ambazo zinaingizwa nchini lakini zimetengenezwa kwa vitu vya bandia nazo zipigwe marufuku. Tujenge viwanda vyetu vya kusaidia. Sido ni mkombozi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naishauri Serikali yetu katika kipindi hiki tujenge kada ya kati. Kada ya kati ya mkulima na wafanyabiashara wadogo na wanaviwanda wadogo. Hawa ndiyo ukombozi wa nchi yetu. Wakiwa wengi uchumi utaongezeka na tuwatambue kama tulivyokuwa tunasema juzi. Wasomi wanaosoma tuwajue kwa majina kila chuo halafu tunajiandaa kwamba hawa watakwenda kuajiriwa, hawa watakwenda viwanda vidogo, hawa watakwenda katika kilimo, hawa watakwenda kwa jambo hili na tuandae hivyo inawezekana.

Hakuna kisichowezekana na uwezo huo tunao kwa sababu tumepata viongozi makini, Rais wetu mtu makini, Mawaziri, hata huyu Waziri ninayemzungumzia ni Waziri mtoto wa mkulima, mtu mdogo. Mimi nakuombea mama watu wa Jimbo lako wakupigie tena kura urudi Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tena wa kumpigia kura wapo hapa hapa. (*Kicheko*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Chami, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuongelea hasa upande wa viwanda, ni lini basi Viwanda vya Kahawa pale Kagera vitaanza kazi, kwani viwanda hivi vinao uwezo wa kuajiri vijana wengi na vijana kupata ajira ya kutosha, hapo tunaweza kupunguza umasikini wa kipato, kwani ajira za viwanda ndio hasa mkombozi wa wanyonge. Pia Kiwanda cha Ngozi pale Mwanza baada ya utambuzi wa mifugo, ambao umepitishwa kuwa sheria hivi karibuni, ninaimani kuwa tutapata ngozi nzuri na zenye ubora.

Sasa basi swalilangu ni kwamba Serikali ina mpango gani kwa ufunguzi wa kiwanda hiki, hata kama kilinunuliwa na mtu binafsi? Serikali inamshauri nini mwekezaji huyu, kwani Serikali sasa imekaribisha *PPP*. Ni vizuri Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza kiweze kifunguliwa ili tuongeze thamani ya ngozi zetu na wafugaji nao wafaidike, pia tupate ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuwajali wakulima wadogo wa matunda kwa kuwawekea viwanda vidogo vya kukamua matunda na kupeki jiusi, kwani matunda tunayo mengi lakini tunakunywa juisi toka nje ya nchi. Ni bora basi tukawa na mipango endelevu ya kuwaendeleza wakulima hawa wa matunda ili waweze kutengeneza juisi na kuuza nje ya nchi, kwa kuwatafutia soko nje ya Tanzania kama wenzetu wa nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na nia tutaweza.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Spika na wewe Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote kwa kuongoza vyema hapa Bungeni katika kazi zenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni muhimu kwa maisha ya Watanzania. Viwanda vyetu vikifanya kazi vizuri ni changamoto kubwa ya kupanua uchumi wa nchi yetu lakini sasa bado hatujajipanga kufufua viwanda vyetu. Tanzania tunayo mifugo mingi lakini ukiangalia viwanda vingi vya kusindika nyama vimekufa na kufanya wafugaji wengi kuwa maskini. Kwa hiyo, tunaomba Serikali waongeze Viwanda vya Maziwa na Nyama ili wafugaji waweze kunufaika kwa kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anijibu ni lini Kiwanda cha Nyama kilichoko Dar es Salaam cha *Tanganyika Packers* kitafufuliwa? Aidha, ni lini watafungua viwanda vya kusindika samaki ili wavuvi nao waweze kufaidika kwa kusafirisha nchi za nje ili kupunguza umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni lini Serikali yetu itaweka viwanda vya kusindika matunda kama vile embe, machungwa ili nchi hii pamoja na wakulima waweze kujigomboa na umaskini kwa kusaifirisha na kuokoa matunda yetu kuharibika na kukosa soko?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza tunamzungumzia mkulima lakini bado mkulima hajafaidika na viwanda kwa sababu hawana soko la kuuzia biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaelekea Soko la Pamoja, naomba muweke milango wazi ili Watanzania waweze kufanya biashara zao kwa ufanisi, kwa kufufua viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, nawatakia kila kheri Waziri na watendaji wake. Amina.

**MHE. BAKAR S. FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia japo kidogo juu ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ni sekta muhimu sana katika nchi yoyote ile, hivyo ni muhimu sana Serikali itoe kipaumbele maalum kwa sekta hii ambayo kukua kwake ni kukua kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua Serikali inazochukua katika kuimarisha na kukuza sekta ya viwanda, je, Serikali inao mpango gani mahususi wa muda mfupi na mrefu wa kuimarisha sekta hii ya viwanda hasa viwanda vidogo vidogo ambavyo vinaweza kuleta ajira kwa vijana wetu?

Nimeuliza swali hapo juu la jinsi ya kukuza viwanda nchini kwa sababu viwanda vingi vimeshakufa kama vile viwanda vya Dodoma, Shinyanga na Mikoa kadhaa hapa nchini. Serikali inao mpango gani wa kuvifufua viwanda hivyo ambavyo vimekuwa? Ni vizuri Serikali ileze bayana hatua ambazo zitachukuliwa kufufua viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBS* ni Shirika linalokagua viwango vya bidhaa hapa nchini lakini mbona bado kuna malalamiko kwamba bado bidhaa zenyenye ubora wa chini zinapatikana hapa nchini. Kuna tetesi kwamba *TBS*, kuna harufu ya rushwa ndio maana baadhi ya wafanyabiashara wasio waaaminifu kwa kushirikiana na baadhi ya wafanyakazi ndani ya *TBS*, ndio hali inayopelekea kupatikana bidaa zisizo na ubora. Sijui Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu tetesi hii ya rushwa ndani ya *TBS*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango yangu, bajeti zilizopita nilizungumza kuhusu biashara kati ya Burundi na Tanzania kupitia mpaka wa Kijiji cha Kagunga. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imejenga soko pale Kagunga.

Mamlaka ya Bandari Tanzania wamejenga gati (bandari) na *TANESCO* wanaunganisha umeme kutoka Burundi. Wizara ya Viwanda na Biashara hajatimiza ahadi yake ya kutembelea mpaka huu na kutusaidia katika juhudu zetu za kuifanya Kagunga kuwa kituo cha biashara. Wizara itimize ahadi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 61 wa hotuba, Wizara imezungumzia kuanzishwa kwa vituo vya *One Stop Border Post (OSBP)*. Mipango ya kuanzisha vituo hivi haigusii kabisa Mkoo wa Kigoma. Kwa nini Wizara ya Viwanda inaitenga Kigoma? Hivi wizara hii imefanya nini Kigoma katika miaka mitano iliyopita?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona taarifa kuhusu ubinafishaji. Naipongeza sana Wizara kwa kazi hii nzuri sana. Mmefanya kazi nzuri inayopaswa kuigwa na Wizara nyingine zote. Sasa mapendekezo haya yaliyotolewa yatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchuchuma na Liganga, Serikali itoe orodha ya makampuni yaliyoomba kuwasilisha mipango ya uwekezaji.

**MHE. PARMUKH S. HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hotuba nzuri na inayoelewka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli viwanda vyetu vina matatizo ya kimsingi na ni ya kimsingi sana. Naamini ikiwa tutachukua hatua za kutosha dhidi ya changamoto hizo, tutaweza kufika mahali pazuri kimaendeleo. Changamoto zenyewe ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, umeme, kwa kweli viwango vya umeme kwa viwanda vyetu ni vya chini mno na umeme wetu si wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, maji, tatizo hilo ni sugu kwa viwanda vyetu na ni la muda mrefu sana. Sioni sababu ya tatizo hilo kwa nchi yetu ina mazima na mito yenye maji ya kutosha ingelikuwa vyema tukaanza kuyatumia vyanzo hivyo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, usafiri (reli, barabara na viwanja vya ndege). Nalo ni tatizo kubwa japokuwa Serikali yetu inajitahidi sana kwa hilo. Hivi sasa ni gharama sana kusafirisha bidhaa au malighafi kutoka na kwenda kwenye viwanda vyetu na ndio maana utaona bidhaa zinazotoka nje zina bei nafuu kuliko viwanda vyetu. Kiwanja cha ndege cha Mwanza hakina ufanisi wa kutosha na hivi sasa samaki wetu wanasafirishwa kwa barabara badala ya kutumia uwanja huo, hili nalo linaumiza sana uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, bandari zetu zote hazina ufanisi wa kutosha na hii inasababisha msongamano mkubwa na hatimaye kuzorotesha uchumi wetu hasa viwanda vyetu. Utakuta pale bandari ya Dar es Salaam meli nyngi zinasubiri kuingia kwenye bandari hiyo wakati kwenye gati hamna meli, hii nayo ni hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu vilindwe, kuna baadhi ya viwanda vyetu pamoja na matatizo niliyoyaeleza lakini kuna haja ya kupongezwa na kulindwa mfano *Whitedent*, *TANELEC*, Chai Bora, Viwanda vya Saruji na kadhalika. Inashangaza kuona *TANESCO* inaagiza *transformer* kutoka India wakati *TANELEC* inazalisha *transformer* nzuri na za viwango.

Leo hatuna sababu ya kuagiza saruji kutoka nje wakati viwanda vyetu vinazalisha saruji nzuri na za kutosha. Ninashauri bidhaa ambazo zinatoka nje wakati bidhaa hizo zinazalishwa hapa zitozwe ushuru mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningeishauri Wizara kwa kushirikiana na *NDC* inapofanya “*study tours*” ihusishe pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara katika ziara kama hizo kwani itasaidia katika kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Naibu Waziri wake kwa jitihada wanazoonesha katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ndio vinavyoinua uchumi wa nchi ingawaje viwanda vingi vimefungwa. Naomba Mheshimiwa Waziri aelezee ni sababu zipi zilizopelekea Kiwanda cha Mbolea Tanga kufungwa na kuhamishiwa Minjingu. Kiwanda hiki kiliwezesha wakazi wa Jiji la Tanga na Mkoa kwa jumla kutoa ajira na kupunguza wimbi la umaskini uliotanda kila pembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kiwanda hiki cha Mbolea pia kipo Kiwanda kingine cha Chuma kilichokuwa Jiji la Tanga (*Steel Rolling Mills*). Kiwanda hiki kimeuzwa kwa mwekezaji toka Arusha na mwekezaji huyu ameanza kuhamisha baadhi ya vipuri na kuvipeleka Arusha. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufufua kiwanda hiki muhimu ambacho kinatoa vyuma na misumari, vifaa ambavyo vinahitajika kila siku katika shughuli za ujenzi?

Naomba Waziri atupe maelezo kwa nini mwekezaji aliyeamua kuwekeza katika kiwanda hiki asiendelee kufufua kiwanda hiki badala yake kuhamisha baadhi ya vipuri na vifaa vingine vivilivoachwa na aliwekeza awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Tanga inaelekea lina bahati mbaya sana. Kilikuwepo pia Kiwanda cha Plastiki cha Amboni, *Kange Spinning Mills* na vinginevyo. Viwanda hivi vimekuwa kabisa yamebaki magofu ya viwanda, cha kusikitisha zaidi hata yale majengo yaliyokuwa katika baadhi ya viwanda wananchi amba si waadilifu wameanza kubomoa milango, madirisha na mabati na kuyauza mitaani. Hivi Serikali haioni umuhimu pia wa kuyatunza majengo yaliyojengwa na waanzilishi wa viwanda hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga ni maarufu kwa kilimo cha matunda na ni Mkoa wenye matunda muda wote. Je, ni lini kiwanda cha kusindika kinachokusudiwa kujengwa eneo la Segera kitaanza? Matunda yetu tumeyauza Kenya na baadaye tunanunua juisi toka Kenya ambayo imetengenezwa kutokana na matunda yaliyotoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi wakulima wetu tunawapa mafunzo gani kuhusu mazao yao ambayo yanakwenda katika Soko la Pamoja. Mazao yanayozalishwa ni mengi lakini tujiulize, je, nini ubora wa bidhaa hizi? Tumeingia katika Soko la Pamoja, hivi mazao yetu yana ubora gani ukilinganisha na mazao yalimwayo katika nchi za wenzetu za jirani?

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua nini hatima ya wafanyakazi amba walikuwa wanafanya kazi katika kiwanda cha kupasua mbao (TWICO) Kilwa Masoko, amba hadi leo hii wanadai malipo yao ya kuachishwa kazi baada ya kiwanda hicho kuuzwa?

Kwa kuwa kiwanda hicho kilikuwa ni cha upasuaji wa mbao na hivi sasa yapata miaka kadhaa hakifanyi kazi ya upasuaji mbao; na kwa kuwa CHC inasimamia na kuhimiza viwanda, mashamba ambayo yameuzwa yafanye kazi ambazo hapo awali zilikuwa zinafanya; je, kwa nini hadi leo hii muwekezaji aliyenunu hajafanya hivyo? Serikali inatoa tamko gani juu ya wale wote amba wamenunu viwanda na hawakuviendeza kwa shughuli ambayo ilikuwepo hapo awali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma, kuna Shirika la Viwango (*TBS*) ambalo huangalia ubora wa bidhaa zote hapa nchini na hata zitokazo nje ya nchi na ninaamini kuwa wanafanya vizuri kazi zao, lakini

kuna mkanganyiko kati ya *TBS* na *TRA* ambapo *TRA* wana wafanyabiashara ambao wanawaamini kuwa ni wa muda mrefu, ambao huleta (huingiza) bidhaa kutoka nje ya nchi. Huwaacha wapitishe bidhaa zao bila kukaguliwa kwa jina la *GREEN BELT* na kigumu zaidi wafanyabiashara hawa wenye *GREEN BELT*, *TBS* hawawezi kuwakagua. Matokeo yake ni uingizwaji wa bidhaa zisizo na kiwango nchini, ambao haieleweki zinapita wapi, mwisho wa yote bidhaa hizi huchomwa moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, Wizara iuangalie huu mkanganyiko wa *TBS* na *TRA* kwenye eneo hili liitwalo *GREEN BELT*, kwani yavezekana ukawa mwanya wa kupitisha na kusafirisha bidhaa zisizo na kiwango. *TBS* wapewe nafasi ya kuzikagua bidhaa hizo bila kujali kuwa wafanyabiashara hao ni wa *category* hiyo ya *GREEN BELT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha hoja yake kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swalii moja tu; Soko la Matunda na Mboga ambalo limepangwa kujengwa eneo la Segera Mkoani Tanga litaanza kujengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na matunda na mboga zinazozalishwa Mkoani Tanga kuendelea kuoza kwa sababu ya kukosa soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakutakia kila la kheri katika Uchaguzi Mkuu ujao.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ninaipongeza hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itazame namna ya kusaidia vijijini kuwapa mkopo kupitia *SIDO* ili waanzishe viwanda vidogo vidogo vyta kusindika mafuta kutoka kwenye Mazao ya Karanga na Alizeti, mazao ambayo kwa miaka miwili mfululizo, Wananchi wa Jimbo la Igalula wanavuna kwa wingi, lakini soko ni dogo ndani ya Jimbo na nje pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Igalula wanahitaji kutengeneza mafuta badala ya kuuza malighafi hizo nje ya Jimbo lao na badala yake kununua mafuta ya KORIE, yenye lehemu nyingi badala ya kutengeneza mafuta ya Karanga na Alizeti ambayo hayana lehemu kwa afya ya walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, Zao la Mpunga linakua mwaka hadi mwaka hasa baada ya uhamasishaji wa kilimo cha ng'ombe hususan kwenye Kata za Miswaki, Loya, Kunalimwa na kuvuna mpunga mwangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kuuza mpunga, wakipata viwanda vidogovidogo ni rahisi kukoboa mpunga na kuuza mchele na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipaye maelekezo ili Wananchi wa Jimbo la Igalula waone nini wachangie katika upatikanaji wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza kwa dhati, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nimeugawa katika sekta mbili kuu; Viwanda na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda: Katika uchumi wa nchi yoyote, Sekta ya Viwanda, inao mchango mkubwa ili Sera ya Kilimo Kwanza ifanikiwe, hakuna budi iende sanjari na Sera ya Viwanda. Katika mazao, yawe ya chakula au biashara ni vyema yamfikie mlaji yakiwa yamesindikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda haviongezi tu thamani ya mazao, bali pia ni chanzo kikubwa cha ajira na pia huongeza mapato ya Serikali kwa njia ya kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Korogwe (V) ni Wakulima wazuri wa matunda, mboga na chai. Mazao yote haya yanahitaji viwanda vya usindikaji kuyaongeza thamani, lakini leo hii Korogwe haina Kiwanda hata kimoja, badala yake mazao haya hupelekwa nchi jirani kama malighafi kwa viwanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati muafaka, Wananchi wa Korogwe tupatiwe viwanda vya usindikaji wa matunda na mboga; mali ghafi tunayo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakulima wa Chai tunao ushirika wetu (*SAKARE Joint Co-Operative*). Ushirika huu unazo eka takriban 400 za chai na una jumla ya Wakulima 1800. Juhudi za muda mrefu zinafanyika ili ushirika huu uwe na kiwanda chake cha kukausha na kusindika chai yake. Tunaiomba Wizara ikishirikiana na Bodi ya Chai, ifanikishe zoezi hili ambalo litakuwa mkombozi mkubwa kwa wakulima hawa wa Dindira, Bungu na Vugiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masoko: Sote tunatambua kuwa mazao yetu ya shambani yanahitaji masoko kama vituo vya kuhifadhi na kuuza. Kwa niaba ya Wananchi wa Korogwe (V), napenda kuipongeza Wizara hii kwa kutujengea soko la mazao katika eneo la Makuyuni upande wa Magharibi wa Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa Jimbo, Wananchi wa upande wa Mashariki mwa Jimbo, wanaomba kituo (Soko) cha kukusanya na kuuza mazao yao, kwani eneo hili ni maarufu sana kwa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri, Naibu wake pamoja na Watendji wote wa Wizara hiyo, kwa kuandaa Hotuba ya Bajeti hii na kuiwasilisha katika Bunge lako Tukufu leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii katika nchi yetu ni muhimu sana kama kweli tunataka kuleta mabadiliko ya kweli kwa Watanzania wetu walio wengi, ambao ni Wakulima na wameendelea kulima kwa bidii lakini bado ni maskini kwa sababu mazao yao yanakosa masoko kutokana na kutokuwa na viwanda vya kutosha katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiona bidhaa mbalimbali zikiingia katika nchi yetu na kuuzwa zikiwa hazina ubora wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tumeona Juice zinazotoka Kenya zinauzwa, cha ajabu matunda wanayotengeneza wanayanunua kwetu Tanzania wanapeleka kwao na baadaye wanarudisha kwetu kama Juice na kutuuzia kwa bei mbaya, wakati wao wanunua matunda kwa bei ndogo sana, ndiyo maana wakulima wetu wanaendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike wakati sasa wa kuwa na dhamira ya kweli ya kuwasaidia Wananchi na dhamira ya kweli ya kuwasaidia Wananchi wa Tanzania na Wakulima kwa kuweza kutafuta wawekezaji wa kweli katika eneo la viwanda ili mazao yao yawe na bei kubwa.

Pia viwanda hivyo vitatoa ajira kwa watu wetu, tumekuwa tunaona wageni wengi wamekuwa wanaingia katika nchi yetu kwa kigezo cha uwekezaji, lakini biashara wanazozifanya zingeweza kufanywa na Watanzania wa kawaida kama watawezesewa hivi kweli kumpa mtu kibali cha kuuza maua ya plastiki na marembo ya aina hiyo kweli tunaisaidia nchi yetu? Tunahitaji wawekezai wakubwa toka nje wa kutujengea viwanda ili tuweze kukuza uchumi wa Taifa letu na watu wake; hivyo basi, tunaiomba serikali ilione hili na ichukue hatua za haraka ili Watanzania tutoke kwenye kadhia hii ya kuletewa bidhaa ambazo hazina ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee viwanda vilivyo katika Mkoa ninaotoka wa Kilimanjaro. Tulikuwa na viwanda kadhaa katika Mkoa wetu mfano, Kiwanda cha Machine Tools, Kiwanda cha Madawa na Kiwanda cha Ngozi. Viwanda hivi vilisaidia sana uchumi na ajira katika Mkoa wetu, lakini ni miaka mingi sasa viwanda hivi havifanyi kazi na hii imesababisha uchumi wa Mkoa wetu kushuka sana. Je, serikali inatuambia nini juu ya viwanda vyetu hivyo kwa sababu tumekuwa tukiuliza hapa Bungeni na majibu ni yale yale kwamba tuko kwenye utaratibu wa kutafuta wawekezaji?

Suala hili sasa limegeuka la kisiasa katika Mkoa wetu na baadhi ya watu wasiojua kazi za Mbunge, wamekuwa wakilaumu Wabunge wakati kazi ya kufufua viwanda au

kujenga barabara ni ya serikali iliyoko madarakani na siyo kazi ya Mbunge. Hivyo basi, tunaomba majibu ya kina katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, nami pia nichangie kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Ninapenda kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Mary M. Nagu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Chami na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza kitafanikiwa kama wakulima watapata soko la uhakika la mazao yao baada ya kulima. Mara nyingi wakulima wanapozalisha kwa wingi, mazao yao hushuka bei, matokeo yake hupelekea kupata bei hafifu. Serikali ifanye juhudhi za kuwatafutia wakulima masoko ya mazao yao kama vile kahawa, chai, tumbaku, mahindi na matunda mbalimbali kama maembe mananasi na machungwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikali itafute wawekezaji kwa ajili ya kuja na kujenga viwanda vya kusindika matunda kama vile viwanda vya maembe, nyanya, mananasi, ndizi na kadhalika. Serikali inakuwa na Sera ambazo huishia kwenye makaratasi bila utekelezaji, wakati wa kuwashudumia Wananchi ni sasa hasa tunapoingia kwenye Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kujenga viwanda lazima yatengwe, siyo kujenga maeneo ya makazi. Ujengaji wa viwanda maeneo ya makazi huhatarisha afya za Wananchi. Maeneo mengi katika halmashauri zetu yamejengwa kwenye makazi ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nifahamu ni jinsi gani serikali inavyovisaidia vikundi mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo na mikopo hasa vikundi vya akina mama katika Jimbo la Tarime?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoingia kwenye Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, Tanzania tutakuwa nyuma sana ukilinganisha na nchi kama vile Kenya, ambayo ina viwanda vingi. Tanzania hatutakuwa na bidhaa za kuuza nje; ni lazima serikali iwe na mkakati wa kuhakikisha kuwa, viwanda vingi vinajengwa ili nchi iweze kuuza nje bidhaa na kupata fedha za kigeni na kuimarisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunashindwa kuwa na viwanda vya kusindika matunda kama vile nyanya, machungwa, mananasi, ndizi na maembe? Ninaishauri serikali iingie ubia na makampuni mbalimbali ya ndani na nje na kujenga viwanda ambavyo vitasaidia wakulima kupata bei nzuri kwa mazao yanayozalishwa na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongozi kwa Waziri, Naibu na wataalam wote wa Wizara hii kuandaa hotuba na kuleta hapa Bungeni. Lengo la kuwepo sera ya ubinafsishaji ilikuwa ni kuleta ufanisi kwenye mashirika na viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya viwanda na mashirika yaliyobinafsishwa hayafanyi kazi kabisa vingine vinafanya kwa viwango kidogo sana na hivyo Taifa kukosa stahili yake ya mapato. Vingine vimekiuka makubaliano ya mikataba na kubadili matumizi yaliyokuwepo.

Serikali itueleze ni mkakati gani umeandaliwa kuhakikisha mashirika haya yanafanya kazi na kusaidia kuinua uchumi wetu. Suala la Kiwanda cha *TUICO* kilichopo Arusha kubadilishwa matumizi na kugeuzwa kuwa karakana ya magari badala ya *ku-process* nyara za Serikali za wanyamapori. Imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ilinde viwanda vya ndani, nchi imegeuzwa kuwa dampo la kuletwa bidhaa duni kutoka China na nchi nyingine. Serikali haoni? Tumekubali mali zetu zikose soko kwa kuruhusu biashara huria kwa kila kitu. Hii ni aibu!

Mheshimiwa Spika, ukienda Marekani, Uingereza, Canada, Nigeria hata hapo Kenya na Uganda utakuta bidhaa zinazotoka China, ni za viwango kwa kuwa China wanajua nchi hizo ziko makini na zina viwango vya bidhaa zinazokubalika kuingia ndani ya nchi zao.

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu Wizara hii imelala usingizi kabisa. Hakuna viwango vyovyothe tulivyojiwekea, tumeacha biashara huria, tumeacha wafanyabiashara wanaagiza bidhaa duni kwa bei kidogo.

Mheshimiwa Spika, sikubaliani na msemo au kauli zinazotolewa na watendaji wa Serikali kwamba uwezo wa Watanzania wa kununua ni mdogo. (*low purchasing power*) hakuna.

Mheshimiwa Spika, tuwe na viwango vya bidhaa ndani ya nchi yetu. Unanunua kiatu asubuhi, mchana kinakatika, aibu gani hii jamani?

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye uchunguzi wa kina kwenye bandari ya Dar es Salaam, makontena ya mizigo yanatolewa usiku wa manane bila kulipiwa ushuru wowote.

Mheshimiwa Spika, mizigo inapakuliwa Kariakoo kuanzia saa nane usiku hadi saa 11.00 asubuhi. Serikali na Taifa tunakosa stahili ya mapato. Kuna hujuma nzito zinafanyika kwa wafanyabiashara wakubwa wakishirikiana na watendaji wasio waaminifu wa bandari.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke viwango vya bei kwa bidhaa ambazo ni kimbilio la walala hoi. Bidhaa za vyakula na zile za vifaa vya ujenzi mfano sukari sasa ni Sh.1,800/= - 2,000/= kwa maeneo mengi sana sukari imekuwa anasa kwa familia maskini.

Mheshimiwa Spika, sukari imeona inapanda kutoka Tsh.600/=, Sh. 800/=, Sh. 1,000/=, Sh. 1,200/=, Sh. 1,400/=, Sh. 1,600/=, Sh. 1,800/= na sasa Sh. 2,000/= sababu ni nini.

Mheshimiwa Spika, tunapoacha kuweka viwango tunawapa wafanyabiashara mwanya wa kuongeza bei wanavyotaka wao kwa kutaka faida zaidi wakati huo huo wanaoumia ni wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ila ni kwa bidhaa zote ikiwa ni pamoja na mafuta ya magari.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba hatua kali zaidi zichukuliwe kwa wanaoingiza bidhaa feki nchini kwa kuwa zinahatarisha maisha ya watumiaji.

Mheshimiwa Spika, hatua zaidi zichukuliwe za kulinda viwanda vya ndani. Viwanda vya ngozi ziimarishwe kama ilivyokuwa jirani zetu Ethiopia.

Mheshimiwa Spika, kazi njema.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuiwezesha zaidi nchi yetu kukuza sekta ya viwanda, biashara na masoko. Nchi imepiga hatua sana na hili pia limeondokana na umaskini na busara za Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Waziri wa Wizara hii na wasaidizi wake wote akiwemo Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Cyril Chami.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Jiji la Dar es Salaam wana mpango wa kuendeleza eneo la machimbo ya mawe la Kunduchi kwa kulitayarisha eneo hilo na kulifanya kuwa ni eneo la viwanda vidogo vidogo vya aina mbalimbali na kuweka benki kwa ajili ya kutoa mikopo na huduma za kibenki kwa wajasiliamali hao.

Mheshimiwa Spika, wazo hili ni zuri sana hivyo, naomba uongozi wa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko kushirikiana kwa karibu na uongozi wa Jiji la Dar es Salaam kwa nia ya kufanikisha mpango huu na kuangalia uwezekano wa kutoa nyenzo zinazoweza kuharakisha nia hii.

Mheshimiwa Spika, bado pia nasisitiza Serikali kuhamasisha wawekezaji kujenga Kiwanda cha Kusindika Samaki katika eneo la Kigamboni ili kuwawezesha wavuvi wa eneo hilo kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nawapongezeni nyote kwa kutuletea hotuba nzuri licha ya ufinyu wa pesa mnazopata, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, nichangie kwa kukumbusha mambo machache ya kule Wilayani kwetu Hai. Viwanda eneo la *Machine Tools*. Muda umekuwa mwingi sana wa kukifufua Kiwanda cha Kilimanjaro *Machine Tools* pamoja na uanzishwaji wa viwanda vingine katika eneo hili. Swali, ni nini kinachoendelea katika eneo hili?

Mheshimiwa Spika, eneo la *KIA*. Tulishatenga eneo katika Wilaya yetu ya Hai na kukubaliana kuhusu uwekezaji wa viwanda katika eneo hili lakini bado hatuelewi kinachoendelea. Hili ni eneo muhimu sana ikizingatiwa na miundombinu muhimu yote ipo ni kiasi cha kuamua kuitumia tu. Kwa niaba ya wananchi wa hai naomba tufanye maamuzi ya haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, sekta ya biashara na viwanda ni mionganoni mwa sekta muhimu zinazoweza kuchochea maendeleo ya kiuchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi kama yetu ambayo kilimo ndio kimekuwa ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa imekuwa inazalisha mazao kadhaa ya chakula na biashara. Lakini imekuwa ni bahati mbaya sana kwamba wakulima wetu wamekuwa wanaiza mazao yao kwa bei ya chini kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya kutosarifu mazao na hivyo kuyaongezea thamani ili mkulima apate kuuza mazao yake kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya viwanda nchini yanakuwa taratibu mno, hususan viwanda vyta kusindika mazao ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, kasi hii ya ukuaaji wa viwanda ndiyo inayopelekea wakulima kuuza mazao yao kwa walangazi kwa bei ya chini. Ni dhahiri kwamba ipo haja kwa Serikali kuendeleza kushawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuendeleza sekta ya viwanda vitakavyoweza kusindika mazao ya wakulima yakiwemo, matunda ambayo yamekuwa yanaiza tu kwa kukosa soko, nyama, ngozi na mazao ya biashara.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa viwanda nchini ni lazima uende sambamba na ukuaaji wa shughuli za kibiashara, kinyume cha hivyo, wananchi watazalisha bidhaa zao kwa gharama lakini hatimaye watapata hasara iwapo masoko yatakuwa hayapatikani.

Mheshimiwa Spika, suala la soko la bidhaa zinazozalishwa nchini ni lazima liangaliwe kwa undani zaidi hasa ukitilia maanani makubaliano yaliyofikiwa ya kibiashara na *Customs Union* ya nchi za Afrika Mashariki. Makubaliano haya yasije yakapelekeea bidhaa zetu hapa nchini zikakosa soko na badala yake tukaishia sisi kuwa ni soko la bidhaa kutoka kwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni lazima mazao au bidhaa zinazozalishwa mashambani na viwandani yakidhi viwango vya ubora ili bidhaa hizo zihimili soko la ushindani na hatimaye wananchi wetu waweze kufaidi fursa hizo za soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini pia na masoko mengine duniani.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilituahidi hapa kwamba itaanzisha Mfuko unaoitwa *Export Development Fund* kwa ajili ya kuikuza sekta ya biashara nchini. Ni vyema basi Serikali ikatueleza utaratibu wa uanzishwaji wa Mfuko huu umefikia wapi na umesaidia kiasi gani kuisaidia sekta hii ya biashara nchini.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2010/2011. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Dr. Mary M. Nagu, Naibu Waziri Dr. Cyril A. Chami, Katibu Mkuu Bibi Joyce K. G. Mapunjo na timu yao yote kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa na kuleta mabadiliko makubwa ndani ya Wizara na Mashirika na taasisi zilicho chini yake. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nina maoni kwenye maeneo yafuatayo:-

Upande wa utumiaji wa bidhaa zinazotengenezwa ndani pamoja na Wizara kuwa na taasisi zake kuonesha mfano, bado jitihada ziongezwe hasa kwenye upande wa vifungashio (*Packing materials*) ili bidhaa ziongezwe mvuto kwa watumiaji hasa vyakula na vifaa vingine vitumikavyo majumbani. Nafikiri matangazo kwa bidhaa zingine yaendelee kutolewa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa stakabadhi ya mazao ghalani umesaidia sana kwa mazao ya chakula kwa kuwasaidia wakulima kuuza mazao kwa bei nzuri kidogo. Ushauri jitihada ziongezwe ili kuwawezesha watumiaji na waendeshaji maghala kupata masoko yenye bei nzuri ili kuzuia mrundikano wa mazao kwa muda mrefu, wasaidiwe kupata masoko ya mazao.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani inaelekeza kabisa aina ya mahali na jinsi yanavyopaswa kuendeshwa. Wengi hawajakidhi haja ya sheria hiyo, ukaguzi uwe unafanywa ili kuona kama yanafikia kiwango.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* imesaidia sana kuongeza ajira nchini, tatizo linaloipata *SIDO* ni mtaji mdogo kuweza kuwafikia walengwa wengi. Wizara ione umuhimu wa kuitafutia mtaji shirika hili badala ya kutegemea misaada au ufadhili zaidi. Bado ombi langu ni kuona Serikali inaiongezea *SIDO* mtaji ili kuwasaidia wajasiriamali wengi badala ya kutumia benki ambazo haziwafikii walengwa.

**MHE. FATMA A. FEREJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la *EPZA* ni la muhimu sana na litakapofanikiwa litakuwa ndio mkombozi kwa kukuza uchumi wa nchi yetu, lakini bado inasikitisha kuona jamii ya Watanzania haijelimishwa vya kutosha, kuhusu faida yake kwetu. Hii ndio sababu bado kuna ugumu wa kupata ushirikiano wa kutosha katika kupata maeneo ya ardhi yenye ukubwa wa kutosha kwa ajili ya shughuli za *EPZA*. Nashauri elimu ya kutosha itolewe kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kufanya kila linalowezekana kuhakikisha maeneo ya *EPZA* yanatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya maji na umeme ambayo ni muhimu kuvutia wawekezaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iijitahidi kuhakikisha vijana wetu wanajengewa uwezo ili waweze kupata ajira katika uwekezaji katika maeneo hayo hasa katika kipindi hiki cha soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vinginevyo faida ya kuwapatia ajira vijana wetu itakuwa haipatikani.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ikajitahidi kutafuta wawekezaji ambao watatumia *raw materials* zinazotoka hapa nchini kwetu, mfano, viwanda vya kusindika matunda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha viwanda vya mafuta ya kupikia vilivyopo Morogoro ambavyo vinashindwa kuzalisha kutokana na mafuta yanayoingizwa kutoka nje, vinasaidiwa ili viweze kuingia katika uzalishaji?

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika vbunjeni bila ya kushikwa mkono. Hii dalili tosha kuwa nimeamka mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hotuba ya Mheshimiwa Dr. Mary Nagu ni dhahiri kuwa Wizara imejiandaa kuinua uchumi wa nchi yetu. Kwa mtazamo wa Wizara ni wazi bajeti ya Wizara ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inahitaji mageuzi ya uchumi kiutekelezaji na sio kwa maneno tu. Kutokana na bajeti ilivyo ni wazi Wizara itashindwa kufanikisha azma yake kivitendo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kauli mbiu ya Serikali ya Kilimo Kwanza, ni lazima kuwepo kwa viwanda pia na masoko. Mkulima ni mzalishaji, kupatikana kwa maendeleo juu ya kilimo chake ni lazima pawepo na viwanda na masoko. Ili Serikali

iweze kufanikisha uchumi wake ni lazima tufufue viwanda vyetu, kwani katika dunia nchi haiwezi kukua bila viwanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhuru wa biashara. Serikali mara nyingi imekuwa ikizuia wakulima kuuza mazao nje ya nchi na hivyo kuwafanya wafanyabiashara na wakulima kugandamizwa katika dimbwi la umaskini. Kufanya hivi ni kumnyima mkulima uhuru wake na kumlazimisha kuuza kwa bei ndogo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na tatizo sugu lililoikabili nchi yetu. Wafanyabiashara mara nyingi tunashuhudia vyombo vyatilizwa na hapa nchini. Hiki ni kitendo cha kupongezwa kwa Serikali. Lakini tujiulize hivi mfanyakisho huyu amepewa taaluma ya kujuua ubora wa kifaa kinachohitajika hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, napenda kuiomba Serikali imwongezee fedha Mheshimiwa Waziri ili aweze kuvifufua viwanda vyetu ambavyo vimeshindikana kufufuka.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. FATUMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa kuwapongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuwa na mipango mizuri ya Bajeti yeke. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kama ifuatavyo, mizani inayotumika kupimia pamba vijijini ni mizani ambayo inaiibia wananchi kwani ni vipimo vyatilizwa na hapa nchini. Ni bora sasa ziangaliwe upya ili mazao yapimwe vizuri. Wananchi wanapopunjwa kutokana na mizani mibovu, basi hulipia kisasi kwa kuongeza uchafu katika mazao ili kuongeza uzito na kutokana na hilo, ubora wa mazao yetu Tanzania hupungua na thamani yake hushushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa Kilimo Kwanza ni budi kuwa na viwanda vingi zaidi ili kuthaminisha mazao. Viwanda ni budi viimarishwe ili kusindika mazao na yawe na thamani na hivyo kuneemesha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko bidhaa zinazosindikwa katika viwanda ni budi ziwe na soko. Kwa hiyo, kitengo cha masoko ni lazima kiimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mchuchuma na Liganga, mradi huu ni muhimu sana. Serikali ifanye juhudhi zote ili kuendeleza mradi huu kwa ajili ya faida ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Ukanda wa *Mtware Corridor* (Kusini) haina viwanda vyatilizwa na kutosha pamoja na kwamba kuna malighafi. Kuna *gypsum*, samaki wengi, chuma, mkaa, gesi, malighafi ya kutengenezea mbolea, kuna bahari, kuna miti ya mbao za kila aina. Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kuelekeza viwanda katika mikoa iliyopo ukanda huo? Tuelezwe leo kuna mkakati gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vilivyobinafsishwa na sasa havifanyi kazi hadi sasa wanyang'anywe haraka virudishwe Serikalini na kuuzwa upya.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungunzia juu ya bidhaa mbovu zinazoingia katika soko la Tanzania kwani zinaipotezea Tanzania fedha nyingi hasa bidhaa hizo hafifu zinaposababisha ajali mfano nyaya za umeme na vifaa duni nya umeme vinasababisha nyumba nyingi kuungua moto na kusababisha hasara ya maisha na mali za watu wengi. Serikali ichukue hatua muhimu kuzuia uharamia huu ili kulinda viwanda vyetu, maisha na mali za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu wenyewe vinavyotengeneza bidhaa hafifu mfano kiwanda cha viberiti, wananchi wanalamikia upungufu wa njiti za viberiti katika boksi moja, pili njiti zisizotiwa baruti au baruti hafifu hivyo njiti hizo haziwaki kwa wakati na hivyo kuwatia hasara wananchi maskini wanaovitumia. Wizara ya Viwanda, ifuatilie tatizo hili ili wananchi wapate bidhaa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masoko ya nje kwa bidhaa zetu na mazao ya mashamba, tunaomba Mkoa wa Rukwa na hususan Wilaya ya Kalambo, Wizara hii itusaidie kupata masoko ya mazao yetu ya mahindi, maharage, alizeti na kadhalika. Tunalo soko la Kimataifa pale Matai lakini toka lijengwe hakuna juhudi za Wizara hii ili soko hili lifanye kazi yake ipasavyo ili kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kama ilivyo kwa Kibaigwa badala yake tunafungiwa mipaka tusiuze mazao nje hivyo kushindwa kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka yote Wizara hii naiomba ituboreshee mnada wa mpakani Kasesya, hakuna lolote lililofanyika kwa nini? Badala yake ni ahadi hewa tu ndizo hutolewa. Inasikitisha kuendeleza viwanda Mkoa wa Rukwa itasaidia kuboresha bei ya mazao yetu tatizo hatuna umeme wa kutosha. Serikali isikilize kilio chetu. Nawasilisha.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu, wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kwamba haya yote yaliyopendekezwa ndani ya hotuba hii myafanyie kazi, vitendo viwe zaidi kuliko maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mkubwa ni la matunda mengi kuoza kwa sababu ya kukosa masoko au viwanda nya kusindika matunda haya. Zamani Korogwe Mjini kulikuwa na Kiwanda cha *Tangold*. Kiwanda hiki kilikuwa na manufaa

sana kwa wakulima wa matunda katika Mkoa wa Tanga hasa Wilaya za Korogwe, Muheza na Lushoto ambao wanalima sana machungwa, maembe, *passions* na nyanya. Wananchi hao walijikwamua sana na umasikini kwa kuuza matunda yao *Tangold*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kile kiliwahi kupata medali ya dhahabu kwenye *products* zao hasa *mango juice* na *mango pickle*. Nataka kufahamu Wizara ina mkakati gani wa kukifufua kiwanda hiki? Mimi nimekuwa nikichangia kuhusu suala hili kila mwaka, lakini cha kusikitisha sipewi majibu. Eneo hilo sasa linaendelea kuwa gofu. Kwa bahati nzuri miundombinu yote inayohitajika kufanikisha kujenga kiwanda ipo. Kwa hiyo, kinachohitajika tu ni kupata mwekezaji. Naomba kusisitiza sana ujenzi wa kiwanda hiki na ningefurahi kupata jibu la uhakika. Ahadi kwa suala hili imekuwa ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo mchango wangu ni hilo tu la kuwakwamua wanacnhi wa Mkoa wa Tanga. Wakulima wa matunda kujikwamua na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, suala hili sasa limekuwa la kisiasa naomba jibu.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naipongeza hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa jinsi gani imeandaliwa kwa uchambuzi makini. Pia naiunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Kiwanda cha Saruji – Shinyanga. Katika Kikao cha Bajeti mwaka 2008/2009 Wizara hii ilikuwa na mkakati wa kujenga Kiwanda cha Uzalishaji Saruji Shinyanga kwa mwekezaji fulani. Je, mpango huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya saruji, moja ya hatua katika maisha bora ni kuwa na nyumba bora. Hoja yangu ni kuwa na bei ya juu sana ya saruji hii. Saruji inapozalishwa Dar es Salaam na baadaye kusafirishwa hadi Mwanza bei hupanda hadi mara mbili ukilinganisha na bei ya Dar es Salaam. Hivyo, kama tutalenga kupunguza bei hii ombi langu ni lile la jitihada za kusogea huduma za viwanda karibu na maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa wajasiriamali inayohusu uendeshaji wa viwanda vidogo vidogo ndio itawakomboa wanapozalisha mazao yao, wanapaswa wajue watapeleka wapi, atasindikaje na baadaye iweje kwa manufaa yake. Bajeti izingatie hili na ajira kwa maana ya tatizo litapungua.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, mtani wangu, dada yangu na jirani yetu Mkoa wa Singida kwa juhudhi na umahiri mkubwa katika kazi na jukumu alilopewa na Mheshimiwa Rais la kuongiza hii Wizara nyeti ya Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, nampongeza Naibu Waziri na Katibu Mkuu pia watendaji wote. Kazi yao nzuri imeonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kuishukuru Serikali kwa kuleta Kiwanda cha Kuchuja (*purify*) mafuta ya alizeti Mkoani Singida. Naamini sasa Wanasingida watazidi kunufaika nacho.

Ombi langu kwako ni kutokana na mwitikio wa Kilimo Kwanza umeitikiwa kwa kasi zaidi na wakulima wa Mkoa wa Singida, hivyo Kiwanda cha ku-*purify* kitazidiwa, kwa hiyo, naomba tuongezewe tena Kiwanda kikubwa zaidi ili kiweze kukidhi mahitaji ya wakulima na wakamuaji wa mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni shukrani kwa Wizara kwa kutambua umuhimu wa COSOTA na hivyo kutoiacha ifanye kazi zake bila Bodi hatimaye kuteua wajumbe wa Bodi, swali langu, je, Bodi hiyo imeshaanza kazi? Na kama imeanza, lini? Na kama bado, itaanza lini? Na je, Serikali inawaambia nini wasanii au tumaini gani toka COSOTA kulinda kazi zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Namwamba mtani wangu, dada yangu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu achaguliwe tena. Mungu awe pia na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami katika mchakato ujao na hatimaye sote turudi hapa Bungeni mwezi Novemba, 2010. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza mtani wangu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, mwanangu mpendwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenyenye mtazamo wa kuboresha sekta zote ndani ya Wizara hii kwa kuanza na vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi kabla sijaanza kutoa mchango wangu napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono Bajeti hii mia kwa mia.

Hivyo basi ninawaomba wapiga kura wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, wawape kura za kishindo ili warudi Bungeni kwani kwa uwezo wao mkubwa nina amini Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye naye atapata ushindi mnono atawarudishia tena madaraka haya ili waweze kutekeleza azma yao kupitia Bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha pamba, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Mary Nagu kupitia swali langu hapa Bungeni juu ya kutafutiwa mwekezaji kujenga Kiwanda cha Kusafirisha Mafuta ya Alizeti kwani tayari alishamleta na ameshajenga. Hii inaonyesha jinsi gani Mheshimiwa Dr. Mary Nagu anavyojali hoja za Wabunge kwa niaba ya wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufikisha ombi langu tena kwa Serikali kuona uwezekano wa kutujengea Kiwanda cha Kuchambua Pamba. Ni imani yangu itarudisha ari za wakulima wa zao la pamba kwa kiasi kikubwa kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko la mafuta ya alizeti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuondoa ushuru wa zao la alizeti jambo ambalo lilikuwa kikwazo kwa wakulima na wafanyabiashara wa zao la alizeti. Tatizo ambalo bado lipo ni soko la uhakika la mafuta ya alizeti pamoja na mashudu yake, ukweli zao hili uzalishaji wake huongezeka mwaka hadi mwaka hivyo wananchi wakijua soko la kudumu la mafuta ya alizeti wataongeza uzalishaji kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kiwanda cha ngozi na cha kusindika maziwa kijiji cha Msungua katika Kata ya Sepuka Wilaya ya Singida, napenda kupongeza juhudzi za Mkurugenzi wa Halmashauri ya Singida Vijijini kwa kushirikiana na watendaji wake pamoja na wananchi kujenga Kiwanda cha Ngozi pamoja na cha kusindika maziwa huko Sepuka.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuendelea kuunga mkono juhudi hizo kama alivyoonyesha Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa ziara yake mkoani Singida Aprili 27, 2010 hadi 01 Mei, 2010 kwa kutenga fedha za kukipanua na kukiimarisha kiwanda cha ngozi na cha maziwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ninaomba Serikali kututafutia soko la asali la kudumu kwa zao hili, Singida lipo na ni ya kutosha kabisa bali soko lake ni duni sana, wenyewe asali hutegemea wasafiri wanaopita na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuitahadhalisha Serikali kuwa ni bora kuthamini uzalishaji wa mazao na vyakula vya ndani kuliko kuthamini uzalishaji wa vyakula au mazao ya nje. Hii itatusaidia sana kutangaza na kukuza uchumi wetu na kuinua vipato vya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mazao ya nje na vyakula vya nje visiingie kama tunavyo vya ndani ama bei za mazao ya nje yawe na ushuru ili bei yake iwe kubwa ili kusaidia soko la vyakula na bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. NDASSA M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono, na nampongeza mheshimiwa waziri, naibu wake pamoja na katibu mkuu na watendaji wote wa wizara pamoja na taasisi zilizochini ya wizara. Kitabu chako cha hotuba yako ni cha kiwango cha aina yake *TBS* imekipitia vizuri, lakini swalii langu dogo gharama ya kuchapa kitabu ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza kitafanikiwa kama kuwa na viwanda vidogo vidogo, vya kati na viwanda vikubwa. Bila kuwa na viwanda hivyo itakuwa ni kazi bure, Kilimo Kwanza hakitafanikiwa kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua maandiko na machapisho yapo mengi kwenye ofisi za Wizara, tafiti nyingi, zimeshafanyika nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya maandiko, machapisho na tafiti mbalimbali kama yatafanyiwa kazi kwa kutekeleza, tutahama hapa tulipo na kwenda mbele ambapo sekta ya viwanda itazalisha *GDP* kubwa zaidi kwenye Pato la Taifa kuliko hivi sasa ambalo halizidi asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu vinavyofanya kazi vina tatizo la umeme unaokatikakatika, uzalishaji mkubwa wa viwanda unategemea umeme usiokatika. Hapa nashauri Wizara yako na Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla kuwa viwanda vyetu vinapata umeme wenye uhakika ili uzalishaji uongezekere.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu hoja za Wabunge anijibu suala zima la viwanda vya kuchambulia pamba vilivyokuwa katika Mkoa wa Mwanza ambavyo vilikuwa vinatoa ajira kubwa katika maeneo yetu kama vile *Nyambiti Ginnery*, *Ngasamo Ginnery*, *Nassa Ginnery*, *Kasamwa Ginnery*, *Manawa Ginnery* na kadhalika. Hivi tatizo ni nini? Serikali imesema nini kuhusu viwanda hivyo. Lakini pia tuelezwe ki-ukweli viwanda vya Mwanza *Tanneries* kitafufuliwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ithubutu kutenda, Serikali itembee juu ya maneno yake, maandiko yake na tafiti zake. Ahsante.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi kwa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na kutopata fedha za kutosha katika malengo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi nazitoa kwa Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Mary Nagu, Naibu Waziri C. Chami, Katibu Mkuu, Bibi J. Mapunjo na wataalamu wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi yenye utajiri mwingi, lakini bado nchi yetu inasuasua kutumia raslimali tulizonazo hapa nchini. Hata hivyo, hatua kubwa tumepiga tukilinganisha na miaka ya nyuma tulikotoka. Hata hivyo, ni vyema tupate tamaa ya kujilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya biashara na mbinu za kuuza na hasa kupata masoko kwa mazao yetu ni jambo muhimu la kuangaliwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo moja, zao moja ni sawa kabisa na ni muhimu, kwani ni rahisi kupata misaada ya pembejeo, uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na pia katika kutoa utaalamu na kutafutiwa masoko, mafunzo ya kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao muhimu yanayovumilia ukame, magonjwa kama mihogo, nanasi, ndizi, embe, nyanya na aina nyingi za mboga, ni muhimu yakazalishwa kwa wingi na kwa pamoja ili kuwezesha kupata soko kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, embe zilizokatwakatwa (*sliced*) na kukaushwa vizuri na katika hali ya usafi zina soko kubwa nje ya nchi. Serikali ijitahidi katika kutafuta soko na utaalamu na mafunzo katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la nazi ni zao ambalo hivi karibuni limekuwa la muhimu sana duniani kote, kutokana na mafuta ya nazi kuwa mafuta bora duniani katika afya zaidi ya mafuta ya *Olive Oil*. Mafuta ya nazi yamepita mafuta ya *Olive Oil*. Bei ya mafuta ya nazi mwaka 2008, *American* ilikuwa US 30 kwa nusu lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta ya nazi ya kula hayaleti *cholestrol* kabisa. Mafuta ya nazi pia hutumika kwa kupakwa mwilini, kupaka nywele na kadhalika. Inashangaza sana mpaka sasa hivi Seikali yetu haijahamasisha wananchi hasa waishio Pwani kupanda minazi mingi, kwa biashara. Wizara hii ijitahidi sasa kufanya utafiti wa kina kujuu kuwa nazi kiasi gani tulizonazo na kutafuta soko la nje na kuhamasisha wananchi kupanda zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu aliyekiye salama katika Bunge hili kwa kipindi cha miaka kumi ya Ubunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Marehemu Mama yangu Anne Schubert na baba zangu Dr. Joseph Mutahangama na Baba Marck Macheja kwa kunilea. Sir Clement George Kahama kwa kunitia nguvu katika kazi zangu za uenyekiti wa UWT Mkao wa Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka kumi na kwa Ubunge kwa kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wanangu George Andrew Kahama, Anna Kahama Rupia, Joseph Kulwa Kahama, Josephine Doto Kahama, Djakpasum na Clement Kiiza Kahama kwa kunivumilia. Pia nawashukuru wakwe zangu, Veronika Kahama, Nancy Kahama, Peter Rupia, Devine D'Jakpasu na wajukuu wangu Pieta, Paul, Sammy, Bina, Sigfride, Taffy Janet, George Peter, Andrea Nikolai, Adriana na Mathew.

Nawashukuru sana dada zangu Mary Haise Mackeja (*late*) Martha Jene Mtebe, kaka Charles Mackeja (*late*) Capt. Joseph Mutahangama. Julie Kahangi, Patrick Mutahangama (*late*) Angel Kagwa, Regina Wandiga na ndugu zangu wote na marafiki na wapigakura wangu, wanawake wa UWT toka Mkao wa Dar es Salaam. Mwenyezi Mungu awabariki.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tangu niingie Bungeni nimezungumzia kila mwaka juu ya umuhimu wa Serikali kushawishi wawekezaji wawekeze kiwanda cha sarufji eneo la Itigi ambako kuna malighafi ya *gypsum (jas)* na udongo mwekundu (*red soil*).

Pia kuna “deposits” za chokaa (*lime*) ingawa inasemekana ni kwa kiasi kidogo kuliko *jas*. Hata hivyo, malighafi ya chokaa iko kwa wingi eneo la Ugwandi (Wembere) ambako utafiti wa kutosha bado haujafanyika kubaini kiasi cha chokaa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi zangu zote kuhusu hili, Serikali bado inasuasua juu ya kufanya utafiti wa kutosha. Nashauri utafiti ufanywe upya badala ya kutegemea kumbu kumbu ya “Research” zilizofanywa na Wakoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba Serikali ishawishi/ilete wawekezaji Itigi kuweka kiwanda cha saruji. Tuepuke “Misallocation” ya viwanda kama ilivyotokea enzi za Marehemu Amir Jamal alivyolundika viwanda vyote muhimu Morogoro. Itigi tuna umeme, tuna reli, tuna barabara, tuna maghala ya Shirika la Reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, *gypsum* inayochimbwa Itigi hulisha viwanda vya saruji vya Wazo, Tanga, Mbeya na viwanda vya saruji vya Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wachimbaji wadogo wadogo wananku kwa ufukara, hawalipwi vizuri na kwa wakati. Wengi huishia kulipwa na wakala wanaosafirisha *gypsum* kwenda kwenye viwanda hivi. Hata kama viwanda vinawalipa wakala wa usafirishaji bado fedha haiwafikii wachimbaji hawa wajasirimali kwa visingizio mbalimbali, matokeo yake watu hawa wanakopwa nguvu zao (ambazo ndiyo mtaji wao wenyewe).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba haki itendeke kwa viwanda husika kuliwapa wachimbaji moja kwa moja badala ya mtindo wa sasa wa kuwalipa wakala.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani na pongezi zangu kwa niaba ya wananchi wa Rarya, kwa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu - Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara. Mheshimiwa Waziri na timu yake wamefanya kazi nzuri sana tangu wapewe uongozi wa Wizara hii. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *SIDO* ndiyo mkombozi wa wanyonge waishio vijijini. Fedha zinazotengewa *SIDO* ni ndogo sana. Hivyo, kushindwa kutoa mafunzo kwa wajasirimamli vijiji. Ushauri *SIDO* itengewe fedha za kutosha kwa kutunisha mfuko kwa ajili ya wajasirimamli vijijini.

Nampongeza Meneja wa *SIDO* Mara kwa kazi nzuri kwa kutoa vifaa na mafunzo kwa wajasirimamli Wilaya ya Rarya. Naomba waongezewe fedha kwa kuwa wajasirimamli katika vikundi mbalimbali wanaomba mafunzo. Mara kadhaa Mheshimiwa Mbunge wa Rarya amekuwa anachangia au kuomba wafadhili wachangie kwa lengo la kulipia gharama za usafirishaji wa vifaa au mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa 87 kifungu 172/F nampongeza Waziri na timu yake kwa kuamua viwanda vidogo na vya kati kwa kuandaa na kutekeleza *program* inayolenga kujenga miundombinu (*industrial villagers/clusters*) itakayowezesha viwanda vidogo na kati *SME* kuongeza uzalishaji wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Rorya kuna wajasiriamali ambao wamejiunga katika vikundi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (i) Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vya wanawake viko katika Kata zote 21 na jumla ya vikundi 107, hawana hata kiwanda kimoja.
- (ii) Vikundi vya vijana akina mama vikundi vya uvuvi, viko katika kata 10 jumla ya vikundi ni 36, wanaanza samaki kwa bei ya kutupwa.
- (iii) Vikundi vya wakulima wadogo – kilimo cha umwagiliaji jumla ya vikundi 28. Wana vikundi 228. Wanashughulika na kilimo cha bustani. Wanahitaji viwanda vidogo vya usindikaji.
- (iv) Vikundi vya wajasiriamali vya useremala, wahanzi, ufundi balskeli na ushonaji ni vikundi 35 kila Kata, wanahitaji viwanda vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni mtaalam katika fani ya viwanda, naomba atamke wakati akijibu hoja zilizotolewa kuwa vikundi 206 vilivyoko Wilaya ya Rorya vitapata nafasi ya kuingizwa katika mpango wa *industrial villages/clusters*. Baada ya kuwezeshwa kujenga viwanda vidogo katika Tarafa.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya pekee natoa pongezi kwa jinsi swali langu lililohusu madai ya mafao ya wafanyakazi wa Shamba la Mpira Kihuhwi Wilaya ya Muheza kwa uwazi na kwa hatua za dhati katika kufuatilia haki ya wafanyakazi hao dhidi ya wawekezaji wawili ambao walikodishiwa shamba hilo na Serikali na wakavuna mpira na kujipatia fedha bila kulipa haki za wafanyakazi na hatimaye kuondoka nchini kinyemela. Ni matumaini yangu kwamba kwa niaba ya Serikali suala hili litaendelezwa kwa moyo na dhati na kutoa mafanikio kwa Watanzania.

Pia natoa pongezi kwa Wizara na Bodi ya Biashara ya nje kwa kuendelea kuboresha uwanja wa maonesho ya Saba Saba – Dar es Salaam. Tuendelee kuboresha barabara ndani ya eneo, kuboresha barabara na nje ya eneo kuboresha maeneo ya maegesho ya magari na kuongeza milango ili kupunguza foleni wakati wa kuingia. Pia kuendelea kuondoa gereji zinazoharibu mazingira na hali ya hewa wakati wagoni wakiwepo katika maonesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuikumbusha Wizara kuhusu ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais, ya mwaka 2005 kwa Wilaya ya Muheza. Katikati ya mwaka 2005 nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kuhusu ahadi hiyo na jitihada nilizofanya kutafuta wawekezaji. Mwanzoni mwa mwaka 2010 nilikuwa Italy na kufanya majadiliano na wawekezaji. Inahitaji Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kusaidia katika jitihada hizo na nyingine nje ya nchi. Nitakabidhi Wizara taarifa na mawasiliano ya moja kwa moja na wawekezaji hao eneo la (*ECILLIA ITALIA*).

Meneo ya EPZ – Tanga, Halmashauri ya Jiji la Tanga imetenga maeneo makubwa kwa ajili ya EPZ na kukabidhi Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) muda mrefu. Maeneo haya yaliyokuwa na wakazi bado yanahitaji kulipiwa fidia na jinsi fidia inavyocheleweshwa ndio gharama zinavyopanda na hata uwezekano wa kupoteza maeneo hayo unavyoongezeka. Iwapo dhamira ya uwekezaji Tanzania ipo, basi ni lazima Serikali iiwezeshe NDC ili iweze kuendeleza maeneo hayo yanayotengwa kwa EPZ na mikakati mingine kutengewa fedha kidogo kwa NDC kunadhoofisha azma ya kuwezesha EPZ kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la ujenzi wa Soko la Matunda la Kimataifa Segera limechukua zaidi ya miaka sita sasa. Pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kutoa eneo kubwa kwa ajili ya ujenzi bado jitihada za kuwezesha ujenzi wa soko hilo ni mdogo na hazielekei kuzaa matunda.

Tatizo ni “nani”, anayewajibika kubeba jukumu la kutafuta uwekezaji na ujenzi wa soko hilo. Je, ni Mkoa wa Tanga: Je, ni Wabunge wa Mkoa wa Tanga, na je, ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko! Iwapo wawekezaji kutoka nje wamekosekana Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko iandae tathmini gharama za ujenzi wa soko hilo na kuitisha Halmashuri zote za Mkoa wa tanga ili kwa pamoja wajenge wazo la utekelezaji wa gharama za ujenzi wa soko hili chini ya mpango wa matumizi ya fedha zilizopo chini ya mpango wa kilimo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Tanga.

Upo uwezekano pia wa kushirikisha fedha zinazotengwa kwa mkakati wa Kilimo Kwanza ili kusaidia ujenzi ukizingatia kwamba masoko ni sehemu kubwa ya mafanikio ya Kilimo Kwanza.

Kuboresha *SIDO*, *SIDO* inafanya kazi nzuri ya kuanzisha viwanda vidogo. Pamoja na kuwepo wabunifu, zimekuwa zikionekana sana katika maonesho ya biashara kila mwaka *SIDO* haipewi fungu la kutosha kuweza kuwaendeleza wabunifu hao.

Kiasi cha fedha za mikopo zinazotolewa kwa wajasiriamali ni kidogo kuwezesha uzalishaji mkubwa kwa gharama nafuu inayowezesha faida ya kutosha. Nashauri pia *SIDO* iwe na kitengo cha kusaidia wajasiriamali kuandika miradi, kuwezesha kusaidia ubunifu na uwekezaji wa thamani kwa ajili ya mikopo mikubwa kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika swala la kina mama wajasiliamali. Mafunzo kwa wakina mama ni muhimu sana ili kumpunguzia ukali wa maisha mwanamama, mafunzo hayo ni ya usindikaji kutengeneza sabuni na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nimesha wapa elimu wanawake wa mkoa wa Tabora Elimu ya Ujasiliamali mkoa nzima kwa gharama zangu nimewafundisa kutengeneza Batiki, Sabuni za vipande, Sabuni za unga, sabuni za maji, mafuta ya kujipaka, maziwa ya soya.

Je, wizara ina mpango gani sasa ili vikundi hivyo viweze kuangaliwa na *SIDO* kwani nafahamu kuna pesa za kuwawezesha wanawake kila mkoa lakini sioni vikundi nya ujasiliamali mkoa wa Tabora kwa kina mama mpaka na shirikisho la *SIDO* katika mikutano yangu ili kutambulisha sido inafanya nini, kwani serikali imeweka sido kwa kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu naomba wizara itambue vikundi hivyo kwa kuvitembelea na kuvijengea uwezo, usemi wa mwanamkea anaweza uwe na tija nimewawezesha kama wajasiliamali maeneo mbalimbali wanavyojaliwa na *SIDO* naomba kupta majibu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri walizofanya majimboni mwao na katiika wizara hii kwa muda wote walioyofanya kazi katika wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naimani majimboni mtarudi, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu (Mb) Waziri Mwenye dhamana ya Viwanda na Biashara, pia nimpongeze Mheshimiwa Dr. Cyril Chami - Naibu Waziri Viwanda na Biashara, niwapongeze Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali upo vipi katika kuimarisha Viwanda vya ndani katika kuvijengea uwezo ili kukabiliana na ushindani wa uzalishaji wa bidhaa kufanya ushindani wa soko la pamoja la Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara mipango yake iko vipi juu ya kuwezesha Viwanda vidogo vidogo vya usindikaji bidhaa mbalimbali zitokanazo na kilimo mfano, mbegu za mafuta ili kumwondolea Mkulima adha ya kutafuta soko la mazao jambo ambalo mara nyingi huleta hasara kwa Mkulima na kushindwa kufanya maandalizi ya msimu wa kilimo unaofuatia.

Katika eneo hili ningeomba ufanuzi wa dhati kwa viwanda vya usindikaji wa mbegu za Alizeti ambazo zinalimwa sana na Wakulima wa Jimbo la Iramba Magharibi. Naomba Wizara kuitia *SIDO* kuandaa mpango wa kutoa mikopo ya Viwanda hivi vidogo vidogo kwa vikundi au Mwananchi mmoja mmoja mwenye mtazamo na shauku

la kuhitaji Kiwanda cha aina hii. Utaratibu utumike kama unavyotumika ule wa mfuko wa Pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa bidhaa zinazozalishwa na Viwanda nya ndani na zile zinazoingizwa nchini kwa hivi sasa upo uholela wa bidhaa feki zinazoingizwa nchini umekithiri udhibiti uko vipi wa *Tanzania Bureau Standard (TBS)* kudhibiti hali hii ambayo sasa inahatarisha hali ya nchi kugeuzwa Dampo la bidhaa feki bado kama tatizo kubwa ambalo lipo *TBS* kushindwa kudhibiti bidhaa hizi feki, naiomba sasa Wizara kuonyesha meno ili kukomesha hali hii.

Kwa Viwanda nya ndani ni muhimu kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kiwanda kinachogundulika basi hatua kali zichukuliwe dhidi ya kiwanda hicho. Kwa mujibu wa Sheria na ili kukomesha tabia hii kabisa kwa Viwanda nya ndani Wizara ilete sheria Bungeni ya kudhibiti hali hii ambayo adhabu yake itakuwa ni kafilisiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama ya Wafanyakazi Viwandani. Wizara ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Kazi katika kuhakikisha hali ya usalama kwa Wafanyakazi wa Viwandani, ni dhahiri upo ukiukwaji mkubwa katika kuzingatia hali ya usalama kutokana na kutokuzingatia kwa masharti yanayofanywa na wamiliki wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na watendaji walio chini ya wizara hii wakiwemo Mkurugenzi wa *TIRDO*, Dr. Nanyaro na Mkurugenzo wa *SIDO*, Ndugu Mike Laizer na wengine. Kwa kazi nzuri sana waliofanya kwa kipindi cha miaka mitano ya awamu ya nne na pia kwa kuandaa hotuba ya bajeti hii iliyo na mwelekeo wenye kuleta matumaini kwa watanzania. Pamoja na poneza hizo nina maoni machache yafuatayo:-

- (i) Kuwezesha taasisi za *TIRDO* na *SIDO*, kutokana na mahitaji makubwa ya wananchi wengi walio katika kada ya chini ambao wanahitahi kupatiwa mafunzo ya stadi mbalimbali na mikopo kwa ajili ya kuanzisha / kuendeleza miradi ya kiuchumi. Je serikali kwa kutambua kuwa *TIRDO/SIDO* ni mkombozi kwa wanyonge walio wengi iko tayari kuipatia fedha za kutosha ili ziweze kuendesha mafunzo na kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo.
- (ii) Kilimo kwanza na uwekezaji, serikali itilie mkazo zaidi na ufuataliaji wa karibu zaidi kwa kuanzisha maeneo ya uwekezaji katika kilimo kwa kuanzisha mashamba makubwa na miundo mbinu ya uwamwagiliaji kujenga viwanda nya kusindika mazao mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kujenga nyumba za maofisa ugani na watumishi wengine walio na fani ya katika masuala ya kilimo ni ufugaji kwa kutenga eneo la

uwekezaji katika kilimo kutaleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na tutaweza kuua ziada chakula nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongea sana Mwenyezi Mungu awabariki watendaji wote.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri inayotoa mwelekeo sahihi kwa sekta za viwanda na biashara na masoko. Wakulima wa mboga na matunda Lushoto wanaiomba wizara itume wataalamu wa kutathmini kwa kina hali ya sasa ya uzalishaji, ufugaji, usafirishaji, uuzaaji, uhifadhi, usindikaji, na bei za mazao hayo kwa lengo la kuboresha sekta hizo kuinua vipato vya wakulima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania sasa tuko katika program ya kuendeleza kilimo na kaulimbiu iliyopo ya kilimo kwanza hakiwezai kuendelea ikiwa hatuna viwanda tija ya wakulima haitaonekana kwani mazao yao hayatapata na yataendelea kuuzwa kwa bei ndogo, kwani soko la bidhaa zao ni finyu ukilinganisha na nchi yenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kingekuwa na tija kingevutia hata vijana kwani wangeona ni ajira yenye manufaa kwao kwa kuwa wangeona lipo soko la kueleweka kuza mazao wanayozalisha. Hivyo bila viwanda nchi haiwezi kuendelea kwani mazao yetu yanaweza kama malighafi ambayo inaendelea kufeed viwanda vya nchi nyingine matokeo yake bidhaa zinazozalishwa zinaletwa kuuzwa tena nchini kwetu. Kwa mfano tungekuwa na viwanda vyangozi, ngozi yetu inayozalishwa nchini ingetengeneza viatu vyetu, mkanda, mikoba na kadhalika, badala yake ngozi inaendelea kuuzwa kama malighafi halafu tunaletewa kuuziwa bidhaa kwa bei ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi nyingi zilizoendelea, zimeendelea kwa kuwa na viwanda mfano China, tuige mfano mzuri wa wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itueleze ina mpango gani wa kufufua viwanda vya *General Tyre*, *Kilimanjaro Machine Tools*, Kiwanda cha Ngozi, Mwanza, Morogoro na Moshi. Na je serikali inasemajie kuhusu viwanda vilivyokuwa kama cha *Tanganyika Packers* cha Dar es salam na kile cha Mbeya vyote vya nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ninaloona kwa nchi yetu kutopiga hatua katika mipango yake ni kutojitegemea katika bajeti yetu ya maendeleo mfano bajeti ya 2010/2011 ni Sh. 28,917,667,000/= kati ya hizo Sh. 12,529,808,000/= za nje na Sh. 16,387,859,000/= za ndani.

Bado tunategemea pesa za nje na kwa karibia nusu ya bajeti nzima ya maendeleo tubadili mindset ili tuwezejitegemea kikamilifu tupige hatua ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tumekuwa tukiisikia uzalishaji umeongezeka wa kiwanda cha Cement, TBL, Kibuku, hatuambiwi viwanda vipyta vilivyoanzishwa katika kila baada ya kipindi cha mwaka wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inaweza kutueleza ni viwanda vingapi vimeongezeka katika kipindi cha 2005 – 20010 na sasa vimeduwa viwanda vingapi jumla nchi nzima.

**MHE.CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kwa hotuba yake nzuri. Mchango wangu utahusu zaid suala la masoko, aidha niangeomba Waziri wakati anatoa majumuishio atoe maelezo juu ya jambo hili. Tumekwisha pitisha sheria ya kuunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko kinachosubiriwa ni uteuzi wa bodi hii ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Wakulima ambao wanafanya kazi kubwa katika kuchangia uchumi wetu wanapata matatizo ya kupata bei nzuri kwa mazao wanayozalisha hali hii inafanya jitihada zao kuonekana hazina tija yoyote, wilaya yangu huzalisha mazao ambayo hayami kwenye traditional export crops kama vile mpunga mahindi ufuta alizeti na kadhalika. Mazao hayo soko lake linatawaliwa na ulanguzi kupitia watu wa kati yaani (*middleman*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwakombua wakulima hao bado ya mazao mchanganyiko ingekuwa ni chombo madhubuti katika kuwatafutia bei wakulima hao ili juhudzi zao za uzalishaji ziwe na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ombi tunaomba wizara iunde bodi hiyo mapema ili iwasaide wakulimia wengi wenye kulima mazao ambayo hayasimamiwi na bado yoyote.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nydingi zilizoendelea zimefikia hatua hiyo baada ya kufanya mapinduzi ya viwanda (*Industrial Revolution*). Bila viwanda ni vigumu sana kuendelea kwani malighafi zilizopo zitapotea bure au zitauzwa kwa bei ndogo.

Tanzania ni nchi ilijojaliwa malighafi nydingi hasa ikizingatiwa kuwa asilimia zaidi ya 80 ya watu wetu ni wakulima. Tuna mazao kama katani, pamba, ufuta na kadhalika. Ni wazi kama hatuna viwanda itakuwa vigumu kuchakata malighafi hizi na kuwa nguo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa hata vile viwanda vichache tulivyokuwa navyo pia vimeuzwa na kutekelezaww mfano, *Tanganyika Packers, Kilimanjaro Machine Tools* na kadhalika. Hii ni aibu kubwa sana kwa Taifa. Ni lini serikali itafufua viwanda hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa viwanda tulivyo navyo vingi vimeingia ubia na nchi rafiki mfano kiwanda cha Urafiki Textile kuna malalamiko mengi kuhusu manyanyaso wanayopata wazawa hasa katika mishahara kuwa na tofauti kubwa huku

wakifanya kazi za kufanana. Lakini pia kumekuwa na taarifa kwamba baadhi ya vifaa vimekuwa vikiuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifuatilie malalamiko ya wafanyakazi hao kwani tunategemea sana bidhaa zinazotokana na kiwanda hiki hasa khanga na vitenge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza orodha ya wachangiaji waliopata nafasi. Kwa hiyo, kwa nafasi hii nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri aanze kutoa majibu kwenye hoja mlizotoa na tutampa dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza kuichangia hoja hii kwa kumshurkuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima na afya.

Pili, namshukuru Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani ambayo ameendelea kuwa nayo juu yangu na kunipa fursa ya kuendelea kulitumikia Taifa letu katika nafasi hii ya Unaibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa ushauri na maelekezo yake mbalimbali yanayonisaidia kuyamudu vyema majukumu yangu. Namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dr. Mary Nagu kwa imani yake kubwa anayoonesha kwangu kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika kuiongoza Wizara hii.

Namshukuru sana Katibu Mkuu Bi. Joyce Mapunjo ambaye kama alivyo Waziri Nagu ni Mwanamama mahiri, mzalendo, mchapakazi na asiyechoka kulitumikia Taifa letu. Namshukuru sana Ndugu yangu Naibu Katibu Mkuu - Dr. Shaban Mwinjaka kwa uchapakazi wake wa kutolea mfano na ushirikiano mkubwa wanaonipa.

Aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa Wakurugenzi wote walio Makao Makuu na wa taasisi zilizochini ya Wizara na pia Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa uchapaji kazi wa kiwango cha juu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, nampongeza Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote Wabunge kwa jinsi mnavyoshirikiana kuliendesha Bunge letu vizuri. Naomba kwa namna ya pekee niwashukuru kwa dhati kabisa wapigakura wangu wa Moshi Vijijiini kwanza kwa kunichagua kuwa Mbunge wao, lakini zaidi sana kwa kuniunga mkono kwa vitendo katika kipindi chote cha Ubunge wangu.

Mimi najivunia sana kwa jinsi walivyo mstari wa mbele kujitolea nguvu zao za hali na mali katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu katika sekta zote. Najivunia sana kwa kunielewa na nakubaliana nilipowaleza kuwa maendeleo sio umahiri wa kununua pombe na nyama choma kwa wapigakura, bali maendeleo yanaonekana katika elimu bora, barabara zinazopitika misimu yote, maji yaliyo safi na salama na afya bora.

Wananchi ni mashahidi kuwa Jimbo letu, wameshuhudia maendeleo ya kasi na ya kutolea mfano na katika kipindi hiki cha miaka mitano chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi kuliko miaka kumi Jimbo lilipokuwa chini ya Upinzani. Wahenga walisema, ukiona vyaelea, vimeundwa. Haya yote yamepatikana baada ya kuchagua Chama cha Mapinduzi na baada ya uongozi wa CCM kufanya kazi kwa karibu sana na wananchi wa Moshi Vijijini. Hivyo, nawaomba sana tuendelee kukichagua Chama cha Mapinduzi na wagombea wake wote wa ngazi za Urais, Ubunge na Udiwani na wasinisahau mimi Mbunge wao ambaye tumeshirikiana nao kwa miaka hii mitano. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ya awali, naomba kwa kuanza kuunga mkono hoja hii na pili niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuichangia hoja hii na tatu naomba nijielekeze katika kutoa mchango wangu katika hoja hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja ya kwanza ambayo imesemwa na Wabunge walio wengi, ni umuhimu wa kuboresha mazingira ya biashara katika nchi yetu na Wabunge wengi wameuliza kwamba Serikali inafanya nini? Mbunge wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Kigoda, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, wote walizungumzia suala hili.

Mheshishimiwa Naibu Spika, majibu ni kwamba napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara imeendelea na juhudzi za kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kukamilisha taratibu za utekelezaji wa Sheria mpya wa shughuli za usajili wa biashara. Napenda wananchi waelewe kwamba katika Sheria mpya na hata ile Sheria ya zamani ilirekebishwa kwa wale wafanyabiashara wanaofanya biashara chini ya shilingi milioni 20 leseni ipatikane bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina hakika hii ni hatua madhubuti ya kuweza kuhamasisha Watanzania wafanye biashara kwa kuanzia, Wizara imeanza na uhamasishaji jamii juu ya utekelezaji wa Sheria hiyo katika Halmashauri 16 kwa sababu tusingeweza kujitawanya na tukawa tumefanya kazi ipasavyo katika Wilaya zote za Tanzania.

Kwa hiyo, tumeanza na Wilaya 16 ikiwemo Wilaya ya Tanga, Babati, Arusha, Moshi, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Temeke, Kinondoni, Ilala na Singida na katika Halmashauri nane za Lindi, Mtwara, Mikindani, Pwani, Mbeya, Sumbawanga, Njombe, Iringa na Songea.

Zoezi hili linatarajiwa kutoa fursa ya kuanisha mafanikio na maeneo yatakayohitajika na yatakayohitaji maboresho na elimu kwa wafanyabiashara inatolewa kupitia Shirika letu la *SIDO* ambalo kwa kweli limefanya kazi kubwa sana kwa wajasiriamali wadogo na mimi naamini kwamba *SIDO* imekuwa mkombozi wa Watanzania wanyonge na kwa hiyo, kuanzisha viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo.

Aidha, Wizara imekuwa ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu *TAMISEMI* katika kufanya tathimini ya kutambua uwezo wa Halmashauri zilizoteuliwa ili kuzijengea

uwezo kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hiyo. Changamoto zinazojitokeza ni pamoja na kukosekana na mfumo imara wa ufuatiliaji wa wawekezaji na wafanyabiashara wanaopewa leseni za uwekezaji na hii inatokana na uwezo mdogo wa Halmashauri ambaao Serikali inajipanga kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa ni elimu ya ujasiriamali. Waheshimiwa Wabunge walisema ni vyema kabisa tukaboresha elimu hiyo na Mheshimiwa Kigoda alizungumzia suala hilo, Mheshimiwa Shally Raymond, Kambi nzima ya Upinzani kama alivyowasilisha maoni yake Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Tatú Ntimizi, Mheshimiwa Ndesamburo, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, wote wamezungumzia umuhimu wa kuimarisha mafunzo ya ujasiriamali.

Kulingana na matamko ya sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo, tayari vyuo mbalimbali kikiwemo Chuo cha Kikuu cha Dar es Salaam na *CBE* ambacho kiko chini ya Wizara yangu, vimejumuisha kazi ya biashara na ujasirimali. Kwa mfano *CBE* kwa kutumia mitaala yake mipya imeingiza somo la ujasirimali katika ngazi zote za mafunzo ili kuwajengea wahitimu wake uwezo wa kijasirimali na kwamba mbinu mbalimbali za biashara. Tumeongeza idadi ya wanafunzi na nina hakika watakapohitimu hawatakwenda kufanya kazi za maofisini tu bali watakuwa wajasiliamali wazuri.

Aidha, Wizara kupitia shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo *SIDO* limeendelea kutoa elimu ya ujasirimali kwa Mikoa yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa ni umuhimu wa kuwatafutia wajasiriamali maeneo ya kufanya kazi zao na kuwawekea vivutio vyta makusudi ili kuwawezesha. Mheshimiwa Kigoda alizungumzia hili. Kutokana na sera ya viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo na uhamasishwaji uliofanywa na Wizara tayari Halmashauri 153 zimetenga maeneo ya wajasiriamali ya kufanya kazi. Aidha, changamoto iliyopo ni maeneo hayo kuyafikishia umeme maji na huduma mbalimbali zitakazosaidia maeneo hayo kutumika vizuri na Serikali inajipanga katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nne ilikuwa umuhimu wa kuboresha masoko ya wajasiriamali. Hili lilisemwa na Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Tatú Ntimizi na Mheshimiwa Dr. Kigoda.

Majibu yake ni kwamba eneo maalum limetengwa uwanja wa maonesho ya Mwl. Julias Kambarage Nyerere kwa ajili ya wauzaji wa bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini. Vilevile Serikali kupitia *SIDO* inaendelea kujenga maalum ya maonesho ya bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo. Mpaka sasa mabanda hayo yameanzishwa mkoani Kilimanjaro, Ruvuma na Mbeya.

Aidha, uwezeshaji wa maonesho ya bidhaa za wajasiriamali ulifanyika katika maonesho ya kanda za mashariki, kati na nyanda za juu kusini. Jumla ya wajasiriamali 634 walishiriki na kufanikiwa kuuza bidhaa za mamilioni ya shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, sekta ya viwanda vidogo kwa Tanzania inayo nafasi ya kufanya vizuri katika soko la Kimataifa kutokana na kwamba wapo wadau ambao wamejitokeza kushirikiana na wajasiriamali wa Tanzania kwa mfano kampuni ya *Fair wind* ya Marekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano ilikuwa ni hoja kuwa kutokana na kutokutumia gesi ya Mkuranga tumechelewa kujenga kiwanda cha mbolea pale Mkuranga. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Kampuni inatafuta gesi asili katika eneo la Mkuranga ilikwisha chimba visima vitatu, kisima cha kwanza kilionekana kina gesi lakini viwili havikuonekana na gesi kwa sababu hiyo hakuna kampuni ambayo imejitokeza kwenda kuwekeza kiwanda pale hadi hapo itakapohakikishiwa kwamba visima vyote vitatu vina gesi ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita ilikuwa ni kuhusu kuijengea *NDC* uwezo na *STAMICO* vilevile, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Lucy Owenya, Kamati ya Bunge yenewe ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ilihakikisha kuwa Shirika la *NDC* halibinafsishwi ili liendelee kuwa na mkono wa Serikali katika uendelezaji wa Viwanda na hasa viwanda mama, hii ni pamoja na kuingia ubia na wawekezaji mbalimbali katika kutekeleza azma hiyo. Kwa sasa *NDC* imeingia ubia na kampuni ya *Pacific Corporation East Africa* ambapo kampuni ya ubia ya *Tancol Ernogy Ltd.* imeundwa ambayo inasimamia mradi wa kuchimba makaa ya mawe ya Ngaka na kuzalisha umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *NDC* iliingia ubia pia na kampuni ya *Emol Steel Resources* kwa ajili ya kuendeleza mradi wa kasi mpya wa kuzalisha chuma ghafi. Juhudi zinaendelea ili kuingia ubia na makampuni yatakayowekeza katika miradi ya chuma Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Aidha, *NDC* ina leseni ya umiliki wa maeneo yote hayo ya Ngaka, Liganga na Mchuchuma ili kuweza kuchimba *Industrial Minerals* kwa ubia na wawekezaji binafsi, hata hivyo Wizara imepokea maoni ambayo yameendelea kutolewa na Wabunge mbalimbali kama alivyomalizia Mheshimiwa Kabwe Zitto kuhusu namna gani ya kuweza kuboresha utendaji kazi wa *NDC* kwa kuwaongezea nyenzo pamoja na nguvu kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni hoja ya uperembaji nayo imesemwa kwa lugha mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge hasa wakiuliza kwamba jitihada zifanyike kufufua viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa na havikufanya kazi kama tulivyokuwa tumetizamia. Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Mheshimiwa Paul Kimiti wamezungumzia juu ya hoja hii, Wizara imekamilisha uperembaji wa viwanda vyote 74 vilivyobinafsishwa vikiwa vizima chini ya sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, viwanda vilivyobinafsishwa chini ya sekta nyingine navyo pia vimefanyiwa uperembaji kwa hiyo, ile hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba na viwanda vingine vifanyiwe uperembaji kwa kweli tumekwishaimaliza hivyo tumefanya viwanda vyote siyo tu vile vilivyo chini ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Masoko imetembelea viwanda hivyo na kwa bahati nzuri maoni ya Kamati ya Bunge na maoni ya Kamati ya wataalamu yanaendana kwa kiwango kikubwa. Sasa hivi Waraka wa Baraza la Mawaziri umetayarishwa tayari kuwasilishwa na maamuzi yatakayofikiwa na Baraza la Mawaziri Bunge lako Tukufu litaarifiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuwa viwanda viongezeke kiidadi watu wanasema kwamba tuna mkakati hivi na vile lakini viwanda haviongezeki hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mbunge wa Chonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ni kwamba tunapoendeleza viwanda kwanza tunaangalia vile ambavyo viro na tunaviboresha. Lakini kama suala ni takwimu ni kwamba kwa upande wa viwanda vipyta juhudzi zimekuwa zikifanywa na Wizara pamoja na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) ambapo kati ya mwaka 2005 hadi 2009 Desemba jumla ya miradi 950 ya sekta ya viwanda ilisajiliwa na *TIC* aidha, viwanda vipyta 379 vilianzishwa kati ya mwaka 2005 na 2009 Desemba. (*Makofi*)

Hoja nyingine ni umuhimu wa viwanda vya kusindika mazao na hasa kuongeza thamani yake Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Balozi Abdu Mshangama na Mheshimiwa Masoud Abdalah alizungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali katika soko huria ni kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya sekta binafsi kuwekeza. Hivyo Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi, kuanzisha viwanda vya usindikaji ikiwa ni pamoja na viwanda sita vya *EPZ* ambayo vinatakiwa kuanzishwa hivi karibuni. Aidha, Serikali imeanzisha mfuko wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ikiwa na lengo vilevile la kuhifadhi mazao ili kupata bei kubwa zaidi sokoni vilevile maonyesho mbalimbali ya Kimataifa yanayofanyika hapa nchini yanalenga katika kuwaongeza wananchi ujuzi wa kuongeza thamani ya mazao yao, kuna hoja ambayo imetolewa kuhusu kulinda viwanda ambayo ametoa Mheshimiwa Siraju Kaboyonga. Mkakati wa kuviedeleza umeandaliwa na Wizara kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji katika sekta hii kwa mfano Wizara iliandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kuweka mfumo wa matumizi ya lazima ya magunia ya katani ili kupambana na ushindani usio wa haki wa magunia ya *jute* yanayoingizwa kutoka nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waraka huo ulijadiliwa na *IMTC* ambao ilielekezwa uandalawe waraka kuhusu viwanda vyote ambavyo havijafufuliwa vikiwemo vya magunia ili maamuzi ya kulinda viwanda yatolewe kwa viwanda vyote vinavyostahili. Vilevile Mheshimiwa Siraju Kaboyonga alishauri Serikali iwekeze katika *soda ash* na hapa jibu ni kwamba mradi wa magadi wa Ziwa Natron tafiti zimeendelea ili kuhakikisha athari za mradi huo za mazingira na kijamii zinaepukwa, tafiti hizi zinangojea ukamilishwaji wa mpango wa usimamizi wa eneo owevu la Ziwa Natron unaotegemewa kukamilika Januari, 2012 na ambao utatoa dira ya shughuli za kimaendeleo katika eneo oevu la Ziwa Natron. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *NDC* kwa kushirikiana na kampuni ya *Geological Study of Tanzania* imekamilisha utafiti katika eneo linalozunguka Ziwa Natron ili kubaini uwezekano wa kuwepo kwa hazina ya magadi chini ya ardhi. Vilevile *NDC* imeshafanikiwa kupata hati za umiliki wa maeneo mbadala la Engaruka lenye ukubwa wa kilomita za mraba 293 kwa ajili ya kufanya utafiti wa magadi kwa njia ya uchorongaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo vilevile suala la umuhimu wa viwanda vya pembejeo kuendelezwa kama alivyouliza Mheshimiwa Charles Keenja. Mheshimiwa Keenja tunasema juhudzi za kuhakikisha kuwa Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Mbeya kinafuliwa, zinafanyika ambapo Wizara imekwisha wasiliana na mnunuzi kampuni ya *CMG Investment* na kumtaka awasilishe mpango kazi wa kufufua kiwanda hicho. Wizara itaendelea kuwasiliana naye kuhakikisha anatekeleza jukumu lake la Kimkataba. Aidha, mapendekezo ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu viwanda vinavyobinafsishwa pamoja na Kiwanda cha Zana za Kilimo kuwa kimojawapo, Kiwanda cha *Ubungo Farm Implements (UFI)* kilishafufuliwa na mwekezaji anatekeleza wajibu wake wa kuzalisha mabomba ya kipenyo kikubwa ya maji safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo hayo yamesaidia sana kukamilishwa kwa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria. Aidha, juhudzi za kuhakikisha kuwa mwekezaji huyo anazalisha plau za kukokotwa na wanyama kazi zinaendelea na tayari mwekezaji huyo anatakiwa kuwalishwa mpango kazi, kiwanda cha *Tanzania Fertilizer Ltd.* kilisimamisha uzalishaji mwaka 1994 kutokana na kuanguka kwa bomba la hewa taka. Aidha, kwa vile kiwanda hicho kilikuwa katika makazi ya watu Serikali iliamua kifungwe na kiondolewe katika eneo kilipokuwa la Raskazone, Tanga kwa vile ni makazi ya watu. Pia Serikali imefanya jitihada za kuhakikisha kwamba Kiwanda cha Minjingu kilichokuwa kinazalisha mbolea ya *Minjigu Raw Phosphate* ya unga kinapanuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kufuatia ubinafsishaji wa kiwanda hicho ambacho sasa kinazalisha mbolea ya unga na chenga chenga. Juhudi za kuzalisha mbolea aina ya *NPK* yenye ubora zaidi zinaendelea na mitambo inaendelea kusimikwa, napenda kukushukuru sana na kwa mara nyingine napenda kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hebu maliza hiyo juhudzi za nini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile juhudzi za kuanzisha kiwanda cha mbolea cha kutumia gesi asili Mtware zinaendelea ambapo maombi ya wawekezaji kumi yalipokelewa yamechambuliwa na kubakiza kampuni tatu ambazo zilishinda vigezo vya awali. Uchambuzi wa mwisho wa mapendekezo ya wawekezaji yenye nia ya kumpata mwekezaji utafanyika baada ya wawekezaji hao kupatiwa taarifa kuhusu bei ya gesi ili waweze kukamilisha kwa maandiko yao na kuyawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na kwa mara nyingine tena naomba kuunga mkono hoja hii kwa asiliamia mia moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kwanza hiyo ni habari nzuri sana hata kwangu pia maana sisi tunakula mbolea kama nini. Lakini mmechukua muda mrefu mno hiyo habari na tumeisikia siku nyingi Mheshimiwa mtoha hoja Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, nawaambia kuwa leo wameva rasmi ili mjue hata vitu vya Tanzania navyo vina meremeta. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo ninaanza. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nataka kukuambia kuwa majina utakapoanza kuyataja hatutahesabu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kurudia tena shukrani zangu za dhati na pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa umahiri mkubwa wa kuliongoza Taifa letu katika kipindi cha kwanza cha Awamu ya Nne ya Serikali ya CCM. Namtakia kila la heri katika uchaguzi ujao ambao naamini atashinda kwa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Spika wetu, Waheshimiwa Wenyeviti na Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati nilipokuwa nikiwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwa upendo mlionionyesha mtayapitisha Makadirio haya ya Bajeti yangu bila ya vikwazo. Vilevile nachukua nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na ni Mbunge wa Makunduchi kwa kuwasilisha kwa upendo tena mkubwa. Ushauri na maelekezo ambayo yatatusaidia kuboresha uendelezaji na utekelezaji wa majukumu ya sekta yetu. (*Makofi*)

Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa ushauri na changamoto alizotoa. Ameonyesha ushirikiano kwangu wa kujenga sekta hii na uchumi wa Taifa letu ila nina hakika muda wa CHADEMA kuwa Chama Tawala bado. Siyo sawa kutaka kuchukua majukumu ya mzazi ungali bado mchanga kwani siyo rahisi kuyamudu, siyo lelemama kuwa Chama Tawala na mkitaka kujua mtuulize na tuwaeleze kama tulivyowakuza hapo mlipofikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kupitia hotuba za Bajeti za Wizara mbalimbali zilizokwishesomwa kuhusiana na maendeleo ya sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maadishi na kwa kauli hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu katika Bunge lako Tukufu na wote wamepongeza Wizara na kutoa hoja za kujenga Taifa letu. Hoja na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili hotuba yangu inaonyesha nia thabiti ya ushirikiano wenu na Wizara yangu katika kuziendeleza sekta

za Viwanda, Biashara na Masoko na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa letu, Taifa hili ni letu sisi wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefaidika sana kwa mambo mawili kwa kukubaliana na mimi katika mambo ya msingi na pili kutetea kwa nguvu zenu zote maslahi ya Taifa na wananchi tunaowawakilisha Bungeni. Kwa ujumla hoja na michango mingi imelenga katika maeneo makuu yafuatayo:-

Kwanza ufinyu wa Bajeti na umuhimu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu kuendeleza viwanda katika maeneo ya uanzishwaji wa viwanda, ubinafishwaji na ufufuaji wa viwanda, usindikaji na maliasili hususani mazao ya kilimo na teknolojia mambo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyajibu vizuri sana na nampongeza sana kwa sababu amerahisisha kazi yangu.

Kuhusu uhusiano wa sekta ya viwanda na sekta zingine hasa kilimo, sekta ya viwanda ikifunganishwa na sekta zingine itasaidia kuongeza tija na ufanisi ukiangalia kilimo bila pembejeo huwezi kuwa na tija wala ufanisi bila kuwa na zana ambazo zinatokana na viwanda huwezi kuendeleza kilimo, na bila kuwa na masoko ya kilimo huwezi ukaendeleza kilimo kwa hivyo, sekta ya viwanda ni sekta kiongozi wakati kilimo ni uti wa mgongo na Kilimo Kwanza na baadaye vingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zililenga vilevile kuendeleza biashara na viwanda vidogo. Viwanda vidogo ni chimbuko la viwanda vikubwa, kwanza kwa nchi zilizoendelea viwanda vidogo vinatengeneza *spare parts* kwa ajili ya viwanda vikubwa na biashara ndogo ndiyo inayotengeneza kada ya matajiri wa kati ambao ndiyo watumiaji wa bidhaa za nchi yoyote ile. Kwa hiyo, sekta hii ya viwanda vidogo ni muhimu sana kwa Watanzania na naipongeza sana *SIDO* kwa kazi nzuri inayoifanya katika nyanja zote ambazo ni majukumu yake. Kwanza naipongeza kwa undelezaji wa wajasiriamali na vilevile naishukuru sana kwa kusimamia mfuko wa ukopeshaji na vilevile naishukuru sana katika kuanzisha karakana mbalimbali na kuwa na maeneo mbalimbali ambako wajasiriamali ama wamejifunza biashara ama wamejifunza kutengeneza bidhaa kwa kutumia malighafi za humu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya biashara shughuli za uchumi haziwezi kuchangamka kwa hiyo, sekta ya biashara ni muhimu sana na hakuna mtu anayejitosheleza na kwa vile hakuna nchi inayojitosheleza biashara lazima iwemo ili shughuli za uchumi zichangamke. Kwa hiyo, Wizara yangu inasimamia sana sekta ya biashara na kitu cha kwanza ambacho tumekifanya ni kurahisisha biashara kupitia Sheria mpya ya Bara na vilevile toka Bodi ya Biashara ya Ndani ilivyovunjwa. Biashara ya ndani imeparanganyika na ili kuimarisha biashara ya ndani tumehakikisha kwamba sasa tunarudisha bodi ambayo itasimamia biashara ya ndani na ile Biashara ya Nje ili biashara ya ndani iwe ni chimbuko sasa la kuendeleza biashara ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka bidhaa mahiri, ukitaka bidhaa zenye ubora unaotakiwa lazima kuwe na ushindani. Kwa hiyo, Wizara yangu inasimamia ushindani wa haki. Ni kweli kwamba viwanda vyetu bado ni vidogo na ni kweli kwamba nchi yetu

kutokana na uchumi wake kuwa finyu haiwezi kutoa ruzuku na kwa hiyo, tunapopata bidhaa za nje ambazo zinapata ruzuku kwenye nchi zao ambazo uzalishaji ni mkubwa, lazima Serikali ichukue hatua kupitia kodi mbalimbali na ushuru mbalimbali katika kulinda viwanda vyake na Serikali yetu kupitia Wizara yetu ya Fedha imekuwa ikifanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ilipewa jukumu muhimu sana la kusimamia masoko ya mazao ya kilimo. Wabunge wengi wameongelea juu ya wasiwasi wa bei ya mazao kuhusu kupanda na kushuka lakini napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la bei ni la ugavi na watumiaji kama ugavi ni mdogo kwa vyovyyote vile bei ya mazao ya kilimo itakuwa ni kubwa. Kama uzalishaji unakuwa mkubwa kama mwaka huu bila shaka bei inakuwa inapungua na kwa hivyo suala la bei ya mazao ya kilimo kushuka na kupanda ni jambo la kawaida dunia nzima isipokuwa Serikali yetu imechukua hatua kwanza kwa kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ili pale mkulima anapoona bei ni ya chini aweze kuwekeza mazao yake na kutumia mazao yake na kutumia stakabadhi kupata mikopo kwa ajili ya matatizo yake mbalimbali na wakati bei inavyopanda aweze kuuza na kupata faida inayotakikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kutumia *strategic grain reserve*, għala letu la Taifa badala tu ya kuwa għala litakalotumika wakati wa baa la njaa sasa litakuwa linanunua mazao wakati yakiwa mengi ili bei isishuke sana na wakati wa uhaba itakuwa inauza mazao haya ila bei isipande sana. Kwa hiyo, mtaona kwamba Serikali yenu inajitahidi sana katika kuhakikisha kwamba Serikali inachukua hatua zinazotakiwa ili kuweka uchumi vizuri na ili kutokuwapa hasara kubwa sana waklima wetu, utaona kuwa nimeenda kwenye hayo mambo ya jumla kabla sijawataja Wabunge ambao wamechangia hoja yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia, kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge 52 walichangia hoja zinazohusu Wizara yangu wakati wakichangia hotuba za Bajeti za Wizara mbalimbali na nakiri kwamba sitawenza kurudia majina hayo kwa sababu yatakuwa yametajwa katika Wizara zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 16 walichangia hotuba yangu kwa kauli na Waheshimiwa Wabunge 43 walichangia kwa maandishi. Michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mingi na ni muhimu na inayohitaji majibu ya kina kwa muda mfupi nilio nao majibu yangu yameelekezwa katika maeneo makuu yaliyochangiwa kama nilivyoyataja hapo juu. Hata hivyo, ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwamba majibu ya kina yanayojibu kila hoja yameandaliwa kwa maandishi na yatagawiwa kwenu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja zinazohusu Wizara yangu wakati wakichangia katika hotuba za Bajeti za Wizara mbalimbali ni hawa wafuatao, nilisema sitawata lakini wale waliochangia kwa kauli ni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Dr. Cyril

Chami, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Mbunge wa Moshi Vijijini, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, wote waliochangia kwa kuzungumza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwataje waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa *Engineer* Laus Mhina, Mheshimiwa Tatou Ntimizi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Mohammed Sinani, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Anne Makinda Spika, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Pindi Chana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu yale ya jumla sasa naomba niende kwenye mambo mahsusini ambayo nilitaka kulielezea Bunge lako Tukufu kuhusu sekta ya viwanda. Hoja iliyotolewa ni kwamba Wizara ina umuhimu mkubwa katika uchumi wa Tanzania lakini si sekta ya kipaumbele na hii inapelekea kupata *ceiling* ndogo na taasisi zake kushindwa kutoa huduma inayotarajiwa, hoja hii imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara na vile vile imetolewa na Msemaji Mkuu wa Upinzani wa Wizara yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mchango wa viwanda katika maendeleo ya Taifa, ufinyu wa Bajeti ya Serikali ndio unaosababisha kutotekelezwa mipango mingi mizuri ya kuimarisha sekta ya viwanda. Kwa mfano, Wizara imeandaa mkakati unganishi na mpango kabambe wa maendeleo wa viwanda ambao lengo lake ni kumaliza matatizo yanayoikabili sekta hii na kuiwezesha kusimama katika nafasi ya kuleta maendeleo ya viwanda kama ilivyo katika nchi zilizoendelea. Kwa ujumla tunakubaliana na ushauri wa Kamati ya Viwanda na Biashara, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Viwanda na Biashara na Waheshimwia Wabunge wote waliochangia katika eneo hili akiwemo Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya,

Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Waheshimiwa wengine ambao sitawataja hapa lakini nimejaribu kuyataja majina yote katika orodha ile ya ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kutilia mkazo sekta ya viwanda, sekta ambayo ndiyo inatumia sayansi na teknolojia, sekta zingine zote haziwezi kuendelea. Sekta ya madini inatumia mitambo inayotengezwa viwandani, sekta ya kilimo inatumia zana zinazotoka viwandani, sekta ya utalii inatumia magari na ndani ya hoteli kuna vijiko na mambo mengi, kwa hiyo, hatuwezi kujidanganya tukasema kwamba kilimo kwanza bila ya kufunganisha na sekta ya viwanda. Kwa hivyo, nawashukuru kwa ushauri wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ni ubifsishaji wa viwanda na mashirika ya umma kati ya viwanda 336 na makampuni 66 yaliyobinafsishwa, ni makampuni 12 tu ndiyo yanafanya kazi. Hoja hii kwa kiasi kikubwa imetoka Kambi ya Upinzani. Nataka niwaambie kwamba tumebinafsisha viwanda na makampuni mengine au Serikali imeacha biashara ili kusudi ifanye kazi yake ya utawala na kuwawezesha wafanyabiashara na wenye viwanda na wengine wote wanaoshughulika na uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiwa na soko huru, uchumi wa soko maana yake kuna viwanda ambavyo vitakufa na viwanda ambavyo vitakuja kwa kutegemeana na mahitaji ya nchi na mahitaji ya Kanda na mahitaji ya Kimataifa. Kwa hivyo, msishangae kuona viwanda vingine ambavyo vinaondoka na vingine vipyta vinakuja. Kwa mfano viwanda vyta za zana za kilimo, hatuwezi tukaendelea na viwanda vyta kutengeneza majembe sasa ni wakati wa kuwa na viwanda vyta za zana za kilimo ya kutoka matreka madogo na matreka makubwa kwa sababu wananchi hawataki kuendelea na kilimo cha jembe.

Kwa hiyo, ukikuta *Ubungo Farm Implements* au *Mbeya Farm Implements* ilikuwa inatengeneza majembe, ilikuwa labda inatengeneza visu, sasa ni wakati ambapo tumeperemba na ye yote ambaye atakuwa hajafufua kiwanda Serikali itakichukua na kukipeleka kwa anayeweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama ni zana za kilimo tutahakikisha zana zile zinazotakiwa na soko na wananchi kwa kiasi kikubwa ndizo zitakazotengenezwa na Serikali itaweka mazingira wezeshi. Kwa hivyo, naomba niende kwenye viwanda vyta ngozi, wengi hawafahamu kwamba viwanda vyta ngozi vingi vinafufuka, kwa mfano *Morogoro TANNERIES* ambayo inaitwa *East Hides* sasa hivi inazalisha kwa asilimia mia moja kwa sababu bidhaa za ngozi sasa zinatakiwa sana nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo kufanikisha uzalishaji Morogoro kutakifanya na kiwanda cha Mwanza kifufuliwe kwa sababu ambaye amenunua kiwanda cha Mwanza ni yule yule aliyenunua kiwanda cha Morogoro, kwa hivyo kazi yetu kubwa ni kuona kwamba kiwanda cha Mwanza kinafufuka na kama hawezi kukifufua basi kiende kwa mtu mwagine. Kiwanda cha Moshi kinafanya kazi vizuri, Kiwanda cha Kibaha kinafanya kazi vizuri, ninafarrijika kuona kwamba viwanda vyta ngozi sasa vimeanza kufufuka na vinatengeneza ngozi ama kwa kiasi cha mwanzo au cha katni na

hata vingine vinatengeneza ngozi ambayo imetengenezwa kikamilifu na inatumika na wale ambao wanatengeneza viatu na bidhaa za ngozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja nyingine ambayo ameileta Ndugu yangu Mheshimiwa Felix Mrema kuhusu *General Tyre*, napenda kumpongeza Mheshimiwa Felix Mrema kwa kukazania kiwanda chetu cha *General Tyre*, hiki ni kiwanda ambacho kwa kiingereza *demand* yake ni kubwa, lakini mwekezaji aliyejukwepo alikuwa anasusua ni kama vile alikuwa hapendi Tanzania kutengeneza viwanda. Sasa hivi tuna maongezi ya kuondokana na ubia naye ili tupate mbia mwingine na wapo wengi wanaotaka kuingia ubia na Serikali katika kutengeneza matairi, lakini hatuwezi tukaingia ubia na mwingine kama yule wa awali ambaye ni *continental AG* hatujamalizana naye ubia wetu. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira naomba niendelee kuhakikisha kwamba ni azma yangu kwamba *General Tyre* siku moja ifanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo aliliongelea ni kuhusu mafao ya wafanyakazi, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba wafanyakazi wengi sana walilipwa na tena walilipwa vizuri na walilipwa kutockana na fedha za Hazina kwa sababu kiwanda chenyewe kilikuwa kinazalisha kwa hasara. Sasa kama kuna wachache waliobaki basi suala hilo nalichukua na ninalifanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Kilimanjaro Machine Tools*, kwa sababu ya m dororo wa uchumi, *Kilimanjaro Machine Tools* wakati ilipopata mwekezaji kidogo alisita lakini sasa amerudi na nimeonesha ari ya kuweza kuendeleza kiwanda cha *machine tools* ni mategemeo yangu kwamba Kilimanjaro watafurahia matunda ya mwekezaji huyu ambaye ameingia ubia na *NDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea suala la *EPZ*, ndege wanaweka kiota chao mahali ambapo mti una uhakika wa vifaranga kuwa salama, wawekezaji watataka kwenda mahali ambapo wapo salama na mahali ambapo miundombinu ni mizuri, *EPZ* ndiyo mahala pake. Kwa hivyo, Wizara yangu itakazania sana *EPZ* na Serikali kwa ujumla inaweka msisitizo mkubwa sana katika *EPZ* ili tuweze kupata na kuwavutia wawekezaji walio wengi, suala ambalo ni changamoto ni kuwa na Bajeti finyu, lakini tutajaribu kuangalia vyanzo vingine zaidi ya hivi vya ndani kuweza kujenga miundombinu na tutajitahidi sana kutumia sekta binafsi ambayo imeshaonesha ari ya kuendeleza maeneo ya *EPZ*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijafanya haki kwa Mkao wa Kigoma, mko a ambao wanafikiri tunauacha nyuma, Kigoma inatuunganisha na Kongo ambalo ni soko kubwa la Tanzania, kwa hivyo tutajitahidi sana, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba hata kama mimi sijakwenda lakini watumishi wengine wa Wizara wamefika Kigoma na tumeangalia mahitaji ya Kigoma na tutaangalia jinsi ambavyo tutaendeleza uchumi wa nchi yetu kupitia Kigoma kwa kuunganisha soko la Tanzania na soko la Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ningependa kumalizia kwa kusisitiza kuwa nafasi ya sekta ya viwanda katika kubadilisha uchumi kuwa wa kisasa kwa nchi

yetu hauna mjadala ni kwa sababu hii Mheshimiwa Rais ameamua kuteua sekta ya viwanda kuwa moja ya ajenda yake ya kwanza katika muhula wake wa pili katika uongozi wake na kwa ajili hiyo kwa sababu wote tunakubaliana tutampa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kengele karibu itagonga naomba nirudie tena kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Hanang, wananchi ambaa walinipa mimi kura mwaka 2005 kwa asilimia zaidi ya 91, ni mategemeo yangu safari hii wote watanipa kura, walishaniomba nitangaze kugombea tena mwaka huu wa 2010 na nilisema kwamba kwa sababu naendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi nisingeweza kutangaza wakati ule walivyoniomba na wamenichangia hata hela za kuchukua fomu, napenda mbele ya Bunge lako Tukufu na mimi nichukue fursa hii kuwahakikishia wananchi wa Hanang kwamba nitagombea Jimbo la Hanang na nina hakika nitapata kura zote kwa kazi nzuri tuliyofanya kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imelipa kipaumbele suala la uimarishaji wa masoko ya mipakani ili kuzipa fursa bidhaa nyingi za Tanzania kuingia katika masoko ya nchi jirani, ni pamoja na kuimarisha Kigoma na Tunduma, ni pamoja na kuunganisha Sirari, kuimarisha Namanga na kuunganisha maeneo yote ya mipakani ili tuweze kuongeza biashara ya Tanzania katika nchi jirani hasa zile za Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *EPA* tulikataa kutia saini ule mkataba wa awali kwa sababu maslahi ya Afrika ya Mashariki yalikuwa hayajazingatiwa, kama tulivyoona maslahi mengi ya Afrika Mashariki yamo kwenye *EPA* kamili. Ni mategemeo yangu kwamba majadiliano yataendelea vizuri na ifikapo mwezi Novemba labda tutatia saini mkataba ule lakini lazima tusimamie maslahi ya Tanzania na bila shaka hatuna sababu ya kufanya biashara na Ulaya kama biashara hiyo haitatuendeza na ndiyo sababu ambayo imetufanya tukashindwa kutia saini mkataba ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na ninaomba waniwie radhi kwa sababu sijataja majina yao moja moja, kwa mfano Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Martha Mlata ambaye anapigania wasanii na wengine wote ambaa wamepigania maslahi ya wapiga kura wetu, ninasema kwamba mambo yote nitakuwa nimeyaandika katika majibu yangu ya hoja na nitayaweka kwenye *Hansard* na ni mategemeo yangu kwamba Wabunge wote na Watanzania watapenda kusoma *Hansard* ile ili waone nilichokuwa nimetayarisha katika majibu yangu haya ya kuhitimisha hoja yangu. Kama kutakuwa na mambo ambayo sijayajibu wakati wa Kamati niko tayari kuyajibu na sasa naomba nitoe hoja kwa kuwashukuru sana kwa nisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**NAIBU SPIKA:** Hiyo safi kabisa, na ndiyo utaratibu unavyotakiwa, ile Kanuni inayotakiwa kuungwa mkono hoja inataka siyo Mawaziri tu, walipokuwa wanasimama Mawaziri tu ilikuwa wakati wa chama kimoja kwa sababu upande ulikuwa Serikali na upande mwingine ilikuwa *back benchers*, sasa hivi ni vyama vingi kwa hivyo mlichofanya ni sahihi kabisa na ndivyo inatakiwa. (*Makofi*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

Kifungu 1001- *Administration and General*.....Sh. 6,860,262,000

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kupitia programu ya 10 kifungu kidogo cha 1001, 210100. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimezungumzia kuhusu kiwanda kidogo cha kusindika ngozi na kusindika maziwa kilichofunguliwa juzi na Waziri Mkuu katika ziara yake Mkoani Singida, kiwanda hicho kingeweza kusaidia sana Singida endapo kitaboreshwa kwa kuongezwa kwa miundombinu na kupanuliwa zaidi, nikamwomba Waziri.

Je, katika Bajeti yake haoni kwamba kuna kila sababu ya kuongeza na kupeleka pesa katika kiwanda hicho kidogo ili kuweza kukiboresha zaidi na kuweza kufanya kazi vizuri zaidi kwa maslahi ya Singida na nchi kwa ujumla?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo kwa kutaka kujuu namna ambavyo tunaweza kuboresha kiwanda cha maziwa na kiwanda cha ngozi ambacho kipo Singida. Kwanza ye ye anafahamu kwamba Wizara yetu ikitoa ahadi huwa inatekeleza kwa sababu mwaka uliopita aliomba kiwanda cha kusafisha mafuta ya alizeti na bila shaka najua kwamba kiwanda kile kimeanza na hata sisi wa Mkoa wa Manyara tutakuwa tunaleta alizeti yetu Singida kuja kusafisha mafuta ya alizeti.

Kwa hiyo, kuhusu kiwanda cha maziwa na ngozi kilichopo Singida kwa sababu mkuu wa Shirika la *SIDO* yuko hapa naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumuagiza kwamba aone namna ambavyo anaweza akaongeza kama ni mkopo au namna ambavyo atasaidia andiko ambalo litafanya kiwanda hiki kikaongezwa miundombinu inayotakiwa kusudi kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. (*Makofi*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jina langu ni John Paul Lwanji, Paul Lwanji ni baba yangu na ni marehemu.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, tumekutambua.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kuhusu suala la Kiwanda cha Saruji - Itigi. Kwa muda mrefu nimezungumza sana na ilionekana kuwa mwanzo nilisaidiwa katika kuwapata wawekezaji na mimi mwenyewe nilishughulika

sana mpaka na Mheshimiwa Mossy Suleiman, Mbunge kutoka Zanzibar tukapata mtu aliyeonesha *interest* Mchini, akaja mpaka Itigi akaangalia na akapapenda sana kwa sababu nilitaja miundombinu yote tunayo hapa pamoja na malighafi, pamoja na wengine ambao walitoka Ujerumanu na Uingereza lakini waliishia Mtwara ingawa walikuwa na nia ya kuja huku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katikati Wizara imenyamaza kimya, sasa sijui wanatusaidia vipi sisi wananchi wa eneo hilo ambao kwa kweli ni zuri sana kwa uwekezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge umejadili kwa kirefu sasa ungetaka *specifically* wafanye nini?

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni kwamba watusaidie basi kwa kuongeza juhudji ili tuweze kupata mwekezaji wa uhakika wa kuweza kufika kule na kuona uwezekano wa kuweka kiwanda pale.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi kwa kunikumbusha suala la Saruji - Itigi. Yeye anajua kabisa kukiwa na kiwanda Itigi na sisi wa Manyara tutakuwa tumepona na watu wengi wa Manyara wako kule Manyoni, kwa hivyo iko kwenye *interest* yangu kiwanda hicho kuwepo pale Itigi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini mdororo wa uchumi uliotokea duniani ndiyo sababu hasa ya wale wawekezaji kurudi nyuma, lakini tutaendelea kuhamasisha wawekezaji na kuwaeleza raslimali ambazo ziko Manyoni ambazo ndiyo malighafi ya kuweza kutengeneza saruji na kuwa na kiwanda cha saruji.

Naomba Mheshimiwa John Paul Lwanji ajue kwamba Serikali imejitoa kwenye uwekezaji wa viwanda na kazi yake sasa ni kuweka mazingira wezeshi jambo ambalo Serikali ya CCM imeshafanya hilo kwa kuwa na barabara, reli na umeme. Nina hakika tukiweka juhudji kidogo wawekezaji watapatika na ahsante. (*Makofii*)

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Niko kwenye *sub-vote 1001*, kifungu kidogo cha mshahara wa Waziri lakini sina haja na mshahara wake kwa sababu ninaelewa kabisa ile dhana ya wanawake wanaweza iko *reflected* kwa mama Nagu, ila nilikuwa naomba anipe maelezo kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wote tunajua kwamba viwanda vinachangia Pato la Taifa na *actually* ni dhana mojawapo ya maendeleo katika nchi yoyote, na kwa kuwa viwanda vingi vilivyobinafsishwa kama Waziri alivyosema ni wazi kwamba vingi vimetelekezwa na mifano hai ipo, kama *Kilimanjaro Machine Tools, Tanganyika Packers, General Tyres* na vingine vingi, na vilevile Mheshimiwa Waziri amesema

kwamba sasa Serikali imejitoa katika masuala ya biashara ili ku-concentrate zaidi katika masuala ya kiutawala jambo ambalo ninakubaliana nalo.

Je, lile ombi la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo kwamba auziwe baadhi ya viwanda kule Kilimanjaro ili aweze kuviedeleza na vilevile kuweza kuwapatia ajira wananchi wa Kilimanjaro litazingatiwa hasa kwa kuzingatia uzalendo aliouonesha Mzee Ndesamburo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba anakubaliana na mimi kwamba viwanda vinachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi yoyote kupitia kuchangia katika Pato la Taifa. Ni kweli kwamba toka tulivyobinafsisha kuna viwanda ambavyo havijafufuliwa na baada ya Wizara yangu kufanya lile jukumu la kuperemba tumejua ni viwanda vipi ambavyo vinafanya kazi vizuri na vipi ambavyo havifanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kilimanjaro Machine Tools* ni kweli kilikuwa kimesimama kwa muda mrefu, lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba sasa yule mwekezaji ambaye alikuwa ameahidi kuja kuwekeza kwa kuingia ubia na *NDC* amerudi tena na ni mategemeo yangu kuwa *Kiliamanjaro Machine Tools* itafufuka na itachangia uchumi wa Kilimanjaro na uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vingine ambavyo havijafufuliwa baada ya kuperemba nimesema kwamba tumepeleka taarifa ile kwenye Baraza la Mawaziri ili tuwe na uamuzi wa pamoja na mimi sioni kwa nini Mheshimiwa Philemon Ndesamburo akose. Nakumbuka mwaka jana nilimwambia afike Wizarani, lakini mpaka hivi leo alivyochangia sijawahi kumuona Mheshimiwa Philemon Ndesamburo amefika Wizarani kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ndesamburo ni kama baba yangu kwa hiyo siwezi kumsema sana naomba tu nimsihi tu kwamba, aje Wizarani atuoneshe uwezo wake wa kuwekeza na anataka kuwekeza kwenye nini ili Wizara iweze kuwajibika. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi katika mchangano wangu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kilio cha wasanii kimekuwa ni wimbo usioisha mpaka pale mambo yatakapokuwa barabara katika maisha yao.

Nilimuuliza kwamba *COSOTA* ndiyo kimbilio kubwa la wasanii, lakini imekuwa ikifanya kazi bila ya uangalizi wa bodi yoyote. Je, bodi ipo na kama ipo imeshaanza kufanya kazi na kama bado itaanza lini? Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Martha Mlata kwa hoja yake ambayo ameitoa wakati huu wa sasa hivi kuhusu kilio cha wasanii na kwamba *COSOTA* ni kimbilio lao wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliteua Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya COSOTA mwezi Septemba, 2009 na ni mategemeo yangu kuwa mpaka sasa Bodi hiyo ingekuwa inafanyakazi. Lakini nafikiri kuna mlolongo mrefu au utaratibu ambao bodi hiyo inapaswa ipite ili Wajumbe wale na Mwenyekiti waweze kuisimamia COSOTA ipasavyo na nikitoka hapa nitafuatilia ili kujua ni wapi mambo yamekwama na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba bodi itaanza kufanyakazi muda si mrefu. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nipo kwenye *vote* hiyo hiyo 44, programu ya 10, *sub-vote 1001* mshahara wa Mheshimiwa Waziri, nautaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko katika ukurasa wa 55 ameleeza na ninanukuu; “Kwa mfano kiwanda cha Mazava cha uwekezaji kutoka Madagascar kimeanzisha mkoani Morogoro na tayari kimeuza nguo katika soko la AGOA zenye thamani ya dola za Kimarekani 32,498.9 katika kipindi cha mwezi wa Februari hadi tarehe 8 Juni, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kinachozungumzwa ni uwekezaji wa Madagascar ambao wako Morogoro wanatengeneza nguo kwa ajili ya kuuza kwenye soko la AGOA, kwenye kitabu hiki kuna sehemu nyininge ambayo imeelezea Watanzania wawekezaji ambao wametumia fursa hii ya AGOA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri anieleze, Tanzania imetumiaje fursa hii ya AGOA ambalo ni soko zuri na la uhakika ambalo tumepewa kwa lengo la kuinua maisha ya Watanzania. Je, tumelitumiaje soko hili kwa sababu nimeona hapa umezungumza habari ya wageni tu Madagascar, Tanzania imetumiaje fursa hii ya soko la AGOA ili kunyanya mazao ya Tanzania?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhsukuru Mheshimiwa Salim Hemed Khamis kwa hoja yake aliyoitoa na kuonesha umuhimu wa soko la AGOA katika kupanua mauzo yetu nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazava inatoka Madagascar lakini imewekeza Tanzania na wanaofanyakazi kwenye kile kiwanda ni Watanzania na ni vijana wadogo maana yake mimi ni mmoja wa wale watu ambao nilivyoona mambo kule hayaendi vizuri nimejaribu kuwavutia wale wawekezaji waje Tanzania. Wameajiri wafanyakazi 600 katika muda mfupi na wataajiri zaidi na ajira itafika 1,200 pengine na zaidi na wanatengeza mavazi ambayo yanauzwa kwenye makampuni yale makubwa kama ya Nike, kama ya wale wa Adidas na wengine na wanatengeneza mavazi nadhifu kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kwa maneno ya Mkuu wa ile kampuni alisema kwamba alipokuwa Madagascar alikuwa anatumia miezi mitatu kutengeneza mavazi kiasi cha 23,000 lakini Tanzania

ametengeneza kwa mwezi mmoja tu. Napenda kueleza kwamba Watanzania kwamba wana uwezo na kwa hivyo wala wasiwe na wasiwasi kwamba wanaweza wakashindana na nchi zingine na kwa hivyo hii ni namna moja ya kutumia soko la *AGOA* kwa sababu tunauza sehemu ya mavazi hayo Marekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tuna kiwanda kama cha *Sun Flag* kinauzi mavazi kule Marekani. Tuna kiwanda kile kingine cha Arusha kinachotengeneza vyandarua cha *A to Z* nao wanauzi kule, na kuna viwanda vingine Dar es Salaam vinajitahidi sana kuza kwenye soko la *AGOA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tunaweza kuongeza jitihada na katika kufanya hivyo tuliongea na kampuni fulani ya Marekani ambayo imikuja kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na kujaribu kuonesha namna ya kupata mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ambayo hatimaye bidhaa zake zitauzwa kwenye soko la *AGOA*. Ni mategemeo yangu kwamba kwa kiasi kikubwa tutaweza kutumia soko la *AGOA* na hasa tukisimamia jitihada hizi ambazo zimeanza sasa hivi. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii. Mimi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri ameeleza vizuri sana katika uwasilishaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anawasilisha alizungumzia kuhusu viwanda vya ngozi na vingine, lakini katika andiko langu nilimuomba Mheshimiwa Waziri anisaidie katika viwanda vya vinu vya kuchambulia pamba vilivyoko Mwanza kama Ngasamo, *Nasa Ginnery* na vingine, kwa sababu viwanda hivi vilikuwa vinatoa ajira, sasa Serikali inasemaje kujusu viwanda hivi?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Richard Ndassa kwa kuona umuhimu wa vinu vya kuchambulia pamba kwa sababu pamba ni zao muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na kwamba katika kilimo kwanza tunapaswa kusindika pamba kwa kuanzia na vinu hivi na baadaye viwanda vya kutengeneza nyuzi na hatimaye nguo na hadi mavazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo katika kulitilia mkazo suala la Kilimo Kwanza naomba nimuahidi Mheshimiwa Richard Ndassa kwamba kama siyo mimi watendaji wa Wizara yangu wataenda kule kuangalia ni tatizo gani haswa ili tushirikiane kwa pamoja katika kuondoa matatizo ya vinu vya kuchambulia pamba kwa sababu ndiyo namna pekee ya kuanza kuongeza thamani kwenye pamba ya mkulima wa Usukuman. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ambaye awali ya yote napenda nimpongeze sana kwa jinsi alivyoshughulikia matatizo ya Kiwanda cha Nyuzi Tabora, mpaka sasa kiwanda kinaendelea vizuri. Nampongeza sana Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumza pamoja na mambo mengine kuhusu rasilimali muhimu sana ambayo nchi yetu inayo, nayo ni ya *soda ash* kule *Lake Natron*. Mradi huu wa *Lake Natron* unaratibiwa na *NDC* lakini mpaka leo hii nchi yetu bado inaagiza *soda ash* kutoka nje wakati Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na *soda ash* hapa hapa nchini ambayo tungeichimba, tungeuza na tungetumia wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lini mradi huu utakuwa wa manufaa kwa nchi yetu na kwanini unachelewa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo matatizo ya kutegemea wawekezaji kutoka nje, tungekuwa na wawekezaji wetu sisi wenye pengine leo magadi ya Ziwa Natron yangeshaanza kutumika na kama *NDC* ingekuwa na uwezo wa kimitaji pengine tunganeanza kutumia magadi ya Ziwa Natron. Lakini hivyo ndivyo ilivyo, hatuwezi kuendelea bila kushirikiana na wawekezaji kutoka nje. Suala kubwa kwenye uwekezaji wa magadi ya Ziwa Natron ni suala la uhifadhi wa mazingira hasa ambao una uhusiano na *Flamingo*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo wenzetu wanajali sana kuona Korongo kule Ziwa Natron wakati sisi tunalia njaa. Lakini tumejaribu kuangalia namna mbadala ya kuweza kutumia rasilimali hiyo hata kama si pale Ziwa Natron basi lile eneo la Engaruka pengine linaweza likatumika ambako ni mbali kidogo na Ziwa Natron na kwa hiyo wale Korongo hawawezi kuathirika na bila shaka ifikapo mwaka 2012 tunaweza tukawa tumefanikiwa kutumia rasilimali hiyo kwa ajili ya kutengeneza kemikali mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba kemikali ambazo tunaweza kutengeneza kutokana na magadi vilevile inaweza kutokana na gesi na sisi Watanzania tuna bahati, tuna magadi na huko tuna gesi, kwa hivyo tunaweza kuwa nchi ambayo itatengeneza kemikali nyingi kama *nitrate* ambayo inatakiwa kwenye migodi ya dhahabu na migodi mingine. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ili mradi tu urasimu uondoke.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts..</i>	.....	Sh. 306,068,600
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning..</i>	.....	Sh. 4,517,859,000
Kifungu 1004 – <i>Information, Education &amp; Communication.</i>	.....	Sh. 134,839,200
Kifungu 1005 – <i>Internal Audit Unit</i>	.....	Sh. 154,014,500
Kifungu 1006 – <i>Legal Service Unit.</i>	.....	Sh. 44,877,800

Kifungu 1007 – *Management Information System*... ... Sh. 88,451,100  
 Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*. .... Sh. 129,195,900

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2001 – *Industry*... ..... Sh. 5,075,268,600

Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises*

*Division* ... ..... Sh. 4,437,380,000

Kifungu 3001 – *Commerce* ... ..... Sh. 1,783,554,100

Kifungu 4002 – *Commodity Market*

*Development*... .... Sh. 8,011,050,200

(*Vifungu vilivyotajwa*

*hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 44 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ..... Sh. 0

Kifungu 1003 – *Policy and Planning*.... .... Sh. 18,302,690,700

Kifungu 2001 – *Industry* ... ..... Sh. 197,995,500

Kifungu 2002 – *Small and Medium Enterprises*

*Division* ... ..... Sh. 2,947,324,800

Kifungu 3001 – *Commerce* ... ..... Sh. 1,277,852,000

Kifungu 4002 – *Commodity Market*

*Development*... .... Sh. 6,191,804,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe Makadirio hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka  
2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Makadirio ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko yamepitishwa na Bunge hili. Sasa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hii ni Wizara inayoongozwa na akinamama, kwa kweli hata kitabu chao ukisoma kinavutia na habari zilizomo humu pia zinavutia. Kwa hiyo, hiyo ni dhahiri kabisa hamjamwangusha Mheshimiwa Rais kwa kuwakeni katika Wizara ile na muendelee hivyo hivyo ili wanawake wengine waweze kupata nafasi kutokana na ufanisi wenu ninyi. Kwa hiyo, anaomba Watanzania muendelee kuvala mavazi ya Tanzania na mfufue viwanda vyetu vya mavazi. Sera ya Awamu ya Kwanza ya nchi hii ilikuwa asilimia 60 ya pamba yetu itengenezee nguo. Hivi juzi soko la pamba bei zake zimeshuka nadhani ingekuwa nguo ingekuwa shuka zaidi. Hatua mlizoanza Mheshimiwa Waziri muendelee nazo. *Speed* nayo ni muhimu kwa sababu urasimu kwa Tanzania nadhani ndio tatizo kubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sina matangazo mengine naomba kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.45 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,  
Tarehe 2 Julai, 2010 saa tatu asubuhi)*